Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Hamsini - Tarehe 18 Agosti, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

***D U A***

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali la kwanza. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni takribani miezi 10 sasa imepita tangu tumefanya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani na katika uchaguzi huu zilifunguliwa kesi mbalimbali zinazohusu Uchaguzi Mkuu.

Tunapozungumza sasa kuna kesi 37 zinazohusu chaguzi ambazo zinasubiri kusikilizwa na kwa mujibu wa Sheria ambazo tumewekeana kesi hizi zinatakiwa ziwe zimekamilika katika kipindi cha miaka miwili na sasa ni mwaka mmoja unaelekea kwisha.

Katika mgao wa fedha kwa sababu ya kusikiliza kesi hizi Jaji Kiongozi amesema waliomba shilingi bilioni 3 kwa ajili ya kuwezesha kusikiliza na kumaliza kesi hizi.

Lakini hadi sasa Serikali imewapa shilingi milioni 300 ambazo zina uwezo wa kumaliza kesi tano kati ya kesi 37 na Bajeti ya mwaka huu itatupeleka mpaka kipindi cha kumaliza miaka miwili wakati tayari kipindi kinachoruhusiwa kisheria kitakuwa kimekamilika. Waziri Mkuu unaliambia nini Taifa kuhusu jambo hili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbowe maelezo aliyoyatoa ni sahihi kabisa na Serikali inalitambua hilo tatizo. Kesi ambazo tunaweza tukasema ziko tayari kwa ajili ya usikilizwaji ni 25 kati ya zile ambazo amezitaja. Kwa hiyo, Serikali kwa kweli inalitambua jambo hili. Tunaendelea na sisi kuhakikisha kwamba tunakidhi mahitaji yale ya kisheria kwa namna zozote zile ambazo Serikali itaona inafaa. Kwa kuwa ni jambo ambalo lipo kwa mujibu wa taratibu, wajibu wetu ni kuona kama tunaweza tukalitekeleza hivyo.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ningeomba nimwulize swali lingine la nyongeza ambalo lina uhusiano wa karibu sana na swali langu la msingi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu bado narudia pale pale kwamba baada ya Uchaguzi Mkuu, miezi 10 imepita na tunatambua kwamba baada ya Uchaguzi Mheshimiwa Rais ana mamlaka ya

kikatiba ya kuteua Wakuu wa Wilaya ya kuteua Wakuu wa Mikoa, kuziba mapengo ambayo pengine yamejitokeza kutokana na masuala mbalimbali ya kiuchaguzi na mengineyo na wewe kama Mshauri wa karibu wa Rais na kama Waziri Mkuu ambaye ndiyo msimamizi wa Mikoa na Wilaya hadi tunapozungumza kuna baadhi ya mikoa ambayo kwa zaidi ya miezi 10 imekuwa haina Wakuu walioteuliwa na Rais ila wamekasimiwa kwa mikoa mingine kuitunza. Waziri Mkuu una kauli gani ya kuzungumza kuhusu jambo hili pamoja na kwamba ni jambo la Rais.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe swali la nyongeza linakuwa kwenye swali lile la msingi. Hili lingine kabisa. Naomba sana kwa heshima zote tusiendelee na hilo. Kwa sababu nilifikiri unauliza swali la nyongeza yale yale uliyouliza mwanzo la Mahakama na kesi. Sasa wale wengine wanaosikiliza wanafikiri hapa ni kumwonea Mheshimiwa Mbowe. Yeye mwenyewe kabisa ni swali jipya. Tunaendelea Mheshimiwa Rosweeter Kasikila. *(Makofi)*

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika kwa nafasi hii ili na mimi niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali moja. Mheshimiwa Waziri Mkuu kama unakumbuka miaka ya nyuma miaka ya 1970 na 1980 wahitimu wa vyuo mbalimbali walikuwa wakikaribia kumaliza mafunzo yao tulikuwa tunajaza mikataba kwamba mimi nitaitumikia Tanzania *at least* kwa miaka mitano kabla sija-*opt* vinginevyo na kwamba mkoa wowote au sehemu yoyote ile nitakayopangiwa kazi mimi nitakwenda kufanya na ndivyo ilivyokuwa Wizara ilikuwa ikimpangia mtu anakwenda mkoa ule aliyopangiwa akifika mkoa ule anapangiwa wilaya habishi anakwenda huko, pengine hata kwenye Kata na Kijiji. Lakini hii imekuwa ni tofauti na siku za hivi karibuni. Watu wanachagua sehemu za kwenda kufanya kazi na hii imesababisha mlundikano wa watumishi kwenye baadhi ya mikoa. *(Makofi)*

Lakini mikoa ya pembezoni kama vile Kigoma, Rukwa, Lindi, Mtwara, Ruvuma kule hakuna watumishi kabisa wa Serikali

**SPIKA:** Swali usituhutubie swali, swali.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali ina tamko gani kuhusu suala hili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika analolisema Mheshimiwa Rosweeter ni kweli kwamba tumekuwa na hilo tatizo tena kwa muda mrefu kidogo na tumekuwa tukitumia njia mbalimbali za kujaribu kudhibiti jambo hili ikiwa ni pamoja na kuona kwamba wale ambao wanakataa kwenda kwenye maeneo hayo hawapangiwi maeneo ya kazi sehemu nyingine.

Lakini uzoefu umeonyesha kwamba si rahisi muda wote kiasi hicho. Upande mmoja hii linatokana tu na ukweli kwamba mikoa au baadhi ya mikoa mazingira yake bado si mazuri sana.

Kwa hiyo tukaona kwamba pengine njia rahisi ni kutafuta namna ya kuwavutia hawa watumishi ili waweze kwenda huko pamoja na matatizo ambayo wanayapata wakiwa huko, usafiri wa kwenda huko na mambo mengine. Kwa hiyo tumeamua sisi, ndiyo maana tumeamua kuja na hiyo sera ya kujaribu kutoa upendeleo kwa wote watakaokubali kwenda kufanya kazi katika maeneo yenye mazingira magumu.

Nafikiri tutaianza mwaka huu na tumetumia uzoefu vile vile wa mkoa wa Rukwa ambapo tuliamua kutumia *incentive packages* kwa ajili ya walimu na ikaonekana imefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, tumeona pengine hiyo ni namna chanya badala pengine hiyo njia nyingine watu tumewasomesha kwa fedha zetu lakini kutokana na mazingira fulani fulani wakati mwingine inakuwa si rahisi sana.

**SPIKA:** Swali la nyongeza na kama hakuna swali la nyongeza siyo lazima umwulize.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na mikakati mizuri hiyo muliyoiweka. Je, hamwoni kwamba watu wakirudishiwa taratibu za kusaini mikataba na hiyo itasaidia sana? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Ni jambo jema. Mimi sidhani kama lina tatizo. Lakini ni lazima mkubali mazingira yamebadilika vile vile. Kwa hiyo ni lazima twende na yote mawili, mkataba sawa, tutaendelea kuwabana wale wengine ambao wanaonekana jeuri hawataki kukidhi mahitaji yetu. Lakini vile vile *incentive package* tumeona tuingize pale kwa makusudi kabisa. *(Makofi)*

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi na mimi nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu. Leo ni wiki mbili zimepita tangu Mheshimiwa Waziri Mkuu ulipotangaza kuunda Tume ya kufuatilia bei ya pamba, ambayo iliporomoka ghafla. Wakulima wamekuwa wakisubiri kwa hamu kusikia tamko la Serikali na ikizingatiwa kwamba mwaka huu ni mwaka wa njaa katika Ukanda wa Ziwa labda na maeneo mengi ya Tanzania. Lakini mbaya zaidi sasa kuna wanunuzi wanawakopa pamba wananchi. Serikali au Waziri Mkuu unatoa tamko gani sasa kuhusiana na kadhia hiyo? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba nilieleza kwamba tutaunda timu na tumeshaiunda ile timu na ni mchanganyiko wa wataalam mbalimbali baadaye itakwenda *of course* kwenye l*evel* ya Makatibu Wakuu na hatimaye nitaletewa. Kazi ile kwa taarifa niliyoipata majuzi inakaribia kufikia ukingoni ili tuweze kuona kilichobainishwa ni kitu gani katika mchakato mzima. Kwa hiyo, tutakapokuwa tumemaliza tutaona namna ya kutumia taarifa hiyo kwa ajili ya kuona namna ya kutatua tatizo hili kama ndivyo itakavyokuwa imependekezwa.

Lakini kwa upande mwingine hili la wakulima kukopeshwa lazima nikiri kwamba ni jambo ambalo nilikuwa sijalipata vizuri kwa sababu muda wote kilio kimekuwa ni kwamba pamba haiuzwi kwa sababu bei ni ndogo. Sasa hawa wanaokwenda kule wanainunua kwa misingi gani na kwa nini wafanye hivyo wakati wanajua fedha haipo. Mimi nadhani tutawaagiza tu Wakuu wa Mikoa kama wapo wafanya biashara wa namna wasimamishwe wasifanye hiyo shughuli kwa sababu huwezi ukaendelea kuchukua pamba wakati huna uhakika na fedha zinatoka wapi.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba niulize swali moja dogo. Kwa kuwa kibali cha kununua pamba kimetolewa tu kwa wanunuzi wachache ambao inawapa nafasi ya kufanya *sindicate* ya kupanga bei. Haioni haja sasa Serikali ikaruhusu soko likawa huru ili bei iweze kujipandisha yenyewe. Sasa hivi nasikia bei imeanza kupanda katika soko la dunia?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza hapa kati kati nilipata taarifa kwamba bei ya pamba ambayo sasa inatumika kununua pamba ni karibu kati ya shilingi 900 na 1,000 ambayo ilinitia farasa kubwa sana. Mimi nakubaliana na Mheshimiwa Kamani kwamba katika mazingira tuliyonayo ambayo soko lake pamba ni hili ambalo ni tete. Njia rahisi kabisa ilikuwa ni kuruhusu wanunuzi wajiingize huko kwa nguvu zao zote ili mradi waweze kununua kwa bei ambayo inamridhisha mkulima kule Mwanza.

Sasa labda nitumie nafasi hii ambayo nimepata leo kutamka kwamba hawa wafanya biashara kama wapo waende wakanunue ile pamba kwa bei ambayo wananchi wataridhika. Tusikae tunasubiri mchakato ambao tunajua kabisa mwisho wa safari haimnufaishi sana mkulima. Kwa hiyo mimi nadhani watakuwa wamenielewa na kama wapo mimi nafikiri tuendelee kama tulivyokuwa tumefikiria tangu mwanzo.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika kunipa nafasi ya kumwuliza MheshimiwaWaziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Tanzania ni nchi iliyotokana na Muungano wa nchi mbili yaani Tanganyika na Zanzibar. Baada ya Muungano ikaonekana kwamba bendera ipeperushwe ya Jamhuri ya Muungano peke yake. Baadaye ikaja kukubalika Zanzibar ipeperushe bendera nyingine ya kwake.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni sababu zipi za msingi ambazo zimepelekea bendera ya Tanganyika isipeperushwe lakini Zanzibar ipeperushe bendera ya Zanzibar na bendera ya Jamhuri ya Muungano?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika jibu ni rahisi tu kwa sababu pande zote hizi mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndivyo zilivyokubaliana. *(Makofi)*

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu Muungano ni kitu kikubwa sana ambacho tumeachiwa na Baba wa Taifa ambacho naamini kabisa tunatakiwa kukilinda kwa nguvu zetu zote.

Lakini kwa kuwa kuna malalamiko na mimi nikiwa mmojawapo kama Mtanzania ambaye ni Mtanganyika, sioni fahari ya kwamba nchi iliyoungana, wenzetu wengine kupeperusha bendera na upande wa pili tusipeperushe bendera yetu ya Tanganyika, huoni kama hatukutendewa haki upande wa Tanganyika?

Mheshimiwa Spika, Swali la pili ...........

**SPIKA:** Hakuna swali la pili. Hilo ni swali la nyongeza. Huwezi kuwa na maswali mawili tena. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naona Mama Abwao amenogewa na maswali haya. Magumu lakini. Nirudie kusema, inawezekana wewe ndivyo unavyopenda hivyo. Lakini sivyo mfumo ulivyo sasa. Mfumo ulivyo sasa ni huo ambao tunautumia, tunapepea bendera ambayo ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa makubaliano tukakubali Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wapepee bendera upande wa Zanzibar. Sasa matakwa yako hayawezi kuwa ndiyo matakwa ya kikatiba hata siku moja. *(Makofi)*

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kunipatia nafasi niulize swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu nilikuwa napenda kujua kwamba Serikali imeamua kwamba nchi nzima ipatiwe pembejeo kwa ajili ya kilimo ili tuweze kupata mazao bora. Ningependa kujua hili jambo limeshaanza kutekelezwa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba dhamira ya Serikali ni kuona kwamba tunaweza tukafikisha ruzuku ambayo ni kwa ajili ya pembejeo katika nchi nzima kwa wakulima wele ambao ndiyo walengwa ambao hawana uwezo wa moja kwa moja kuweza kujisaidia wenyewe.

Lakini programu hii inakwenda hatua kwa hatua. Kama mtakumbuka tulianza na mikoa ya Nyanda za Juu Kusini baadaye tupanuka kidogo tukaongeza mikoa mingine. Tunakwenda tunaongeza kidogo kidogo kulingana na uwezo wa bajeti ya Serikali kwa hiyo inshallah iko siku ambayo tutafika maeneo yote kama tunavyodhamiria.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi hii ili niulize swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri Mkuu utakumbuka ulipotembelea katika Jimbo letu la Nkenge, ulituahidi kwamba na sisi sasa angalau mwaka huu tutaingia katika programu ya kupata vocha. Sijui jambo hilo litatekelezwa katika msimu wa kilimo cha mwaka huu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba nilipofanya ziara Mkoa wa Kagera, nilivutiwa sana na hali ya hewa iliyoko kule Misenyi na hasa nilipotembelea shamba moja la uzalishaji wa zao la mahindi ambalo ni kwa ajili ya mbegu na nikasema nikirudi nitajitahidi kuzungumza na wenzangu wa Kilimo tuone kama Wilaya hii inaweza ikaingizwa katika mpango huo.

Kwa hiyo ni kweli nimejaribu kuwasilisha jambo hili kwao. Ingawa najua wakati ule nimerudi *of course Budget process* ilishaanza tayari. Lakini tutajitahidi tu, tukishindwa tutawaingiza katika mwaka wa fedha unaokuja.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Bunge la Jamhuri ya Muungano huwa linapitisha Bajeti ya matumizi na ya maendeleo. Miongoni mwa Bajeti inayopitishwa ni pamoja na bajeti ya *CDCF.*

Kuna tetesi kwamba huko Zanzibar inaonekana kumetoka kama barua rasmi au kama haijatoka barua lakini kuna tetesi kwamba pesa hizo zitumike kwa namna ambapo hata Wabunge hawajaidhinisha wa upande huu.

Je, unasemaje kuhusu pesa hizi za *CDCF* na wajibu wa Wabunge kuhusu pesa hizi? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri jana nilipata nafasi tu ya kuzungumza na Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais, tulizungumzia mambo mengine baadaye ndiyo akanidokeza kwamba anazo fununu kwamba jambo hili linaleta kidogo hali ya kutokueleweka kwa upande wa Bunge wanaotoka Zanzibar. Akaniambia kwamba halina tatizo jambo hili hata kidogo, wanatambua uwepo wa Sheria hiyo na taratibu zilizomo katika hiyo Sheria. *(Makofi)*

Akaniambia vilevile kwamba, siku za nyuma aliwahi kukutana na Wabunge wote kutoka Chama cha Mapinduzi na vilevile upande wa Vyama vingine vya Upinzani, *particularly CUF,* mkalizungumza jambo hili na yeye akatoa kama ombi kwenu kwamba, muangalie uwezekano wa kusaidia kutatua tatizo la lile. Sasa sijui kama ndio Kiswahili chake, kinachoitwa upungufu wa vikalio katika shule upande wa Visiwani; nadhani kwetu tunaita madawati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, akasema aliwaomba hilo na bahati nzuri alikuwa amezungumza na Mheshimiwa Rais, wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, juu ya jambo hili. Yeye wakati linajadiliwa hakuwemo kwenye kikao, anasema Rais amenihakikishia, la hasha, halikutoka kama agizo isipokuwa tumelitoa lile kama ombi kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa vyama vilivyomo humu Bungeni, kuona uwezekano wa namna ya kutatua hili tatizo hata kama ni hatua kwa hatua au kwa mchango mdogomdogo katika maeneo yenu.

Kwa hiyo, akasema Rais, amemhakikishia kwamba, si agizo kama ambavyo pengine limeonekana. Lakini wamelitoa kama rai ni juu ya Mbunge kuamua, na akaniambia atakayesema hapana, sawa! Atakayesema ndio, vema! Atakayesema nitatoa madawati kiasi fulani! Kwa hiyo, kwa kweli halikutoka kama agizo anasema ni bahati mbaya, pengine kama kuna kitu kimeletwa kitakuwa kimeletwa lakini hakikushika haswa maudhui ya mjadala ulivyokuwa.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa jibu zuri la Mheshimiwa Waziri Mkuu. Swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu katika *briefing* moja hapa Dodoma, uliwahi kueleza namna gani Ofisi Ndogo ya Bunge ya Zanzibar itatumika ipasavyo.

Je, huoni sasa kwa kuwa ile Sheria ya *CDCF* kwa upande wa Zanzibar, inaleta mkanganyiko kiasi kwamba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hana mamlaka ya kukagua kule. Huoni sasa wakati umefika wa Sheria hii kubadilishwa ili iweze kufanya kazi vizuri Zanzibar? Unasemaje kuhusu hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyaa, alitakiwa aniambie vilevile kwamba, sisi ndio tulisema tuone namna ya kubadilisha hiyo Sheria. *Anyway, in short* tunasema tu kwamba, tumelitazama hili jambo na ninafikiri Mwansheria Mkuu wa Serikali yuko hapa ananisikiliza; na tunadhani rai mliyoitoa kwenye Kikao ni ya msingi. Kwa maana ya kurahisisha kazi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, inapokuwa ni mkondo uleule, badala ya kwenda kuingia tena katika mfumo mwingine kule ambao kidogo unaweza ukampa tabu namna ya kulisimamia.

Kwa hiyo, tunalifanyia kazi na kwa ushauri wa *AG,* nafikiri tutafika mahali tunaweza tukaona turekebishe namna gani ile Sheria, ili pengine kama unavyopendekeza kama itaonekana inafaa basi Ofisi Ndogo ya Bunge pale Zanzibar, kwa sababu ni chombo cha moja kwa moja kinachotokana na Bunge hili, ingeweza ikawa pengine nyepesi na rahisi zaidi kuweza kulisimamia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunalifanyia kazi na ninafikiri tutafikia pazuri tu. *(Makofi)*

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kumwuliza swali Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, inafahamika kwamba, mapema mwaka

huu katika Jimbo la Ukonga, wananchi wa Gongo la mboto, walipata ajali ya kulipukiwa na mabomu. Lakini watu wengi wengine walipoteza maisha na wengine walipoteza mali zao. Serikali ilishughulikia vizuri sana wale watu ambao walipoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia watu ambao wamepoteza viungo vyao? Wengine walipoteza mali zao, ziliungulia ndani na hata wale wengine ambao hawakuweza kupata fidia wakati husika?

Mheshimiwa Spika, lakini (b)…

**SPIKA:** Aah, (b) hakuna! (b) hamna.

Tunaendelea, haya. Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, mwezi wa pili tulipata janga hilo la mlipuko wa mabomu kule Gongo la Mboto. Kama anavyosema Mheshimiwa Maiposa, ni kweli kuna baadhi ya maisha ya binadamu yalipotea, wako waliojeruhiwa, kuna nyumba ambazo ziliharibika kabisa, ziko ambazo zimepata uharibifu lakini si kwa asilimia zote, lakini mali vilevile vyombo mbalimbali vimepotea.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, zoezi zima Serikali inalifahamu sana na tumeshalifanyia kazi karibu lote. Sasa hivi tumejipanga tu kwamba, zile nyumba 71 ambazo ziliharibika kabisa, zile tumeamua kwamba, *SUMA JKT* au *JKT* wasimamie ujenzi wa nyumba zile moja kwa moja. Na kama utakavyokumbuka Mheshimiwa Mwaiposa, tulikuwa tumepata hata eneo kule, nafikiri Kinyerezi, kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizo, ukiondoa mtu mmoja aliyeamua yeye kujengewa sehemu nyingine.

Lakini bahati mbaya, tumepata kikwazo kidogo pale kwa sababu, wananchi wengine wamesema eneo hili ni lao kwa hiyo, haiwezekani. Tuko Mahakamani, lakini nadhani tutalimaliza na zoezi hilo litaendelea. Tayari tumeshapiga matofali karibu 25,000 kwa ajili ya nyumba zile na zoezi hilo linaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa maeneo mengine yaliyobaki kwa maana ya wale ambao waliharibiwa kiasi, tumeshakubaliana na lenyewe halina tatizo. Fedha zimetengwa kwa ajili ya kuwapa wale wote ili wao wenyewe waweze kufanya yale marekebisho kwa sababu hayakuwa makubwa sana. kwa hiyo, nalo hilo tutajitahidi kulifanya nadhani muda si mrefu.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa maeeneo mengine yote yaliyobaki, tumefanya tathmini ya mali zilizoharibiwa na fedha zake tumeshajua ni kiasi gani. lakini vilevile tunakubali kwamba, hata wale ambao waliumia wakati ule na wenyewe tutawafidia kulingana na viwango ambavyo tumeshavipanga tayari. Kwa hiyo, kwa ujumla suala la maafa na yale yaliyojitokeza kule Gongo la Mboto, yote tumeshayazingatia na ninafikiri baada ya muda sio mrefu sana, utaona utekelezaji wake utaanza. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wabunge wengi hawana Ofisi. Na wale wachache waliojengewa, fedha zilizotolewa ni milioni 40, zinajenga Ofisi ndogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hamwoni kwamba inafaa kukaa tena na kupanga fedha za Ofisi za Wabunge, ili zijenge Ofisi zenye hadhi? Tofauti na ilivyo sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, toka tunaanza Bunge hili la 10, Serikali kwa maana ya Serikali Kuu, imetoa jukumu la kujenga Ofisi za Wabunge kwa Ofisi ya Bunge. Hivi tunachokifanya sasa ni kuangalia ile ramani upya, ile ramani ya zamani, na pia kwenda kwenye Ofisi ambazo tayari zilikuwa zimejengwa ziko katika hali gani, zina kitu gani, kwa sababu ni lazima tuwe na *standard furniture,* lazima tuwe na ramani inayokubalika, lazima tuwe na mahali ambapo inaamuliwa hapa itakuwa Ofisi ya Mbunge leo na kesho na keshokutwa. Maana zilivyojengwa sasa hivi, wengine

walijenga nyumbani kwao, Ubunge hawakurudi, sasa Ofisi iko huko, hakuna mtu anayekwenda! Kuna haya yote tunayaangalia, kwa hiyo, hili suala liko katika Ofisi yangu siyo Ofisi ya Waziri Mkuu.

Tunaendelea. Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata nafasi hii adimu. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imeshajitokeza kwamba, katika nchi yetu biashara ya kuuza wanyama nje ya nchi ni ya kisheria; lakini biashara hii inaonekana kwamba, haina tija na hivyo kuwafanya baadhi ya watu kuendelea kuiba na kupora wanyama wetu kupeleka nje, ambapo watu hawa tunaweza kuwaita wahujumu uchumi.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inatamka nini kuhusiana na hilo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ingelipendeza kama Waziri Mwenyewe wa Maliasili na Utalii angelisema hili, lakini kwa sababu nimeulizwa kwenye kipindi, labda niseme tu tulichoamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza tunataka tukubaliane na mawazo ya Wabunge kwa ujumla kwamba, inaonekana eneo hili bado utaratibu wake wa usimamizi na hata namna biashara yenyewe inavyofanyika, ni eneo ambalo kwa kweli linahitaji kutazamwa upya. Kwa hiyo kama Serikali tumeamua kwamba, tutasimamisha usafirishaji au biashara za wanyama zote na tuangalie tena upya jambo hili, ili kama itatokea kwamba tunakubaliana kwamba, tuendelee nalo ni dhahiri lazima masharti yabadilike kwa sababu hayawezi kuwa haya tena. Lakini vilevile ni lazima tuhakikishe kwamba, sasa ni wanyama wa aina gani hasa tunaotaka wasafirishwe kwenda nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tatu hata hiyo tozo au ada inayotozwa, hivi mnataka tuendelee na hii ambayo hatuoni kwamba inatusaidia kitu chochote, wakati wao wanafaidi mara mbili?

Kwa hiyo, tumeona hili pengine ndio namna bora ya kujaribu kulizingatia ili na Wizara yenyewe ijipange vizuri kuweza kusimamia eneo hili kikamilifu kabisa. Nadhani, tukisimama kwa muda wa mwaka mzima mmoja hivi au na zaidi kidogo, itakuwa ni muda tosha wa kutuwezesha kwa pamoja tukishirikiana na Bunge, tuone haja au kutokuwepo kwa haja hiyo na baadaye tuweze kufanya uamuzi wa moja kwa moja.

**MHE. ALLY K. MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika ziara yako ya tarehe 2 Mei, 2010 katika Kata ya Mkwamba, uliwahidi utawasaidia barabara kati ya Itindi – Kibaoni, kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi haina uwezo na hiyo barabara na wewe uliwaahidi utawasaidia. Lakini mpaka leo Mheshimiwa Waziri Mkuu, wananchi wa Mkwamba wanaulizia kuhusu hiyo barabara, mpaka leo hamna lolote linalofanyika na wewe ulitoa ahadi katika vijiji vya Lyelye, Itindi, Tambaruka na Swaila. Unasemaje kuhusu hilo Waziri Mkuu?

**SPIKA:** Angekuwa Waziri Mkuu, hakuahidi lingekuwa sio swali. Lakini kwa sababu, aliahidi mwenyewe, basi jibu hilo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, hata hivyo kanionea tu! Tunatoka pamoja, angekuja tukanong'ona tu yakaisha, lakini nadhani anataka wapiga kura wasikie kule kwamba, anafuatilia jambo hili kwa karibu sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nataka tu nimhakikishie kwamba, ahadi hiyo haijafutwa bado tunayo na hiyo kazi tutaifanya kupitia kwa upande fulani, upande wa Halmashauri yetu lakini vilevile tumekubaliana kwamba, tutaomba na watu wa *TANROADS* kama kuna uwezekano na wenyewe wakachangia kidogo. Kwa sababu, eneo lile inabidi tupande mlima ambao si rahisi sana kwa fedha ndogo ya Halmashauri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kessy, waambie wapiga kura, tuko imara kabisa na ahadi yetu na tutaitimiza bila wasiwasi wowote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimejitahidi sana kuchanganya hapa leo, karibu wote waliokuwa wameuliza siku za nyuma sikuwapa nafasi. Nimewapa tu *CUF* kwa sababu, wote wawili walikuwa wamechangia, ingekuwa sio vizuri kama *CUF* wasingeingia humu ndani, lakini wote pia walishachangia. Kwa hiyo, nimemaliza maeneo hayo yote na tunakushukuru sana kwa majibu na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge pia kwa maswali yenu ya msingi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu.

## MASWALI YA KAWAIDA

**SPIKA:** Wakati wa Maswali hatufanyi Muongozo, kwa sababu muda hautoshi. Maswali ya kawaida, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Kapteni John Chiligati.

Na. 445

### Tatizo la Maji – Vijiji vya Jimbo la Manyoni

**MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI** aliuliza:-

Katika kutekeleza Mradi wa Maji wa Bonde la Ufa miaka ya 1970, Kata ya Sasajila na Majiri ilijengwa miundombinu kadhaa kama vile visima vinne vilichimbwa, matanki ya kuhifadhia maji yalijengwa kwenye Vijiji vinne na mtandao wa mabomba lakini baadaye mradi huo ulikufa kutokana na kung'olewa kwa mabomba:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuufufua mradi huo ili kuondoa tatizo kubwa la maji linalowakabili wananchi wa vijiji vilivyo jirani na mradi huo vya Mpandagani, Chinangali, Chibumagwa na Chinyika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kapteni John Zephania Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa mradi huu uliojengwa miaka 1970 uliwekewa miundombinu yote lakini baadaye ulihujumiwa na wananchi kwa kung'oa mabomba, mashine na vipuri vilivyokuwa vimewekwa; kwa sasa, mradi huo unahudumia Kijiji cha Chibumagwa peke yake.

Aidha, katika kipindi hicho Kijiji cha Sasajila kilijengewa mradi wa maji ambao nao kwa sasa haufanyi kazi; miradi hii miwili, kimsingi imeshindwa kukidhi matarajio ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini *(RWSSP)* katika Vijiji 10 ambapo wananchi wanahamasishwa na kushirikishwa kikamilifu si tu kuchagua teknolojia inayofaa ambayo inatoa unafuu wa uendeshaji wa miradi hiyo, lakini pia gharama za uchangiaji kwa maana ya ankara za maji kwa wakati wote. Katika mwaka 2011/2012, Halmashauri imepanga kutumia shilingi bilioni 1.0 kwa ajili ya miradi ya maji. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 630 ni fedha zilizotengwa mwaka 2010/2011 na shilingi milioni 370 zimeidhinishwa mwaka 2011/2012 kwa ajili, ya kutekeleza miradi ya maji katika Vijiji 10 vilivyopo katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa program. Vijiji hivyo ni Majiri, Kintinku/Lusisile, London, Mpapa, Solya/Kilimatinde, Makanda, Lungwa, Kayui, Makala na Mitundu.

Vijiji vya Mpandagani, Chinangali, Chibumagwa na Chinyika, vitaingizwa katika awamu ya pili ya utekelezaji wa program hii. *(Makofi)*

**MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa jibu zuri kwamba, vijiji vya Mpandagani na Chinangali, vitaingizwa katika awamu ya pili, inatia matumaini. Hata hivyo, nina swali moja tu dogo la nyongeza. Kwamba, katika Kijiji cha Kintinku ambacho kiko katika awamu ya kwanza ya mradi huu, kisima kimechimbwa, maji hayakupatikana! Lakini katika mwinuko huo huo kuna visima ambavyo vimechimbwa vimefunikwa, pale Mbwasa.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ipo tayari kuwaambia, kupitia mradi wa *World Bank,* sasa maji kutoka Mbwasa Mlimani, yafanyiwe mradi yateremke mpaka Kintinku na Lusulile?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kapteni Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninaelewa anachozungumza. Leo nilikuwa nazungumza na Injinia wa Maji, Magoma, kumwuliza kuhusu jambo hili analilozungumza hapa. Kijiji hiki anachozungumza Mheshimiwa Chiligati, kilikuwa katika Kikundi ambacho kinaitwa ni *Group Scheme,* tukataka wafanye wote kwa pamoja kwa sababu tulitaka wanufaike na mradi huu wote kwa pamoja.

Lakini wale wa eneo la Majiri, wakaona kwamba hawanufaiki na mradi huu kwa sababu maji yanakuwa yanakatika yakiwa upande wa juu.

Mheshimiwa Spika, sasa kinachosemwa hapa ni kwamba, sasa hivi tunapozungumza hapa, kijiji hiki anachosema Mheshimiwa Chiligati, hakina maji ndicho tunachozungumza hapa.

Kwa hiyo, kwa njia yoyote anayotaka kupendekeza hapa, sisi tunachosema hapa, *already* tunasema hapa mbele ya nyumba hii kwamba, tunazo bilioni 1 katika Wilaya ya Manyoni. Kwa shilingi bilioni moja, 630 zimetoka mwaka jana kwa Mwaka wa Fedha uliopita na milioni 370 zinatoka mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kiyo mimi ninachoweza kusema hapa, tunapokea rai ya Mheshimiwa Mbunge, kwanza amekuwa anafuatilia kwa karibu sana, napenda nimpongeze.

Mimi nitazungumza na watu walioko Manyoni pale, tusaidiane. Hela tulizopeleka sasa hivi ni milioni 100, tumepeleka kwa ajili ya Mji wa Manyoni na milioni 90 zimewekwa kwa ajili ya Manyoni na milioni 10 zimewekwa kwa ajili ya Mji wa Itigi, ndizo tulizotenga katika *Local Government Capital Development Grant.*

Kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba, sisi tuko tayari lakini itabidi waka-*rearange priorities* zao. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa, vijiji vilivyoko katika Kata za Kikio na Misughaa, zilizoko katika Ukanda huo wa Bonde la Ufa katika Jimbo la Singida Mashariki, wana uhaba mkubwa sana wa maji safi na salama.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaondolea wananchi wa Kikio na Misughaa, tatizo kubwa la maji lililowakabili kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Haya, hilo swali jipya, unataka kujibu tu. Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu sasa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lisu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, labda nikiri hapa kwamba, hivyo vijiji anavyovitaja hapa sijaweza kuvielewa vizuri ni vijiji gani. Lakini mimi sina tatizo na hili, kwa sababu Waziri wa Maji pia atakuja hapa ataeleza kwamba, wamepanga kufanya nini.

Mheshimiwa Spika, ninachojua ni kwamba, programu zetu zinaonesha kwamba, kila Wilaya imetenga vijiji 10 ambavyo ndivyo hivyo vinavyosaidiwa na *World Bank,* wansema wanafadhiliwa, wanahisaniwa! Maana Mfadhili ni Mungu tu. *(Makofi)*

Ninachoweza kusema hapa, mimi nitakwenda kuangalia kama hivi anavyovisema viko ndani yake kama haviko ndani yake tuje tukae mimi na yeye tuzungumze Bajeti imeshaipita inakuja Bajeti ya maji, Mheshimiwa Waziri wa Maji atatuambia kwamba itakuwa ni kiasi lakini sisi tuko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Lissu ili wananchi hawa waweze kupata haya maji. *(Makofi)*

Na. 446

**Madai ya Askari Waliopigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Askari waliopigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia waliokwisha staafu muda mrefu wamekuwa wakifanyiwa uhakiki mara kwa mara na Ofisi za Wakuu wa Wilaya kwa ahadi ya Serikali ya Uingereza kupitia Chama cha Askari wao wa zamani, ambacho kilikuwa tayari kuwalipa kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Je, ni lini Askari hao watalipwa madai yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na JKT napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge na Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chama cha Askari wa Uingereza waliopigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia kinachojulikana kwa jina la *Royal Commonwealth Ex-Service Leave (RCEL)* huwa kinafanya michango ya hiari kwa madhumuni muhimu ya kuwapa msaada Askari waliopo nchi mbalimbali waliosaidia nchi ya Uingereza katika Vita Kuu ya Pili ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi ni za msaada na si fedha za Serikali ya Uingereza. Fedha hizo sio malipo ya mafao au posho na wala hazilipwi kila wakati bali hulipwa pindi zinapopatikana. Kwa utaratibu uliokuwepo, fedha hizo hupitia ubalozi wa Uingereza na kulipwa walengwa kupitia Chama chao cha *Tanzania Legion*. *(Makofi)*

Kutokana na mgogoro wa uongozi ndani ya *Tanzania Legion*, watoaji wamesitisha kutoa fedha hizo mpaka mgogorohuo uishe. Hivi sasa Wizara yangu inakamilisha kazi ya uhakiki wapiganaji waliopo nchi nzima ili kupata takwimu sahihi ya wapiganaji hao wa vita kuu ya pili ya dunia.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na JKT itakuwa tayari kuwalip wahusika kupitia kwa wakuu wa wilaya, fedha hizo zitakapoanza kutolewa tena na *Royal Commonwealth Ex-Service League.*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekuwa inafanya zoezi hili la kuhakiki wazee hawa wilayani.

Lakini pia kumekuwa na baadhi ya maeneo hasa wilayani Namtumbo kuna watu wanaowaambia wazee askari hao au familia za marehemu askari hao kuwa wanawaandikisha

kwa kuwatoza fedha ili wapate vitambulisho na kuwaambia kwamba fedha zitakapokuja walioandikishwa na waliotoa fedha ndiyo watalipwa fedha hizo.

Je, Serikali inaeleza nini kuhusiana na utapeli huu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Zoezi la kuhakiki ni zoezi la lazima kwa sababu hawa ni wapiganaji ambao walipigana vita kuu ya dunia ambayo ilikwisha mwaka 1945. Kwa hiyo, unaona kwamba ni kipindi kirefu kwa hiyo ipo haja ya kuhakiki kuona ni wangapi ambao bado watakuwa wako hai.

Lakini kuhusu hao wanaokwenda katika utaratibu wa kuwaona wengine. Kwa mfano katika eneo lako ulilolisema Mheshimiwa Mbunge hicho ni kinyume na utaratibu lakini hii inatokana na hali ambayo si nzuri katika *Tanzania Legion* Chama chao ambacho nimeizungumza hapa wana matatizo ya uongozi na wana matatizo mengine ya utendaji kazi.

Lakini upande wa Serikali nikasema kwamba utaratibu ambao tunautumia ni kuhakiki na kuweza kupata idadi ambao bado wako hai. Lakini haya masuala mengine bado ni matatizo ya uongozi ndani ya chama chenyewe ambacho ningesema kwamba uongozi uweze kuchukua mamlaka ya kuhakikisha utapeli wa namna hii haufai ndani ya chama chake.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona na kunipa fursa hii, ningependa kujua wananchi wa Kilwa, Songea, Liwale na mikoa yote ya Kusini tulipigana vita vya Majimaji. Ni lini Serikali itadai fidia kwa nchi ya Ujerumani ambayo ilikuwa imewaonea wananchi hawa katika nchi yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mangungu, swali jipya maandalizi ya watu huwa hayawi kama maswali yamekuwa mapya, Swali la maji maji tena. Tunaendelea na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Vicent Josephat Nyerere atauliza swali hilo. *(Makofi)*

Na. 447

**Kuboresha Hali ya Walimu Nchini**

**MHE. VICENT J. NYERERE** aliuliza:-

Elimu bora nchini inategemea sana walimu bora na kuwa na matokeo mabaya ya mitihani ni ishara ya kuwa na walimu ambao maisha yao ni duni na hawana moyo wa kufundisha.

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kuboresha hali ya walimu kote nchini ili tuwe na walimu bora watakaoweza kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa na kuwa na matokeo mazuri kwa wanafunzi wanaowafundisha?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vicent Josephat Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuinua taaluma, mazingira ya kazi ya Ualimu na maslahi yao. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha miundombinu ya shule kwa kukamilisha majengo ambayo hayakukamilika wakati wa utekelezaji wa MMES I ikiwemo ujenzi wa nyumba za walimu, madarasa, maabara na vyoo vya shule. Hata hivyo, shule 1,200 zinatarajiwa kukamilishwa kabla ya mwaka 2015.

(ii) Kuwajengea walimu uwezo wa kufanya kazi kwa kuwapatia mafunzo kazini ili waweze kumudu kazi zao vizuri zaidi. Walimu zaidi ya 2000 wa masomo ya Fizikia, Kemia, Biolojia na Hisabati tayari wamepata mafunzo hayo kati ya Julai, 2010 na Julai, 2011. Vilevile Serikali inatoa asilimia 100 ya mkopo kwa walimu wanaosomea masomo ya Sayansi katika Taasisi za Elimu yaani Vyuo Vikuu.

(iii) Kuimarisha ufundishaji wa ujifunzaji kwa kutoa ruzuku ya kununuliwa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Ruzuku hii inapaswa kumpa mwalimu nyenzo muhimu za kufanyia kazi ili kurahisisha kazi yake.

(iv) Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali imejipanga kuwapa motisha ya shilingi 500,000 walimu wanaopangiwa kaufanya kazi katika maeneo yenye mazingira magumu kwa mara ya kwanza kama mlivyoona kwenye hotuba yetu.

Mheshimiwa Spika, kupitia mpango wa maendeleo wa elimu ya msingi MMEM II mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari (MMES II) na juhudi za wananchi, wahisani na wadau mbalimbali wa elimu, ni matarajio ya Serikali kwa mazingira ya kazi na maisha ya mwalimu yataboreshwa.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwa kuwa walimu wengi wameingia katika wakopeshaji wenye riba kubwa, Serikali inaona ugumu gani kuwadhamini walimu hao ili wakope benki kwa riba nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Vicent Joseph Nyerere, Musoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wote tutakumbuka kwamba mwaka 2008, Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria ya mikopo ya nyumba, kwa wananchi wakiwemo na walimu. Iliyopelekea sasa kuanzisha kampuni iitwayo *TMRC,* yaani *Tanzania Mortgage Refinancing Company,* ambayo itakuwa sasa inatoa mikopo yenye riba nafuu kwa mabenki.

Mabenki kumi sasa yameungana pamoja na hazina kwa kufanya biashara hiyo kwa riba nafuu itawakopesha walimu pamoja na wakulima wa kawaida, tofauti sasa ilivyo katika riba hizi kubwa kwa mabenki haya ya sasa hivi.

Lakini ukifungua ukurasa wa 32, Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi utakuta maelezo mazuri yapo pale, kwa mwaka huu wa fedha Serikali imejipanga kuwasaidia wananchi kwa mikopo ya nyumba ikiwemo pamoja na walimu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona, katika swali la msingi liliulizwa swali kuhusiana na kuboresha hali ya walimu nchini kote, sasa nafahamu kwamba kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu ya madeni ya walimu. Ambayo kwa mujibu wa Chama cha Walimu, yanafikia shilingi bilioni 29.

Tarehe 1 Agosti, 2011 Serikali ilikaa pamoja na walimu baada ya walimu kutangaza mgogoro wakakakubaliana kwamba ndani ya wiki mbili, walimu watakuwa wamewasilisha jina la Mwalimu kiasi anachodai kama ni cha mishahara na posho na kadhalika na Serikali ikawa tayari kwamba kuyahakiki na kuyalipa madeni husika.

Ningeomba kauli ya Serikali ni lini madeni hayo ya takriban bilioni 29 ya mishahara pamoja na marupurupu mbalimbali na posho mbalimbali watalipwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI YA UMMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa John Myika, Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo;

Ni kweli tulikaa na chama cha walimu, na tukakubaliana siku ya tarehe 15 watuletee madai hayo yakionyesha na majina ya walimu. Siku ya tarehe 16 Chama cha Walimu

wamewasilisha madai ambayo makaratasi yaliyowasilishwa ni *pick up* nzima, tunafanyia kazi na tumekubaliana kukutana kabla ya tarehe 30 ili tuone jinsi gani tutaweza kuyamaliza kwa pamoja.

**SPIKA:** Haya hiyo *pick up* nzima kabisa.

Na. 448

**Kuipatia Gari Idara ya Uhamiaji Wilayani Kondoa**

**MHE. JUMA S. NKAMIA** aliuliza:-

Serikali iliahidi kuipatia Idara ya Uhamiaji Wilayani Kondoa gari ili kurahisisha kazi za idara hiyo;

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hiyo?

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nipate kuuliza swali Na. 448, kwa kuwa swali hili lilishapatiwa ufumbuzi wakati wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani, naishukuru Serikali, naomba kuondoa swali langu.

**SPIKA:** Ukiwa unaondoa unasema naomba kuondoa swali, fulani siyo mniandikie vinoti iko kwenye *order paper* kwa hiyo kuna utaratibu huo. Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia.

Na. 449

**Kuweka Minara ya Simu Wilayani Tarime**

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE** aliuliza:-

Wakzi wa Tarime wanaotumia simu za Mikononi wanasumbuliwa na tatizo la uhaba wa mitandao ya kampuni za simu hizo na kulazimika kutumia mitandao ya Safaricom na Airtel ya Kenya ambayo ni gharama sana:-

(a) Je, ni lini Serikali itazihimiza kampuni za simu kuweka minara yao katika vilima vya Tagare, Nyarusuni, Mumwamu, Nyamwaga na hata Gibaso ili kurahisisha mawasiliano kwa wakazi wa Tarime?

(b) Je, mpango huo utaanza na kukamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutambua juhudi mbalimbali za makampuni ya simu nchini katika kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini. Mheshimiwa Spika, maeneo ya Tagare, Nyarusuni, Mumwamu, Nyamwaga na Gibaso yapo katika mpango wa kampuni ya Mawasiliano ya Simu za Mkononi ya Airtel unaoanzia Machi, 2011 hadi Machi 2012 ya kufikishiwa huduma ya mtandao wa mawasiliano kutoka *Airtel,* ili kurahisisha mawasiliano kwa wakazi wa Tarime na pia kuwapunguza adha na gharama za mawasiliano wa maeneo hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, kuna mchakato mkubwa sana unafanyika kuanzia tafiti za kimasoko, kimazingira na kiufundi kabla ya eneo kuwa na vigezo vya kuwekewa mnara wa mawasiliano ya simu. Hivyo muda wa kutekeleza mpango wa kuweka minara ya simu hutegemea

zaidi matokeo ya tafiti hizo. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge, na wakazi wa Tarime wawe na subira wakati mipango inaendelea kufanyiwa kama nilivyoeleza.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza katika swali la msingi amejibu kwamba makampuni yanayofanya utafiti ni mawili ya *Airtel* na *VODACOM.*

Je wale watumiaji wa kampuni ya Tigo, niwaambie nini?

Swali la pili, kupitia kampuni ya *TTCL,* kuna kipindi fulani ilianzisha utumiaji wa simu za mkononi, Waziri anasema nini kuhusiana na mitandao ya *TTCL* kujengwa wilaya Tarime?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge awaeleze wananchi wa Tarime kwamba nimetaja makampuni ya *Airtel* na *VODACOM,* lakini Wizara yangu itawasiliana na Tigo, kuona mipango yao na namna ambavyo wanaweza kufikisha mawasiliano katika jimbo la Tarime.

Kuhusu *TTCL* nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, hivi sasa tumeunda Bodi mpya, ambayo inajipanga kuangalia mpango mkakati wake, na programu yake ya kusambaza simu za mkononi itaendelea kama ambavyo wamejipangia katika mpango kazi wa mwaka 2011 hadi mwaka 2013, yakiwemo hayo maeneo ya Tarime.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, asante kama ilivyo na matatizo katika jimbo la Tarima na ndivyo kwenye kata za wilaya ya Iramba, Ulugu, Mwangeza, Nkungi, Iyambi, na maeneo mengine network ni shida watu wanapanda mpaka kwenye miti kwa ajili ya kupata *network.* Waziri unawaambia nini watu wa maeneo yale, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mlata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo katika wilaya ya Iramba ambayo hayana mtandao, vilevile yako katika mpango wetu ambao siku zote nimekuwa nikiueleza hapa wa *UCAF.*

Mpango wetu wa UCAF unaangalia kwanza mahali ambapo hawana kabisa halafu tunaenda angalau baada ya kuwa tumemaliza ambao hawana kabisa, tutaenda sehemu ambazo angalau wanafikiwa kidogo inapendeza angalau wanapanda kwenye mti wanapata lakini kuna wengine hata wakipanda kwenye mti hawapati kabisa mawasiliano. *(Makofi)*

Lakini katika muda wa miaka miwili hii watu wote tunajipanga kuhakikisha kwamba wanapata mawasiliano hata wakiwa kitandani wako na mawasiliano.

**SPIKA:** Mheshimiwa Capt. Komba, pole na matatizo ya kuunguliwa na nyumba, uliza swali la nyongeza.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru jimbo langu karibu nusu halina mawasiliano ya simu, kata kama ya Ngumbo, Baha, Lihundi, Liparamba na Kyagara hamna kabisa na hata ukipanda kwenye mti au kwenye mlima hakuna mawasiliano. Kuna mpango gani wa kunisaidia kwa vile jimbo hili liko mpakani kati ya Malawi na Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpe pole sana Mheshimiwa Komba, kwa kuunguliwa na nyumba yake. Vilevile kwa niaba ya

Waziri wa Mawasiliana, Sayansi na Teknolojia naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Komba kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema ni kwamba maeneo ambayo hayajafikiwa kabisa ambayo hayana mtandao kabisa tumeshayaainisha na nimhakikishie Mheshimiwa Komba, katika baadhi ya maeneo aliyoyataja yako kwenye awamu ya kwanza ya programu yetu ya UCAF kuhakikisha kwamba yanafikiwa na mawasiliano. Kwa hivyo niombe ushirikiano tu na Waheshimiwa Wabunge wote watu wa mfuko wa UCAF watakapokuwa wanafika kule waweze kutoa ushirikiano na tuweze kuhakikisha kwamba wananchi wanafikiwa na mawasiliano.

**SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge maswali yameisha na muda pia umeisha, kwa hiyo naomba niwatambue wageni. Katika jukwaa la Spika. Tuna wageni wa Mheshimiwa Freeman Mbowe Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, hawa Ndugu Mussa Hamad Yussuf, Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Zanzibar, asante tunakukaribisha sana katika ukumbi huu wa Bunge. *(Makofi)*

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo wapo wanafunzi 12 kutoka Chuo Kikuu cha Sebastian Kolowa, kilichopo Lushoto, Tanga. Wanaweza kusimama walipo, ahsante sana. Tunawatakieni masomo mema.

Nina wanafunzi 41 na Walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari ya Msalato, Dodoma. Naomba wasimame mahali walip. Hii ni shule maarufu sana kwa wasichana naomba msome kwa bidii sana. Karibuni sana na ahsante sana.

Tuna wanafunzi 55 wa Shule ya Msingi Chalula na Mvumi Makulu, Dodoma. Ahsante sana, someni kwa bidii. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 50 kutoka Shule ya Msingi Makole, Dodoma. Karibuni sana ninyi ni wenyeji wetu pamoja na Walimu wenu. Ahsante.

Tuna wageni 15 kutoka Kanisa la Menonite Tanzania Dayosisi ya Kati Dodoma. Tunashukuru kuwaona. Ahsanteni sana na karibuni sana.

Tuna Madiwani wanne na msaidizi wa Mbunge Hilda Ngoye kutoka Wilaya ya Kyela na Rungwe ambao wako hapa Bungeni. Tunawashukuru na kuwatakia kazi njema huko mliko. *(Makofi)*

Kuna wageni kwa *Speaker`s Gallery* wengine siwajui sijaambiwa, lakini nikiambiwa nitawataja baadaye.

Shughuli za kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo watakuwa na kikao saa 7.15 mchana katika ukumbi namba 231.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali Mheshimiwa Zaynab M. Vullu, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.30 watakuwa na kikao chao chumba namba 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Peter J. Serukamba, anaomba niwatangazie Wabunge wa Kamati yake kwamba watakuwa na kikao leo saa 7 katika ukumbi wa Msekwa B.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, anaomba niwatangazie Wabunge wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 watakuwa na kikao katika Ukumbi wa Msekwa C.

Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mwenyekiti wa Tawi la *CPA* hapa Tanzania anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Utendaji wa *CPA* tawi la Tanzania kwamba leo saa 7.15 baada ya kuahirisha kikao hiki watakuwa na kikao muhimu katika ukumbi Namba 133.

Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, Mheshimiwa John J. Mnyika ,anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kwamba leo saa 7.15 kutakuwa na kikao ghorofa ya pili ofisi ya Kiongozi wa Upinzani.

Lakini wakati huohuo leo nina Waheshimiwa Wabunge ambao wana sikukuu yao ya kuzaliwa tena wengi tu, nao ni Mheshimiwa Susan Anseim Jerome Lyimo, Mheshimiwa Benardetha Kasabago Mushashu na Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono. Hao wote wamezaliwa siku kama ya leo. *Happy Birthday to you all!* (Makofi)

Lakini wakati huohuo siku ile kulikuwa na *party* ya Yanga ikiwakaribisha wale Simba kwenye ushindi wa mpira lakini leo Simba wanawakaribisha Yanga maana yake wamewashinda. Kwa hiyo, wana Simba wote wanapongezwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Ismail Aden Rage hajarudi naona bado anasherehekea huko Dar es Salaam kwa magoli mawili dhidi ya Yanga. Kwa hiyo, mimi nawapongeza sana. Katika kipindi cha *Clous Radio* wanaomba mwongozo wa Spika kama Simba waje pia. Wakipenda na wao Simba waje Dodoma! *(Makofi)*

Pia kuna *FITNA Association,* kuna mwanachama mmoja wa Simba namba yake ni 00114 anasema ule mchezo wale wachezaji wa Bacelona walikuwa siyo halali, hiyo ni *FITNA Association.* Ahsante sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Laizer uliomba mwongozo kuhusu nini?

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka mwongozo kuhusu swali ulilonIuliza lakini ukanikatiza na nikataka mwongozo wako kwa sababu ofisi za Wabunge tukitaka kuuliza sikujua mahali popote ambapo ningestahili kuuliza kwa sababu Katibu wa Bunge haulizwi maswali na Spika haulizwi maswali.

Kwa hiyo, sikujua mahali pengine popote pa kuuliza swali la ofisi za Wabunge isipokuwa kwa Waziri Mkuu kwa vile ni kiongozi wa shughuli za Serikali hapa Bunge na fedha zinazojenga ofisi za Wabunge, ni fedha za Serikali chini ya Ofisi ya Bunge. Kwa hiyo, nadhani niko sahihi kabisa kumWuliza Waziri Mkuu maswali.

Halafu kwenye Kanuni zetu….

**SPIKA:** Mwongozo unatakiwa uwe mfupi maana yake unataka uongozwe tu siyo unihutubie.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, kwenye kanuni zetu hakuna, hakuna kanuni inayomkataza Mbunge kumWuliza Waziri Mkuu kuhusu ofisi za Wabunge.

Mheshimiwa Spika, tuna Viongozi watatu tuliowachagua yaani Waziri Kuu, Spika na Naibu Spika ambao wanatuita sisi ni wapiga kura wao, inastahili mtujibu siyo kwa hasira, umenijibu kwa hasira jambo ambalo sikustahili unijibu kwa hasira.

Naomba mwongozo!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa kwanza mwongozo wenyewe umejaa utata. kuna mambo ya aina mbili. Kuna mambo ambayo moja kwa moja yanahusu Serikali tunaweza kuuliza. miaka yote niliyokaa ndani ya Bunge hili, maswali ya ofisi za Wabunge yalikuwa yanaulizwa kwa Serikali kwa sababu ndiyo iliyokuwa inasimamia.

Sasa mambo ambayo yanatuhusu Wabunge kwa mfano jana kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja alikwenda Benki, cheki za Bunge zilikuwa hazijakwenda Benki, alipokwenda Benki alikwenda kugombana na watu wa Benki kule halafu anakuja kuuliza swali hapa. *(Makofi)*

Sasa unajua ni vitu ambavyo vinanvyotuhusu sisi ni vya kwetu, toka tunaanza Bunge la kumi (10) ofisi za Wabunge ziko chini ya usimamizi wa Ofisi ya Spika. Hivi unavyomwambia Waziri Mkuu hapa hajui hata tunaendelea kufanya nini, ndiyo maana nikasema hili liko kwangu wala sikujibu kwa hasira.

Lakini nilisema kwamba hili liko kwangu na humWulizi Katibu wa Bunge bali unaniuliza mimi na nilivyokujibu ndiyo sahihi na mengine yote yanayotuhusu sisi kama Wabunge mtamWuliza Spika sana sana Spika ataingiza katika Kamati yake ya Huduma za Wabunge. Huduma za Wabunge ndiyo zinajibu mambo yetu ya kila siku.

Swali la ofisi za Wabunge ndiyo maana tunaanza kuliacha halitakuwa chini ya Serikali, liko kwetu, sanasana mtanilalamikia mimi kwamba imakuwaje na mimi nawajibu kwa kutoa taarifa kwenu kwamba tunaendeleaje kujenga ofisi za Wabunge, haliko kule walishahamisha, lilishahamishwa rasmi.

Kitu ambacho bado kiko sehemu ya Serikali ni Mfuko wa Maendeleo ya Wabunge kwa sababu gani?

Sheria ile ilipitishwa kwamba ofisi ya Serikali ndiyo itahudumia mpaka tutakapofanya *amendment Zanzibar CDTF* nayo itakuwa inawajibika kwetu sisi, kwa sasa hivi haiwajibiki kwetu sisi kwa sababu bado *amendment* ya Sheria bado hatujaifanya.

Kwa hiyo, kuna mambo ambayo yanatuhusu sisi wenyewe hamuwezi kuuliza na mara nyingi Wabunge wanafanya makosa mambo yanayotuhusu sisi wenyewe wanakuja kuuliza hapa sasa unataka ajibu nani? Nitajibu mimi, ndiyo hivyo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Michael L. Laizer, siyo kwamba tumekurusha au tumekushambulia, hapana! Hili swali halali kabisa liko chini ya Ofisi ya Spika na tunalifanyia kazi kama nilivyokueleza.

Naomba sana tusiwe tunatumia mwongozo kupoteza muda. Mwongozo mwingine nani alisimama? Mheshimiwa Mkosamali!

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. EZEKIAH D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, mimi naitwa Wenje!

**SPIKA:** Alah! Samahani Mheshimiwa Wenje!

**MHE. EZEKIAH D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, naomba ridhaa yako kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge namba 47(1) ambayo inasema.

"Baada ya muda wa maswali kwisha, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa shughuli za Bunge kama zilivyoonyeshwa kwenye Orodha ya Shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa Umma."

**SPIKA:** Soma yote vizuri na ya pili!

**MHE. EZEKIAH DIBOGO WENJE:** Mheshimiwa Spika, ya pili inasema; "Hoja ya namna hiyo itakuwa ni maalum na inaweza kutolewa wakati wowote hata kama majadiliano yatakuwa yanaendelea."

**SPIKA:** Ipi sasa?

**MHE. EZEKIAH DIBOGO WENJE:** Mheshimiwa Spika, leo niliposimama hapa ni siku ya nne Jiji la Mwanza hakuna umeme mfululizo yaani usiku na mchana, leo niliposimama hapa maeneo mengi sana ya Jiji la Arusha hakuna umeme, leo niliposimama hapa maeneo ya Kigoma, Mbeya na maeneo mengi sana ya Dar es Salaam hakuna umeme usiku na mchana.

Mheshimiwa Spika, Mwanza leo hakuna hata maji kwa sababu umeme ndiyo unatumika kusukuma maji, watu wameshindwa hata kwenda kusaga unga kwa sababu mashine zinatumia umeme, kwa hiyo watu wanakwenda kulala njaa kwani hakuna umeme.

Mheshimiwa Spika, wiki mbili kabla ya Bajeti kuletwa hapa ya Wizara ya Nishati na Madini mgawo ulipungua kwa kiasi kikubwa kweli, sasa nashindwa kuelewa huu sasa siyo mgawo tena ni kwamba hakuna umeme uchumi umekuwa *paralysed.* Watu wanapiga simu wanalalamika kweli uchumi umekufa, Mwanza uchumi umekufa, Arusha na Dar es Salaam pia uchumi umekufa.

Mheshimiwa Spika, hili suala lina *impact* kubwa kiuchumi naomba nitoe hoja ili hili suala lijadiliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Kwa mujibu wa Kanuni hiyohiyo aliyoisoma Mheshimiwa Wenje ni kwamba hoja itatolewa na Mbunge kwa kusimamia mahali pake na kuomba idhini ya Spika kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge kwa madhumuni ya kujadili jambo halisi na la dharura na muhimu kwa umma.

Namba nne yake inasema; 'Iwapo Spika ataridhika kwamba jambo hilo ni la dharura halisi na lina maslahi kwa umma, basi ataruhusu hoja hiyo itolewe kwa muda usiozidi dakika tano na mjadala juu ya hoja hiyo utaendelea kwa muda ambao Spika ataona unafaa kwa kuzingatia mazingira ya suala lililotajwa.'

Sasa suala lililotajwa na Mheshimiwa huyu nimemruhusu nimemruhusu amezungumza na mimi niaiagiza Serikali ije itutolee maelezo*. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea!

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 - Wizara ya Maliasili na Utalii**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, watakaochangia sasa hivi ni Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kutoa pole kwa wana Jimbo wa Serengeti kutokana na madhara ya mvua kubwa iliyonyesha juzi jioni kwa taarifa ambazo Mkuu wa Wilaya alinipatia. Nawapa pole katika kipindi hiki cha mtingishiko waweze kuwa na subira na kupata kheri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba nitoe maelezo kwa kifupi katika wizara hii. Wilaya ya Serengeti ni mdau mkubwa sana wa utalii nchi katika nchi hii. Lakini kwa masikitiko makubwa sana Wilaya hii imetelekezwa.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa kumuomba Waziri kwa ukomavu ambao ameshaupata kwenye Wizara hii kwani alikuwa Naibu Waziri, utendaji wake mzuri amepandishwa daraja na kuwa Waziri katika Wizara hii. Uzoefu huo ambao ameupata atembelee Wilaya ya Serengeti ndiko atajionea uhalisia wa haya ambayo nayaeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mapato katika Wilaya ya Serengeti ni duni kuliko kawaida, taarifa za mapato katika utalii tukijaribu kuangalia katika *survey* ambayo Wizara ya Utalii waliifanya. Mwaka 2005 bilioni zipatazo 824 zilipatikana, mtiririko huo tunaona kweli unakwenda kupanda mpaka mwaka 2009 takribani trilioni 7.4 zilipatikana, mwaka 2010 trilioni 9. Hivi Wilaya ya Serengeti kuna kosa gani? Miaka miwili iliyopita mbona hatukulipwa?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mpunguze kelele!

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Miaka miwili iliyopita hapakuwa na mapato ndani ya Wilaya, mwaka huu kwa sababu tumekaribia Bajeti ndiyo zimepelekwa shilingi milioni 34. Hivi tafsiri ya mapato haya ambayo yameongezeka ni vipi tafsiri yake isije katika Wilaya ya Serengeti?

Kwa hiyo, hii inakwenda sambamba na mgao ambao si mzuri wenye uwiano katika Wilaya ya Serengeti kwa sababu hata katika Kanuni ya kugawa mapato mfano ya maendeleoya *CDG.* Kanuni inasema kwamba unaangalia wingi wa kazi katika eneo 70%, unaangalia suala la umbali ndani ya Wilaya 20%, unaangalia kiwango cha umaskini 10%.

Lakini katika mgao ambao unakuja Wilaya ya Serengeti ambayo ina eneo la mraba kilomita zipatazo 10,373 lakini eneo linaloangaliwa katika mgao huo ni eneo lipatalo kilomita za mraba 696, sasa kiwango hiki kidogo ambacho Wilaya inakasmiwa katika Kanuni hii ya mgao ni nyanyaso kubwa katika mapato ya Wilaya ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika, cha msingi kingine ni suala zima la mgao wa ajira. Nakumbuka mwaka 2008 aliyekuwa Waziri Mkuu wakati ule Mheshimiwa Lowassa alitembelea Wilaya ya Serengeti, hoja hii ilipokuja katika mkutano wa hadhara pale mjini Uwanja wa Mbuzi, wananchi walitoa mfano halisi katika bendi iliyokuwa pale Mugumuuwanjani kwamba katika bendi hii ya *TANAPA* hivi angalau ni wafanyakazi wangapi wako kwenye bendi hii ambao wametoka Wilaya ya Serengeti wala Mkoa wa Mara hakupatikana hata mtu mmoja.

Mheshimiwa Spika, mgao huu wa ajira na Serikali itazame kwa makini, kunakuwa na *polarisation* ya kimaendeleo katika nchi yetu, nchi ambayo tunaamini ni ya uongozi wa kisheria, haki na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia cha kushangaza hawa wenye hoteli walio katika mbuga ya Serengeti ajira zile hivi wanaajiri kwa kutumia vigezo gani? Mwongozo na Sheria hizi ambazo Serikali wanaweka hivi wanaweka kwa ajili ya kuvutia wawekezaji au kwa sababu gani? Maelekezo kwamba angalau 75% ya wafanyakazi katika maeneo wanayotoka wakazi waweze kupatiwa ajira.

Lakini utashangaa kwa mfano kuna hoteli pale zamani ilikuwa inaitwa VIP, kuna mchezo pale wa kuuzianauziana baada ikaitwa *Grunimet Conservation,* baadaye ikaitwa *Sasakwa Hotel.* Wapo pale wageni, kweli ni utamaduni mzuri tuweze kupata *experience*.

Lakini kwenye ile *Senior Management* unakuta kwamba wako 20 wametoka nje ya nchi, si vibaya kutumia neno wazungu lakini pia wako wenzetu kutoka nchi nyingine za jirani wako 18 kwenye *Senior Management* kwenye hoteli ile sasa hawa ambao ni wakazi wa maeneo wataajiriwa lini?

Je, kutoka Mkoa wa Mara wataajiriwa lini? Kwa sababu ndivyo maelekezo yanavyosema na ndiyo Sheria zinavyosema. Kwa hiyo, itafika mahali katika kutekeleza Sheria hiyo tunapindisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba suala hili la ajira liende katika mtiririko mzuri ili tuondoe suala la *Polarisation*.

Mheshimiwa Spika, lakini pia suala la uzabuni, hivi wazabuni ambao wana *supply* vitu mbalimbali katika hoteli ambazo zimewekeza kwenye Wilaya ya Serengeti na hata *TANAPA* ni kwa nini hawa wasitokane na Wilaya ya Serengeti? Kwa sababu wako jirani na *running cost* zinakuwa ni kidogo na hivyo utakuta kwamba kwa masikitiko makubwa hivi hata karatasi za chooni mpaka zitoke Arusha?

Hizi *toilet papers* mpaka zitoke Arusha, hakuna watu Mugumu wa kuweza ku-*supply*? Wako watu wanauwezo na mitaji mizuri, hawa wafanyabiashara wa kati wafanye kazi hizi.

Kwa hiyo, ushauri ninaoutoa kwa Wizara ya Maliasili iangalie *across the boarder* ili kusudi Wana-Serengeti waweze kushiriki kikamilifu katika ulinzi wa mbuga hii. Kwa sababu bila Wanaserengeti kulinda hawa wanyama, leo hii usingeweza kuwaona kuendeleza urithi wa dunia ambao Mwenyezi Mungu alitupa kwa sababu wenyeji tangu asili wameweza kuitwa majina ya wanyama hawa na wengine wanaabudu, wanatambikia wanyama hawa. Hii ilikuwa ni njia nzuri ya ulinzi wa asili kuwalinda wanyama hawa. Ndio sababu tembo akienda maeneo ya Machochwe, Ikoma Kabanda wale wanaamini kwamba tembo ni Mungu wao, hawamuui tembo yule, lakini wako wengine wanaamini pundamilia wanamwabudu hawamuui pundamilia na wako wengine waanamini hata fisi, wanafika hatua hata wanachinja mbuzi wanaweka kule fisi ale kama Mungu wao. Ilikuwa ni njia nzuri ya kulinda maliasili. bila utamaduni huu mzuri wa kulinda wanyama hawa, leo hii wanyama hawa tungeweza kuwa nao tunajivunia. Asilimia 70 ya Wilaya ya Serengeti ni *National Park* ya Serengeti. Kwa hiyo, tunaweza kuona kwamba ile *Lions Cake* iko Serengeti lakini hawaioni.

Mheshimiwa Spika, katika uzabuni viko vikundi vya wajasiriamali wadogo wadogo na hao ndio njia ya kuwapa fursa kuweza ku-*supply* kwenye hifadhi, wako akinamama wana vikundi vingi. Pale sokoni wana uwezo wa ku-*supply* matunda, mboga, mchele na kadhalika kwenda katika wawekezaji hawa pamoja na Taasisi za *TANAPA*, lakini utashangaa wazabuni hawa wanatoka mbali kuliko Serengeti. Lakini pia cha kushangaza katika suala zima na kero nyingi ambazo zinawasibu hawa Wanaserengeti wanapata matatizo makubwa ya wanyamapori hawa. Tembo wanaua wananchi kitu ambacho ni jukumu la Serikali kuwalinda wananchi pia kuwalinda wanyama. Lakini hivi karibuni ilikuwa ni tarehe 3 Agosti, niliuliza swali la msingi kwamba hawa wananchi ambao wanauawa na wanyama wakali na wanyama wa porini pamoja na mazao na mali ambazo zinaharibiwa na wanyamapori ni kwa nini wasipate fidia. Lakini hapa ninao ushahidi rahisi ambao tarehe 30 Agosti, 2010, barua ilikwenda kwa Waziri na kulingana na sheria ile ambayo inaelekezwa kwa *SMM* fomu zile zimejazwa za 1963 kwa *Government Notice* 357 ambayo imekwenda kwa Waziri, mpaka leo ni mwaka taarifa kweli haziko Wizarani. Napenda nipate majibu kwamba huyu ndugu Maro Nestory Mataiga aliyeuawa na kiboko, majibu haya niyapate nirudi nayo kwenye Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kikubwa na cha msingi, wako wananchi ambao wameuawa na tembo jirani pale Tarime. Tarehe 17 kuna mzee mmoja aliuawa na nyati na watu wengine wanane walijeruhiwa na pia ni wiki moja iliyopita ilikuwa ni tarehe 10 Agosti, 2011 ameuawa mtu, huyu ni binti wa shule ya sekondari pale Gibaso. Taarifa hizi Wizara wanazifahamu lakini matatizo haya yanapotokea na watu wanapata madhara, hivi fidia inapatikana vipi?

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza kingine na siungi mkono hoja ya Wizara hii, ni suala zima la utekelezaji wa Sheria Namba 5 ya Mwaka 2009, juu ya suala la kuanzisha *WMA*. Kazi ilikuwa inakwenda vizuri na mapato yalikuwa yanapatikana, lakini baada ya kuja mtu anaitwa *CITES* ambaye jukumu lake kubwa ni kuangalia kutotoweka kwa wanyama hawa ambao wako hatarini kutoweka wakiwemo Twiga, lakini tunaona Twiga wanaondoka lakini CITES amegeuka kwamba ni chombo cha Serikali cha kukusanya mapato. Hili hatulikubali na naomba wananchi wote wa Serengeti wasiunge mkono na kama hili halitachukuliwa hatua nitaleta hoja binafsi ndani ya Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, *CITES* hatumkubali kwa sababu mwaka 2008 kwa mfano, Kijiji cha Ikoma Kabanda waliweza kukusanya fedha zipatazo shilingi milioni 358 kwa mwaka mmoja. Ni ajabu *CITES* huyo ameingia kwa miaka mitatu sasa amekusanya shilingi zipatazo bilioni 700. Vijiji vitano ambavyo viko chini ya *WMA* ya Ikoma wameweza kupata shilingi milioni 38 kwa kila kijiji, kitu ambacho hakiridhishi.

Mheshimiwa Spika, suala la *CITES* kukusanya mapato siliafiki na Wanaserengeti hawaafiki na wote hawa walio na hizi *WMA* ambayo *CITES* wanakusanya ikiwemo *WMA* ya wenzetu kule Babati pamoja na Loliondo hatulikubali suala hili la *CITES*. Kwa sababu hata *CITES* maeneo mengine walishakataliwa. Tunisia takwimu zipo alikataliwa pamoja na Ghana. Sasa inakuwaje leo hii sisi Watanzania tunakumbatia halafu iweje hizi *WMA* tatu ndio pekee *CITES* wakusanye mapato maeneo mengine kuna *WMA,* kwa nini iwe ni kaskazini peke yake. Kwa hiyo hili nalipiga vita na Wanaserengeti wananisikia na wananiona, naomba tuungane ili kusudi *CITES* tuachane nayo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna huyu mtu anaitwa Mlawala, kwa utaratibu wa kuanzisha hizi WMA mwekezaji pamoja na maeneo wanapashwa kuweka *bond* ya shilingi bilioni moja. Fedha hizi Mlawala amezipeleka wapi na inatakiwa kwenye *bilateral agreement* ambako kunakuwa na *signatories* ambao mmoja anatoka kwa mwekezaji na mwingine anatoka katika vijiji. Fedha hizi shilingi bilioni moja hazijulikani ziko wapi kwa sababu vijiji havijasaini na wala hatujui wanazifanyia nini na iweje hii hoteli ya Sasakwa wakubaliane na Mlawala ambaye ni Mwanasheria wao aweke fedha hizi katika akaunti yake. Naomba fedha hizi zijulikane ziko wapi kwa sababu hii ni kuwaibia wananchi, ni kuwadhalilisha na kuwafanyia ufedhuli, kwa sababu gani hili lifanyike!

Mheshimiwa Spika, lakini pia kitu cha msingi, haya maslahi ambayo yako kwa wafanyakazi katika mahoteli waliowekeza kwenye hifadhi yaangaliwe upya kwa sababu wale wengine unakuta ni vijana wadogo, wengine wameajiriwa *TANAPA*, maslahi kidogo, sasa hata *outing* ni za shida hawakai na familia zao katika maeneo ya kazi, hivi hawa hatuoni tunawapeleka katika janga la kupata UKIMWI. Kwa sababu hawa wakipata *off* wakienda zao mjini na mchemko wa kiumri wanafanya masuala mengine kulingana na mahitaji ya kiasili, ni maumbile, kwa hiyo wanaweza kujiingiza katika masuala ya UKIMWI. Naomba watengenezewe mazingira mazuri ili waweze kukaa na familia zao wafanye kazi wakiwa wametulia na kuleta tija. Lakini pia naomba nishauri, kuongezwe vituo vya ulinzi katika maeneo haya ya hifadhi. Ukijaribu kuangalia mtandao wa umbali katika *National Park*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dokta Kebwe kengele ya pili.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja hadi nipewe maelezo ya kuridhisha.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita mchangiaji anayefuata Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, kwanza niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba yuko peke yake Wizarani, lakini anafanya kazi nzuri. Anajitahidi sana na nafikiri anahitaji *support* yetu na hasa ya watendaji kumsaidia katika kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimeshtuka kidogo baada ya kuangalia kitabu cha miaka mitano ya maendeleo, sikuona sekta ya utalii ikizungumziwa chochote na sekta hii ni sekta ambayo kwa Taifa letu inachangia katika pato la Taifa kwa kiwango kikubwa kulinganisha na sekta nyingine. Kwa hiyo, la kwanza nilitegemea sana katika hii *five years planning* program tuliyonayo kwamba sekta ya utalii imezungumziwa kwa kina na programu zote na kuonekana ni kiasi gani tunaweza tukafikia angalau watalii milioni moja na zaidi wanaweza kupatikana. Sasa hilo halimo na linanipa mashaka kwamba Serikali iko *serious* katika kujipanga katika suala zima la kutumia rasilimali tulizonazo katika nyanja za utalii kwamba zitatusaidia.

Mheshimiwa Spika, la pili ili utalii uweze kuwa na tija kwetu, yako mambo kadhaa lazima yaangaliwe. La kwanza, ni vile vivutio vya utalii tulivyonavyo na wananchi wa ndani vinawasaidiaje na wanafaidikaje? Hili nafikiri ndilo jambo la kwanza kabisa la kuliangalia kwamba sisi wenyewe tutathmini hivi vivutio tulivyonayo kwa kiasi gani vinatusaidia na kusaidia wananchi. Sasa ukiangalia takwimu zetu tulizonazo zote tunaonekana bado hali ya umaskini inaendelea kuwa chini na hasa ukiangalia ukanda huu wa bahari ambapo kuna utalii wa zaidi wa kutumia *marine products*. Sababu yake kubwa ni kwamba bado kipato cha wananchi ni kidogo na sekta hii ya utalii bado haijasaidia kuwapa kipato cha ziada wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa natoa ushauri kwanza, ni vizuri sisi wenyewe tuka-*identify* kwamba eneo hili tunataka kuendeleza utalii, ni kwa kiasi gani wananchi watafaidika na utalii huu. Kwa mfano, kama unayo Ngorongoro *crater,* je, wananchi wanaozunguka Ngorongoro wao wenyewe watafaidika kwa kiasi gani na *facility* iliyoko pale na Serikali inatoa mchango gani katika kuwaendeleza wale wananchi ili wafaidike na kile kilichopo pale. Hili halifanyiki na ndio maana tukaona kila wakati tukiendelea wageni wanavuna, wenyeji wanaendelea kuwa maskini kwa sababu hatukujipanga katika kuwatajirisha wenyeji waliozunguka maeneo ambayo yana huduma za kiuchumi. Nasema hili ni la kwanza ambalo ni vizuri tukalifanyia kazi. Unaweza kwenda mahali ukaona kuna hoteli nzuri, lakini watu wanaozunguka hoteli ile hali yao ni mbaya. Kuna mgodi, lakini watu wanaozunguka mgodi hali yao ni mbaya. Hili ni tatizo la msingi ambalo kama hatukuli-*address,* kwa hiyo, tatizo kubwa litakalotokea ni migongano na migogoro ambayo haitakwisha.

Mheshimiwa Spika, hili lazima tulielekeze kwanza, migogoro na migongano inayotokea ni kwa sababu akiwekwa mwekezaji wanaojua ni Serikali tu wananchi ushirikishi wao ni mdogo sana na hata fedha za kuwasaidia ili watoe huduma pale hazipo. Sasa wenzetu wengine wanavyofanya ni kuhakikisha kwamba angalau yale mambo ambayo yanatakiwa katika huduma fulani yanatokana ndani ya nchi. Sasa hapa kwetu sisi jambo hilo halipo na nafikiri jambo la kwanza la kufanya ni kuangalia ni kwa kiasi gani wananchi watafaidika na uwekezaji wowote unaofanywa na wageni ili hii migongano isiwepo na kuondoa tofauti ile ya maskini na tajiri. Kama halikufanyika hilo migogoro itaendelea kuwepo na usuluhishi wake utakuwa ni mgumu sana mbele ya safari. Hilo lilikuwa ni jambo la pili.

Mheshimiwa Spika, lakini la tatu ukitazama takwimu zetu za miaka 1995/1996 bado mtalii anatumia wastani wa dola 300 mpaka 400. Hiki ni kiwango kidogo sana. Ukichukua takwimu za miaka 1995/1996 kwa nchi nyingine wameshafikia dola 1,200 na 1,300. Sasa unakuta bado mtalii anatumia kidogo sana katika nchi yetu, matokeo yake mapato yanayotokana na uharibifu wa mazingira ya utalii ni mkubwa zaidi kuliko mapato. Hili ni jambo ambalo bado hatujaliangalia kwamba ni kwa kiasi gani utalii kwa sababu unaharibu mazingira sana ya tabia, mila, vifaa na bidhaa wanachukua na kadhalika. Vitu vingi sana vinaharibika, sisi katika hiyo tunapata nini?

Mheshimiwa Spika, nashauri lazima Serikali ijipange vizuri, mseme katika eneo fulani utalii upo. Tunatakiwa tufanye nini na nini ili huyo mtalii alipe zaidi, leo asubuhi nilikuwa kwenye kipindi nilitoa mfano wa Maldives Islands zisipokwenda pale ukiangalia kwenye ile hoteli moja kuna aina ya vitu kama 13 mtalii akifika pale huduma atazipata. Atakuta maktaba ipo, kuna *wireless internet* ipo, kuna *sauna* za aina mpaka ya sikio mbali, ya mguu mbali, nyayo mbali na kila kitu mbalimbali, kwa hivyo kila mahali anakwenda mtalii analipia. Akiondoka pale ametumia si chini ya dola 2,000 au 3,000 kwa siku moja ukiacha kitanda anacholala si chini ya dola 600 au 700. Sasa kama kwetu sisi bado kitanda akiingia mtalii kuna mbu anamtafuna *let us say* atakuja mtalii wa kawaida, mtalii ambaye hasa anataka kupumzika hatokuja na hili ni jambo la kuangalia kwamba *how much revenue are we getting* katika kila *unit* moja ya utalii, ni vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo hatujalifanya vile vile sio kila mtalii anakuja kuangalia wanyama. Kuna watalii wengine wanakuja kuangalia ndege tu. Ukiangalia ukanda huu wa Tanga, Moshi mpaka Zanzibar huko kuna ndege wa aina nyingi tu wanarukaruka, kuna watalii wengine wanafuata ndege tu. Sasa soko hili lazima tulitafute na katika mahali ambapo tuna *species* nzuri za ndege Tanzania tuna *species* kama vile 1,000 za ndege, watalii wengi wangependa kuziona *species* za ndege. Sasa hilo soko lake liko wapi? Kwa hiyo, katika suala la *marketing* tunatakiwa tuangaliwe hawa ndege soko gani ambalo lipo ili tulifuate lile soko. Kwa hiyo, tunapokwenda kutangaza tusitangaze tu kwa jumla, tutangaze mahali ambapo watu

wanapenda aina ya jambo fulani kuona. Sasa wengine wanapenda *diving*, wanapenda tu waje wawinde samaki na kadhalika. Soko letu lipo hapo tulitafute lile soko, kwa hivyo kuwe na *specialization* ya *marketing,* sio twende kijumlajumla tu tunatangaza tangaza au mwingine unamtangazia ndege hana hamu ya ndege, mwingine unamtangazia uvuvi, hana hamu ya uvuvi, ukimpelekea rafiki yangu pale Mheshimiwa Waziri Mkuu mambo ya kuogelea hayamhusu hawezi kwenda kuogelea. Sasa kila mtu ana mambo yake anayapenda. Sasa hii *specialization is very important* katika *marketing*.

Mheshimiwa Spika, la nne, bado tunalo tatizo la soko. Ukifungua *website* ya wenzetu kila *website* unayoifungua unakuta nchi fulani inatangaza utalii. Jana nilikuwa nafungua *website* moja ya Afrika, kufungua Afrika nikakuta Uganda, natazama Tanzania siioni, je Afrika ni Uganda tu peke yake? Kwa hiyo wenzetu wanazitumia hizi *website* tu kutangaza nchi zao. Wabunge wao wanasafiri wanawapa *brochures* mbalimbali, Mawaziri wanasafiri, watendaji wanasafiri wanapa *brochures* mbalimbali wanaitangaza nchi yao na wanatangaza vivutio vyao, sisi bado katika suala la *marketing* hatuna. Sasa hili ni tatizo la *mindset.* Mtazamo wetu wa kibiashara bado ni duni na tutaendelea kulalamika kwamba tunanyonywa na wageni wanaokuja kwa sababu sisi mtazamo wetu bado sio wa kibiashara. Anakuja mwekezaji anataka kuwekeza badala ya wewe kujitayarisha, huyu mwekezaji akija unahitaji wewe kupata nini na nini unamngojea yeye aseme anachokitaka, yeye anachokitaka ni kuchuma na kuondoka *nothing else. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wewe kama huna mkataba, huna matakwa yako wewe mwenyewe unamwacha yeye ndio awe na *power of negotiation,* atakushinda kila siku na ndiyo matatizo ambayo bado tunayo Tanzania. Kwa hiyo, moja ambalo naliomba, Serikali katika shughuli yoyote mtakayofanya ninyi kama Serikali mseme mnataka nini? Mnataka nini lazima muwaulize na wananchi wenu walioko pale wao wanataka nini ili mwekezaji akija hii migongano na migogoro iliyopo iondoke. Nilikuwa natoa mfano wa wenzetu Ghana wamepata mafuta wanasema hapana. Hawa wananchi wa Ghana haya mafuta yakiondoka watapiga kelele yatatokea kama yaliyotokea Nigeria, tufanye nini? Wakasema tutafute njia mbalimbali, akaenda Alaska na pengine wakakuta *cash distribution system* inafaa wakasema 30 *percent of the production* tunaingia kwenye *cash distribution system,* kila Mghana apate angalau dola 60 aone mafuta yake yamechangia, sisi tunapata nini? Sasa hivi ndio vitu vya kuviangalia na vya kufanya ili kuondokana na matatizo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, suala hili la *concensation*. Bahati mbaya ilikuwa huko nyuma kila Waziri anakuja na sera ya kwake. Nafikiri tuondokane na hili tatizo na hapa naomba sana Waheshimiwa Wabunge katika Kamati zetu hili tuling'ang'anie. Tukishapitisha hapa kitu, tukishakubaliana kama kuna mabadiliko turudi tena Bungeni. Tulikuwa tukipata mapato mazuri katika hizi *concensation* za hoteli zilizoko kule, sasa amekuja mwenzetu mmoja kidogo akabadilisha zikarudi chini, mapato yameteremka sana. Nafikiri Waziri hili tukusaidie katika *concensation* ziwe viwango ambavyo tutakubaliana ndivyo vitozwe na kila mmoja akubali, hatutaki mtu atusamehe, maana yake lazima tufike mahali tuamue juu ya rasilimali zetu, kama hutaki basi, lakini hatuwezi kuendelea kunyonywa namna hii tunavyonywa. Kwa hiyo, nafikiri hili lazima tukubali tulisimamie *concensation* zile zitolewe vizuri watu wafaidike na rasilimali zilizoko katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri na bahati mbaya Wizara hii ni mtambuka. Ili utalii ulete matunda kwetu lazima mtalii awe na kitu cha kununua, awe na shughuli ya kufanya, bado huduma zetu ziko *very poor*. Leo Kenya *Airway* inautangaza utalii wao wa Kenya kwa sababu wana Kenya *Airways*, ile *landing* tu kwamba Kenya *Airways* imetua tayari umeshatangaza utalii kwamba kuna nchi inayoitwa Kenya. Ndio maana ukienda kwa wenzetu wanasema hivi iko Tanzania au ni Kenya kwa sababu Kenya *Airways* inatua kila mahali. Tusaidiane na Waziri na pamoja na juhudi za Waziri wa Uchukuzi kwamba hebu tujitahidi hivi sasa tupate *Airline, Air Tanzania* ipatikane tufanye kazi, tutangaze utalii wetu, nafikiri tutafika mahali pazuri sana.

Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie kusemea suala la uvunaji wa magogo. Miti inavunwa vibaya inauzwa kiholela, ukienda takwimu za Wachina utaona magogo yaliyofika China ni mengi kuliko takwimu za Tanzania. *Data* zipo za kutosha, wizi wa magogo ni mkubwa. Nawaomba sana

watendaji warudi kwenye uzalendo na rasilimali zetu zitalindwa na sisi wenyewe Watanzania, hakuna mtu mwingine. Tuwe wazalendo tusimamie rasilimali zetu, miti inavunwa, miti inayopandwa sina hakika kama inaota. Nilikuwa natoa mfano leo asubuhi kama barabara ile ya Dar es Salaam kuna bustani ya Dar es Salaam na miti inaota pale kwa kudra ya Mwenyezi Mungu, je, mti unaopandwa uko porini unaota katika hali gani? Kwa hiyo, nasema bado suala zima la kupanda miti ni la muhimu lakini suala la uvunaji wa magogo yetu nalo lazima lisimamiwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naona tumpatie fedha hizi ndogo alizopata Waziri akafanye kazi.

**SPIKA:** Ahsante. Naomba nimwite Mheshimiwa Mendrad Kigola na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa ajiandae.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupewa nafasi hii niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii ambayo ni Wizara muhimu sana katika nchi yetu ya Tanzania. Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, nimeipitia taarifa yake ni nzuri, imeandikwa vizuri inaeleweka kwa hiyo namshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana, ukiangalia uchumi wa Tanzania kwa sasa hivi tunategemea masuala ya utalii. Sasa nimeshangaa kidogo kuona kwamba Wizara hii haina Naibu Waziri na Waziri ni mmoja na Wizara ni nyeti ambayo mategemeo ya uchumi tunategemea kwenye Wizara hii. Sasa nitaunga mkono kwa kazi yake nzuri kwa sababu yupo peke yake, naunga mkono lakini wangekuwa wawili nisingeunga mkono. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye mada. Tukitaka kuangalia uchumi wa Tanzania, kwanza mimi huwa nashangaa sana kuitwa maskini. Nadhani baada ya miaka minne naweza nikafuta kwamba sisi siyo maskini. Kuna mwingine ananiambia nifute kuanzia sasa hivi. Kwa sababu ukiangalia Mbuga za Wanyama katika Afrika, Mbuga za Wanyama ziko Tanzania, ukiangalia Mlima Mrefu katika Afrika upo Tanzania, ukiangalia Maziwa Makubwa yapo Tanzania, ukiangalia misitu mikubwa iko Tanzania, ukiangalia watu wenye heshima na wanaishi kwa amani wapo Tanzania. Sasa kwa nini sisi tunajiita maskini na utalii tunao umekamilika. Jana nimeshangaa hapa mwezangu amechangia, amesema hata kumwajiri Mmasai anayeishi katika eneo la utalii kwenye eneo la mbuga inakuwa ni tatizo. Hili nimesikitika sana. Sasa labda sisi tatizo kubwa lipo kwenye uaminifu. Hiki kipengele cha uaminifu itabidi tukiangalie sana. Kwa sababu tukiweka urasimu kwenye vitu ambavyo vinakuza uchumi wa Tanzania hatutaendelea hata siku. Hilo lazima tuliangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine, katika Wilaya ya Mufindi ni Wilaya ambayo ina neema kubwa na katika sehemu kubwa ambayo inanyesha mvua kwa mwaka mzima ni Wilaya ya Mufindi na kule kuna utalii mkubwa, kuna watu wengine wanapenda kuangalia mvua tu ikiwa inanyesha. Wanaweza wakaangalia, ukitaka kuangalia mashamba makubwa ya chai ambayo hayapo katika Afrika yapo kule. Ukitaka kuangalia misitu ambazo tunavuna nguzo za umeme iko Mufindi. Sasa cha ajabu kinakuja, ukiangalia katika ule msitu tulionao sasa hivi umeshavamiwa na wageni. Wenyeji wa pale miaka ya sabini wakati sisi ni wadogo nakumbuka hata mzazi wangu walitoa maeneo ya kupanda miti na Wizara hii ilijitahidi sana kuwaelimisha wananchi kwamba watoe maeneo na watapata faida baadaye.

Mheshimiwa Spika, wananchi walikuwa wasikivu na nawapongeza sana wananchi wa Wilaya ya Mufindi, ni wataratibu na walitoa maeneo. Ukienda sasa hivi watu wamebanana, hawana hata maeneo ya kulima kwa sababu walitoa kwa Wizara kwamba tupande miti, baadaye tunakuja kuvuna. Sasa tunakuja kwenye ulaji, wanaopanda misitu na kuhenya kazi ya kupanda misitu si kazi nyepesi. Ukiangalia watoto wetu wanavyopanda misitu unaweza ukalia. Sasa unakuja kwenye uvunaji watu hawapewi vibali. Mheshimiwa Waziri jana niliongea na wewe na nikakwambia ile Kamati yako inayopendekeza vibali na bahati nzuri mwaka huu hamjatangaza, napendekeza ile Kamati Mheshimiwa Waziri ifute kabisa, itakuharibia. Ifute kabisa ile Kamati uanze upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani Kamati inaundwa halafu mwenyeji wa mazingira ya kule hana hata mjumbe mmoja. Uliona wapi hiyo? Hata sisi Wabunge hatuingii kwenye Kikao, hatujui na moto pale ukitokea wananchi wote wa Wilaya ya Mufindi wanakwenda kuzima moto ule. Sasa itakuwaje wasiwemo kwenye kujadili kuvuna? Kwenye moto tumo, kwenye kupanda miti tumo lakini kwenye uvunaji na ulaji huu sisi hatumo. Hili hatutakubaliana hata siku moja. Nakuomba Mheshimiwa Waziri kuanzia leo, ile Kamati tusiisikie na vibali vile visitangazwe mpaka vifanyiwe uchunguzi, hatukubaliani kabisa na wale waliopewa vibali lazima wachunguzwe. Kuna wengine hawana uwezo wa kuvuna, wengine hawaishi kule, wanakodi Wakenya, wanakodi Wasomali sijui watu gani wanatumia majina ya pale. Tunataka tuwatambue wote na tutawashughulikia. Haiwezekani watu waliohenya pale wakatoa maeneo halafu leo wanalala na njaa. Kuna vijana wetu pale wameunda vikundi wapewe mikopo, waanzishe miradi ya kupasua mbao, sasa hivi wananyimwa. Haiwezekani hata siku moja. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri kwa hili alizingatie vizuri.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka siku moja Mheshimiwa Waziri alikuja kule Wilaya ya Mufindi, bahati mbaya sana sisi hatukupewa taarifa na nilimsamehe kwa sababu ilikuwa mara ya kwanza. Huwezi ukaenda kwenye maeneo ya mtu halafu Mbunge asiwepo utapata wapi *information*. *Information* tunatoa sisi Wabunge wenye maeneo yale wala usifikiri kuna uongozi fulani utakupa *information* sahihi. Mbunge ndiye anatoa *information* sahihi ya maeneo yale. Ndiyo maana sisi tunachaguliwa na wananchi kuangalia maslahi ya wananchi. Hatuchaguliwi kwa ajili ya kuangalia maslahi mengine hata siku moja. Ukiona Mbunge anaangalia maslahi mengine, huyo si Mbunge. Sasa nakuhakikishia kwangu naangalia maslahi ya wananchi na wananchi wale waliotoa maeneo hawakulipwa fidia hata siku moja. Maeneo yote wanaohama tunasikia fidia, kifuta jasho. Tukisema Tanzania ilipe fidia kwa Wilaya ya Mufindi nadhani itafilisika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu watu walihama wengi sana na sisi hatuhitaji fidia, sisi tunahitaji ile miti, watoto wetu wavune, waajiriwe pale wafanyakazi. Hatuwezi kuishi maisha magumu wakati uoto wa asili uko pale, imetokea wapi hiyo? Jana watu wa Ngorongoro walilalamika sana na nilisikitika sana hata kazi ya ulinzi kwenye hoteli Mmasai hapewe. Mtu gani anakwenda kufanya kazi pale. Haiwezekani, tukiendelea namna hii tutakuwa maskini, tutashangaa. Halafu watu wengine wanasema Watanzania hatuna akili. Tuna akili sana sema sisi ni wataratibu. Sisi tulifundishwa tabia nzuri ndiyo maana tunakuwa wapole. Lakini tunatumia akili sana na msione watu wamenyamaza mkajua hawa ni wajinga wajinga. Sisi Wilaya ya Mufindi magogo yapo mengi sana lakini utashangaa magogo yanatoka Afrika Kusini wakati sisi tunavuna magogo pale. Kwa nini yasinunuliwe ya kwetu?

Mheshimiwa Spika, suala hili inabidi Mheshimiwa Waziri aliangalie sana. Sisi hata vijiji vingine havina umeme, kwa nini havina umeme wakati nguzo tunazalisha wenyewe pale? Nguzo zote za Tanzania zinatoka pale lakini sisi umeme hatuna na sasa hivi tunasema umeme umekatika, sawa tunakubali ni tatizo la Kitaifa lakini hata kuweka nguzo tu ni kukatika kwa umeme? Inabidi sasa hivi maandalizi yaanze, umeme ukiwaka unakuta nguzo tayari. Tunaomboleza tu huku vitu vinaeleweka. Sisi tukisema tuanze kuweka nguzo hata kesho tutaweka vijiji vyote, tuna nguzo, hatuna shida. Mheshimiwa Waziri hilo ni la kuangalia na lazima tutumie busara. Sasa hivi sisi hata barabara hatuna, misitu pale imejaa, utajiri uko pale lakini barabara ya lami tumepigwa kilomita mbili. Hivi kilomita mbili kweli unaweza ukasimama ukaelezea kwenye Wilaya kama ile?

Mheshimiwa Spika, tunasema barabara ya kutoka Nyololo, Mgololo mpaka kwenye mali kule tunahangaika, hatupewi majibu sahihi. Nashangaa kwa nini hatupewi majibu sahihi sehemu yenye mali kama ile kwa nini? Tunasema tupige lami kilomita tisini tu. Ni maombolezo na sisi hatutakubali. Tunaomba Wilaya yetu itumike vizuri. Tuna viwanda vingi sana na watoto wetu wanafanya kwenye viwanda hivyo. Lakini hata mishahara ya kule viwandani sikubaliani nayo. Pamoja na kwamba wanasema watalipa kufuatana na uzalishaji sisi tunasema uzalishaji ni mkubwa. Wewe huwezi ukamlipa mtu shillingi 140,000/-. Mtu anaamka asubuhi saa kumi na mbili mpaka saa mbili usiku. Hebu nenda kaangalie watu wanaochuma chai kule, sasa hivi utalia. Unajua mfungwa sio lazima uende gerezani hata kazi nyingine ni ufungwa. Kuna kazi nyingine ni ngumu sana, watu wanapanda misitu kule na kupangiwa. Lakini angalia hela wanayolipwa, juzi Kamati yetu tulitembelea kule kwenye bustani ya miti, akinamama wanapiga magoti pale utashangaa. Hebu nenda kapige magoti uone ile kazi halafu unalipwa shingi 1,000/- kwa siku wala sielewi maana niliona napata hasira haraka. Bahati nzuri huyu hapa kasema tusijinyonge. Sisi

Wahehe tuna tabia ya kujinyonga. Sasa nawaambia kabisa sisi Wahehe hatujinyongi na tutalilia haki mpaka tuipate na mpaka kieleweke. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu haiwezekani sisi tuwe maskini. Wilaya ile ya Mufindi hata viwanda vile sidhani kama vinachangia kiasi kinachotakiwa na tunafuatilia na sasa hivi tumeanza kwa sababu tumechaguliwa na tunafuatilia kimoja baada ya kingine. Kuna watu wengine wameuza maeneo bila mpangilio. Kwa mfano, Bonde la Mgololo ni kubwa sana. Sasa sijui utasikia kuna *Green Resource,* anakwenda kwa mtu anampa laki, mbili laki tatu na kama kuna mtu amenunua kwa kumrubuni mwananchi kwa sababu amekosa kumlipia ada mtoto amepata shida, akauza kwa shidashida ardhi ile inarudi. Huwezi wewe msomi sijui umetoka India sijui Kenya unakuja kumrubuni Mwanamufindi pale kwa sababu yeye hajui kusoma na kuandika mkataba wa Kiingereza umemrubuni, ardhi hiyo itarudi. Kwa hiyo lazima tuelewe na hii haiwezekani kabisa. Kuna watu walimechora ramani kumuuzia mtu na kijiji kimo humo halafu wameuza. Halafu jamaa anakuja anawaambia wanatakiwa wahame. Wahame watu walizaliwa pale? Yeye ndiyo ahame na kama aliandaa mkataba ambao mwananchi hawezi kuulewa na wananchi hawakuelewesha wananchi hawatahama, yeye atahama na kama Serikali itaingia hasara iingie hasara. Hatuwezi kuendekeza vitu ambavyo havieleweki. Sisi tunaelewa na sasa hivi bahati nzuri Tanzania imetusomesha lazima tutumike kutetea wananchi wetu, sitakubali hata siku moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nimalizie na kwa sababu jana umeniahidi kwamba tukimaliza Kikao tutakwenda Wilaya ya Mufindi tukakae, tujadili tuangalie matatizo halafu tuangalie jinsi ya kutatua kisheria na bahati nzuri niliuliza swali lililohusiana na miti, Waziri wa Ardhi aliniahidi na yeye alisema tukimaliza kikao tunakwenda. Tutakwenda kukaa kikao katika Wilaya ya Mufindi tujadili vizuri, tuangalie matatizo, tuangalie jinsi ya kutatua hilo.

Mheshimiwa Spika, kuna wafanyakazi wa Kiwanda cha Mgololo mpaka sasa hivi hawajalipwa tangu amezaliwa wamekaa kwenye makambi kule, wengine wanakufa, hiyo nayo lazima lishughulikiwe kikamilifu. Ni suala la kumaliza kesi, watu wachukue *time*. Kesi gani inachukua miaka sita! Watu wanapata shida sana pale. Kwa hiyo, kwa sababu maliasili inajumuisha sehemu ile yote tutakaa tujadili mambo mengi. Kwa hiyo, namwomba sana ndugu yangu Waziri, karibu sana Mufindi na sisi tutakukaribisha na nitakupokea tukae tujadili na tutatue matatizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameniahidi kuja. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ambayo ni nyeti sana katika Wilaya yetu ya Mufindi. Nataka nijikite moja kwa moja kwenye Wilaya yangu ya Mufindi katika Wilaya yetu ya Mufindi, tuna msitu, tuna msitu wa *Sao Hill* na msitu huu ndiyo msitu mkubwa sana katika Afrika. Babu zetu kwa mapenzi makubwa kwa Serikali yetu waliamua kutoa ardhi kwa ridhaa yao wenyewe wakiamini kabisa na baada ya ushawishi mkubwa kwamba itapatikana ajira ya vijana wao na watapata nafasi ya kuokota kuni kwenye maeneo husika na tutaongeza kipato kwa ajili ya Wanamufindi.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa masikitiko makubwa yale ambayo tulikuwa tumeahidiwa yamekuwa kinyume chake. Watu wa Mufindi wamekuwa wageni na wamekuwa watumwa katika ardhi ya kwetu wenyewe. Nataka niseme kwamba, sitaunga mkono hoja. Kuna mambo mengi ya kusikitisha. Pamoja na ardhi tuliyoitoa bado wazee wetu walikuwa ni *part and parcel* ya watu waliohusika kwa njia moja au nyingine kupanda msitu ule. Lakini leo hii kwa kusikitisha zaidi tukiomba vibali tu pale hatupewi. Yakitokea matatizo katika maeneo yale watu ambao wanawajibika kwa asilimia mia moja ni watu wa Mufindi na mara nyingi panajitokeza matatizo ya moto pale na inawezekana tatizo hilo la moto linaweza likachukua hadi mwezi mzima. Watu wa Wilaya ya Mufindi wanafurumshwa kutoka kwenye maeneo yao, wanalazimishwa kwenda kuzima moto ule. Kwa hiyo, muda mwingi wanautumia kuzima moto ule wakati wameacha shughuli za uzalishaji mali. Kwa kweli hili ni tatizo na nafikiri Serikali ingetuangalia kwa njia tofauti kabisa kwamba hawa kutokana na mambo makubwa ya msingi waliyoyafanya walitakiwa wapewe upendeleo wa kipekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo moja linaniuma sana na ndiyo maana nimesema siko tayari kuiunga mkono hoja hii. Sasa hivi Wilaya ya Mufindi inaongoza kwa UKIMWI katika Tanzania na moja ya sababu kubwa ambayo imesababisha tuwe na UKIMWI ni ule msitu. Sisi tulitegemea msitu ule ungetusaidia kupata ajira lakini umetusaidia kupata UKIMWI. Hili ni tatizo, watu wanatoka kwenye maeneo mbalimbali, yanatengenezwa makambi ya uvunaji kwa sababu dada zetu hawana ajira na ndugu zetu hawana ajira, kwa hiyo, wanaingia kwenye maeneo ambayo sio. Nataka nikwambie hili linatuuma sana. Kwa sasa hivi tuna watoto yatima na wanaoishi katika maisha hatarishi 16,800 katika Wilaya hii. Hili ni tatizo na ni adha ambayo tunaipata katika eneo letu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu ambao unatumika kugawa migao ya uvunaji pale ni wa kificho. Hakuna mwanamufindi hata mmoja ambaye anashirikishwa katika lile zoezi na nataka nithibitishe hapa kwa wavunaji waliopewa vibali jana 2009/2010, hawazidi hata asilimia thelathini. Wavunaji wote wanatoka nje ya Wilaya ya Mufindi, hii ni mbaya na linatuumiza sana. Sasa wananchi wa Mufindi wameniagiza, wameniomba niwaambie Waziri mhusika kwamba wao walitoa ardhi yao kwa ridhaa yao wenyewe na hawakulipwa fidia yoyote kwa hiyo wanaomba kama hamtaliona hili jambo ni la msingi ni bora muwarudishie ardhi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, Serikali hii inahodhi maeneo makubwa sana na mengine hayajapandwa chochote, katika maeneo yetu, familia zimeongezeka lakini hawana sehemu ya kufanya shughuli zao. Sasa tunaiomba Serikali iturudishie maeneo tuliyowapa kusudi yagawiwe kwenye vijiji watu waendelee na uzalishaji mali. Pamoja na ukubwa wa Mufindi tulionao lakini ni fedheha na ni jambo la kusikitisha kuona wanafunzi wa shule za msingi na wanafunzi wa sekondari wanakaa chini.

Mheshimiwa Spika, pia ni jambo la kusikitisha kuona wanafunzi hawa wa shule ya msingi na sekondari wanakaa kwenye madawati matope kule kwetu tunaita *madobe,* kule kwetu yanatengenezwa kwa udongo. Jamani hii ni aibu kubwa. Nataka niseme msitu hauna tofauti na mgodi wa Kahama. Kwa sababu wote sisi *base* yetu ni ardhi. Hakuna utaratibu wowote ambao Serikali imetenga kuwasaidia wale wananchi wanaopoteza muda wao mwingi kwa njia ya kusaidia Serikali. Naiomba Serikali itengeneze utaratibu wa kutulipa mrahaba kwa sababu kwa mwaka jana nimeona wametenga shilingi milioni 25. Hizo pesa ni kidogo sana ukilinganisha na hela ambazo kama Wilaya ya Mufindi tulitakiwa tupate.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka niseme, hatutakuwa tayari kuona tunaendelea kunyanyaswa kwenye ardhi yetu wenyewe. Serikali itutengenezee mazingira ya kuhakikisha tunapata mrahaba.

Mheshimiwa Spika, mtu wa Mufindi kupata mgao ni kazi sana kuliko mtu wa Kenya au kutoka Somalia. Sijui utaratibu huo unaotumiwa unatoka wapi! Vile Vijiji vyote vinavyozunguka msitu ule, naomba utaratibu wa kueleweka na Serikali itoe tamko rasmi leo hii kwamba tutavipa *consideration*.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo baya kuliko yote, hawa wenzetu wa misitu wana utaratibu wa kurekebisha barabara zao katika maeneo yale ya misitu. Lakini, cha kusikitisha, wanapita na makatapila yao kwenye barabara za wanavijiji, hawataki *kusembua* na zile barabara za wanavijiji. Mimi na wanavijiji wangu tumekubaliana kwa kauli moja, hatutaruhusu greda lolote kupita kwenye maeneo yetu. Bora mpakie magreda yenu juu ya ndege, mkayashushe kwenye msitu wenu! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kama wenzetu wa Serikali wangekuwa wanaweza kulipa kodi ya ardhi kwa maeneo wanayomiliki na Halmashauri ya Wilaya ikapata asilimia yake, nina hakika kuna baadhi ya matatizo tungeweza kuyatatua. Lakini wenzetu hawalipi *land rent*. Hili ni tatizo na Serikali inatakiwa iliangalie kwa upana wake.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa tayari kuiunga mkono hoja hii kama Serikali itatoa upendeleo wa kipekee wa mgao katika Vijiji vinavyozunguka na kama Serikali itakuwa iko tayari kuchangia maendeleo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalopenda kulizungumzia ni suala la utalii. Katika Bwawa la Kihansi tuna Vyura ambao hawawezi kupatikana sehemu yoyote ya Ulimwengu. Wamarekani walichukua wale Vyura, wakawapeleka Marekani na sasa hivi wameturudishia. Lakini, sioni Serikali kama inafanya *effort* yoyote ya kutengeneza utaratibu wa utalii katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, tuna msitu wa asili wa Uhafiwa. Katika msitu huu kuna wanyama wadogo na ndege wazuri ambao hawawezi kupatikana sehemu yoyote. Naiomba Serikali iangalie na ikiwezekana ipandishe daraja msitu huu.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Mpanda *TAZARA*, tuna bwawa kubwa sana. Katika bwawa hilo, kuna vichuguu vikubwa viwili. Vichuguu vile ni vizuri na huwa vinahama, asubuhi utakiona kiko Mashariki, jioni utakikuta kiko Magharibi. Hii ni sehemu kubwa na nzuri sana kwa utalii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia kauli yangu, sitaunga mkono hoja mpaka Serikali itakaponithibitishia kwamba iko tayari kurekebisha na Waziri atakuwa tayari kuandamana na mimi kusudi akayajue matatizo kwa kina katika Jimbo langu la Mufindi Kaskazini. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini, kwanza kabisa, naomba niishukuru Serikali, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Maige, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuchika kwa kupiga simu kwa Mkuu wa Mkoa, mwezi wa Sita kusitisha agizo la Serikali la siku 21 la kuwaondoa wakulima mashambani wakidhaniwa kwamba ni wavamizi wa hifadhi bila kuvuna mazao yao. Nawashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika Wizara hii. Wizara hii ni Wizara nyeti sana kwa maendeleo ya Taifa. Lakini pia nioneshe masikitiko kwamba Waziri anafanya kazi nzito sana. Wizara kama hii kuwa peke yake bila kupewa Naibu Waziri, ni sehemu ya kuidhofisha Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, tutakumbuka miaka ya zamani Wizara hiii, Idara mbalimbali huko Wilayani katika Ofisi za Maliasili walikuwa wanapangiwa bajeti ya matumizi kwa ajili ya kusimamia rasilimali zetu hizi. Lakini leo hii, ukienda katika Wilaya mbalimbali, nikianzia hata Halmashauri yangu ya Kasulu, ukizungumza na watumishi wa Maliasili, ni bajeti kiasi gani mmepata ambayo mtatumia kuhakikisha hifadhi zetu zinalindwa, hakuna hata senti. Sasa leo unaikabidhi Idara ambayo inalinda rasilimali, wakati yeye hujampatia fedha ya matumizi, atatenda haki kweli! Matokeo yake unaendeleza biashara kati ya watumishi kwenda kupambana na wakulima. Kwa sababu Mkuu wa Idara uliyemweka kwenye Idara hii asimamie, hawezi kwenda kutembea porini wakati hana gari, hana fedha za mafuta kwa wakati muafaka. Matokeo yake anakaa ofisini, wakulima wa Tanzania tunaongezeka kila siku na hatuna kazi. Ndiyo maana uvamizi wa hifadhi umekuwa mkubwa. Lakini, hakuna mtalaam yeyote anayetembelea maeneo hayo na kuzuia wakulima wasivamie hifadhi hizo.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake watu walishalima na uzuri kwenye Ilani, Mheshimiwa Rais anatuhutubia kila siku kwamba kilimo kwanza, kwa hiyo, ambaye hana kazi anakwenda kushika pori. Wakulima wanalima kwa jembe la mkono, wakati wa mavuno ndiyo mtalaam wa Maliasii anatokea kwamba aache mazao shambani amevamia hifadhi, inaingia akilini kweli? Yaani kwa mtu yeyote mwenye akili ya kawaida, acha wale waliojaliwa kupata akili za ziada, haingii akilini ndugu zangu. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hili na hili hatumwambii Waziri, Waziri anatakiwa asaidiwe, ana kazi nzito sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, kuna maeneo ambayo tunaimba umaskini, hatuna sababu ya kuitwa maskini ndugu zangu. Kwa mfano, mimi natoka Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Kigoma una vivutio vya kihistoria ambavyo tumejaliwa na Mwenyezi Mungu. Kigoma tuna Ziwa Tanganyika ambalo ni la pili duniani kwa kina kirefu. Kigoma tuna Hifadhi ya Gombe ambako kunapatikana Sokwemtu. Lakini Kigoma huko hakuna ndege hata moja inayotua mpaka leo. Kigoma huko ndiyo leo Rais ametukumbuka kwa barabara. Hizo rasilimali zitaendelezaje Taifa hili kama hatuwezi kutoa vipaumbele kwa maeneo ambayo yana vivutio vya asili.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iwakumbuke sana hawa watendaji wanaowategemewa huko Wilayani. Lakini pia, Mheshimiwa Waziri, nashukuru sana kwa hotuba zilizotolewa na Kamati ya Maliasili ya Bunge na Kambi ya Upinzani. Mimi kama Mbunge wa Jimbo la Kasulu Vijijini niliahirisha kushiriki vikao vya Bunge hapa, nikamwomba ruhusa Spika, nikamuaga kwenda Jimboni kushughulikia migogoro na Mheshimiwa Waziri anajua nilimwandikia barua. Wakati nikiwa Bungeni hapa, napata malalamiko mengi kutoka Jimboni, watu wanasumbuliwa na kufukuzwa kwenye hifadhi Vijijini, kumbe Mheshimiwa Waziri ameweka makada wa Chama cha Mapinduzi kwenye Kamati yako. Watu wengine wameshindwa Ubunge, Daniel Nsanzugwanko nimemgaragaza Ubunge vibaya sana, matokeo yake anapewa ujumbe wa Kamati ya Bodi ya Maliasili, anarudi Jimboni kwenda kuvuruga wananchi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna vitu ambavyo Serikali lazima iviangalie. Nimepigiwa simu, "mama kuna hili," nikasema hapana, hii Serikali ni ya kwetu. Nimekwenda kule, nafika naitisha mkutano, Waziri Mkuchika amempigia simu Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa anasema hizo taarifa sina. Haingii akilini! Nikasema haiwezekani watu wapige kelele wote huko. Namshukuru Mheshimiwa Obama, Mbunge wa Jimbo la Manyovu, namshukuru Mheshimiwa Moses Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, bila kujali itikadi zetu za vyama, kwa maslahi ya wananchi wa Kasulu, wote tulikwenda kutoa kilio chetu kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, sasa kama Wabunge tunafikia hatua ya kutoa tamko, naondoka hapa nakwenda Jimboni, bado Serikali inaagiza, Idara ya Maliasili inachukua gari, inafunga vipaza sauti, Mbunge anapita huku, Idara inapita huku inatangaza wakulima ondokeni wakati Waziri mwenye dhamana amekwishaagiza wasitishe zoezi hilo. Kuna haja ya kuwakalisha chini watendaji wetu, tuwafundishe utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, sina lawama kwa Wizara. Kazi yangu kama Mbunge kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuishauri Serikali. Nimekuandikia barua Mheshimiwa Waziri, naomba baada ya Bunge hili, twende Kasulu kwa maslahi ya Watanzania. Wanaoathirika kule siyo vyama, ni Watanzania wote na tunachokipigania hapa ni namna gani Watanzania tutaondokana na umaskini, *full stop! (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia namna mikataba inavyoingiwa na Halmashauri zetu huko, asilimia kubwa hawawashirikishi wadau wakubwa ambao ni wananchi. Leo Kasulu pale ukisikia kelele zote zilizoko Kagerankanda, tuna kitalu ambacho kina wanyama wa kutosha na mimi sina ugomvi katika hilo. Lakini, tunachohitaji kufanya ni wakulima wakae wapi na kitalu chetu tukilinde namna gani. Lakini leo, unakwenda kutangaza kwamba wakulima waondoke na wakati hao wananchi miaka yote wameishi huko. Leo wanazidi kuzaliana, wanazidi kuongezeka. Ni wajibu wa Serikali kuangalia, hawa watu wameongezeka kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye Jimbo langu, kuna Vijiji vingine, Mheshimiwa Waziri, kama Halmashauri kule haimwambii labda sijui kwa nini, viko ndani ya hifadhi na ndiyo maana nimeomba Wizara yake, nimeomba Wizara ya Ardhi, wanisaidie ili wananchi wake kwa amani. Leo wanasaini mkataba, makubaliano yanaendelea, wajanja wachache, watendaji wanakaa ofisini wanawaita wale Wenyeviti wa Vijiji katika maeneo yale, wanawaita Mjini wale wa Halmashauri, wanawashawishi kuweka saini kwamba wamekubaliana na mkataba ule wakati wananchi wa maeneo hayo hawana taarifa, Mbunge mwenyewe mwenye Jimbo hilo sina taarifa. Ni mambo ya kukaa chini. Naamini ni mambo ya kukaa chini tukazungumza kwa pamoja, yanawezekana. Niombe utashi wako tu Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naongea jambo hili kwa machungu sana kwa sababu unapokuwa kiongozi na eneo unaloliongoza halina utulivu, huwezi kuwa na amani. Naomba Serikali inisaidie sana katika hili kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, sina ugomvi na Waziri wala Wizara ya Maliasili, sina ugomvi nao, ndio wajibu wangu kama Mbunge kufika hapa. Nashukuru, nilipokimbia mlinipokea vizuri. Naomba wananchi wangu wa Jimbo la Kasulu Vijijini mkae kwa amani, viongozi wetu Mawaziri, viongozi wa Serikali huku juu ni wasikivu, tunahitaji kushuka chini. Na niwaombe watendaji wote waliopo Kigoma waanze kubadili tabia. Tusiweke matabaka ya kuendeleza mambo ya kisiasa badala ya

kuunganisha nguvu na kuwatumikia Watanzania. Huu siyo wakati wa kampeni, ni wakati wa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo kwa sababu niliyoyazungumza naamini yameeleweka, nasubiri utekelezaji. Ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ambayo kimsingi ni uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania. Mengi yamekwishasemwa na wenzangu na kwa vile Kanuni hazitaki kurudiarudia, nitajikita zaidi Wilaya ya Kilindi lakini vile vile pengine kwa msaada wa Mungu nitasogea na kwingine.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, niseme tu katika Wilaya ya Kilindi sisi tuna maliasili nyingi kama mnavyojua, misitu, wanyamapori, kila utakachokisema kipo. Lakini cha kushangaza wananchi wa Kilindi tuko maskini sana. Kwa nini basi? Tunahujumiwa maliasili zetu, hatupewi elimu jinsi ya kuendeleza maliasili zetu.

Mheshimiwa Spika, nianze na misitu, pale kwetu katika Wilaya yetu kwa kweli tatizo kubwa ni usimamizi na utoaji wa vibali vya uvunaji wa misitu, kuna tatizo pale. Kuna Afisa Misitu ambaye ni wa *catchment*, huyu nadhani ni wa Serikali Kuu. Lakini pale pale tuna Maafisa Misitu wa Halmashauri, anayetoa vibali ni huyu wa *catchment*. Sasa tatizo lililoko pale ni kwamba baadaye usimamizi wake unakuwa mgumu, hili nadhani liko ndani ya Mkoa wote wa Tanga, usimamizi wake kwa kweli unakuwa ni mgumu sana. Huyu Afisa wa *catchment* yeye yuko mtu mmoja tu anawajibika Mkoani. Ukitoka Kilindi mpaka Tanga ni kilomita zaidi ya 300 na kitu. Sasa, wala hawajibiki kwa mtu yeyote mwingine ndani ya Wilaya. Ni ngumu sana hata Mbunge unapotaka kujua jambo, ni tabu sana. Ukienda kwa wale Maafisa Misitu wa Halmashauri wanakwambia muulize yeye, ukimwendea yeye, humpati na ukimpata, hawajibiki kwako na mara nyingi yeye mambo yake anayapeleka Mkoani.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa kweli inatusikitisha sana. Ndani ya Wilaya ya Kilindi tuna misitu mingi kama mnavyojua. Lakini sasa hivi imeanza kuwa historia. Ukipita nje unaona misitu, ingia ndani, ni kipara tupu. Jangwa hili linakuja. Sisi tulikuwa wakulima wazuri, mvua zimekata. Hatuwezi kuendelea namna hiyo. *Chainsaw* usiseme, *chainsaw* kila mahali hadi nimeanza *Operation* Shellukindo. Unakamata *chainsaw*, unapewa 200,000/=. Tayari tumekwishakamata takriban tano, zimejaa huko zinamaliza misitu na hakuna anayefanya jambo. Kwa kweli hili jambo naomba sana mtuangalie.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile ukipita usiku, malori yamejaa na mpaka mengine yana namba STK yanabeba magogo, yanabeba miti, mbao mbalimbali. Ukiuliza, unashangaa ni ya watu binafsi. Sasa usiku wa saa nane, nani atakuwa ana-*patrol* kila siku na wale watu wana namna yao wamezoea na jinsi ya kupitisha. Kwa kweli naomba sana, niwapongeze sana Baraza la Madiwani wenzangu wa Wilaya ya Kilindi. Baraza hili jamani limefanya makubwa mwaka huu, lina mambo mengi. Sasa hivi tuna *special audit* inaendelea, imesimama kidete chini ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Mussa Semdoe. Naomba niseme, tumekaa chini, tukaona tatizo hili, tukaamua kusitisha uvunaji mashambani na sehemu nyingine yoyote kwa miezi sita ili tufanye tathmini tuone kama mbao kiasi gani zipo na kama kuna uhalali wowote. Kwa hiyo, hili nilitaka niliseme.

Mheshimiwa Spika, lakini, niombe sana kwamba Wizara iweze kutuangalia kwa upande huo. Nishukuru kwamba Maafisa Misitu wanakuja mara kwa mara pale kwetu akina dada Bena na wengine wanakaa vizuri. Lakini tunahitaji elimu zaidi na vile vile tunaomba usimamizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wanyamapori. Nishukuru kwamba Wizara wakati huo kupitia Idara ya Wanyamapori wakati bado ilikuwa kwa kweli inafanya kazi zake ipasavyo, walitusaidia gari, tunashukuru, walitusaidia fedha tunajenga *post* kwenye hii Mbuga ya Wanyamapori. Mbuga hii ilikuwa inaitwa Handeni *Game Reserve*. Lakini utashangaa watu wanavuna Januari mpaka Disemba, majangiri lukuki mpaka ukikuta Kobe amebanwa kwenye mtego inasikitisha. Nishukuru Wizara wamejaribu kufanya *push* mara mbili, tatu. Hapa namshukuru sana Bonaventura Midala na wengine pale. Lakini, nishukuru Wizara pale kwamba tumekubaliwa kuwa *WMA* tangu Mei mwaka

jana, tataribu zinaendelea. Tulitengewa bajeti kutoka *WWF* na Bwana Sosevere, nashukuru sana. Niombe tu Mheshimiwa Waziri awawezeshe sasa akina *Captain* Minja ili waweze kuja, tufanye semina, watu wetu waweze kuanzisha hiyo *WMA* mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye utalii. Utalii, tuna fursa nyingi sana ndani ya Wilaya ya Kilindi. Jamani Idara ya Utalii, hebu naombeni mwangalie Kilindi. Tuna mbuga, tuna milima, hasa milima ya Kilindi ya ajabu ambayo huipati popote Tanzania hii, tuna mapango ya kihistoria ambayo aliingia *chief* na mbwa 100 humo ndani na mambo mengine mengi, lakini *nobody* ana-*bother*. Tumekaa tu huku mjini. Lakini naomba niseme tuna fursa nyingi sana ambazo nadhani zinaweza zikasaidia.

Mheshimiwa Spika, nije kwa upande wa Kitaifa sasa, Kilindi mengine tutayashughulikia taratibu. Kwa upande wa Kitaifa niseme tu nimefanya kazi Wizara ya Maliasili, kwa muda wa miaka kumi, kwa hiyo, naifahamu ndani na nje. Wizara hii ilivyokuwa siyo ilivyo sasa, sasa hivi ni kitu tofauti kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara ile uti wa mgongo ilikuwa Idara ya Wanyamapori, kulikuwa na Mfuko wa Wanyamapori ambao unasaidia mpaka mambo makubwa ya Kitaifa, watu kwenye mbuga walikuwa wanaridhika lakini sasa hivi imekuwa ni kitu kingine, watu wanatafutana mle ndani kwa sababu gani, watu wenye sifa wameachwa kando. Jamani naomba niseme, Tanzania kila mtu aamke usingizini. Kila mtu, siyo Wabunge tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesahau kuweka watu kwenye fani ambazo wana sifa nazo, utashangaa Fundi Umeme anapelekwa kwenda kwenye barabara, Daktari anapelekwa sehemu nyingine, ajira hakuna anakwenda kokote. Mbali ya hawa Viongozi wa juu wengine ambao wapo, tufike mahali tuwachukue watu kwa utalaam wao. Idara ya Wanyamapori kulikuwa na watu wazoefu, namkumbuka Mzee Mdoe pale, yule Mzee amekufa na utalaam wake, alikuwa akifika mahali, watu wote wanajua Idara ya Wanyamapori wapo.

Mheshimiwa Spika, baba yule amekuwa *frustrated* ametupwa kushoto kulia, akahamishiwa TAMISEMI, hajui hata afanye kazi gani, lakini haya yote yanatokea. Utashangaa hawa watu wenye uzoefu akina Mzee Ngomero, akina nani wamekaa pale lakini unashangaa wanakuja wengine watoto wadogo wadogo wanawekwa, siri zinavuja, unapoona siri zinavuja na mambo yanakwenda nje, ujue kuna tatizo kwenye hiyo *organisation* na mara nyingi ni kwenye uongozi.

Mheshimiwa Spika, sikatai, lakini kwa kweli inatisha. Kama mwezi uliopita hivi, nikapata meseji ya mtu anatuma anasema Mama unafahamu Idara ya Wanyamapori imegeuka kuwa ya Wabena, nikasema eeh! Akaniambia Katibu Mkuu kaja na sifa zake, vema, Mkurugenzi wa Wanyamapori naye Mbena, njoo kwenye Kitengo cha *TWPF* Mbena, hata kama kweli ndugu zanguni wana sifa, lakini kiasi hicho? Nenda chini hapo sijafika mbali wenzangu wengine wataendelea mahiri zaidi, najua Wabunge wapo watasema, lakini mpaka chini watu kabila moja, kwa sababu gani tunakwenda hivyo, ndiyo tunaleta matatizo. Hawa watu wote mara nyingi unakuta ma-*god father* na watu wa kuwalea, jamani ifike mahali wasiokuwa watoto wa Shellukindo nao wafikiriwe wana uwezo. Idara tunaiua kwa sababu ya kuweka watu kwa maslahi yetu binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa pana ajenda, angalieni hawa walioongea, sitaki kuzungumzia suala la uuzwaji wa wanyama kwa sababu tangu wakati wa Loliondo niliongea baada ya kuona ile ndege inabeba wanyama, niliongea miaka ile, nusura nipoteze maisha sitaki kuliongelea, lakini wenzangu wameliongelea hapa suala la uuzwaji wa wanyamapori. Hata hivyo, angalieni uundwaji wa bodi kinyemelanyemela tu, watu wa kusimamia vitalu hawana sifa, suala la vitalu ni *technical*. Huwezi kwenda kuweka watu tu kwa sababu unaweka, lakini vile vile angalieni, hata vyombo vya dola vinasindikiza, vinakuwepo!

Mheshimiwa Spika, sasa lazima ifike mahali jamani huu uzalendo umekwenda wapi? Ndugu zangu Watanzania kuweni kama mimi, mimi hata nikifa leo najua nitakwenda peponi kwa

sababu natetea mambo ya Mungu. Lakini ndugu zangu msiogope mambo yamefika pabaya, sasa hivi ni lazima tuangalie tunafanyaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba hii iangaliwe upya, suala la wanyamapori nadhani asubuhi Waziri Mkuu amelisemea lakini na Waziri atasema. Lakini pia niseme maoni yangu kwamba, naomba suala hili liangaliwe upya litangazwe *in a more transparent way*, Kamati iangaliwe upya, wapo wenye sifa sikatai kama dada yangu hapa Mwanjelwa, lakini wapo wengine ambao tunajua kabisa ni *out of contest*, haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli niombe kwamba, hilo suala liangaliwe, lakini Idara ya Wanyamapori bado inaendelea, pale naomba yule Mkurugenzi aangaliwe upya hastahili kuwa pale, mnampa tabu. Amehusika kama wenzangu walivyosema kwenye utoaji vibali 180 majuzi tu. Tunalalamikia utoaji holela wa vibali, aliyetoa ni yeye, leo Mkurugenzi, kuna ajenda gani?

Mheshimiwa Spika, halafu nahisi kuna watu huko juu ambao pia wanalea haya mambo, naomba kama kuna mtu huko juu unanisikia upo kwa sababu Mungu ananionesha upo na wewe upo tunakujua na unajijua upo, imetosha! Huwezi kuweka Wilaya yako yote kwenye uongozi ndani ya nchi hii, huwezi kuweka kabila lako wote ndani ya nchi hii, kuna wengine wenye sifa. Naomba unasikia, Mungu anasikia, Watanzania wanasikia, Watanzania saa tunasema imetosha, tujaribu na sisi basi Wazigua na Wanguu tuweke huko ambao tuna sifa, lengo ni sifa.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme jambo lingine kwa upande wa utalii. Ndugu zangu tunakwenda kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki, sasa hivi wenzetu wapo mbali wana *strategy eyes*, kila fursa inayopatikana yoyote, wenzetu wanakimbizana, Kenya hawalali. Mfano wa Babu tumeuzungumza humu ndani, Babu katokea wenyewe Wafanyabiashara wakubwa wameshakwenda nje ya nchi. Nimefika Malyasia nakutana kule na vikundi vinakuja kwenda kwa Babu, vimekuwa *organised* na *Tour Companies* za Kenya, makampuni ya Kenya yameshafanya utalii yame-organise wanafika pale walipia kila kitu wenyewe wakija wanawaingiza pale. Sisi hapa tumekaa, aah siyo kweli, mchawi, hafai, tumieni fursa, si mchawi watajijua wenyewe waliokuwa na imani na hela zao, sisi tunachotaka ni mapato kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kitu kidogo kikija hatuwazi tufanye *opportunity* gani kwa kitu gani, hili Bunge peke yake ni utalii, tunakwenda nchi zingine aah Bunge la Tanzania jamani lile Bunge zuri sana, badala ya ku-*mobilize* tukae tukasema watu waje kwenye Bunge letu waangalie kwa kulipa kiwango kidogo, tumekaa tunasumbuka kwenye chupa. Naomba Idara ya Utalii fanyeni kazi yenu, hata hapo pana matatizo, ukienda *TTB* pale malalamiko walioteuliwa kila mahali. Hebu tuacheni na hayo matatizo. Tunafanya utalii, tunafanya uwekezaji kwa mdomo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbowe kwa aliyoyasema jana, alisema vizuri kwamba tatizo siyo wageni wala wawekezaji ni sisi wenyewe. Naomba Mheshimiwa Maige, tunamheshimu, najua amewekwa pale kwa sababu ana uwezo wa kufanya kazi, naomba aendelee, awakumbuke watu waliopo kule. Wapo wanaitwa Bruno Kawasange ni *dictionaries*, nimekwenda nao Doha wale watu ni *dictionaries* wa Idara ya Wanyamapori, lakini utashangaa wamewekwa kando, watafute wapo watu na ndiyo chimbuko kubwa, wamekaa kimya wanakuangalia, Mheshimiwa Waziri atagonga mwamba mpaka atakumbuka kumbe hawa Wabena si lolote hapa, ngoja niende na utalaam, hata kama watakuwa wabena lakini wawe wale wenye sifa na utalaam. Sisemi kwamba siyo wazuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niishie hapo. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, lakini naomba tena na tena, narudia ile Kamati ya ugawaji wa vitalu *No*, iangaliwe upya wenye sifa wabaki wengine wapya wawekwe, lakini Mkurugenzi wa Wanyamapori na timu nyingine ambayo Mheshimiwa Waziri anaona kwamba wanakwamisha maendeleo yake tutamnyooshea vidole kumbe siyo yeye, ni wenzake. Tumeshagundua hilo, simnyooshei kidole yeye, nanyooshea mfumo mzima. Huyo wa juu naomba aache tumechoka! Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niwe mchangiaji kwenye hoja hii muhimu, lakini nichukue nafasi hii kumpongeza

sana Waziri Mkuu wakati akijibu maswali asubuhi kwa kauli aliyoitoa kwamba sasa watasitisha biashara ya wanyama nchi za nje ili kuweza kuangalia utaratibu mpya, ili haki itendeke na tusipoteze mali hii ambayo ni muhimu sana. Nampongeza sana kwa sababu hii mali ni mali ambayo iko Tanzania tu na tusipochukua hatua za maana hii mali wajukuu zetu hawawezi kuiona. Ningeomba hatua kama hizi alizozisema asubuhi basi ziende hata katika maeneo mengine ya madini, misitu kwenye magogo na maeneo mengine ili kusitisha mpaka taratibu maalum ziweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, nataka kuongelea suala la pori la Mpanga-Kipengere. Wapo wananchi ambao wameathirika sana na kuanzishwa kwa pori hili ambalo lina manufaa katika nchi yetu. Wapo wananchi wa Makete kutoka Kata za Mfumbi kwenye Vijiji vya Ikovo, Usalimwani na Kimani ambao walikubali azma hii nzuri ya Serikali na wakahama wakaenda maeneo ambayo yalipendekezwa. Lakini fidia zao walizolipwa zilikuwa ni kidogo sana na wananchi hawa wakaeleza wazi toka siku hiyo wanalipwa mwaka juzi, kwamba, fidia hizi ni kidogo kwa sababu hawakulipwa fidia za mashamba yao waliyokuwa wanalima, hawakulipwa fidia za nyumba zao na wapo watu ambao wamepewa fidia za jumla ya shilingi elfu tatu, kitu ambacho hakimwezeshi hata kutengeneza tofali mbili au tatu.

Mheshimiwa Spika, wananchi wamelalamika kwa Mkuu wa Mkoa wametoka wao wenyewe wakasafiri mpaka kwenye ofisi ya Waziri Mkuu na Katibu wa Waziri Mkuu akamwandikia Waziri wa Maliasili na Utalii. Cha ajabu Wizara ya Maliasili na Utalii inamwandikia Mkuu wa Wilaya kwamba afanye tahthmini ili waweze kulipwa, najiuliza hivi Mkuu wa Wilaya atafanya tathmini kwa fungu lipi la fedha wakati hii ni kazi ya Wizara ya Maliasili na Utalii?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba sana Waziri afanye kila linalowezekana kufanya tathmini ili hawa wananchi waweze kulipwa yale mapunjo na nafahamu nilishamwasilishia hili. Hiyo ni sababu pekee inayotosha kutamka kwamba siungi hoja hii mkono kwa mara yangu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili ni kuhusu mipaka, mipaka hii iliwekwa na binadamu, wanaokwenda kuipitia upya ni binadamu ambao ni sawa na wale ambao wanakaa kwenye maeneo yale. Kwa hiyo, tunategemea kwamba inapokwenda kurudiwa kupitia mipaka hekima na busara zinatumika. Sasa wapo wananchi wa Wilaya ya Njombe, Wilaya ya Makete, kwenye Vijiji vya Mpanga, Malangali ambavyo walikubali wito wa Serikali wakahama kwenye maeneo wanayohusika lakini leo wanaambiwa tena mipaka inapimwa upya na unapima ukijua kwamba hawa watu zile fidia za kwanza hawakulipwa zote halafu unataka wahamie eneo lingine ambalo halijulikani. Namwomba Waziri alione hili kwamba, watu wake ambao ndiyo watendaji wanatakiwa kufanya kazi kwa busara na hekima, wanakipa mzigo Chama Tawala ambacho sasa baadaye kinakuja kuhukumiwa kwenye dhana ya mafiga matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mfano ambao kwa kiongozi yeyote ambaye ni mtendaji anaweza akaliona hili. Makete katika Kata ya Mfumbi tuna shule ya Msingi Kinani, watendaji wa Wizara hii wamepitisha mipaka kwenye viwanja vya michezo ya watoto, kwenye ukuta hawawezi tena kwenda nyuma, sasa hili kweli halieleweki kabisa kama ni watoto wanasoma pale, unazidi kung'ang'ania kwamba mpaka ni hapa. Kwa sababu wale wananchi hawawezi kusema wao wenyewe wanaonewa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri kwamba ili niunge mkono hoja hii, afanye mambo mawili. Kwanza, aniambie ni lini atafanya tathmini ya wale wananchi waliopunjwa wa Ikovo, Usalimwani na Kimani. Lakini jambo la pili, aniambie ni lini atakwenda yeye mwenyewe Makete na Njombe kwenye Vijiji vya Mpanga, Malangali na Kimani kuona hasa ile shule ya msingi ambayo mpaka umepita pale lakini watendaji wameshindwa kuelewa hali halisi kwamba wanatakiwa watumie ubinadam. Baada ya hayo, nitaunga mkono sina tatizo, najua Mheshimwia Waziri ni mchapakazi, tulikuwa wote Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa hiyo, namfahamu, lakini kwa leo nimeamua niwe wazi kwake kwamba hili hukuwatendea vizuri wananchi wa Makete.

Mheshimiwa Spika, pili, nataka kuelezea utalii wa Nyanda za Juu Kusini. Tunaipongeza Serikali kwa mikakati yake yote inayofanya, mmetumia fedha nyingi kwenda kutangaza *CNN* na mahali pengine ili mpate watalii wa kutosha, lakini najiuliza unapokwenda *CNN* kutangaza Kitulo,

unapokwenda *CNN* kutangaza Ruaha hivi ni mtalii gani atakayekuja ashuke na ndege Dar es Salaam, halafu aendeshe gari masaa kumi na mbili kufika Ruaha, haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, kama kulikuwa na *promotion* ya fedha kwenye zile milioni mia saba ambazo mlikuwa mnatangaza kwa ajili ya utalii kwa Kitulo na Ruaha, zile hela zingetolewa ziende kwanza kwenye barabara na miundombinu ya Viwanja vya Ndege. Kwa sababu ni dhahiri kwamba ili hifadhi zipate watalii wa kutosha ni lazima usafiri wa ndege uwepo, ni lazima Kiwanja cha Nduli viboreshwe, ni lazima Uwanja wa Songwe uanze kazi yake ndipo tutapata watalii wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, lakini kama tunatangaza tunajua kabisa barabara ya kutoka Mbeya kwenda Kitulo haifikiki, huu ni usanii ambao tunatumia fedha pasipokutakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe takwimu ambazo zinaonesha kabisa kwamba haya maeneo yana utalii mzuri sana na hifadhi ambayo ni nzuri sana kuliko zote kama ingewekewa miundombinu ni Ruaha. Kwa mwaka 2006, Kitulo ilipata watalii 76, Ruaha ilipata watalii 14,842, Katavi ilipata watalii 1549, Serengeti ilipata watalii 135,614 wakati Ngorongoro ilipata watalii 360,000. Sasa ni wazi kwamba hifadhi kama ya Ruaha yenye watalii 14,842, leo ikiwa na usafiri wa ndege, ikiwa na barabara ya lami inaweza ikazidi hizi zingine zote kwa sababu 14,842 unaona ni idadi ya watu ambao wamekwenda wao pamoja na shida yote ya kutoka Dar es Salaam kuendesha gari mpaka Iringa, vile vile Kitulo ikipewa barabara nzuri, Songwe kuanza kazi ni wazi haya yote yatawezekana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini kwamba suala la Miundombinu siyo suala lako peke yako lakini inatakiwa Serikali muangalie vipaumbele kwamba kama tunaongelea utalii basi miundombinu hii ielekezwe kule, Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Miundombinu kwa pamoja na Maliasili muone kwamba barabara hizi zinapitika na viwanja vya ndege vinafanyika ndiyo tutajua kwamba ninyi mmedhamiria kukuza utalii.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile mwelewe kabisa kwamba utalii wa Kaskazini tayari unaanza kuwa *saturated*, tayari huwezi ukawapeleka watu mamilioni kule, ni lazima uangalie kutafuta mazao mengine ya utalii ambayo yako Nyanda za Juu Kusini, kwa mfano, Katavi. Kama watu wameweza kwenda wao wenyewe elfu moja mia tano arobaini na tisa kwa usafiri ulivyo mgumu leo hii, hebu niambie ukipeleka ndege watakwenda wangapi? Watakwenda wengi sana. Kwa hiyo, mlione hilo kama ni changamoto ambayo ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni kuhusu utalii wa Vijijini, *Rural Tourism Development*, sijaona mkakati hapa. Mikakati yote imeelekezwa katika ngazi ya Taifa, lakini tuelewe kwamba kijiji kama kijiji chenyewe ni utalii, kijiji kama kijiji kina mambo yake ya kale, kina mambo ya historia, kina mambo ya utamaduni wake ambayo watu wakienda pale wanaweza wakajifunza mengi zaidi. Lakini la msingi watalii wanapofika kijijini ndivyo wananchi wanaweza kuboresha vipato vyao, kwa sababu utalii uliopo sasa hauendi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ukitaka kujua baadhi ya vijiji ambavyo vinafanikiwa sana kwenye hili la *Rural Tourism Development* ni sawa sawa na Mto wa Mbu pale, wapo barabarani, lami imepita pale, unaweza ukaona watu wanavyouza bidhaa zao za utamaduni na kwa kweli uchumi wa pale ni mzuri. Nadhani hili Waziri analielewa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tujielekeze kuwa na mkakati kwa mfano, kule Makete tuna milima ya Livingstone ambayo watu wangependa kuangalia *views*, wakaangalia Malawi, wakaangalia Msumbiji, inaonekana ukiwa juu ya mlima kule, halafu tuna watu ambao wanapenda kutembea kwa mguu kutoka kule Makete kwenda kwa mguu mpaka Matema. Kwa hiyo, unaweza kuwa ni utalii wa aina mbili kwa wakati mmoja; utalii wa hifadhi ya Kitulo lakini vile vile mtu anaweza kwa wakati mmoja akateremka kwenda Matema *Beach* akapata utalii kwenye Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali ianze mkakati wa kuwa na utalii wa vijijini. Mkurugenzi wa Utalii analifahamu suala hili na ni muhimu sana. Tunayo mazao ambayo ni

mazuri kwa mfano, Makete na Mkoa wa Iringa kwa ujumla, kwa mfano, Ulanzi ukiangalia ile *process* ya kuutengeneza inavutia sana, ni ya kitalii toka mkulima anapopalilia shamba lake, anapogema ule mwanzi, anapotundika ule mwanzi na inavyotiririka Ulaya hawana kitu kama kile. Lakini tunge-*link* watu wangeweza kwenda kutembelea wakafurahia na tukapata fedha za kigeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwamba, suala la ujangili ni hatari sana, tutalaumiwa sana na vizazi vijavyo vya baadaye. Ni vizuri Wizara hata kama tunatengeneza fedha, lakini kama hatuna mikakati ya kusimamia vizuri suala la ujangili ni vizuri biashara hizi zikasimama mpaka hapo tutakapokuwa tumejipanga vizuri. Kwa sababu tunaweza tukawa tunavuna, kumbe kikubwa wanavuna wenzetu ambao wametoka nchi za nje kuja kuvuna kwetu.

Mheshimiwa Spika, namaliza kwa kusisitiza Waziri kwamba, nitaunga hoja hii pale atakaponiambia atakwenda lini kufanya tathmini ya wale waathirika wa Pori la Mpanga–Kipengele, Makete na watalipwa lini fidia zao na kwamba ataniambia ni lini tutakwenda wote Makete ili akaone ile shule ilivyopitiwa na ule mpaka na wananchi na akaone Vijiji vya Mpanga upande wa Njombe, Malangali upande wa Njombe ili aone hali halisi jinsi wananchi hao wanavyonyanyaswa.

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi wale watendaji wanawaambia wananchi, tunawahamisha ili tulete wanyama, sasa unamfukuza binadamu ili ulete wanyama kwenye pori, nadhani hili siyo sahihi. Tunakubaliana kwenye sehemu za kutunza vyanzo vya maji kama Kitulo, ni sahihi tutamwambia mwananchi aondoke, lakini siyo kwenye pori la Mpanga- Kipengele *Game Reserve.*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Christopher ole Sendeka, kama nilivyosema Mheshimiwa Magdalena Sakaya ajiandae na Mheshimiwa Profesa Msolwa pia ajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya kada mwenzangu wa Chama cha Mapinduzi, Waziri wa Maliasili na Utalii katika mchana wa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa ni mwizi wa fadhila kama sitaungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi hii aliyoianza kwa muda mfupi tangu alipopewa dhamana hii na Mheshimiwa Rais. Najua mambo mengi yapo katika Wizara hiyo, lakini muda Alioingia kwenye ofisi ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kusema mambo machache ya Jimbo langu kabla sijaingia katika masuala mapana ya kitaifa. Katika Gazeti la Serikali lililotangaza *Mkungunelo Game Reserve,* ilibainishwa wazi kwamba *Mkungunelo Game Reserve* itakuwa katika Wilaya ya Kondoa kwenye Mkoa wa Dodoma. Waziri ameeleza juu ya jitihada zinazofanywa na Wizara kumaliza migogoro kati ya mipaka ya hifadhi za Taifa, mapori ya akiba na Vijiji vinavyozunguka. Wananchi wa Kijiji cha Kimotorok na hasa Kitongoji cha Alkasupai wanasubiri Mheshimiwa Waziri kazi hiyo Aifanye ili Amalize mgogoro kati ya Kijiji cha Kimotorok na Pori la Akiba la Mkungunelo.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba Mheshimiwa Waziri atafanya kazi hiyo ili wananchi hawa waweze kumaliza mgogoro huo na majirani zao wa Mkungunero. Nichukue pia nafasi hii kutamka bayana kwamba wakati huu ninapoingia kuchangia hoja ya Waziri, nimpongeze kipekee mwandishi wa Gazeti la Raia Mwema, Ndugu Paul Sarwat kwa uamuzi wake wa kijasiri wa kukataa vishawishi na kuwa Mtanzania wa kwanza kufichua njama za utoroshaji wa nyara za Serikali uliofanywa katika uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukweli una tabia moja na nianze kumnukuu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kwa ruhusa yako, katika Hotuba yake ya mwaka 1962 kwenye kitabu

chake cha “Tujisahihishe”, Baba wa Taifa - Mwalimu Julius Kambarage Nyerere anasema hivi: “Ukweli una tabia moja nzuri sana, haujali mkubwa wala mdogo, haujali adui wala rafiki, kwake wote ni sawa. Pia ukweli unayo tabia ya kujilipiza kisasi kama ukipuuzwa. Ukiona nataka kulipiga teke jiwe, nikifikiri kuwa ni dongo au mpira, natumaini utanionya. Lakini nikipuuza onyo lako kwa sababu eti wewe ni mdogo au kwa sababu sikupendi, nikalipiga teke, basi litanivunja dole japokuwa ningekuwa nani. Ukweli haupendi kupuuzwa puuzwa.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba nyara za Taifa hili zinaporwa kwa kiasi ambacho inatia fedheha kwa Taifa letu. Wanyama wamekusanywa na nashukuru sana Waziri Mkuu, leo amesema vibali vyote vya kukamata wanyama *(ku-capture)* sasa vitafutiliwa mbali. Ninaomba hilo lianze na kauli hii ya Waziri Mkuu, ianze kutekelezwa sasa na leseni zote 180 zilizotolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii zifutwe na kuchomwa moto kuanzia leo. Ukizingatia kwamba kazi iliyokuwa inafanywa na Makampuni yote 180 ya kukamata wanyama wetu pamoja na kwamba sheria inakataza makampuni ya kigeni na wageni kukamata wanyama, lakini katika utoroshaji wa wanyama zaidi ya 100 waliotoroshwa kupitia Uwanja wa Kimataifa wa *KIA*, wageni walipewa leseni za kukamata wanyama na wanyama hawa walitoroshwa bila aibu chini ya ulinzi wa baadhi ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, Maafisa wote walikuwepo kwenye Uwanja wa *KIA* na bado hakuna mtu aliyekamatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachotia fedheha kuliko yote ni kwamba waliofanya kazi hiyo wakazawadiwa zawadi nyingine ya kupandishwa madaraka, nataka niseme wazi Mkurugenzi wa Wanyamapori wa sasa, ndugu Mbangwa hawezi kukwepa lawama ya kutoroshwa kwa wanyama hao. Yeye ndiye aliyekuwa *Assistant Director Utilization*. Namuunga mkono Mbunge wa Kilindi, mtandao uliojengwa kwenye *wildlife division* ni aibu tupu. Idara ya Wanyamapori ni Idara ya Wanyamapori ya Taifa zima, siyo Idara ya Wanyamapori kwa ajili ya watu wa eneo moja la nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili niliseme wazi, Mkurugenzi wa Wanyamapori, pamoja na kwamba Idara yake ndiyo iliyohusika kusafirisha wanyama, amepewa hadhi ya kuwa Mkurugenzi wa Wanyamapori, chini yake akawekewa Miss Nebo Mwina - *Assistant Director* anayetoka huko mnakotoka, nikisema mnakotoka, samahani nikisema hivyo huko anakotoka Mbangwa. Lakini pia yuko Luis Nzali wa Mfuko wa *Tanzania Wildlife Protection Fund* anatoka huko huko kwenye Jimbo lako Mheshimiwa Spika. Yuko mwingine anaitwa Nziku, anatoka huko huko, ndiye *Assistant Director Hunting,* wote wanatoka sehemu moja. Lakini nataka kusema na *Cites* wako wenyewe hao hao, sasa sitaki kuhoji mamlaka ya Rais ya kumteua Katibu Mkuu, mchapakazi mama Maimuna Tarish ni mchapa kazi, lakini bahati mbaya sana amekuta mtandao na kama hakuukuta, kama ameshiriki bahati mbaya, mtandao huu wa sehemu moja ya nchi hautoi matumaini.

Nataka kusema kwamba kwa utaratibu huu mnaweza mkamweka pale Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Ole-Nangoro, Mheshimiwa Mollel wakikaa pale wanaweza wakaongea Kimasai na kusafirisha wanyama hao kwenda ughaibuni na hakuna mtu anayekamatwa. Mheshimiwa Waziri una kibarua kimoja kizito sana mpaka uje ugundue na nyaraka hizo itabidi uandike barua yake kwenda *Cites* – Geneva. Ukiandika, utapata majibu ya wote kwa sababu Serikali ya *Qatar* usifikiri kwamba ile ndege ya jeshi iliyoingia *KIA* na kukaa kusubiri wanyama kwamba imefanya kazi hiyo ikijua kwamba inakuja kuchukua wanyama ambao hawakulipiwa. Wanajua taratibu zote zimefuatwa. Lakini kwa sababu watu wetu wamezoea njia ya mizengwe, hii ndiyo maana unakuta pale *KIA* hakuna Afisa wa Idara yako, kuna Afisa Mifugo na wanyama hawa wamekuwa wakisafirishwa na wamefanya hivyo kwa sababu hakuna mtu anayetaka kujitia kamba shingoni na ukitafuta nyaraka zilizosafirisha wanyama wale kama *Cites Permit* au *export certificate* utakuta hizo zimefichwa. Andika barua Geneva kwenye *Cites* utapewa majibu na wale waliojificha wote wataumbuka na wewe utachukua hatua dhidi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mbaya sana kwa Ndege ya Jeshi la nyingine kuingia katika anga la Taifa huru na kuhamisha wanyama kama vile nchi hiyo haina Wazalendo. Mimi nataka kusema, mngeleta hata *diplomatic protest* ya kuwaambia wenzetu wa *Qatar* warejeshe wanyama. Mimi naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba wanyama hao tunawataka warudishwe wakiwa hai na hata kama ni mizoga yao tutazika sisi wenyewe. Lakini tunachotaka

kuanzia leo Mheshimiwa Waziri, Idara ya Wanyamapori uifumue kuanzia leo. Kama wana sifa, wapeleke katika maeneo mbalimbali, weka Utanzania uonekane pale. Hatuna tatizo na watu wanaochapa kazi kutoka sehemu yoyote ya nchi, watawanye, usifanye Idara ile ikawa ya eneo moja la nchi. Ni aibu sana. Lakini mbaya zaidi, *okay,* nashukuru Waziri Mkuu atasitisha ukamataji wa wanyama. Sawa hilo nalo nasema mtakuwa mmefanya jambo jema kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini liko jambo lingine ambalo ningependa kutumia nafasi hii kulizungumza, nalo ni mikataba ya ujenzi wa mahoteli katika Hifadhi za Taifa. Hakuna Mwingereza au Mmarekani au Mfaransa anayetoka kwao kwa ajili ya kuja kufuata hoteli nzuri iliyoko katika labda Serengeti au iliyoko Ngorongoro hafuati hoteli, anafuata mandhari na mazingira mazuri na yaliyohifadhiwa na wanyama walioko pale. Inakuwa ni kitendo cha ajabu kwamba mnapoingia mikataba ya kujenga mahoteli kwenye hifadhi za Taifa, hifadhi za Taifa zenyewe hazipewi *percent* ya umiliki wa hoteli hizo. Nataka kusema mikataba iliyopo ya ujenzi wa mahoteli kwenye Hifadhi za Taifa na katika eneo la Ngorongoro sasa itazamwe upya ili yeyote anayejenga hoteli katika maeneo hayo, siyo tu kwamba *TANAPA* ipewe asilimia 50 ila baada ya kurejesha gharama zake Mamlaka za Ngorongoro na *TANAPA* zimiliki hoteli hizo kwa asilimia 100. Mkifanya hivyo, kweli mtakuwa mmeitendea nchi hii haki. Lakini mkiwaacha wafanyabiashara waweze kutishia Serikali, na leo tumesikia baadhi ya watu Serena na Sopa wanakataa kulipa tozo, wanataka tuendelee kuwatoza dola nane kwa chumba kwa kitanda wakati wao wanakusanya kati ya Dola 450 mpaka 1000, nasema huu ni wizi na ni ufisadi wa asubuhi.

Naomba tu kuanzia sasa kama wenzetu wa Sopa na Serena na Elewana hawataki kulipa tozo hiyo, Mheshimiwa Waziri futa leseni. Umepewa dhamana ya Uwaziri, kalia Kiti ujae, usikae kama una jipu. Maana mwenye kukaa kama ana jipu, utakaa upande umoja. Kalia kiti ujae na hawa wajue wewe ni Waziri wa Serikali iliyo huru na kwamba Taifa hili ni huru na kwamba hawawezi kucheza na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuchukua nafasi hii kuwaonya na wenzetu waliopo *Leopard Tours* na wengine wa *Rangers* ambao wanataka kucheza ngoma inayopigwa na hawa wenzetu wasiige. Nami nawaambieni, ukicheza na nyani utavuna mabua. Haiwezekani mandhari nzuri tuliyoijenga kwenye hifadhi zetu mkawaacha wageni wanufaike kwanza.

Ningetaka Mheshimiwa Waziri utumie nafasi yako, Hoteli zote zitakazojengwa kwenye Hifadhi zetu za Taifa zijengwe na Watanzania, wakikopeshwa na benki yoyote wanaweza kulipa. Wasiliana na Mkurugenzi wa *National Housing* Mchakapa kazi, ndugu yetu Mchechu aweze kuwasaidia kujenga hoteli katika Hifadhi za Taifa. Afadhali *National Housing* pamoja na Ngorongoro na *TANAPA,* mkamiliki Hoteli katika maeneo yetu, pengine mkatafute menejimenti tu, lakini wageni wasipate nafasi tena ya kunufaika kwa kiwango hicho maana ndio wanapata kiburi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine juzi nimesikia tena kwa mara nyingine, bado mamlaka ya Ngorongoro inaendelea kujenga mahoteli katika njia ya Faru. Hili ni jambo baya sana. Ukitoka katika *Crater* kupita Layanai kuelekea mpaka Albalbal kuelekea Oldupai kutokea Serengeti ndiyo njia ya Faru. Unapokuja kujenga Hoteli ya Nyota Tano Alayanai pale kwa sababu tu unampenda mtu anayeomba, nilitaka kusema, kama Bodi hiyo iking'ang'ania, vunjilia mbali asubuhi na unda Bodi yenye sura ya kizalendo. Hamwezi kujenga Mahoteli ya nyota tano pale halafu mkawaacha Wamasai wa Ngorongoro hawaruhusiwi kuishi, nyumba ya bati mnawanyima mnawaambia wakae kwenye nyumba za nyasi. Lakini mwambie leo Mrunya rafiki yangu akalale kwenye nyumba ya nyasi, Mwambia Mwenyekiti wa Bodi Makamu Mwenyekiti wa Chama change, Mzee Msekwa akalale kwenye tembe pale leo hakuna atakayelala. *(Makofi)*

Sasa nilikuwa nataka kusema, lazima sasa mjue wanaoishi pale ni binadamu, wana haki kwa mujibu wa *Bill of Rights* zilizoko kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano, msiwaudhi. Maana kwa kiwango mnachofanya sasa mnawanyima kujenga nyumba za bati, lakini mnawaleta wageni kutoka nje wawekeze kwenye ujenzi wa mahoteli mpaka yenye Nyota Tano na kule Embakai ni mfano. Embakai Marehemu Evis Msiba aliomba kujenga hoteli japo alileta maombi wakati muda umepita akahurumiwa na Bodi, akapewa ajenge hoteli, badala ya hoteli ya vitanda 40 sasa

amepewa ajenge hoteli ya vitanda 100 kwa sababu *Embakai Crater* ni eneo dogo na lina athari zake kimazingira kama walivyosema Watalaam wa Mazingira, lakini bado wanafumbiwa macho.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya aina hiyo ambayo haiwezi ku-*comply* na maelekezo ya *NEMC* na watalaam walioko pale inaweka mashaka ya uhalali wake wa kuendelea kuweko pale. Ndiyo maana nasema wakati umefika sasa wa kufumua Bodi ile, uwe na Bodi yenye sura ya uzalendo zaidi inayojali maslahi mapana ya nchi zaidi inayojali uhifadhi zaidi na ambayo inajua wazi kwamba mkataba wa Sheria ya kuwepo kwa Mamlaka ya Ngorongoro pale unatambua uwepo wa jamii ya wafugaji wanaoitwa Wamasai ambao hamwamilikishi hata hatua moja, lakini wageni mnawamilikisha kwa miaka mingi wajenge hoteli za kitalii na wale wanabaki kuwa mashahidi tu kuangalia yanayotendeka. Ajira zao katika mamlaka ya Ngorongoro hamuwapi katika hoteli zile, hawapati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasikitika tu kusema naomba niishie hapo, baadaye tutaelewana kwenye vifungu na Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, ni-*declare interest* kwamba mimi ni mmojawapo wa Wajumbe wa Kamati hii muhimu ya Ardhi, Maliasili na Utalii na kwa fani yangu pia ni Mhifadhi. Lakini nianze kwa kusema kwamba siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa masikitiko makubwa sana kwa kuelezea hali ya manyanyaso na mateso wanayopata wananchi wa Wilaya ya Urambo yanayofanywa na Maafisa wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Mambo yanayofanywa ndani ya Wilaya ya Urambo, maeneo mbalimbali yanasikitishwa na hayaelezei kama kweli kuna Serikali. Wananchi wale wamekuwa kama wakimbizi ndani ya nchi yao. Wamekuwa hawana uhakika wa maisha. Naomba Serikali leo itoe majibu hapa Bungeni nini hatma ya wananchi wa maeneo mbalimbali nitakayoyaeleza yanatokea kila siku maeneo ya Urambo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tarehe 14 Agosti, 2011, Afisa Maliasili wa Wilaya na Mkoa na Polisi wa Urambo wakishirikiana na Mgambo, waliingia kwenye Kijiji cha Shela Kata ya Usinge, wakaanza kuchoma moto nyumba za wananchi bila huruma.

Mheshimiwa Spika, Kijiji kile kimesajiliwa kisheria, kipo ndani ya mipaka, kina uongozi wake, Serikali ya Kijiji na Vitongoji vyake. Bila huruma wamechoma nyumba 104 mpaka sasa hivi, wamechoma vyakula kama mahindi gunia 3,001 mpaka sasa, wamechoma mpunga magunia 2,011 mpaka sasa hivi, nguo zote zimeteketea ndani, wananchi wale mpaka ninavyoongea wako chini ya mti hawajui waende wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna kikao walichokaa kuwaambia angalau toeni vitu ndani. Polisi walikuwa wanaingia na kuwasha nyumba viberiti. Huu ni unyama namna gani kwa wananchi wa Tanzania! Amani tunayosema iko Tanzania, iko wapi? Wanaoishi kule ni binadamu, siyo wanyama! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka huu tarehe 24 Mei, Polisi hao na Afisa Maliasili na Mgambo kwa maagizo ya Mkuu wa Wilaya waliingia kwenye maeneo hayo hayo ya Shela wakakusanya ng'ombe ndani ya mipaka ya eneo la Kijiji waka-*confine* mahali pamoja kwa muda wa siku sita, hawakula, ndama karibu wote waliteketea. Wanyama wale wamekuja kuachwa baada ya Vyombo vya Habari kutangaza kwa nguvu wanyama wameachiwa kwenda kunywa maji, zaidi ya 100 wamepoteza maisha. Leo hata miezi miwili haijakwisha, bado tatizo lingine limetokea pale pale. Nchi hii iko wapi? Serikali iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana mwezi wa Tisa ndani ya Wilaya ya Urambo Kata ya Igwisi Kijiji cha Mpanda - Mloka, Polisi na Afisa Maliasili na Polisi wameingia Kijiji cha Mpanda - Mloka wameteketeza mashamba ya wananchi, wameteketeza nyumba kwa moto, wamechoma mpaka mashine za kusagia nafaka. Nguo zote zimeteketea ndani. Nimetembelea lile eneo ni mwezi wa Tisa siku chache kabla ya uchaguzi, nilikwenda pale baada ya siku mbili, nililia kilio. Watoto wamepakatwa, hawana hata kipande cha nguo chini ya miti, vyakula vimekusanywa

chini ya mti ambavyo walikuwa wanakimbiza vichache, vingi vimeteketea ndani ya nyumba. Hii nchi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009 Kata ya Kamsekwa Wilaya ya Urambo Kijiji cha Makole, wananchi walichomewa nyumba zao, vyakula vyao hadi kuku waliteketea ndani ya nyumba. Nilitembelea lile eneo, nimekuta shule iliyojengwa na imewekwa jiwe la msingi na Mheshimiwa Mbunge wa Urambo Magharibi, limepigwa nondo limedondoka. Kwa nguvu za wananchi wamejenga, wameshirikishwa wakajenge ili watoto wao waweze kusoma shule. Imepigwa nondo na Maafisa Maliasili na Polisi. Unyama kama huu unafanyika ndani ya nchi ambayo ina usalama, ndani ya nchi ambayo ina Serikali, tuko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu cha kusikitisha, maeneo mengi ya Mkoa wa Tabora, Wilaya ya Urambo hadi maeneo ambayo yana makaburi ya waasisi wazawa wa Wilaya ile, akina Mtemi Mirambo yanaambiwa yako ndani ya hifadhi. Hii inasikitisha. Mwaka jana Mkuu wa Mkoa aliunda Tume, *task force* wakazunguka eneo la Tabora kuangalia Vijiji ambavyo vinasemekana viko ndani ya hifadhi. Vijiji 60 vilionekana viko ndani ya hifadhi na wamekaa kule zaidi ya miaka 30, 40. Tulikaa tukaiangalia ile taarifa hapa Mkoa wa Dodoma, watalaam walituletea Wabunge wote wa Mkoa wa Tabora, tukakubaliana kwamba Serikali iangalie upya suala la Hifadhi katika Mkoa wa Tabora, iwekwe mipaka kamili na maeneo ambayo yamekaa muda mrefu, Serikali iangalie jinsi ya kuhamisha wale watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna kitu chochote kinachoendelea mpaka sasa hivi. Kinachoendelea ni wananchi kunyanyaswa, wananchi kuonewa, wananchi kufanyiwa vitendo vya ajabu. Ninaomba sana Wizara ya Maliasili na Utalii, haiwezekani matukio yote yanatokea na ripoti kila siku, hakuna hatua inayochukuliwa. Kikubwa zaidi Watendaji wa Serikali akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Urambo wanaagizwa wananchi wakafanyiwe madhira yale. Serikali lazima ijiulize swali, ni kwa nini Mkoa wa Tabora una Wilaya sita na kwa nini Urambo ina matatizo? Tena Urambo Magharibi ni tatizo, kila siku kwa nini hamjiulizi swali? Mkuu wa Wilaya amekuja pale, anasema ni kada ametumwa kufanya kazi ya ukada. Kama ni kada, mpeni kazi ya Chama.

Mkuu wa Wilaya anatakiwa ahudumie wananchi walio wa chama chake na wasiokuwa wa chama chake. Kama hayupo tayari kufanya kazi, mpeni kazi ya chama ajulikane anafanya kazi ya Chama. Hawezi kuendelea kuua watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijasahau, Kata ya Igwisi wananchi waliuawa zaidi ya 23 kwa risasi. Nilitembelea eneo lile, nimeshuhudia maiti ziko juu. Nimepiga picha mpaka makaburi ya watu waliouawa siku moja kabla sijafika pale. Cha kusikitisha, nimekutana na mtoto mdogo mama yake kauawa na risasi, na baada ya kumuua wakamweka juu ya mama yake. Mama ni maiti, mtoto analia wakamweka juu yake. Hii ni Tanzania gani?

Mheshimiwa Spika, naomba sana, Serikali hii ni ya wananchi wote, mwananchi yeyote ana uhuru na haki ya kuwa mwanachama wa Chama chochote, tunaongozwa na sheria. Haiwezekani mwananchi akiwa ni Chama kingine cha Upinzani aonekane yeye ni mnyama. Naomba Serikali ichukue hatua, naomba Waziri Mkuu achukue hatua, naomba Rais achukue hatua. Hawa ni Watanzania, kwa nini raia wa nje waje ndani ya Taifa hili waishi kwa raha, Watanzania wenyewe tuishi kwa matatizo? Hatutakubali, hatujafanya maandamano, tulikuwa tunafuata taratibu. Ninawataarifu Mawaziri wote, usalama wa raia wanajua, maliasili wanajua, Waziri Mkuu anajua, kazi yangu ni kutoa taarifa kwa utaratibu unaotakiwa. Lakini hakuna kinachofanyiwa kazi. Inauma sana. Naomba Tume huru iundwe ikaangalie matatizo ya Jimbo la Urambo Magharibi. Tunalia kuna njaa, Watanzania hawana chakula, wananchi wale ni wakulima na wafugaji, leo vyakula vyote vimechomwa moto vimeteketea. Nendeni leo viko pale. Haiwezekani huu ni unyama wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli inauma sana tunajiita nchi ya amani. Nini maana ya amani? Kama Serikali ilifanya makosa ikasajili vijiji ndani ya hifadhi, ifanyie utaratibu, kuwahamisha iwe kwa utaratibu unaotakiwa. Kuwachomea nyumba siyo *solution*, kuteketeza mali siyo *solution* kuchoma vyakula vyao siyo *solution*. Kuna *means* za kutumia mwananchi aondolewe pale, ataishi sehemu

nzuri. Wale ni binadamu ndani ya nchi hii na wana uhuru wa kuishi ndani ya nchi hii. Kama ni wakimbizi watoeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kwenye hoja nyingine. Naomba niende moja kwa moja kwenye suala la Chuo cha Utalii cha Taifa. Lipo tatizo kubwa kwenye Chuo cha Utalii cha Taifa hapa Tanzania, Chuo kile yapo mambo ya kimsingi ambayo sijui kama Wizara imeyaona au haijayaona. Lakini chuo kile kinaendeshwa kidikteta. Mkuu wa Chuo amekuwa na *dictatorship*, anafanya maamuzi peke yake, hashirikishi watumishi wengine. Ndani ya miaka mitatu mwaka 2008 mpaka 2011 watumishi zaidi ya 20 wa kada mbalimbali wameacha kazi na sijui kama Serikali inatoa majibu gani leo kwa sababu kila akitokea Afisa wa Maliasili anataka kwenda kuchunguza kuna tatizo gani, pale anapigwa *stop* na uongozi wa juu huko Ikulu. Inasemekana Mkuu wa Chuo kile analindwa na bosi fulani huko juu.

Tunaiomba Wizara/Serikali chuo kile ni muhimu kujenga taswira nzuri ya Maliasili Tanzania na kutoa vipaji na kada mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Utalii. Wizara kuendelea kunyamaza kimya ikaachiwa mtu mmoja ambaye anasababisha watu wengine, wanaacha kazi kila siku, kuna tatizo la msingi. Serikali kila siku inaajiri wafanyakazi, wakikaa miezi miwili/mitatu kutokana na hali iliyoko pale wanaacha kazi wanaondoka. Leo kwenye Sekta ya Utalii ya Mafunzo ya Utalii ndani ya Chuo kile, kuna Walimu watatu. Kila siku wanaacha kazi na wengine wako mbioni kuacha kazi.

Kwa hiyo, kuna tatizo kubwa kutokana na kulindana. Kama mtu ni mbovu hafai kukaa mahali kwa nini mnamuacha? Kwa nini yule mama haguswi ana nini pale? Amewekwa na nani? Kuna watu wengine ambao wana uwezo wa kuendesha kile Chuo, kwa nini matatizo haya, wafanyakazi wanaondoka mara kwa mara? Naomba sana Waziri afanye kazi pale, iundwe Tume maalum izungumze na mtumishi mmoja mmoja, isiingiliwe na menejimenti kwa sababu watumishi pale wanaambiwa huna ruhusa ya kusema chochote kwenye kikao. Kwa hiyo, mkiitisha kikao kama menejimenti, watumishi wananyamaza kwa sababu wameshaambiwa kabla. Kwa hiyo, huwezi kujua matatizo. Kwa hiyo, unda Tume maalum, uliza mtumishi mmoja mmoja, mtasikia matatizo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Chuo kile kinakuwa ni cha kitaifa, kiwe na sifa. Kwa sababu sasa hivi Chuo cha Taifa kinashindwa hata na Njueni. Njueni kinasifika sana kuliko Chuo cha Utalii kwa sababu ya tatizo la msingi lililoko pale.

Mheshimiwa Spika, niende haraka haraka kwenye suala lingine dogo la *concession fee* Waheshimiwa Wabunge wengine wamelizungumzia, lakini tunasema kwamba kuna wakati wafanyabiashara wanakuja wanakuwa juu ya Serikali. Zipo ishara ndiyo maana tunasema kwamba iweje mfanyabiashara? Serikali itoe maagizo kwenye biashara akatae? Wale wawekezaji wa mahoteli wamewekeza kwenye hifadhi. Kilichowavutia mpaka wakaamua kuwekeza pale ni mandhari ya hifadhi, haikuwepo yenyewe inalindwa, inahifadhiwa. Anapotaka utalii kutokana na mandhari ya hifadhi ile, kwa nini akatae kutoa kinachostahili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nichangie katika hoja hii muhimu iliyo mbele yetu. Pili, ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wa Wizara hii kwa hotuba yao nzuri na kwa namna wanavyotekeleza kazi zao pamoja na mapungufu mengi ambayo yameonyeshwa.

Aidha, niungane na wenzangu waliotangulia kuzungumza kwa kumpongeza sana Waziri Mkuu kwa kauli yake ya leo asubuhi ya kuagiza kuangalia upya juu ya biashara ya kusafirisha wanyamapori kwenda nchi nyingine. Jambo hili nafikiri ni la kimsingi kwa sababu, kama walivyozungumza wengine, iwapo utawapeleka wanyama hao huko nje, maana yake ni kwamba hawa wanyama hawaendi kuchinjwa, wanyama hawa wanakwenda kufugwa kwenye *zoos.* Kwa hiyo, hata biashara yetu ya utalii tutakuwa tumeshaiua, kwa sababu kutakuwa hakuna sababu ya kuja huku mtu alipe Dola 3000 kwa nauli ya ndege, aje akae kwenye hoteli wakati anaweza kuona wanyama hao huko huko ambapo wanyama wamepelekwa. Ni imani yangu kwamba Wizara

italifanyia kazi agizo hili ili hatimaye tuweze kuona kwamba kama biashara hii inaendelea, basi iwe na masharti ambayo yana manufaa kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana, kwa sababu ina raslimali nyingi ambazo ni urithi wa Watanzania na vizazi vijavyo. Lakini kwa bahati mbaya sana raslimali ambazo tunazo na hususan mimi ningependa kuzungumzia misitu. Misitu inatoweka kwa haraka sana kiasi kwamba vizazi vijavyo huenda wasikute chochote, watakuta janga katika nchi hii bila kuchukua hatua madhubuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inachakaa kutokana na matendo ya mwanadamu kwa shughuli za kilimo, ujenzi na mambo mengine na hivyo tunaendelea kutumia raslimali hizi kwa njia ambazo endelevu. Kila mmoja hasa wale ambao wamezaliwa vijijini na wameishi vijijini watakumbuka kwamba maeneo ambayo wametoka leo hii kuna mabadiliko makubwa sana. Maeneo ambayo zamani yalikuwa na miti, ilikuwa na mito, leo hii miti hiyo haipo, imetoweka na vile vile hata mito midogo midogo iliyokuwepo leo hii haionekani katika vijiji vyetu na sehemu mbalimbali. Hali hii ikiendelea ni dhahiri kwamba kutakuwa na tatizo kubwa la nishati baadaye na hasa maji.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa takwimu chache ili kueleza haya ninayosema. Mwaka 1961 tulipopata uhuru, nchi hii tulikuwa na misitu ambayo ilikuwa na eneo la hekta milioni 48. Leo hii tuna eneo la misitu lenye hekta milioni 33. Katika miaka mitano/sita/saba ijayo Tanzania itakuwa na eneo la misitu yenye hekta milioni 29 tu. Kwa hiyo, unaweza kuona namna tunavyozidi kupoteza misitu yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa nini hili linatokea? Kwa wastani ni kwamba, eneo la hekta 400,000 kila mwaka linafyekwa *(deforestation)* kwa ajili ya shughuli mbalimbali za mwanadamu. Shughuli kubwa kusema kweli ni mkaa. Watu wanaoishi vijijini ambao ni asilimia karibu 80, asilimia 95 ya hawa wanatumia kuni, lakini kuni kwa kweli wanaokota siyo kwamba wanakata kwa makusudi, ni chache sana. Lakini asilimia 75 ya watu wanaoishi Mijini wanatumia mkaa. Nikichukua mfano wa mji mmoja tu Jiji la Dar es Salaam, kwa siku moja wanatumia magunia ya mkaa 30,000 yenye kilo 30, kwa siku moja, kwa Dar es Salaam peke yake. Kwa hiyo, kwa mwaka wanatumia magunia 10,950,000. Hizi ni sawa na meta za ujazo 365,000. Sasa mita za ujazo za 365,000 ina maana kwamba eneo linalofyekwa miti ni hekta 10,400 kwa mwaka na hiyo ni kwa ajili ya Dar es Salaam tu. Hujaangalia Majiji mengine makubwa kama vile Mwanza, Arusha, Mbeya na miji mingine mikubwa. Kwa hiyo, kama hii *trend* ndiyo itakuwa hivi, tukiendelea kwa namna hii ni kwamba misitu yetu tutaipoteza kwa muda mfupi ujao.

Eneo ambalo linatumika kwa mwaka kwa ajili ya kukata miti kwa ajili ya mkaa tu peke yake kwa Tanzania nzima ni hekta 162,000 kwa mwaka. Lakini wakati huo huo juhudi za kupanda miti ni hekta 130,000 tu kwa mwaka wakati zinazofyekwa ni hekta 400,000. Kwa hiyo, tunapoteza eneo kubwa sana kwa mwaka na bila kuchukua mikakati madhubuti. Kwa upande wa nishati Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Kilimo kuangalia ni namna gani kunaweza kuwa na mkakati endelevu ili kusudi tuweze kujinusuru katika jambo kama hili.

Mheshimiwa Spika, linalotisha zaidi ni kwamba kwa sasa hivi Tanzania tuko karibu milioni 41 na kufikia mwaka 2025 Watanzania tutakuwa tumefikia idadi ya watu milioni 65 na mahitaji ya nishati, acha maji, yatazidi kuongezeka. Wakati huo huo nishati ambayo watu wengi wanaitumia inazidi kupungua. Kwa hiyo, kuna haja ya kuwa na mikakati kama nilivyotaja Wizara hizi mbili na hata hizi bei za nishati kama umeme kwamba ziangaliwe kwamba zinapungua ili kusudi watu wengi hata wa vijijini waweze kutumia ili kuokoa raslimali, miti ambayo inatumika kwa sehemu kubwa kwa ajili ya mkaa na kuni peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika nchi yetu, sasa hivi sehemu nyingi tayari wameshaanza kupata matatizo ya nishati ya kupikia. Mikoa ambayo sasa hivi angalau bado ina misitu inayoonekana ni Mkoa unaoongoza, kwa mfano Lindi, Pwani, Kigoma, Morogoro, Iringa, sehemu fulani fulani. Lakini ukiangalia Mikoa kama ya Mara, hakuna kabisa. Huko kuna matatizo ya nishati ya kupikia kwa wananchi wanaoishi vijijini. Kwa hiyo, kuna umuhimu sana, tena sana wa

kuweka mikakati kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kuna nishati ya kutosha kwa ajili ya wananchi kwa siku za baadaye. *(Makofi)*

Eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni ulinzi shirikishi. Wizara imetangaza na imeeneza neno hili juu ya ulinzi shirikishi na wananchi wameitikia sana na katika Wilaya yangu ya Kilolo, tuna hifadhi ya Udzungwa ambayo inazungukwa na Kata za Udekwa na Mahenge halafu kuna hifadhi ya milima ya Image katika milima ya Serebu ambako inazunguka na Kata za Ibumu na Kata ya Image watu wameshiriki sana katika ulinzi na utunzaji wa hifadhi hizi. Wamezuia moto, wanazuia majangili, lakini hakuna kitu chochote ambacho wao wananufaika na hifadhi hizi ambazo ziko katika maeneo haya, hata kuchangia katika shule tu ama madawati au barabara hakuna. Ningeomba sana Wizara iangalie uwezekano wa kuona kwamba wananchi wanaozunguka sehemu hizi ambao wanafanya kazi kubwa sana ya ulinzi kwa kweli na wao wananufaika na hizi raslimali ambazo ziko jirani yao.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Waziri ukurasa wa 28 ametaja juu ya uanzishwaji wa Wakala wa misitu, lakini wakala wa misitu pamoja na kuwa na nia nzuri haijaeleza kikamilifu madhumni yake ni nini. Nafikiri kuna haja ya wananchi kupata elimu zaidi wajue faida na hasara zake na kwamba wakala huu vyanzo vya fedha utatoka wapi? Kama watakuwa ni wakala wa misitu na tegemeo lao ni kuvuna misitu wauze ili wapate fedha kwa ajili ya kuendesha wakala, ni dhahiri kwamba hawa wataongeza hasara zaidi kuliko kuleta manufaa. Kwa hiyo, inahitajika elimu ya kutosha ili kusudi wananchi waweze kuelewa. Lakini vile vile kumekuwa na malalamiko ya kodi nyingi sana kwenye upande wa uvunaji wa mbao kwa ajili ya misitu.

Mheshimiwa Spika, kuna kodi kama *TFF* asilimia tatu, *CEZ* asilimia tatu, Safia asilimia mbili, *MLDA* Sh. 10,000/= na watu wanaona kwamba kwa kweli gharama ya hizi mbao inazidi kuwa juu na ndiyo maana siku za karibuni mbao zimekuwa zikiagizwa kutoka nje, zinatoka Mozambique na wanashindwa kumudu gharama ya mbao zinazopatikana hapa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ningependa kugusia tu juu uchimbaji wa *Uranium*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii nami nichangie Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Nianze tu na mimi kuunga mkono hoja suala la *concession fee* kama ambavyo Wabunge wengi wamesema humu ndani. *(Makofi)*

Nasema hivyo kwa sababu nimefanya utafiti na takwimu zinaonyesha kabisa kwamba Tanzania itakosa mapato takribani ya Shilingi bilioni 26 endapo utaratibu huu wa viwango hivi ambavyo vimewekwa havitatekelezwa. Lakini maana ni kwamba tutawapa watu wengine faida, lakini Taifa litaendelea kukosa fedha. Kwa utafiti uliofanyika ni kwamba kwa wiki ya kwanza ya Agosti, 2010 wakati kabla *concession fee* haijabadilishwa, taarifa za wenye mahoteli mathalan Ruaha walionyesha wamepokea wageni 256. Lakini baada ya utaratibu mpya wiki ya kwanza ya Agosti, 2011 watalii waliongezeka wakawa 478. *(Makofi)*

Maana yake wameongezeka watalii 242. Mapato yameongezeka kutoka Dola 5,119 mpaka Dola 21,300. Kwa hoteli ya Tarangire wiki ya kwanza ya Agosti, 2010 walikuwa watalii 1,030 baada ya utaratibu huu mpya wameongezeka wamekuwa 1,562. Mapato yametoka Dola 14,000 mpaka Dola 43,000. Serengeti kabla ya utaratibu walikuwa watalii 4,369. Sasa baada ya utaratibu huu ni 4,998 wameongezeka 599. Mapato yameongezeka kutoka Dola 47,000 mpaka Dola 264,000. *(Makofi)*

Sasa hata kama ni mradi, unaambiwa kwamba utakataa mradi tu endapo *NPV* inaonyesha ni *negative.* Lakini kama ni *positive* unaukubali mradi. Kwa hiyo, kwa *data* hizi inathibitika kabisa kwamba Waziri simamia uamuzi huu. *No research, no data, no right to speak. (Makofi)*

Kwa hiyo, hili linathibitisha kwamba uamuzi wa Serikali usimamiwe, hivyo na hao Serena na wenzake wanaendelea kuwashawishi Simba, sijui hao *Ranger, Sunny* na *Leopard Safaris* waache mara moja. Serikali muwe wakali kwa watu hawa kama wataendelea wanyang'anyeni leseni. Hatuwezi kuendelea kupoteza mapato kwa sababu ya kikundi kidogo tu cha watu kwa maslahi yao binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuweka sawa hilo. Lakini la pili ni kwamba nilikuwa naomba hawa *TANAPA* ndiyo wenye hizo mbuga za wanyama. Lakini utangazaji wanaachiwa Bodi ya Utalii. Kwa nini *TANAPA* wenyewe wasipewe kazi hiyo ya kutangaza? Wewe ndiyo mwenye biashara unampa mtu mwingine. Bodi hawa Watakuwa na visingizio leo mara hatukupewa fedha, hatukupewa hela za kutosha na nini. *TANAPA* wenyewe wapewe jukumu hilo la kutangaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna njia nyingi tu. Kuna kwenye ma-*blogue, Face Book* na kila kitu. Sasa twende na wakati. Ma-*TV* makubwa *CNN, Sky News*, huko kote tutangaze tusiwe na matangazo ya msimu. Rais alisema kubali kuliwa, ule. Kama hutaki kuliwa basi acha kula. Kwa hiyo, tangaza ili upate pesa. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, *TANAPA* wapewe jukumu hili la kutangaza hii biashara. Lakini pia na fedha wanazozipata *TANAPA* wa kutengeneza miundombinu na kusaidia mambo ya jamii. Kuna mabarabara katika Hifadhi, kuna huduma za jamii, nao *TANAPA* hizi fedha zitawasaidia sana katika shughuli hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nije katika Jimbo langu la Mvomero, hasa kwa suala la hifadhi ya Mikumi. Tuna kero kubwa ya wanyama kula mazao. Maana tukisema tembo sieleweki, niseme ndovu. Katika Vijiji vya Doma na Maharaka kumekuwa na tatizo hili kwa muda mrefu. Nimemsikia Waziri Maige anasema tutumie mafuta machafu, pilipili. Miaka yote hii tumeshajaribu kwani hamna utaratibu wa kuwazuia. Ni vyema kuweka utaratibu wanyama hawa wasifike. Mbona wanyama wakitaka kuhamia sehemu nyingine ama kutoka katika mbuga kuna utaratibu mnaoutumia wasiendelee kuhama? Basi tunawaomba muweke utaratibu wa kudumu wasiweze kuingia katika mashamba na kuharibu mazao ya wananchi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, lingine pia ni fidia. Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema wanyama wanakula ekari tano, unamlipa mtu fidia laki moja. Haitamsaidia. Nimeuliza hapa, wakasema kwamba kifuta machozi shilingi milioni moja, tena kimepanda. Nikauliza kama tembo mmoja raia akimwuua ni Dola 3,500 sawa sawa na Shilingi milioni tano. Sasa kifuta machozi kiwe Shilingi milioni moja? Tembo ukimuua Shilingi milioni tano, mtu akiuawa na tembo Shilingi milioni moja. Wapi na wapi? Naomba sana Serikali iliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba katika Kijiji na Maharaka, Waziri alianiambia kwamba suala la mipaka ameshashughulikia. Nakushukuru sana. Lakini, katoweni basi zile *beacon* kwa sababu wananchi wanaogopa. Hawana amani kwamba bado wako katika hifadhi. Kama mmeshakubali na mmeshaelewa kwamba mipaka mmeshaihamisha, basi mkayatoe yale mawe katika Vijiji vya Maharaka na Doma ili wananchi wangu wawe na amani na waendelee na shughuli za maendeleo. Lakini lingine ni ombi. Sisi tuko jirani, Vijiji vya Maharaka, Doma, tunawalindia ile mbuga. Lakini na nyie *TANAPA* basi tusaidieni huduma za jamii kama maji na hospitali katika Vijiji vya Doma na Maharaka. Ndiyo tunawalinda wale wanyama. Lakini Kijiji kinachofuata hakuna maji, hakuna Zahanati. Kwa hiyo, hilo tulikuwa tunaomba tuweze kusaidiwa.

Suala lingine ni hifadhi ya Wami Mbiki. Wami Mbiki imefika mpaka kwa rafiki yangu Mbunge wa Chalinze. Kwangu mimi imekuwa kero. Eneo kubwa liko Jimbo la Mvomero. Juzi tarehe 14 gazeti la Majira limeripoti kwamba askari wa Hifadhi wadaiwa kumuua mvuvi mto Wami. Alikuwa anavua. Mkazi wa Kijiji cha Kidudwe, wamemuua.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko juu ya suala hili, analichukuliaje? Askari wa Wami kujichukulia sheria mkononi na kuwaua raia! Hili suala hatutaweza kulivumilia. Kumekuwa na unyanyasaji, hawa askari wanapiga risasi ng'ombe za Wamang'ati

katika Vijiji vya Mziha, Mlumbiro. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko kuhusu matukio haya.

Mheshimiwa Spikak, pia lipo tatizo la mipaka katika Vijiji vya Mziha, Mlumbiro, Kunke, kote huko kuna tatizo la mipaka. Leo mnaambiwa mko kwenye hifadhi, mwaka mwingine mnaambiwa hamko kwenye hifadhi. Ardhi itahamaje? Leo mwaka huu, miaka mitano mko sawa. Miaka mitano hamko sawa. Naomba sana wananchi wa Vijiji hivyo nilivyovitaja, Vitongoji vya Njeula, Vitongoji vya Makwalu, Mafuleta, wote wanapata matatizo haya, Kaole pia. Naomba Serikali kupitia Wizara yako ikibidi twende mpaka Mvomero akaone haya maeneo na atoe kauli hapa kuhusu unyanyasaji huo unaofanyika sasa.

Mheshimiwa Spika, lingine nimalizie tu na suala la wanyama 166 kupotea. Nilikuwa naomba niseme haiingii akilini wanyama wanatolewa mbugani wanasafirishwa, njiani kuna *traffic,* njiani kuna ma-*gate*, kuna vizuizi mpaka akafika pale *Airport,* wakapakiwa, kuna kila aina ya ulinzi jamani. Haiingii akilini, kuna maswali mengi kuhusu kwa wanyama 166. *(Makofi)*

Rada pale ipo. Kama wale ni wanyama na utaratibu wa ndege kutua na kuondoka upo, imebeba nini? Kwa hiyo, tunaomba maelezo, Mheshimiwa Waziri utueleze suala hili lilifanyikaje? Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Shibuda...

**MHE. MAGALLE J. P. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Magalle Shibuda, ngoja. Mbona una haraka? *(Kicheko)*

Atafuatia Mheshimiwa Said Arfi na Mheshimiwa Cynthia Ngoye pia atapata nafasi.

**MHE. MAGALLE J. P. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii. Kwanza naomba radhi kwamba asubuhi sikuwepo kwa sababu nilipitia hospitali, shingo inanisumbua kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa juhudi zote zilizochukuliwa na Serikali na vile vile kwa juhudi na Mheshimiwa Rais hadi akashiriki katika maziko ya ndugu yetu, shujaa na mpiganaji wa nchi yetu, Luteni Generali Mayunga. Nawashukuru sana kwa wote mlioshiriki. *(Makofi)*

Shukrani za pekee pia napenda kuzitoa kwa Wabunge wote na Bunge pamoja na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika kwa pole ulizotoa. Napenda kusema tu kwamba shukrani zangu hizi ninazozitoa, basi zipokelewe na wale wote walioshiriki kwa hali na mali utu na ubinadamu katika hayo maziko. Nasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, naomba sasa nijielekeze katika hoja ambayo ni ya mambo ya uchumi kwa maslahi ya Taifa letu, hii Wizara ya Maliasili. Nasikitika kusema kwamba hivi sasa Tanzania imekuwa kama tunda pori, halina mwenyewe. Utakuta kwamba inashangaza sana kwamba uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Tanzania pale kuna Afisa Usalama, kuna watu wote. Je, taarifa za ki-inteligensia zilikuwa wapi wakati mali yetu inakusanywa hadi inasafirishwa? Hii ni kudhalilisha Idara ya Usalama wa Taifa. Ni kudhalilisha Polisi. Ni kudhalilisha mambo mbalimbali yanayohusu usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba tuhakikishe ya kwamba Serikali na Viongozi Wakuu wakubali kuambiwa na wasing’ang’anie ujuzi wa madaraka yao kwamba ni silaha na nyenzo ya kuziba masikio. Nasikitika sana kusikia ya kwamba Ngorongoro kunataka kufanyika ujenzi wa hoteli kinyume na matakwa ya kuhifadhi maliasili. Nawaomba viongozi wa kisiasa wenye dhamana mbalimbali wa thamini michango ya mawazo ya wataalam wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Inasikitisha sana kwamba Mheshimiwa Pius Msekwa namheshimu sana, mzee wangu, kaka yangu. Natambua historia yake ya mchango katika Taifa hili. Je, kwa nini Mheshimiwa Msekwa

ameamua kuvunja hayo? Ni lazima tuibue udadisi wa kutambua chanzo cha kusababisha mstaafu aliyewahi kuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, aanze kuvunja uaminifu na utiifu wake na uzalendo wake kwa Taifa letu. Lazima kuna sababu.

Mheshimiwa Spika, ninaweza nikasema kwamba maslahi binafsi ya wastaafu yanahitaji kutazamwa upya. Kwa sababu mifumo ya choyo kwa maslahi ya watumishi ndiyo inayozalisha watu hasa Mabalozi na Magenerali kuwa watu wanaolazimishwa kuwa mawakala na makuwadi wa watu wanyonyaji na wadhulumaji kwa maslahi ya nchi yetu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, thamani ya utiifu na uzalendo wa Watanzania hao inapata vishawishi. Hivi vishawishi napenda kusema kwamba kuwepo uzalendo, uaminifu na utiifu hupikwa na unarutubishwa, ikiwa *TRA* wana mishahara mikubwa na Benki Kuu. Naomba Idara zote ziliko katika Wizara ya Maliasili na Utalii mhakikishe maslahi ya watumishi yanakuwa endelevu ili na wao wasiwe na fikira za kutanga tanga. Ndiyo maana nilikuwa nazungumzia sana ujira wa mwia, hutuliza fikra za watu watumikie na wahakikishe ya kwamba hawatangitangi. *(Makofi)*

Vile vile napenda kusema ya kwamba tung'arishe viongozi wetu wasiwe na masuala ya matatizo. Nasikitika kusema kwamba hivi sasa mfumo uliopo na kama tutaamua kweli wazalendo watumikie nchi yao, hata sisi Wabunge tunapomaliza Bunge hapa, huwa tunaanza kutafakari. Nikienda Jimboni, Mbunge maskini anatumikia watu maskini. Nani sasa wa kumbeba mwenziwe? Mgonjwa kumhudumia mgonjwa mwenzake haiwezekani. Kwa hiyo, nakuomba na wewe Mheshimiwa Spika, ujali maslahi ya Wabunge, tusimamie. Tusiwe na fikra za kutangatanga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, waliowauza hawa ndugu zetu kwenda utumwani walikuwa machifu na manamba, waliowauza Watanzania kuwa watumwa ni machifu na manyapara. Je, aliyeuza raslimali zetu hizi za wanyamapori, ana cheo gani? Misaada ya kuongeza juhudi ni bakshishi au ni nusu kaputi? Nashangaa sana Mheshimiwa Maige, naomba ku-*declare* ni mjukuu wangu kwa mila za Kisukuma. Unapongezwa kwa kitu gani hasa? Hustahili kupongezwa hadi wanyama hawa watakaporudi. *(Makofi)*

Kila palipokuwa na huzuri pana dosari. Dosari hii ya wanyamapori kutokea katika kipindi chako ni dosari. Ni dosari kwa Rais wetu, ni dosari kwa Waziri Mkuu, ni dosari kwa vyombo vya usalama wa Taifa.

Kwa hiyo, hili ni lazima lifanyiwe kazi. Vile vile napenda kusema kwamba wawekezaji wanaokuja ni sawa sawa na mboga ya kuazima haitoi kiu ya njaa. Wakati umefika *TANAPA* sasa mapato yake pamoja na Ngorongoro yaboreshe utamaduni wa ndani. Kwanza kabisa utamaduni wa ndani *TANAPA* na Ngorongoro washirikiane wakaboreshe kwa Baba wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ukienda pale kwa Baba wa Taifa watu wana hamu ya kujua Baba wa Taifa hata Wanasayansi walikuwa wanasema hiki kichwa tukipeleke maabara tukakifanyie utafiti maalum huko Ulaya. Sasa tunaomba Watanzania tuenzi utamaduni wa ndani, kuna machifu. Kuna historia zetu hata Maswa-Malampaka tunawaomba mwende. Kuna maeneo ambapo binadamu alikuwa mchawi amekanyaga mguu wake anaitwa Mwana Malundi.

Wako wazee ambao wana mambo mazito. Sasa msing'ang'anie hizi pesa za *TANAPA,* pesa hutafuta pesa. Basi mhakikishe sasa katika utamaduni wa ndani mnashiriki kuuboresha. Naomba vile vile Serikali sasa hivi inazungumzia maliasili. Jamani, pamba ni maliasili. Kwa hiyo, bei ya pamba ni maliasili ndiyo utalii kwa mkulima wa pamba.

Nimesikia Waziri Mkuu alivyoulizwa leo asubuhi. Sasa nawaomba mkamwambie Mheshimiwa Waziri, Wasukuma walima wa pamba na Mikoa 14 na Wilaya 43 utalii kwao ni bei ya pamba. Yaliyozungumzwa hapa siyo kauli elekezi. Baada ya Waziri wa Kilimo kutamka kwamba bei ya pamba ni Sh. 800/=, wamedhulumika, kuna mapunjo. Tunataka kauli elekezi Waziri Mkuu atoe, aseme ni nani anatakayesimamia makusanyo ya mapunjo walipwe wakulima wa pamba? Zao la pamba ni tofauti na korosho. Kila mwaka lazima ulime. Ni tofauti na pamba, shuruba yake ni kubwa. Hiyo ndiyo maliasili na utalii wa mkulima wa pamba*.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maliasili nyingine ni mifugo. Wanyamapori hata mifugo walikuwa wanyamapori. Lakini nashangaa Mheshimiwa Waziri wewe umechaguliwa, unajua dhiki ya Wasukuma wafugaji wanahamahama, *TANAPA* jengeni mabwawa. Mnapanua hifadhi, hampanui mabwawa, kwa nini? Wamasai wanahangaika, Wamang'ati wanahangaika, Wasukuma wanahama, tunatafuta maji. Kaa na Wizara ya Mifugo na *TANAPA* mchangiane mkajenge mabwawa. Maswa wanahitaji mabwawa sita haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliona hayo niyaseme ya uzalendo. Nilipokuwa kwenye msiba vile vile nimepata mtihani mkubwa sana wa kuulizwa maswali kuhusu hatima yangu katika CHADEMA. Hili vile vile nadhani ni bora nikalizungumzia, kwa sababu...

**SPIKA:** Na wenyewe ni utalii?

**MHE. MAGALLE J. P. SHIBUDA:** Nao ni utalii na maliasili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maliasili kwa nchi yetu ni siasa bora na utawala bora. Hiyo ni ya kwanza. Kwa hiyo, niliona hilo nilizungumze. Viongozi wa dini kazi yao ni kung'arisha binadamu ili waweze kwenda Ahera. Viongozi wa kisiasa kazi yao ni madobi wa kung'arisha Serikali.

Kwa hiyo, niliona hili niliseme kwa sababu wananchi wa Maswa na Watanzania wengi hata nyinyi Wabunge kila saa wananiuliza: Vipi Kamati Kuu wamekuita? CHADEMA wamekufukuza? Itakuwaje? Basi naomba niseme machache kwa sababu kauli zilizotolewa na kunukuliwa na magazeti ni kauli hatarishi. Kwanza napenda kusema jukwaa la Vyombo vya Habari nawatahadharisha viongozi wote, lina mazuri na mema yake. Apendaye kutumia jukwaa la siasa kwa fitina ni sawasawa na mtu fitina, hafi mpaka fitina imerejea kwake.

Ni mfumo rafiki kujali, kutumia vyombo vya habari, lakini napenda kusema kauli za kukwazana kupitia vyombo vya habari, pia inahatarisha na ukificha ukweli, unakaribisha mikosi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema ya kwamba maneno yaliyonukuliwa ya viongozi wa CHADEMA katika vyombo vya habari kwamba mimi msaliti! Nawaambia Watanzania, sio msaliti, wala sijavunja msimamo wa uongozi wa Kikao cha Kamati, nimetofautiana na watu kwa dhamana zao binafsi na ni haki. Mimi siwezi kugandishwa na nikose demokrasia ya Kikatiba kutoa maoni yangu. Kwa hiyo, yeyote ambaye anageuza kutumia cheo chake kwa maslahi binafsi, hatokuwa tofauti na Mzee Msekwa, anayetumia maslahi yake kuharibu Ngorongoro. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mazuri huwa ya baba, mabaya huwa ya mama na bahari ikichafuka, nahodha hupimwa ujasiri wake. Kweli nakiri pana kuchafuka hali ya hewa, lakini napenda kuwaambia Shibuda ni jasiri na Maswa sio tunda pori! Lina wenyewe na wananchi wa Maswa wanasubiri na wamekataa kuwa malighafi ya kuporwa kama wanyamapori kuhusu Mbunge wao. Napenda kutumia maslahi mapana ya Chama cha CHADEMA, Chama cha Mapinduzi kina historia ya demokrasia pana na vilevile Chama cha CHADEMA ni kwa maslahi ya jamii, lakini kila kizuri hakikosi kasoro. Upande huu kuna kasoro na upande huu kuna kasoro! Lakini hekima na busara ndio itakayotuongoza tufike salama. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, uongo humiliki akili za watu ambao wametaharuki na watu ambao mitazamo yao ni ya kuwa makuwadi wa maslahi binafsi ya mtu ambaye anamkuwadia. Kwa hiyo, ninapenda kusema ya kwamba sina makuzi hayo, mimi simkuwadii mtu! Na vyombo vya habari ninawaomba ya kwamba mnaweza kutuzalishia Idd Amin! Nawaomba vyombo vya habari kila mnapoandika, msiandike kwa ushabiki wa mivumo ya kisiasa, kuweni makini! Nawaomba na wahariri vilevile, kama ninyi mtashabikia na kuandika kwa hisia na tafsiri za maslahi binafsi na miegemeo ya fikra zenu, mtatuzalishia viongozi Idd Amin kuongoza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tupo wanasiasa wenye wito wa kutumikia jamii na wapo wanasiasa maslahi binafsi, kwa hiyo, ni lazima mchanganue. Watafiti vilevile napenda kuwaambia ya

kwamba mtafiti na mtafsiri mambo kutokana na hali halisi. Tuna mifumo ya vyama vya kisiasa, tumo zaidi ya 12! Kuna vyama maslahi binafsi, maslahi jamii, ushirika, *SACCOS!* Mchambue wenyewe muwaambie Watanzania maslahi yapi ni chama gani? Kauli na vitendo, vinathibitisha hayo. Yesu alituhumiwa na kusulibiwa na akadhalilishwa, mimi Shibuda kudhalilishwa na kupuuzwa na mtu sijali sana kwa sababu tabia zangu za mtu wa peponi na uwazi na ukweli ndio unaniongoza, dini yangu inanizuia kusema uongo! Kwa hiyo, nasikitika kwa mtu ambaye ninamkwaza! Na hususan masikio ya mtu dhulumati, hayapendi ukweli! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusema bora huchagua viongozi na ibilisi pesa huteuwa viongozi! Watanzania tunawafahamu waliochaguliwa na Mwenyezi Mungu kuwa viongozi! Na wengine ni wa ibilisi pesa, wakateuliwa kuwa viongozi. Sasa mnaoshika dhamana za uongozi, angalau muache dhambi zenu sasa mtumikie jamii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakutakia kila la heri, nashukuru, na ninapenda kusema tu, matarumbeta na mavuvuzela waniache kwa usalama. Amina! *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na mimi kunipa fursa nami niweze kuchangia katika hoja ambayo iko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya maliasili na utalii ni sekta muhimu sana katika kukuza na kuendeleza uchumi wa Taifa hili. Lakini sekta hii ina vikwazo na changamoto nyingi. Nikirejea hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 49, anazungumzia changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Anasema uvunaji haramu na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za maliasili na mali kale na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa! Nataka nizungumzie maeneo yaliyohifadhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, alikuwa akieleza madhila na taabu wanazopata wananchi wa Urambo Magharibi, kwa sababu ya maeneo yaliyohifadhiwa. Maeneo haya yamehifadhiwa kwa muda mrefu sana. Wakati maeneo haya yanahifadhiwa, idadi ya watu katika nchi hii ilikuwa chini ya milioni 10! Idadi ya watu imekwenda imeongezeka, hakuna marekebisho yaliyofanywa, vijiji vimeanziswa, vimesajiliwa na vina uongozi. Na vijiji hivi wakati wa uchaguzi vimekuwa vikitoa kura kwa vyama mbalimbali na viongozi waliopatikana ambao leo ni viongozi katika nchi hii, wametokana na kura za watu ambao wanakaa ndani ya vijiji vilivyomo ndani ya hifadhi. Maeneo ya migogoro ya hifadhi yapo katika maeneo mengi na hususan katika Wilaya ya Mpanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mpanda 63% ya eneo lake ni misitu, na misitu hii imehifadhiwa, ama ni hifadhi za misitu, ama ni *controlled areas,* ama ni *game reserve,* ama ni *National Parks,* ama ni maeneo ya uwindaji wa kitalii. Maeneo yote yamemilikiwa na yanahifadhiwa, wananchi hawana maeneo! Wamekuwa na matatizo, wanalazimika kuingia katika maeneo yaliyohifadhiwa, wanaendeleza huduma zao na haki zao za kibinadamu ili waweze kuishi. Serikali bila huruma inawafunga watu hawa, Serikali bila huruma inachoma nyumba zao, matukio yaliyotokea Urambo, yametokea Mpanda pia! Mifugo inapigwa risasi! Hali hii haiwezi kuendelea kuvumilika! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Watanzania wanateswa ndani ya nchi yao! Wanafukuzwa ndani ya maeneo ambayo wanasema yamehifadhiwa! Maeneo ambayo yako wazi, badala ya Watanzania hawa maskini wanaohangaika wakapelekwa huko, wanatafutwa wazungu sasa wanaletwa wanakuja kumilikishwa ardhi, hatukubali! Ni lazima kwanza Watanzania ambao wana tatizo kubwa la ardhi, wawe wamepata ardhi na wamemilikishwa ardhi, kisha ndio tufuikirie kuwaleta wageni na kuwapa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wala tusijidanganye ndugu zangu kwamba leo tunayo ardhi ya kutosha na tunaweza tukawaita wawekezaji. Tunajidanganya kwa kutazama tafsiri ya uwekezaji kwamba ndio suluhisho pekee la kutuletea maendeleo katika nchi hii! Tunarudisha ukoloni sisi wenyewe ambao tupo huru na tunawakaribisha wakoloni waje watutawale tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunasema tunayo ardhi kubwa na mpaka sasa tumeanzisha benki ya ardhi, ardhi ipo wapi? Katika Tanzania leo, ukiangalia ongezeko la watu, takribani kila mwaka ni watu 800,000 wanaongezeka. Ndani ya miaka 20 ijayo, katika nchi yetu wataongezeka Watanzania milioni 16! Mnawapeleka wapi ardhi mnaigawa hivyo? Hatukuwapa madaraka, hatukuwapa mamlaka ya kuuza nchi yetu ya kuigawa nchi yetu mnavyotaka! Mmepewa dhamana ya kulinda na kuiendeleza na sio kwa kisingizio kingine chochote. Maendeleo ya nchi yetu yataletwa na watu wetu wenyewe. Ni kuwawezesha Watanzania wenyewe ili waweze kujiletea maendeleo na wala kamwe! Kamwe! Wageni hawawezi kutuletea maendeleo, wanakuja kwa ajili ya kujinufaisha wenyewe, hili ni lazima mlitambue na mliweke akilini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wazungu mnaowaleta mnasema watakuja kuzalisha chakula, Watanzania wanajilisha! Juzi nilikuwa nasikiliza Taarifa ya Habari ya *TBC,* Songea kuna tani 51,000 za mahindi mmeshindwa kuzitoa! Sumbawanga mahindi yanaoza, Mpanda mahindi yanaoza! Leo mnamtafuta Mmarekani mje mumpe ardhi yetu Mpanda, haiwezekani! Ni sisi wenyewe tuangalie ni namna gani sasa tunaweza kuwawezesha Watanzania wakazalisha chakula chao, hatuhitaji mzungu aje atuzalishie chakula. Leo ndugu zangu, kila anayepita kuelekea Dar es Salaam, hapa hapa Dodoma, matrekta yamerundikwa pale! Yanapigwa vumbi, yanaota jua! Kwa baridi ya Dodoma, yameanikwa pale juani. Matrekta yale, leo yalikuwa yanatakiwa ama yawe Wilayani, ama Mikoani au yawe tayari yamewafikia wakulima! Hayakuletwa kwa ajili ya kuja kuoneshwa kama maonesho! Yameletwa kwa ajili kuja kubadilisha hali za Watanzania maskini. Matrekta yale yamekopwa, watakaolipa mkopo ule ni Watanzania wenyewe! Leo zaidi ya miezi tisa, Serikali hii inashindwa kupanga bei ya matrekta yale! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kweli mna nia ya kuwaondoa Watanzania kwenye umaskini? Tutabakia tunazunguka katika duara la umaskini Watanzania, kwa uongozi huu! Uongozi ambao unafikiri kwamba wazungu watakuja kututoa katika umaskini! Tunajidanganya ndugu zangu Watanzania! Na hasa pale tunapofikiria kuwapa wageni ardhi yetu kwa zaidi ya miaka 99! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka 99 wewe hautakuwepo! Mimi sitakuwepo! Wabunge wote waliopo humu ndani hawatakuwepo, watoto wetu hawatakuwepo! Hata mjukuu wangu anayezaliwa leo, miaka 99 ijayo hatakuwepo! Tunabeba dhambi kubwa sana viongozi wa leo katika kutaka kuuza ardhi ya Watanzania. Hatukubali ardhi ikauzwa! Machafuko yanayotokea katika dunia sababu ni ardhi! Vita ya Maumau mwaka 1958 ilikuwa ni ardhi! Wakenya wale walinyang’anywa ardhi yote yenye rutuba wakaichukua wazungu! Wakaingia misituni kwa ajili ya kudai ardhi yao mwaka 1958, ni juzi juzi tu msisahau, historia inakumbusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mugabe ana matatizo, wote tunatambua! Lakini viongozi wetu wanafumba macho wanataka waturudishe huko! Tuna tatizo la wafugaji wetu, wanaharibu nchi yetu, wana ufugaji wa kuhamahama kutoka eneo noja kwenda eneo lingine. Na wala hawaoni shida wafugaji hawa kuharibu ardhi kwa sababu, hawana ardhi. Wamilikisheni wafugaji ardhi, wataitunza hiyo ardhi! Lakini kama mfugaji hana ardhi, hana eneo la malisho, atahama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine na uharibifu wa mazingira utaendelea katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima sasa tubadilike na mifugo hii iweze kuwa ni rasilimali katika nchi hii, iweze kuongeza Pato la Taifa! Na tutalipataje, ni lazima tuwaweke wafugaji katika maeneo mahsusi, tujue idadi ya mifugo iliyopo katika eneo lile, malisho yaliyopo pale, ili rasilimali ya mifugo iweze kuvunwa na kuendelezwa, lakini bila mipango thabiti wafugaji wataendelea kuhamahama, nchi yetu itaendelea kuharibika, wataingia kwenye hifadhi, askari wa hifadhi wanaua mifugo ya wafugaji! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie Hifadhi ya Katavi, juzi nilikwenda Katavi, hali ni mbaya sana ya ukame. Nimeona *TANAPA* ina mpango wa kujenga mabwawa, harakisheni kujenga mabwawa Katavi, viboko wanakufa, mamba wanakufa, hakuna maji kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa *Ubende Wildlife Management Area.* Eneo hili wananchi hawakatai, tatizo ni mipaka! Mmepora ardhi yote ya wananchi wa eneo hilo, Kata 11! Mmewanyang’anya ardhi yao! Hawana mahali pa kulima! Ni lazima kama kweli Serikali hii ni sikivu,

nimelisemea mara kadhaa katika Bunge hili, nimepewa ahadi na Serikali kwamba, mtalishughulikia, mpaka leo wananchi wameshakata tamaa juu ya Serikali hii. Ni Serikali inasikia Serikali inayosema, Serikali ambayo haiwezi kutekeleza na kutoa maamuzi! Toeni maamuzi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja iliyowasilishwa mbele yetu kwa mia kwa mia na kuwaomba Wabunge wenzangu tumpe nafasi kijana mwenzangu, aweze kufanya kazi aliyoaminiwa na Mheshimiwa Rais. Kwa kuwa muda bado anao mrefu kwa hiyo, ninaamini kwa namna moja au nyingine atafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wetu wa Pwani, tunayo maeneo ambayo yamezungukwa na Mbuga ya *Selous,* tunayo maeneo ambayo yamezungukwa na Hifadhi ya Saadani. Maeneo hayo kuna migogoro ya mipaka hasa katika maeneo ya Kata ya Mwaseni, Wilaya ya Rufiji na migogoro hiyo imesababishwa na Wizara ya Maliasili na Utalii ya kuongeza eneo ola hifadhi. Sasa tatizo kubwa ninaloliona mimi ni kutoshirikishwa wananchi. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba wananchi hawa wangeshirikishwa, migogoro hii ingepungua kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niiombe Wizara ijitahidi kuwashirikisha wananchi wa maeneo yanayozunguka hifadhi, wakati wakifanya maamuzi ya kuongeza eneo la hifadhi. Migogoro hii inasababisha wakati mwingine wananchi kupata madhara makubwa, kuna tuhuma zingine wananchi wamepoteza maisha kwenye maeneo hayo na hasa eneo la Wilaya ya Kisarawe, Vikumbulu, wapo wananchi wameuawa na askari wanyamapori kwa kuwa tu waliingia kwenye maeneo hayo ya hifadhi kufanya shughuli mbalimbali za kujipatia riziki! Kwa kweli kwa kuwa wananchi hao wapo kwenye maeneo haya, na kama walivyosema Wabunge wengine kwamba vijiji hivyo viliandikishwa na Serikali kwa Sheria, kwa hiyo, ni wazi kabisa kama kuna maamuzi ya kuongeza maeneo hayo kuwa Hifadhi na kwa maslahi ya nchi yetu, basi Serikali ingeliangalia vizuri zoezi hilo kuona athari zake na kuona mapungufu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningeomba nichangie, ni namna gani Mashirika haya ya Hifadhi (*TANAPA* na Ngorongoro) yanavyochangia shughuli mbalimbali za maendeleo. Nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba Mashirika haya kwa mfano *TANAPA* yamekusanya zaidi ya bilioni 94! Lakini katika hotuba hiyo, wameeleza kuna shughuli za maendeleo wanafanya katika maeneo hayo, lakini ningeomba wangeainisha ni shughuli gani? Hata kwenye kiambatanisho, shughuli gani zimefanyika, kwa sababu kwa maeneo yetu, kwa mfano maeneo ya Kata ya Mkange, Kijiji cha Matipwiri kule Saadani, Gongo, kuna changamoto kubwa. Hamna Kituo cha Afya, kuna tatizo kubwa la maji, hamna Zahanati, lakini hizi mamlaka zetu zinakusanya mapato mengi lakini hatuoni jitihada zozote! Pamoja na kuwa yapo maeneo machache wanafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kungekuwa na uwazi zaidi ni kiasi gani wametumia na kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa jana *TANAPA* imetoa bilioni tatu tu! Sasa bilioni tatu kwenye bilioni 94! Pamoja na kuwa tunajua wana kazi ya kuhifadhi mazingira hayo, lakini itutazame wananchi tunaozunguka maeneo hayo. Kweli bilioni tatu, kwa maeneo yote yanayozungukwa na hifadhi hizo kwa ajili ya shughuli za maendeleo! Kwa kweli naona kwamba ni tatizo kidogo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuzitaka mamlaka hizo zichangie kwenye Pato la Taifa. Kwa kuwa zinakusanya mapato kwa kiwango kikubwa, lakini pia inaonekana hizi mamlaka zetu kwa kweli, kiwango kikubwa cha mapato kinatumika kwenye safari, posho, posho za vikao! Kwa hiyo, ni wazi Serikali kuamua Mashirika haya yachangie walau 10% si jambo baya, pengine ikae tena na Mamlaka hizo kuangalia kama ni kiwango kikubwa labda kipunguzwe. Lakini kwa kweli Waheshimiwa Wabunge, tuliunge mkono kwa sababu Serikali yetu ina mambo mengi ya kufanya na tunajua kwamba sungura anasemekana ni mdogo. Sasa kama

haiwezi kutumia vyanzo vyake yenyewe inaweza ikawa Serikali ambayo inategmea Bajeti tegemezi, jambo ambalo tunalipigia kelele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninaomba niliunge mkono ni suala la kuongeza tozo, uamuzi ulioufanya Mheshimiwa Waziri ni mzuri. Naomba hao wamiliki wa hoteli hizo walipe! Walipe ile $40, hivi kweli $40 kwenye $500 mpaka $1,000 kwa chumba ni kiasi gani? Hivi kweli hawa wapo juu ya Sheria? Hivi ni kwa nini nimeona ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu zaidi ya bilioni 19 hazikukusanywa kwa sababu tu kukubaliana nao kurejesha kiwango cha zamani. Kiwango cha tangu mwaka 1990! Zaidi ya miaka 20 sasa hivi! Bado kweli kina-*suit* katika ulimwengu wa sasa hivi wenye changamoto mbalimbali! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninadhani muda wa kuwabembeleza umekwisha! Hawa watu wachukuliwe hatua kali! Tena sasa hivi hizo leseni wanyang'anywe! Kwa kweli sisi tuna changamoto nyingi katika maeneo hayo ambayo tumepitiwa na hifadhi kama nilivyosema. Nafikiri kupitia tozo hii inaweza ikatusaidia, leo tunalalmika *TANAPA* haichangii vizuri au Ngorongoro haichangii vizuri, lakini kwa nini? Wao wanagoma! Kwa hiyo, mimi ninampongeza Waziri, kaza buti, uamuzi ni ule ule, wembe ni uleule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni uharibifu mkubwa katika misitu yetu. Kwa kweli, hapa ninaomba niseme kuna baadhi ya watendaji wa Wizara hiyo, hasa Maafisa Maliasili katika Wilaya zetu mbalimbali, kwa kweli kwa kiwango kikubwa wanachangia. Maafisa Maliasili wapo, lakini unaona kabisa uharibifu mkubwa katika misitu yetu, hawasimamii Sheria! Mfano, msitu wa Kazimzumbwi, upo pale, sasa hivi umeharibika badala yake umeleta matatizo ya tabia ya nchi katika maeneo ya Kisarawe, hata huko Saadani ninakokusema. Lakini Maafisa wa Maliasili wapo wanaona! Lakini wengine wanajihusisha na biashara ya mbao, kwa hiyo ndio hao hao! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachomuomba Mheshimiwa Waziri, atazame kwamba wapo watendaji wenye nia ya kumuangusha, angaalie hiyo Idara ya Maliasili kwa kina pia niungane na Mheshimiwa Msolla, kwamba hii Wakala wa Maliasili inayoanzishwa ingeainishwa vyanzo vyake vya mapato vitakuwa vya namna gani. Isiwe kama wakala huo inaongeza matumizi maana tumeona *experience* ya kuanzisha wakala mbalimbali, inakuwa gharama kubwa sana, matumizi yanaongezeka, lakini hakuna kinachopatikana. Isijekuwa kuanzishwa kwa wakala huu ikaongeza matumizi ya maliasili zetu! Ikaongeza matumizi hasa katika hiyo misitu! Kwamba misitu ivunwe ili ipatikane pesa kwa ajili ya kuendesha wakala huu. Kwa hiyo, niiombe Serikali iwe makini sana wakati inapoanzisha wakala. Pamoja na kwamba ina nia nzuri lakini pia ipime faida zake na hasara zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine labda kwa kumalizia, naomba niwaongelee wananchi wa maeneo ya *Delta,* Mkoa wa Pwani ambao wapo katika Wilaya za Rufiji hasa katika maeneo ya Salale, Kiongoroni, Mbuchi, maeneo yale Mheshimiwa Waziri, hawana maeneo kabisa ya kulima. Kata hizo zimezungukwa na visiwa na kulikuwa na amri ya Serikali ya kuwazuia kulima kabisa. Sasa mimi nimesikia kwamba Mheshimiwa Waziri, umeridhia wakati uamuzi huu ulitoka waliambiwa haraka sana wahamishwe, watu wamekaa kule zaidi ya miaka 40, 50, wapo katika mazingira magumu lakini waliambiwa wahamishwe hata kabla hawajavuna mazao yao! Nikushukuru tu kwamba umeongeza muda au umetoa pendekezo kwamba, pengine Serikali mlitazame upya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mlitazame upya, wale wananchi hawana maeneo ya kulima! Hawana kabisa, wakivua mnasema nyavu zao hazifai! Wale Maafisa Maliasili wa maeneo yale, wanawapiga sana kwenye masuala ya mikoko! Tunathamini kweli jitihada za Wizara za kuongeza mapato katika masuala ya mikoko na uhifadhi wa mazingira, lakini hebu tuwatazame mazingira yao! Mheshimiwa Waziri, nitafurahi sana kama utafanya ziara kuja kabisa maeneo yale uone mwenyewe ujiridhishe kwamba hivi maamuzi haya yatajenga? Kwa sababu yametuweka wakati mbaya sana sisi! Tena yalitokea karibu na kipindi cha uchaguzi! Kwa kweli tumeathirika kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kuunga mkono hoja na kuomba kwamba suala la utoroshwaji wa wanyama, walivyosema wenzangu, warejeshwe haraka iwezekanavyo! Kama

kuna Tume imeundwa, ifanye kazi haraka sana, na kama kuna tuhuma ambazo zimejitokeza humu, zifanyiwe uchunguzi. Wabunge wanaposema ninaamini wanakuwa wengine wana ushahidi, lakini pia wanaielekeza Serikali kwa nia njema. Kwa hiyo, ninaomba kama kuna watu walihusika katika Idara hiyo ya wanyamapori basi wajulikane wachukuliwe hatua ili wananchi waendelee kuwa na imani na Serikali yao. Kwa sababu tunaamini kabisa wanyama wale waliotoroshwa ni rasilimali yetu ambayo inaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, lakini nimalizie nimeona kuna baadhi ya taarifa za fedha za Wizara hii, hoja ambazo zinasababisha upotevu wa mamilioni ya pesa kwenye taarifa ya Kambi ya Upinzani iliyowasilishwa, hasa eneo la misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tozo ambayo ilikuwa chini ya Kanuni na Sheria zilizowekwa na badala yake milioni 824 hazikukusanywa. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kwenye majumuisho atoe taarifa, Serikali imefikia wapi katika kuhakikisha kwamba zile hoja zimejibiwa, lakini pia kuwachukulia hatua endapo itathibitika watendaji katika Wizara yake wanazembea na kusababisha hoja nyingi na nyingine zinaashiria matumizi mabaya ya pesa za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuunga mkono hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, ushiriki wa wakazi wa karibu na vivutio vya utalii katika shughuli za kibiashara haupo. Kuna sehemu za vivutio vya utalii kama Mapango ya Amboni Tanga, ambazo viko karibu na makazi ya Wananchi. Je, Wizara haioni ingekuwa vizuri wakazi hawa wakaruhusiwa kushiriki katika mambo ya biashara ya huduma za msingi katika sehemu za vivutio hivyo?

Pale Amboni Wananchi wangeweza kuwezeshwa au hata kuruhusiwa tu kutoa huduma za migahawa na pia kuuza bidhaa za vivutio.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tanga na Wilaya ya Pangani ina vivutio vingi vya Kumbukumbu za Kale ambazo haionekani kutunzwa ipasavyo na kutangazwa ipasavyo ili kuvutia Watalii wengi na kuliongezea Taifa kipato. Naomba Wizara ilishughulikie hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, shukrani za dhati na zito kwa Mheshimiwa Ezekiel Maige, ambaye ni Waziri wa Wizara hii, pamoja na Menejimenti ya Utawala, kwa kuandaa hotuba nzuri, ambayo tunaijadili hapa Bungeni. Shukrani nyingine nazitoa kwa Katibu Mkuu wa Wizara, hii Bibi Maimuna Tarishi na Naibu Katibu Mkuu, Bibi Nuru Millao, kwa uongozi wao makini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa mia moja. Katika kuijadili hoja hii, mchango wangu nitauelekeza katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu *concession fees*; napenda kuchukua uamuzi wa dhati, kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri, kwa kuchukua maamuzi magumu ya kutaka tozo hizi zifanyike kwa kufuata viwango vya asilimia. Inasemekana kwa dhati kuwa, Serikali imekuwa ikipoteza takriban Shilingi 27,000,000,000 kwa kutokutoza malipo hayo kwa njia hii. Hivyo, nasisitiza Serikali iendeleze mpango huu na wala isirudi nyuma ili kuongeza mapato katika Sekta hii ya Utalii. Imedhihirika wazi kuwa, malipo kwa njia ya asilimia maalum ya viwango kwa muda wa siku saba tu yaliongezeka karibu asilimia 460 katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, kwani mwaka 2010 zilikusanywa US$ 47,342, lakini mwaka huu katika kipindi hicho hicho zimekusanywa US$ 264,935. Hifadhi ya Ruaha kwa mwaka 2010 zilikusanywa US$ 5,119 lakini mwaka huu zimekusanywa US$ 21,300 na Tarangire mwaka 2010 zilikusanya US$ 14,358 lakini mwaka huu zimekusanywa US$ 57,800. Makusanyo hayo ni kutoka tarehe 1 – 7 Julai, yaani kwa muda wa siku saba tu kwa mwaka 2010 na siku saba tu kwa mwaka 2011. Hivyo, kwa kulinganisha takwimu hizi ni dhahiri kuwa utajiri wa asili wa nchi hii unaporwa bila aibu!

Mheshimiwa Spika, namshauri Waziri pamoja na Wizara yake, kuchukua maamuzi magumu juu ya Kampuni za *Tour Operators* ambazo hazikubaliani na utozo wa ada ya kitanda (*Concession Fee*), kwa misingi ya viwango vya asilimia. Makampuni hayo ambayo mengi huendeshwa na Wahindi ni kama vile *Ranger Safaries, Leopard Tours, Sunny Safaris* na *Simba Safaris.* Tunataka tufahamu kiburi cha makampuni hayo kinatoka wapi? Pia tunataka tufahamu nani anayapa makampuni haya jeuri! Kwa nini haya makampuni yanatumia mitandao kuichafua nchi yetu? Mheshimiwa Waziri, chukua uamuzi mgumu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuna faida nyingi za kutoza ada ya kitanda kwa misingi ya viwango vya asilimia. Fedha zinazopatikana zitasaidia sana kuendeleza uhifadhi, kuendeleza miradi ya kijamii, kuboresha miundombinu na kutatua matatizo ndani ya *TANAPA.*

Mheshimiwa Spika, ifahamike wazi kuwa kuna migogoro na uhasama usiokwisha juu ya mipaka kati ya hifadhi/mbuga zetu na wanavijiji wanaozunguka maeneo hayo. Hivyo, naishauri Serikali ifanye vitu vifuatavyo:-

- Wizara ifanye kila iwezalo kuweka mipaka inayoeleweka.

- Wizara itoe elimu kwa wanavijiji waelewe maana ya uhifadhi.

- Kujenga mahusiano mazuri baina ya vijiji vinavyozunguka na hifadhi/mbuga hizo kwa kuviwezesha vijiji hivyo kwa kuvipatia huduma mbalimbali kama vile maji, hospitali, shule, malambo, fedha na kadhalika.

- Kulipa fidia halali kwa waathirika wa mazao na vifo vinavyotokana na wanyama waharibifu kama vile Ndovu, Nyati na hata Fisi.

- Wizara ihakikishe inatafuta njia endelevu kuhusu matatizo ya wanyama dhidi ya raia hasa wanyama kama vile Nyati, Ndovu, Simba, Chui na Fisi.

Mheshimiwa Spika, biashara ya wanyama ni hatari sana na inahusisha watu hatari na zaidi ni matajiri wakubwa na ina mtandao mkubwa sana hapa Duniani. Zaidi biashara hii hughubikwa na vituko pamoja na rushwa. Katika nchi yetu, kupitia Idara ya Wanyamapori, mbuga zetu zimegeuzwa shamba la bibi. Mfano dhahiri ni wanyama wa aina mbalimbali waliochukuliwa tarehe 25 Januari, 2011 katika uwanja wa ndege, inasadikika kuwa walichukuliwa na ndege ya Kijeshi ya Quatar (Doha). Maswali ya kujiuliza:-

- Je, Serikali ilifahamu hilo tukio?

- Je, ilichukua hatua gani ili kuzuia?

- Je, vyombo vya usalama vilifahamishwa kuhusu tukio hilo?

- Je, ni wanyama wangapi walio hai waliouzwa kwa njia hii?

- Kama wahusika wamekwishafahamika; Serikali inasema nini?

Pia tutafakari maswali haya:-

- Wanyama hao wali-*check in?*

- Wanyama hao walipita katika *scanner?*

- Wanyama hao walipewa *vaccination card?*

- Wanyama hao walikuwa na pasipoti?

Mheshimiwa Spika, inaumiza sana na wala siyo utani!

Mheshimiwa Spika, namtaka Waziri achukue uamuzi mgumu na naamini Umma wa Watanzania utamuunga mkono, ikiwa kuna Kiongozi yeyote aliyehusika achukuliwe hatua kali za kisheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Gawio la *TANAPA* kwa Hazina: naungana na uamuzi wa maoni uliotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuwa gawio la asilimia kumi toka *TANAPA* kwenda Hazina (Serikalini) lisitishwe ili lisaidie kuiendeleza *TANAPA.* Naamini kwa dhati kuwa, *TANAPA* ina matatizo makubwa yafuatayo: Ukosefu wa watumishi; ukosefu wa Hosteli; ukosefu wa hoteli; ukosefu wa nyumba za watumishi; na ukosefu wa vitendea kazi kama vile magari na kadhalika. Hivyo basi; ni matumaini yetu kuwa ile asilimia kumi inayolipwa Serikalini ikibaki *TANAPA* itasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua matatizo hayo yanayoikabili *TANAPA.*

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa inawaendeleza Watanzania Wazalendo ili waweze kushika usukani katika biashara hii ya utalii badala ya kushikwa na Waasia?

Je, Waasia walioshika nafasi hii kwa kuendesha biashara za utalii wanalipa kodi na ushuru halali Serikalini?

Je, Wizara inasema nini juu ya unyanyasaji wanaofanyiwa wafanyakazi wenye asili ya Kiafrika (Tanzania) katika Hoteli za Kitalii zinazoendeshwa na Waasia hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, *Cultural Tourism* ni utamaduni wa asili unaohusisha utalii. Hii ni pamoja na uchongaji wa vinyago, uhifadhi wa historia, Makumbusho ya Taifa na kadhalika. Je, Wizara ya Maliasili na Utalii imejipanga vipi ili kuhakikisha kuwa nchi yetu inaanzisha *Cultural Tourism* katika nchi yetu? Je, Makumbusho ya Taifa yanaiingiziaje Wizara mapato? Je, Makumbusho ya Mwalimu Nyerere yaliyoko Butiama yanatembelewa na Watalii? Je, Serikali imefanya mpango gani ili kuhamasisha suala la utalii katika Makumbusho ya Butiama?

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kumwuliza Waziri maswali yafuatayo kuhusiana na Utalii wa Ndani:-

- Je, Serikali imejipanga vipi kuutangaza utalii wa ndani hapa nchini?

- Je, Bodi ya Utalii nchini *(TTB)* imefanya juhudi zipi za kuhamasisha utalii wa ndani hapa nchini?

- Je, Wizara inaisaidiaje *TANAPA* ili iweze kujenga hosteli ndani ya hifadhi zetu kwa lengo la kuwasaidia/kuwalaza Watalii wa ndani kwa gharama nafuu?

Mheshimiwa Spika, napenda kuizungumzia Biashara ya Magogo/Misitu. Je, Wizara ina mkakati gani wa kukomesha kabisa biashara ya magogo katika nchi yetu?

- Je, Wizara haioni kuwa misitu ya asili inateketea?

- Je, Mabwana/Mabibi Misitu wanajua wajibu wao?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ili nichangie kidogo katika Wizara hii. Kwanza, naomba nimpongeze Waziri na Katibu Mkuu, pamoja na Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara, hotuba na mipango yote iliyopo ni mizuri sana na inaleta matumaini. Japo tatizo kubwa ambalo mimi naliona ni bajeti ambayo haikidhi mahitaji ya kutekeleza mipango mizuri ya Wizara na kibaya zaidi ni tabia ya Hazina, ambao huchelewesha utoaji wa fedha iliyoombwa na kusababisha malengo kutotimia. Kibaya zaidi ya vyote ni kutotoa

fedha yote iliyoombwa. Naiomba Serikali itoe fedha kwa wakati, tena ifikapo mwisho wa mwaka wa bajeti wawe wametoa fedha zote zilizoombwa.

Mheshimiwa Spika, je, Mkoa wa Singida utakuwemo kwenye mpango wa Wizara wa kuendeleza ufugaji wa nyuki kwenye wilaya 30? Tafadhali naomba sana tusaidiwe, kwanza, kupanda miti kwenye maeneo ambayo yamefyekwa na kuharibu uasilia wa misitu ambayo maua na hali halisi kwa wafugaji wa nyuki, asali yake ni bora kuliko sehemu yoyote. Mfano, katika Wilaya ya Iramba, eneo la Tarafa ya Ndago, kulikuwa na misitu mikubwa lakini inazidi kwisha na eneo lingine kulianzishwa Magereza ya Ushora Ndago, huko wafungwa walihimizwa kukata miti kwa kuchoma mkaa na kuchoma matofali, kitu ambacho kimeondoa kabisa mandhari nzuri ya misitu hiyo ya asili na yenye miti ya matunda na ambayo ni chakula cha Tembo. Tembo walikuwa wengi sana enzi hizo kwenye maeneo ya Sabe na hata Chui na Simba walikuwepo, sasa hivi wamehama, yaani inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara itoe msukumo kwa Jeshi la Magereza kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kushirikiana na Wizara ya Mazingira, wafungwa wale wale waliotumika kukata miti, watumike kupanda miti tena maeneo yale ili kurudisha msitu uliotoweka na hivyo kuwawezesha wafugaji wa nyuki kuendelea na shughuli hizo. Pia naomba Wizara itusaidie kuongeza ufanisi na uwezo wa kufuga zaidi nyuki Mkoani Singida na hususan Iramba, ambako asali yake huwezi kuipata popote ila Iramba hasa Ndago.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kwa nini Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB);* imeshindwa kupata namna ya kutangaza au kuifanya Tanzania iwe kiongozi wa utalii katika Ukanda wa Afrika kwani vivutio tele tulivyonavyo nchini ni vingi? Kwa nini wameshindwa? Mimi naona watendaji wake hawana ubunifu wa kutosha, yaani wao wanatumia Maonesho ya Kimataifa kama utalii tu; jamani ni aibu sana! Naomba hili liangaliwe kwani wapo hapo kuonesha mabadiliko na tofauti. Je, miaka 50 ya Uhuru wao wana lipi jipya?

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina maeneo yaliyotangazwa urithi wa Dunia kutokana na uzuri wake lakini mbona nchi hainufaiki navyo?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 kuna kikundi cha Wamasai kilikwenda kushiriki *London Marathon* kwa ajili ya kuchangisha fedha za kuchimba visima vya maji kijijini kwao. Walipokuwa kule walipokelewa kwa hisia kubwa na walikuwa kivutio na walikuwa kwenye vyombo vya habari na walitumia muda huo kuitangaza nchi yetu na vivutio vyake. Je, Wizara inalijua hilo; na kama inalijua Wamasai hao walitambuliwaje?

Je, kwa nini Wizara isitumie *Marathon* hizo kama njia mojawapo ya kutangaza vivutio vyetu vya utalii, kwani Kenya wanatumia sana mbio hizo kutangaza nchi yao na utalii kwa ujumla kwa kupeleka washiriki na mwaka ule wa 2007, Wakenya walishika nafasi za juu japo Wamasai wetu walitia fora kwani walitumika pia kuvutia washiriki wa wahudhuriaji? Je, Tanzania tupo tayari? Kama hamkuwa na habari ulizeni Ubalozi wa London UK (Tanzania) au hata mimi nitawapa ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko ya mishahara yaliyoelekezwa kutekelezwa *TANAPA* hayakutekelezwa na Waziri, ambayo yanabagua kada; maaskari tu ndiyo wanapandishwa lakini wataalam wengine waliopo hawapewi umuhimu. Mishahara hii haizingatii kiwango cha elimu, utaalamu na wajibu wa kimamlaka. Je, malalamiko hayo ni ya kweli; na kama kweli yatatekelezwa lini ili kuleta usawa katika utendaji wa kazi na kutenda haki, pia kuondoa chuki na ama kudhoofisha utendaji kazi kwa baadhi ya wafanyakazi hao? Pamoja na malalamiko hayo, naipongeza *TANAPA* kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mwisho, je, Wizara wanajipanga vipi kutangaza utalii au vivutio vilivyopo Mkoa wa Singida?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba Waziri atusaidie sisi wasanii kuhusu Nyumba ya Sanaa iliyoko Dar es Salaam kwani shughuli zilizokuwa zinafanyika pale zimebadilishwa na jengo kuporwa. Nilipouliza kwenye Bajeti ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo,

akanijibu kuwa nisubiri Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii niulize kwani Jengo lile lilikuwa chini yao. Naomba kujua kama kweli lilikuwa nchini ya Wizara hii? Je, ni mali ya nani? Nani alitoa kiwanja? Ninavyojua mimi jengo lile ni msaada wa nchi za kigeni (Nordish/Sweden) na kiwanja alitoa Baba wa Taifa kwa wasanii wote Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali inijibu ili wasanii wajue nini ni nini.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MADEYE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nathibitisha kuwa naunga mkono hoja.

Pili, nampongeza sana Mheshimiwa Ezekiel Maige (Mb), Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, kwa jitihada wanazofanya kurekebisha na kuboresha utendaji wa Sekta zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Jedwali Na. 4 kwenye hotuba ya Waziri, linaonesha kuwa baadhi ya Wilaya nchini zilipokea mgao wa fedha zilizotokana na uwindaji wa kitalii. Hata hivyo, Wilaya nyingi ikiwemo Halmashauri ya Arusha, haikupata mgao wowote. Kwa kuwa Wilaya hiyo ina misitu na Mlima Meru huingiza fedha kutokana na mauzo ya mazao ya misitu na Watalii wanaopanda Mlima huo; je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kuwa Wilaya kama Arumeru inapata mgao kutokana na shughuli za Wizara zinazofanywa kwenye maeneo yao?

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, kutokutoa mgao kwa Wilaya hizo, hatutakuwa tumewatendea haki kwani wale wanaopata mgao kwa sababu ya shughuli za uwindaji kwenye Wilaya zao hutendewa hivyo kwa sababu ya kushiriki kutunza maliasli kwenye maeneo hayo. Vivyo hivyo, wilaya zinazotunza maliasili nyingine zinastahili pia kupatiwa mgao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu kwenye changamoto kubwa zinazoikabili Sekta ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, uongozi thabiti unakosekana. Hakuna hatua kali zinazochukuliwa kwa matukio yanayokiuka sheria; kwa nini suala la kuibiwa wanyama wetu ndiyo linafukuta leo Bungeni tukio lililotokea miezi tisa iliyopita? Viongozi wako wapi? Hawakuliona hili kuwa tukio la ajabu na la kuidhalilisha nchi? Serikali iwawajibishe viongozi wabovu.

Mheshimiwa Spika, hakuna ubunifu wa kuleta ubora ili kuongeza pato kutokana na Maliasili na Utalii. Hakuna *sense of commitment* katika kutekeleza majukumu. Miaka 50 iliyopita, bado utalii wetu haujaboreka, licha ya zawadi hii tuliyopewa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la ubinafsi na kupendeleana; ajira isiyozingatia ujuzi na uwezo; wawekezaji wana maslahi na viongozi kuwaziba midomo; hatufiki wala hatusogei tulipo; na suala la ukabila katika Sekta hii liangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, kwa nini uteuzi wa Waziri kwa Wajumbe wa Kamati ya Vitalu usizingatie *CV* na *seniority* ya Mbunge? Naomba wakati mwingine *CV* ziangaliwe vizuri.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, ujenzi holela katika hifadhi zetu; ni jambo la kusikitisha kuona baadhi ya wawekezaji wanataka kujenga Hoteli ya Nyota Tano kwenye *Rein* ya Ngorongoro! Hii ni hatari sana, kuna njia ya wanyama pale watakimbia hata maji hayatatosheleza kwa wanyama. Tutapoteza ile *beauty ya Creter* na ule uhalisia hautakuwepo.

Mheshimiwa Spika, ninashauri ujenzi huo usitishwe mara moja na washauriwe watumie mahema zaidi ambayo yatalinda hifadhi yetu. Ikumbukwe wageni wengi wanapotembelea

Tanzania, hawategemei kuja kulala kwenye Hoteli za Nyota Tano, wanataka kuona vitu vya asili. Siku zote moja ya vivutio kule Ngorongoro ni Wamasai, *especially* wanavyoishi na wanyama wale bila kudhurika. Tusiuwe huu utamaduni wetu. Wamasai wasinyanyaswe, kama ni kilimo wapewe sehemu mbadala kwa kilimo lakini wandelee kuishi huko kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, naomba zoezi ku-*camp* kwenye *Crater* Mlima Kilimanjaro lisitishwe mara moja, kwa sababu mazingira kule yanaharibika; hakuna vyoo, hakuna maji; wanatumia theluji kuyeyusha. Naomba tuulinde mlima wetu wa kipekee Duniani, ambao ukiwa pale Moshi Mjini nyuzi joto ni 32°C, lakini ukipanda baada ya siku tano nyozi joto ni chini ya 0°C. Hii ni zawadi ya kipekee tuliyopewa na Mwenyezi Mungu. Tafadhali, Mheshimiwa Waziri sitisha hili zoezi la ku-*camp Crater*.

Mheshimiwa Spika, utalii siyo mbuga za wanyama tu; ni kwa jinsi gani Wizara imejiandaa Dar es Salaam kuwa moja ya Jiji la Vivutio vya Utalii ukizingatia imezungukwa na bahari? Sisi kama wadau, soko la samaki Watalii walikuwa wakilitembelea lakini sasa hivi soko hilo ni chafu, pananuka; je, kuna mikakati gani ya kuongeza vivutio katika Jiji letu?

Mheshimiwa Spika, napendekeza shughuli zote za uendeshaji kuhusu utalii zimilikiwe na wazawa kwa sababu ndiyo njia pekee ya kuhakikisha pesa zote zinabaki nchini, kuliko ilivyo sasa fedha nyingi hubaki nje ya nchi. Vigezo vya kuanzisha Kampuni ya Utalii vilegezwe ili Watanzania wengi zaidi wafanye shughuli hii. Wawekezaji wapewe fursa ya kujenga hoteli na Serikali iwe mbia wa hoteli hizo.

Maofisa wa *TRA* huwa wanatembelea hoteli za Watanzania; ningependa kujua kama kwenye hoteli za mbugani kama Serengeti na Ngorongoro huwa wanafanya ukaguzi wa kustukiza ku-*check bed occupancy* kama ilivyo kwa wazawa au wao wapo juu ya sheria?

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuchangia hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwanza, niwapongeze Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wote na Serikali, kwa jinsi wanavyosimamia shughuli za Wizara hii, licha ya kuwepo kwa changamoto lukuki.

Mheshimiwa Spika, inaonekana kuwa kuna udhaifu mkubwa kwa askari wa wanyamapori. Jambo lililopelekea mpaka wanyama wanatolewa nchini wakiwa hai, lakini siyo hivyo tu bali wameshindwa kuwadhibiti majangili wanaingia katika misitu ya hifadhi na kusababisha wanyama wengi kuuwawa. Ninaishauri Serikali iweke utaratibu wa kuwashirikisha wenyeji waliopo katika maeneo ya hifadhi ili kulinda na kutunza hifadhi hizo, lakini pia Vijana wa Kimasai ni wazuri na wanaweza kuisaidia Serikali katika ulinzi wa hifadhi hizo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 19 Julai, 2011 nimesoma katika Gazeti la Mtanzania Daima kuwa, walikamatwa majangili wenye silaha na nyara za Serikali katika Mkoa wa Kigoma. Majangili hawa walikuwa 14 na walikuwa na silaha za kivita, bangi, bunduki 17 (*smg* 8, *mark* 4, magobole 8 na risasi 68). Nimemwomba Waziri wakati wa kutoa ufafanuzi atueleze kama watu hawa wamefikishwa mahakamani na je; ni Watanzania au ni wageni?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni nguvu zinazotumika na askari wa wanyamapori katika mazoezi ya kuwavunjia Wananchi waliojenga katika au karibu ha hifadhi. Askari hawa pamoja na kuwa wakati mwingine wanatekeleza wajibu wao huwa wanachukua mali za Watu/Wananchi (ng'ombe, mbuzi na mazao) na kuwabomolea nyumba zao. Mambo haya hufanywa bila hata kuwapa taarifa wahusika au viongozi wao katika maeneo husika. Mfano halisi ni kama ilivyofanyika Nzasa – Chanika, mwezi wa pili mwaka huu, ambapo Wananchi walipoteza mali zao nyingi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, Serikali haioneshi kutambua nafasi ya Wizara hii na majukumu yake katika ufanisi wa ujenzi wa uchumi ndiyo maana Wizara nzito kama hii haina Msaidizi wa Waziri (Naibu Waziri); inashangaza kuona Wizara kama ya Habari na Michezo ina

Waziri na Naibu Waziri, lakini Wizara nzito kama Maliasili na Utalii haina Naibu Waziri! Huu ni mtazamo hasi na ni kielelezo cha namna Chama cha Mapinduzi (CCM), kisivyotambua nafasi na uzito wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, utalii uliofanywa na Kamati ya Miundombinu mwaka 2001, unabainisha wazi kuwa, asilimia 60 ya mapato yote ya utalii yanaishia kwenye malipo ya usafiri wa ndege. Katika mazingira ambayo Taifa halina hata ndege moja; ni wazi kwamba, Taifa linapoteza mapato mengi na hivyo fedha nyingi za utalii zinaishia kwenye makampuni ya ndege ambayo yote ni ya kigeni.

Mheshimiwa Spika, Mkoa kama Kigoma una vivutio vya utalii vya kihistoria, fukwe na Ziwa Tanganyika na Ziwa lenyewe kuwa la pili kwa kina kirefu Duniani, kuna Sokwe Mtu, Hifadhi ya Gombe na Hifadhi za Mahale, lakini kuna ukosefu wa miundombinu ya usafiri wa kufika maeneo yenyewe. Zaidi sasa Mkoa huu hauna usafiri wa ndege na hivyo tunapata hasara kubwa za kutofaidi fursa za utalii.

Kuna tatizo la maeneo mengi yaliyofanywa hifadhi kupelekea migogoro baina ya Wanavijiji na Serikali. Mfano ni eneo la Hifadhi ya Lukunda lililopo Tarafa ya Nguruka. Katika Bunge la Tisa, Mheshimiwa Zitto Kabwe, alipata kuzungumza ndani ya Bunge hili na Mheshimiwa Maige mwenyewe alipata kujibu kuwa, angefuatilia na kutembele eneo hili, kujionea mwenyewe ili atatue mgogoro huo. Mpaka leo Bunge la Kumi, Mheshimiwa Maige sasa ni Waziri, lakini bado hajatekeleza ahadi yake hiyo na tatizo la utaratibu wa kufanya eneo hilo kuwa hifadhi linaendelea kuwa mgogoro mkubwa. Naomba kauli ya Serikali kuhusu eneo hili kuepusha machafuko katika Kata za Nguruka, Mtego na Mganza.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mwekezaji wa Kampuni ya *Mufindi Papers Mills*, ambaye anauziwa mita moja ya ujazo kwa shilingi 10,000 ilhali bei ya Serikali ni shilingi 29,000; ni ushahidi wa namna Serikali inavyopoteza mapato yake katika mazingira yanayoashiria ufisadi. Haiwezekani, Wananchi maskini wauziwe mita moja ya ujazo kwa Sh. 29,000, lakini mwekezaji huyu alipe shilingi 10,000 tu!

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kusisitiza kuwa, Wizara hii ni nzito, inapaswa kupata Naibu Waziri kwa majukumu yalivyo mengi na mazito, yenye maslahi ya uchumi wa Taifa hili. Inasikitisha kuona nchi ndogo kama Turkey inapata *dollar* 15 bilioni kwa mwaka jana kutokana na utalii tu, lakini nchi yenye fursa zote za Mwenyezi Mungu kuvutia utalii kama Tanzania, inachechemea na *dollar* bilioni moja. Mapato ya utaliii ya *dollar* bilioni 15 Turkey ni zaidi ya mara mbili ya mapato yote yanayokusanya katika uchumi wote wa Tanzania. Sasa ni wakati wa kuuifanya Sekta hii izalishe.Naomba kuwasilisha.

**MHE. YUSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, mweza wa yote, kwa kuniwezesha kutoa mchango wangu kwa maandishi katika Wizara hii muhimu sana kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, mimi naanza mchango wangu kuhusu wanyamapori. Wanyamapori ni sehemu ya maliasili ambayo tunajivunia. Wanyamapori ni kivutio kwa Watalii ambao hutoka sehemu mbalimbali Duniani kuja kutembelea mbuga zetu za wanyama Tanzania. Kuangalia na kufurahia rasilimali hii ambayo Mungu katubariki, mbuga zetu zinachangia sehemu kubwa ya pato letu. Hili ni jambo zuri, mimi binafsi napongeza.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunao wanyama wa aina mbalimbali; wakubwa, wadogo, wakali, wapole, wanaotambaa na wanaotembea kwa miguu minne; wote ni kivutio kwa wageni na hata wenyeji.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mbuga za wanyama zimekuwa zikitoa usumbufu mkubwa kwa Wananchi wanaoishi jirani na mbuga hizo. Wanyama wakali wanasumbua Wananchi na wakati mwingine Wananchi huwaua. Wananchi hushambuliwa mazao yao na kuharibiwa kabisa kabisa. Kwa hiyo, pamoja na faida nzuri lakini kuna hasara pia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na faida inayopatikana kwa wanyamapori, lakini Serikali inapaswa kuzingatia kwa makini maisha ya watu na mazao yao. Kwa sababu thamani ya binadamu haifananishwi na chochote. Mimi naomba Serikali ijipange vizuri na kwa umakini mkubwa, kuboresha miundombinu na mipango endelevu, kuondoa usumbufu wa wanayamapori na binadamu na mazao yao. Naiomba Serikali kuwa, binadamu apewe thamani na athaminiwe.

Mheshimiwa Spika, ujangili umekuwa kikwazo kikubwa kwa wanyamapori ndani ya nchi yetu. Majangili huvamia hifadhi za wanyama na kuwauwa na kupora nyara, ngozi na vitu vingine muhimu. Hii ni hasara kwa Taifa kwa sababu wanyama wanatoweka na mali za Taifa zinapotea.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri kudhibiti na kulinda rasilimali hii muhimu isitoweke kwa manufaa ya Taifa na vizazi vyetu. Mimi naomba Askari wa Wanyamapori wapewe motisha, wapewe mafunzo madhubuti, wafanye kazi kwa ufanisi. Vilevile wapatiwe mishahara mikubwa pamoja na kuangaliwa vyema maslahi yao. Askari wa Wanyamapori muda wote anapokuwa kazini ni sawa sawa na yupo vitani, anastahili kuangaliwa mchango wake kwa umakini sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, nami nachukua fursa hii, kuchangia Hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la wanyamapori; kumekuwa na wafanyakazi wasiokuwa na uadilifu katika mbuga za wanyama. Wafanyakazi hawa wamekuwa wakishirikiana na wafanyabiashara haramu, wanaowasafirisha wanyama hawa bila vibali na kuingiza hasara kubwa kwa Taifa. Yapo maswali mengi ya kujiuliza kuhusu suala hili la utoroshwaji wa wanyama hao; kama ndivyo; je kwa nini Sheria ya Wanyamapori inayozuia raia wa kigeni kupewa leseni ya kukamata wanyama wakiwemo Twiga ambao ni Nembo ya Taifa haikuzingatiwa?

Wahalifu hawa wanapokamatwa huwa tunawaona kwenye vyombo vya habari, hatujui hata kuhukumu ya kesi zao; kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na uzembe na kulindana ndani ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii na ndiyo maana kumekuwa na kigugumizi kushughulikia suala hili. Ukweli wa mashaka haya unajidhihirisha katika zoezi zima lililofanyika hivi karibuni ndani ya Idara husika la kuhamisha maafisa, ambalo halikuwagusa kabisa Maafisa wa Kitengo cha Uwindaji *Cites* wakiwemo wa Arusha; licha ya kutorosha wanyama, badala yake baadhi ya maafisa hao wakapandishwa vyeo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la hawa majirani zetu wa Kenya, wamekuwa wakitangaza utalii wao kupitia kivuli cha Tanzania, wanasema kuwa Mlima Kilimanjaro upo kwao. Wamekuwa wakitangaza vivutio vizuri vilivyoko hapa kwetu Tanzania kuwa ni vya kwao na imefikia kumtangaza Babu wa Loliondo, anayehudumia watu kwa kutoa dawa za maradhi mbalimbali kuwa yupo kwao! Hawa majirani zetu wa Kenya tusipowaangalia vizuri, watatupotezea Watalii wengi kuja hapa Tanzania kutembelea hatika mbuga za wanyama, kwa sababu Kenya wanatangaza kuwa vivutio hivi vipo kwao. Je, Serikali na Wizara itatuhakikishiaje kuwa vivutio hivi vizuri vilivyopo katika nchi yetu kuwa vipo kwetu?

Pia naishauri Serikali na Wizara ihakikishe inaweka mitandao nje ya nchi na ndani ya nchi ili kutangaza vivutio hivi vizuri vilivyopo katika nchi yetu kuwa vipo kwetu.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana endapo Sekta ya Utalii itasimamiwa kwa uangalifu mkubwa; ina uwezo mkubwa wa kutoa ajira, kupunguza umaskini wa kipato miongoni mwa Wananchi na kuchangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wanaojenga hoteli katika hifadhi za wanyamapori; kunakuwa na Mikataba kati ya mwekezaji na Wananchi waliozunguka hifadhi hizi za wanyamapori. Hakika wawekezaji hawa wamekuwa hawawasaidii Wananchi wanaozunguka hifadhi hizi kwa kuwapa huduma za kijamii mfano kuwajengea hospitali, barabara na nyinginezo. Ndiyo maana kunakuwa na migogoro baina ya Wananchi na Wawekezaji. Nilikuwa naishauri Serikali na Wizara ipitie upya

Mikataba ya Wawekezaji na watakaobainika kukiuka Mikataba hii kwa maslahi yao binafsi, wachukuliwe hatua za kisheria na ikiwezekana wafukuzwe kazi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na migogoro baina ya Wananchi wanaozunguka Hifadhi za Wanyamapori na Hifadhi hizi. Wananchi wamekuwa wakivamiwa na wanyamapori waharibifu na wakali kama Tembo, Nyati, Simba, Fisi, Nyani na wengineo na mazao yao pia huharibiwa na wanyamapori hawa kwa wakati mwafaka. Kutokana na uwezo wa Serikali kutenga kiasi cha asilimia 30 ya ardhi ya nchi yetu kama hifadhi ya maliasili, pamoja na jitihada hizo za Serikali, kumekuwa na migogoro mingi ya mipaka kati ya jamii na Hifadhi. Migogoro hii inasababisha usumbufu mkubwa kwa Wananchi; hivyo, kuathiri maisha na ustawi wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali na Wizara itumie vifaa vya kisasa kama *GPS* katika kuhakikisha mipaka na kisha kuweka eneo maalum na kushirikiana na Wananchi wa maeneo husika. Kwenye maeneo ya misitu ambayo huduma za kijamii kama Shule, Zahanati na nyinginezo zimeshawekezwa ndani ya misitu; ni vyema maeneo haya yakaondolewa ndani ya misitu; hii itasaidia kuondoa migogoro hii.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja endapo nitapata majibu kwa haya yote niliyochangia kwa maandishi.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa hotuba nzuri, japokuwa Wizara yake ina uozo mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina shutuma nzito ya kusafirisha kinyemela rasilimali za nchi kwenda nje ya nchi. Rasilimali hizo ni pamoja na wanyama hai wakiwemo Twiga na ugawaji vitalu vya uwindaji usioendana na sheria na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa kuna mabadiliko makubwa kwa Watendaji wa Wizara, lakini bado kuna matatizo hasa katika utekelezaji wa sheria mbalimbali. Wizara hii ni muhimu sana kwa maslahi ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya marekebisho, aeleze kwa ufasaha kwa nini wanyama wetu wanasafirishwa nje ya nchi ndege kwa ndenge na Wizara yake iko kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha sana kuona walinzi wa wanyamapori hawalipwi posho zao kama inavyostahili na hawalipwi kwa wakati. Hii ni balaa, ndiyo maana majangili wameongezeka, inawezekana kabisa hawa walinzi huenda wanajaribu kutafuta njia mbadala kuweza kujikimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani watu wanasafirisha wanyama nje ya nchi huku wale wanaowalinda wanyama hao wakiwa wanaendelea kuwa maskini. Askari hawa wanahatarisha maisha yao, mfano, leo kuna baadhi ya Hifadhi kama Tarangire, posho zao za kawaida mpaka bosi ajisikie vizuri ndiyo anawalipa na ni baada ya manyanyaso; mishahara yenyewe wanacheleweshewa; *night* zao siku hizi kwa walinzi kama Hifadhi za Mkomazi, Sadani na kwingineko ni mpaka mabosi wajisikie wakati ni halali yao kulipwa. Kiukweli Wizara zote zina uozo ila hii imekithiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa kuna sheria njema tu inayomlinda mzawa, kifungu cha 58 (1)na (2) cha Sheria ya Utalii ya Mwaka 2001; lakini bado Sheria hizo hazimsaidii mzawa kwani hazisimamiwi kama inavyopasa. Kampuni nyingi za kigeni zinafunguliwa hapa nchini kiulaghai, haziwashirikishi wazawa kabisa; asilimia mia moja inakuwa wageni wanafanya biashara na faida kubwa inakwenda nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waziri alivyoelezea katika hotuba yake, *page 67* kuwa, *TTB* itatangaza Vivutio vya Kihistoria vya Miji Mikongwe ya Pangani, Bagamoyo, Kilwa na Ujiji na michoro ya miambani – Kondoa; ninamwomba Mheshimiwa Waziri, hii isiishie kwenye makaratasi tu; naomba Wizara iiangalie Bodi hiyo kwa macho mawili ili kutimiza hayo kwani ni kweli kabisa Miji

hii ya Kihistoria kama Pangani ni kivutio kizuri sana kwa Watalii wa ndani na nje. Ninaishauri Wizara ihakikishe kuwa, inatoa motisha kwa wazawa (Watanzania) na kuwahamasisha vya kutosha ili kuweza kuwa na utamaduni wa kutembelea vivutio vyetu wenyewe (utalii wa ndani) ili kuweza kuongeza Pato la Taifa. Ahsante.

**MHE. MBAROUK S. ALI:** Mheshimiwa Spika, naendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa uzima huu nilionao na kuniwezesha kuchangia Hotuba hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, yapo baadhi ya mambo niliweza kuchangia kwa kuzungumza na kuna baadhi ya mambo sikupata fursa ya kuyazungumza kutokana na muda; hivyo nachukua fursa hii kuchangia kwa maandishi mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, athari za ukataji wa misitu ni upoteaji wa aina nyingine za viumbe kama vile ndege na wengineo. Tatizo kubwa viumbe hivyo vinapotea lakini hukuna *recovery programme* mpaka sasa ya kuweza kurudisha uwepo wa wanyama hao.

Mheshimiwa Spika, uhifadhi shirikishi ndiyo ukoo wa viumbe adimu hususan wanyama katika mbuga zetu. Ni muhimu sana kuwashirikisha wadau wote, ikiwemo jamii na ushirikishwaji huo unatakiwa uwe wa dhati kabisa, kwa maana kwamba, jamii iweze kufaidika ili wajisikie kuwa rasilimali hizi ni za kwao.

Mheshimiwa Spika, tutakapoishirikisha jamii kikamilifu, tutapunguza gharama kwa kiasi kikubwa. Sasa hivi Wizara inanya *monitoring* ya Vifaru katika Hifadhi ya Serengeti, mfumo unaotumika kufanya *monitoring* hiyo ni ghali sana. Hiyo ni aina moja ya wanyama; sasa wanyama hao walioongezeka kazi ya *monitoring* itakuwa kubwa na ya gharama zaidi na hivyo haitakuwa Hifadhi tena.

Mheshimiwa Spika, nigusie kidogo shughuli za utalii; inaonesha ukuaji wa utalii ni mdogo sana na hatutafikia ile azma ya Serikali ya ongezeko la asilimia nane ifikapo 2014. Hali hiyo inatokana na udhaifu wa utangazaji wa kujitangaza kama nchi jirani Kenya wanavyofanya na miundombinu mibovu hususan Kusini na Magharibi ya nchi yetu. Mwisho, kukosa usafiri wa ndege tunazomiliki wenyewe. Haya ni matatizo makubwa ambayo kwa kiasi kikubwa, yanachangia ukuaji mdogo wa biashara ya utalii nchini petu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru tena Mwenyezi Mungu, kwa uwezo alionijalia wa kuchangia hotuba hii. Ahsante sana nawashukuru.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, je Serikali imewaandaaje Watanzania kupiga kura ili kuuwezesha Mlima Kilimanjaro kushinda kura ya kuingizwa katika maajabu mapya saba ya Dunia dhidi ya Mlima Plate uliopo South Africa? Kwa nini Serikali haijatoa taarifa kwa Wananchi wake badala yake tunapata taarifa kupitia vyombo vya habari? Nini majukumu ya Wizara?

Mheshimiwa Spika, je, Waziri hakufahamu kuhusu upotevu wa Twiga na wanyamapori wengine 130 katika Uwanja wa Ndege wa KIA? Nani anahusika katika uhujumu uchumi huu; na hatua gani mpaka sasa zimechukuliwa? Naomba Waziri atupe ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Wizara ya Maliasili na Utalii inakuwa na upotevu mkubwa wa fedha ilhali kuna watendaji katika Wizara wanaohusika na masuala ya fedha na utawala? Ni nini tafsiri kwa Taifa? Tujifunze nini kutoka katika Wizara hii? Tunaomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. REBECCA M. MGONDO:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii ili niweze kuchangia maoni yangu kuhusu Hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige, alipowasilisha Bungeni Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Spika, wizi wa shughuli za utalii ni changamoto ambayo kwa muda mrefu, viongozi waliomtangulia Mheshimiwa Waziri Maige, hawakujali kuitatua.

Mheshimiwa Spika, ni mara nyingi majirani zetu hasa Kenya, wamejitangaza Duniani na hasa kwa nchi zile zinazofanya utalii mkubwa kama Amerika ya Kaskazini, Ujerumani, The Netherland, Italy na kadhalika, kwamba Serengeti ipo nchini kwao na hata mlima mrefu kuliko yote Afrika (Kilimanjaro) upo Kenya.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, hatujawahi kusikia tamko la Wizara au Serikali kukanusha matangazo hayo ambayo yamedumu kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Spika, inawezekana imewahi kufanyika mara moja, lakini maelezo ya mara kwa mara huzaa matunda zaidi.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa Wizara itenge fungu la kutosha kutangaza mbuga zetu na milima yetu. *Website* ya *TANAPA* ina Lugha moja ya Kiingereza, nashauri Kiswahili pia kitumike kwa ajili ya watumiaji wa lugha hiyo. Pia taarifa zilizopo ni chache sana, ziongezwe na ziendane na wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige, ni kwa nini fukwe zetu nzuri kwa mfano Dar es Salaam Kando ya Bahari ya Hindi, fukwe hizo zinatumika kuwanufaisha watu wachache wafanyabiashara na wengine kujenga Majengo makubwa ya kuishi badala ya Serikali kuzitumia kwa utalii ili kuwanufaisha Wananchi wote kwa ujumla?

Mheshimiwa Spika, nitapenda kupata majibu katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu swali langu hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha hoja.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Liwale ni miongoni wa Wilaya zinazopakana na Pori la Akiba la Selous *(Selous Game Reserve)* na inakadiriwa kwamba, mbili ya tatu ya eneo la Wilaya ya Liwale, sawa na km 25,586, ipo ndani ya Hifadhi ya Pori hili la Selous.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizi, unaweza kuona kwamba, Wilaya ya Liwale ni wadau wakubwa wa Hifadhi hii ya Wanyama ya Selous na tunategemea kabisa kwamba, wakazi wa Wilaya hii tutaweza kufaidika na Mbuga hii kwa njia moja ama nyingine, lakini sisi ndiyo waathirika wakubwa wa Hifadhi hii.

Mheshimiwa Spika, Wakazi wa Wilaya hii mara kwa mara wamekuwa wakipata hasara ya kuharibiwa mazao yao na wanyamapori wakali na waharibifu wa mashamba kama Tembo, Nguruwe na kadhalika, kwa kula mazao yao yote na kuwaacha Wananchi hawa na maumivu makubwa. Wakati wa msimu wa Zao la Korosho, tembo hungia mashambani na kufanya uharibifu mkubwa na kuwaaachia Wananchi hawa hasara.

Mheshimiwa Spika, fidia ya Shilingi 100,000 kwa ekari ya mazao au kifuta machozi kwa wanaoathirika na wanyamapori wakali ni ndogo sana, haitoshi na baya zaidi ni kwamba, mwathirika huyu anatakiwa kulipwa mwisho ekari tano tu, kwa maana ya shilingi laki tano tu na kama uharibifu umezidi ekari tano, zinazozidi hazilipwi! Hii siyo sahihi; ninaiomba Wizara yenye dhamana, ifikirie upya maamuzi haya, kama mkulima shamba lake lote la ekari kumi limeharibiwa, basi alipwe lote.

Kwa niaba ya Wananchi wa Liwale, ninaomba kuleta salamu hizi; kiwango cha fidia au kifuta machozi kiangaliwe upya kwa walioharibiwa mashamba yao na kwa watu waliojeruhiwa au kuuawa na wanyamapori wakali, viwango vilivyoko sasa havioneshi utu zaidi kuliko tunavyowajali wanyama hawa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utaratibu uliowekwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa waathirika hawa wa wanyama wakali, bado fidia hizo hazitolewi kwa wakati mwafaka.

Waathirika hawa hutumia muda mrefu kufuatilia fidia hizo bila mafanikio na hata sasa wapo waathirika wa miaka mingi ambao hawajapata kifuta jasho hicho.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa mpaka ulioko ndani ya Wilaya hii na Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous. Vijiji vinavyopakana na Hifadhi hii ya Selous ni Kikulyungu, Barikiwa, Chimbuko, Mlembwe, Ndapata, Naujombo, Mirui, Mpigamiti na Kimambi na Vitongoji kadhaa.

Mheshimiwa Spika, mpaka kati ya Vijiji hivi na Hifadhi ya Wanyama ya Selous uliwekwa mwaka 1974, kwa Tangazo la Serikali la mwaka huo, pamoja na ramani yake inaonesha mipaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kikulyungu kimekuwa na mgogoro wa mipaka na *Selous Game Reserve* kwa muda mrefu sasa, huku Wizara ya Maliasili na Utalii wakiusikia na kutochukua hatua yoyote ya kuumaliza mgogoro huo!

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iingile kati mgogoro huu umalizike. Naunga mkono hoja.

**MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Watendaji wake, kwa kufanikisha kuleta Bajeti ya Wizara yao katika Bunge lako Tukufu ili nasi Waheshimiwa Wabunge tuweze kuiboresha. Ninapenda kutoa maoni yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rufiji ni moja kati ya Wilaya zilizobahatika kupitiwa na Pori la Akiba la Hifadhi ya Solous katika Vijiji vilivyopo katika Kata ya Mwasemi, ambavyo ni Mloka, Mtanza Msona, Nyaminywili, Mibuyu saba na katika Kata ya Ngarambe kuna Vijiji vya Tapika, Ngasambe na vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wanavijiji wanaozunguka Hifadhi hii ya Selous ya kunyanyaswa na Askari wa Wanyamapori na pia wazawa wa vijiji hivi kutonufaika kutokana na wawekezaji waliowekeza katika Hifadhi hii. Kwa mfano, tatizo la kutowapatia hata ajira ndogo ndogo za muda zinazotokea ndani ya Hifadhi kama kufyeka au kufanya kazi za usafi.

Mheshimiwa Spika, watumishi waliopo ndani ya Hifadhi wamekuwa na tabia ya kuwaleta watu kutoka nje ya vijiji hivi hata katika kazi ndogo ndogo, ambazo hazihitaji ujuzi wala elimu kubwa na wazawa wanapoomba vibarua hivi basi huombwa rushwa; mfano, kuingia Hifadhini ili upate kibarua cha kufyeka ni lazima ulipe shilingi elfu ishirini. Je, huu siyo unyanyasaji? Watu wanaozunguka hifadhi hizi watanufaika vipi na rasilimali hii waliyopewa na Mungu?

Mheshimiwa Spika, natambua juhudi zinazochukuliwa na Wizara katika kuhakikisha kuwa, wanadhibiti uvunaji na usafirishaji haramu wa mazao ya misitu, lakini tatizo la uvunaji na usafirishaji haramu wa mazao ya misitu bado ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Rufiji, wafanyabiashara (watu), bado wanaendeleoa kuvuna na kusafirisha mazao ya misitu kwa njia haramu, lakini inapotokea askari wa maliasili wanapomkuta mzawa wa Rufiji amebeba kipande kimoja cha mbao ambacho amekilipia, bado watamnyanyasa na kumdhalilisha, je, huu siyo unyanyasaji?

Mheshimiwa Spika, wanavijiji wanaendelea kuona miti ama misitu yao inamalizika kwa kupelekwa magogo nchi za mbali kama Uchina, lakini wao wanabaki maskini na Jangwa linawakaribia.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Wizara ni kwamba, ihakikishe Watumishi wa Idara ya Maliasili hawawanyanyasi Wanarufiji kwani misitu na hifadhi za wanyamapori walizopewa na Mwenyezi Mungu ni mali yao na watambue kuwa hawa ndiyo wahifadhi wa kwanza wa rasilimali hizi. Ahsante.

**MHE. MUSSA HASSAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, natanguliza shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa umahiri na umakini wake wa kuwasilisha vyema hotuba yake Bungeni. Aidha, nitumie fursa hii adimu, kuwapongeza Watendaji Wakuu wa Wizara katika kutayarisha hotuba iliyosheheni taarifa na mikakati ya kuhakikisha kwamba, Wizara inatekeleza kiufanisi majukumu yao kimsingi.

Baada ya shukrani hizo, naomba nijielekeze na kuchangia hoja hii katika eneo la utalii.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kueleza kuwa, mimi ni mdau wa utalii kwa upande wa Zanzibar, nilikuwa mmiliki wa hoteli mbili; za nyota tatu moja na nyingine ni ya nyota nne ziitwazo *Whiterose Beach Resort* na ya pili inaitwa *Ras Shugi Beach Resort*.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Wizara iwe na mpango mkakati na kuongeza bidii ya kutangaza vivutio vyetu vya utalii kama zinavyofanya nchi za wenzetu kwa kuandaa Maonesho ya Utalii. Kufanya hivi ni kwa kuwaonesha kuwawezesha wajasiriamali kupata fedha nyingi zaidi na hata Serikali kupata kodi. Utaratibu wa sasa, Watalii wengi hasa kwa upande wa Zanzibar, utaona wengi wa Watalii wanakuja au kuletwa na *tour operator* wa kigeni na kulipiwa au kulipa fedha ughaibuni na kukosa kodi kiasi kikubwa. Hata hivyo na wale wamiliki wa hoteli waelimishwe na wawezeshwe kutangaza hoteli zao kwenye *website* au hata kwenda nje kuzitangaza na kuwaeleza ni vitu vipi ambavyo viwepo katika hoteli zao ili kuwezesha kupata fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa heshima kabisa, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DONALD K. MAX:** Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ifike Geita ili tusaidiane Mgodi wa GGM, ambapo kampuni hii inajitahidi sana katika kazi ya upandaji miti lakini Viongozi wa Wilaya hawatoi ushirikiano wa karibu.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya mapato ni vidogo na bajeti zetu ni finyu sana; sasa kama yupo mtu anayetaka kusaidia utunzaji wa mazingira tumpe moyo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara pamoja na Wizara ya Mazingira, mtutembelee ili tufanye mazungumzo ya Mgodi wa GGM.

Mheshimiwa Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri kila la kheri. Naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, pamoja na Watendaji wake wote, kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba kutoa rai zifuatazo kwa nia ya kuboresha:-

Mheshimiwa Spika, wanyama waharibifu kama Tembo na Nyati, Nyani na Ngedere, wanawatesa sana Wananchi hususan wakulima wa mpunga na mahindi katika Wilaya ya Morogoro Vijijini. Jinsi hasara ilivyo kubwa, Wananchi wengine wamekata tamaa ya kilimo. Naomba Wizara iangalie namna ya kudhibiti wanyama hawa ili Wananchi waone kwamba, Serikali yao inawajali. Aidha, naomba Wizara ichangie kidogo Miradi ya Maendeleo katika Wilaya hii kama ishara ya kuwafuta machozi wakulima kutokana na athari za wanyama hawa waharibifu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010, niliahidiwa mifuko 150 ya *cement* na nondo tani moja, kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Mto Mbezi, eneo la Lung'ala. Mpaka sasa Wananchi hawa wanasubiri hiyo *cement* kwani niliwajulisha kuhusu msaada huo; naomba Selous iheshimu ahadi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iangalie uwezekano wa kuvuna Mamba wanaowashambulia na kuwaua Wananchi wangu. Juzi tu aliuawa mwanamke mmoja katika eneo la Dete, Kata ya Tonunguo. Akina mama hawa wanashambuliwa wakati wanavuka mto kwenda zahanati iliyo upande wa pili wa mto. Naomba Idara ya Wanyamapori iangalie

uwezekano wa kuchangia ujenzi wa zahanati eneo la pili ili Wananchi wasivuke kufuata huduma za afya upande wa pili.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wapo tayari kulinda na kutunza misitu ya Milima ya Uluguru. Naomba Idara husika isaidie kuwapa angalau *a revolving Fund* kwa vikundi vya vijana na wanawake ili waweze kuanzisha shughuli za ujasiriamali ili wasiwe na sababu ya kuharibu misitu kwa sababu za kiuchumi. Mimi kama Mbunge, nimeanza Mradi wa Ufugaji Sungura na ninao mpango wa kuanzisha Ufugaji wa Nyuki. Naomba Wizara iwasaidie Wananchi ili waweze kuiimarisha Miradi hii ambayo ni mbadala wa kuharibu misitu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wananchi wanapokamata mazao ya misitu iliyovunwa kinyume na sheria au utaratibu, basi Maafisa Maliasili wasiwanyang'anye hizo mbao. Naomba vijiji viachiwe hizo mbao ili watengenezee madeski. Wananchi wangu wa Kijiji cha Mwarabi, Kata ya Mkuyuni, wamekamata magogo na mbao zilizovunwa katika Msitu wa Kimboza. Maafisa Maliasili kutoka mkoani wamezichukua mbao na magogo yote; wanapeleka wapi? Hawa Wananchi waliokamata magogo na mbao wanapewa motisha gani? Hivi wakikata tamaa wakasitisha ulinzi hatima ya hii misitu itakuwaje? Naomba maafisa hawa waonywe.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri Wizara iangalie namna ya kuanzisha utaratibu wa kuboresha utalii wa ndani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na namtakia Mheshimiwa Waziri kila la kheri katika utekelezaji wa Bajeti hii ya 2011/12.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie Wizara hiii kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kero ya mipaka kati ya Hifadhi ya Mikumi na Kijiji cha Mharaka, Kata ya Doma. Taarifa ya Serikali kupitia Waziri Maige ni kwamba, Serikali imesharekebisha mipaka lakini bado mawe (*beacons)* hawajazitoa katika Kijiji cha Mharaka; naomba sasa wazitoe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni fidia ndogo itolewayo kwa wanyama wanaoharibu mazao na pia kusababisha vifo. Fidia ya shilingi laki moja ni ndogo sana kwa Tembo wanaoharibu mazao. Hata kifuta machozi cha shilingi 1,000,000 ni kidogo kwa wanyama wanaosababisha vifo. Mbona Tembo mmoja akiuawa ni shilingi milioni tano? Serikali iangalie upya fidia na kifuta machozi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ijenge uzio wa kudumu kuzuia wanyama kutoka katika hifadhi kuingia mashambani na kuharibu mazao na kusababisha vifo.

Mheshimiwa Spika, nitaeleza kama ifuatavyo juu ya matatizo makubwa yanayosababishwa na Askari wa Wami Mbiki:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, askari kuua mifugo. Hivi karibuni kumetokea unyanyasaji wa askari kuua ng'ombe wa Wamang'ati katika Vijiji vya Mhumbilo na Mziha. Matukio haya si ya kuyaacha hivi hivi; huu ni unyanyasaji na ni uvunjifu wa amani.

Mheshimiwa Spika, pili, askari kuua raia na kudhalilisha Wananchi. Gazeti la Majira la tarehe 14 Agosti, 2011 liliripoti kwa kichwa cha habari "Askari wa Hifadhi Wadaiwa Kumuua Mvuvi Mto Wami." Imeripotiwa askari hawa kumuua Ndugu Riamai Amos, Mkazi wa Kijiji cha Kidudwe, akivua Mto Wami.

Mheshimiwa Spika, tukio hili ni kubwa na linatia uchungu, namna askari hawa wanavyoweza kujichukulia sheria mkononi kwa kumuua raia asiye na hatia. Naomba maelezo ya kina, Waziri atoe kauli juu ya tukio hili. Natamka siungi mkono hoja na nashika shilingi bajeti hii mpaka nipate maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na kero ya kuwasumbua Wananchi kwa kisingizio cha mipaka. Tatizo la mipaka lipo katika Vijiji vya Mhumbilo, Kitongoji cha Mesagalawe; Kijiji cha Kunke katika Vitongoji vya Makwalu, Mbagali na Makwalu; Kijiji cha Mziha katika Vitongoji vya Njeula na Mapagano; na Kijiji cha Dihinda katika Kitongoji cha Kaole. Naomba sana Serikali iingilie kati hawa Wami Mbiki wasiendelee kuwasumbua na kuwanyanyasa Wananchi wa Vijiji na Vitongoji hivi kwa kisingizio cha mipaka na madai kuwa Wananchi kuingia maeneo ya hifadhi. Suala hili likiachwa, litapelekea uvunjifu wa amani. Naomba maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Shamba la Miti Mtibwa limekuwa linatoa upendeleo wa uvunaji miti kwa watu wa nje ya Jimbo la Mvomero, kwa kuwasilisha maombi feki wakionesha ni wakazi. Ninavyoelewa, asilimia 30 ya miti inapaswa kupewa vikundi vya wanavijiji walio karibu na Shamba la Miti ndani ya Jimbo la Mvomero. Cha kushangaza, Wananchi wangu wamekuwa hawapewi vibali na wanapewa watu toka nje ya Mvomero. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, hivi sasa wizi wa wanyama au wizi wa wanyamapori umekithiri sana; taarifa inaonesha kuwa wanyamapori hai 130 wakiwemo Twiga na wengine wenye kuvutia waliibiwa. Serikali ifanye utafiti wahusika wote wachukuliwe hatua na wanyama hao warejeshwe Tanzania. Hii itakuwa fundisho kwa watumishi wengine ili wasirejee kosa walilofanya wenzao.

Mheshimiwa Spika, ujangili katika mbuga zetu umekithiri; ni dhahiri kuwa, Askari wa Wanyamapori wahatoshi. Vijana wengi hawana ajira, wapelekeni mafunzo wafanye kazi ya kulinda maliasili zetu. Taarifa ya mwezi Oktoba 2010 hadi Machi 2011, inaonesha Tembo 55 waliuawa kwenye mbuga kama Katavi (Tembo 7), Kilimanjaro (3), Lake Manyara (4), Mikumi (4), Mkomazi (1), Ruaha (4), Serengeti (17), Tangarire (10) na Udzungwa (1). Serikali ichukue hatua za haraka kutatua tatizo hili ikiwemo kuongeza Askari wa Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, kadiri miaka inavyokwenda mbele ndivyo idadi ya watu inazidi kuongezeka, lakini Serikali nayo imekuwa na tabia ya kuongeza maeneo ya Hifadhi ya Wanyama. Siyo vibaya kuongeza maeneo, lakini hali halisi ya eneo husika izingatiwe kwani maeneo mengi Wananchi hukosa makazi au maeneo ya uzalishaji mali ikiwemo kilimo, huchukuliwa kwa ajili ya hifadhi. Vilevile fidia inayolipwa ni ndogo sana na pia hucheleweshwa. Haki itendeke katika hili na busara itumike katika kuongeza hayo maeneo ya hifadhi ili Wananchi wasikwazike.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Misitu na Nyuki ni duni, elimu haijatolewa vya kutosha. Naishauri Serikali iongeze juhudi za kuelimisha Watanzania juu ya ufugaji nyuki, kwani asali ina faida sana kwa wanadamu, kwani ni chakula, ni dawa na pia ni zao la biashara.

Mheshimiwa Spika, ni vyema na ni busara sasa Jengo la Shirika la *TANAPA* liitwalo *Mwalimu J. K. Nyerere Conservation Center,* ambalo ni mali halali ya Shirika hili linalotumiwa na Mahakama ya Afrika, lirudi kwa matumizi yake ya ofisi. Haiingii akilini *TANAPA* wanakosa ofisi wakati wanalo jengo lao. Jengo hilo lirudi mkononi mwa shirika kwa matumizi ya ofisi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni kwamba, Hifadhi za Wanyama ya Gombe na Mahale Mkoani Kigoma zimetelekezwa. Hivi ni vivutio vizuri sana; wapo Sokwe na Nyani wazuri lakini hapafikiki kirahisi kwa kuwa miundombinu hasa ya usafiri hairidhishi. Hivyo, ni dhahiri kuwa, siyo wajibu wa Wizara hii kujenga miundombinu lakini Serikali ndiyo hiyo hiyo moja; ni vyema Serikali ione umuhimu wa kuboresha miundombinu ya maeneo yanayoliongezea Taifa mapato.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Uchukuzi, kuhakikisha tunapatiwa *speed boats* kwa ajili ya Hifadhi ya Gombe iliyopo Kaskazini mwa Ziwa Tanganyika na Mahale iliyopo Kusini mwa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, Serikali iirudishe *Air Tanzania,* itachangia katika kuongeza kasi ya mapato ya Wizara hii kwani usafiri utakuwa wa haraka. Reli pia iboreshwe ili Watalii wengine

waweze kutumia usafiri huo hasa wenye *interest* na kuliona Bonde la Ufa la Tanzania na mazingira ya vijiji vyetu.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri na yenye kuleta matumaini. Pia nawapongeza Watendaji wote, kwa umahiri wao katika ufanikishaji wa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili Wizara hii ni kama zifuatazo:-

Wakati tunatembelea viwanda tuligundua kwenye viwanda vinavyotengeneza bidhaa zenye kutumia mbao, vina matatizo ya kupata mali ghafi na kuathiri utendaji wa kazi kwa ukamilifu na tayari kuna viwanda vimeshapunguza wafanyakazi na vingine vipo njiani kufungwa kabisa na vikifungwa maana yake ni ukosefu wa ajira kwa vijana. Namwomba Waziri alione hilo na kulitafutia ufumbuzi wa haraka ili vijana wetu wasikose ajira na kupunguza au kuondoa kabisa usafirishaji wa mbao nje ya nchi ili viwanda vyetu vipate malighafi ya kutosha na kusafirisha bidhaa iliyokwisha ongezwa thamani na hapo ndipo Pato la Taifa litakapoongezeka na kuhuisha uchumi wetu, tofauti na ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iruhusu fursa ambazo zipo katika Mkoa wa Kigoma na Kanda nzima ya Magharibi, kwa kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, tangu vijiji vilipoanzishwa kumekuwepo na ongezeko kubwa la watu na ardhi haitoshi, maeneo ya kulima hayatoshi, na hata maeneo ya uchimbaji chokaa nayo ni tatizo. Naomba Serikali iliangalie hili na ilete sheria Bungeni ili mipaka isogezwe na Wananchi waweze kupata maeneo ya kulima, malisho na kadhalika, kwa ajili ya kujikimu.

Mheshimiwa Spika, Kigoma kuna Hifadhi ya Gombe, kuna wanyama ambao hawapo katika sehemu nyingi mfano Sokwe mtu. Naomba Serikali iongeze kasi katika kutengeneza miundombinu ya barabara na Kiwanja cha Ndege cha Kigoma ili Watalii waweze kwenda Kigoma kwenye Hifadhi ya Gombe.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kasulu, vijiji karibu asilimia 90 vimepakana na Hifadhi ya Pori la Malagarasi na Wananchi hawana kabisa maeneo ya kulima; mfano, Kijiji cha Kagera Nkada, Mugombe, Nyachenda, Nyakitonto, Makewe, Mvugwe, Nyamyustsi na vingine vingi. Je, ni lini Serikali itasogeza mipaka ili Wananchi wapate maeneo ya kulima?

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuishukuru Wizara, kwa kuandaa Bajeti hii. Vilevile naipongeza Kamati kwa kuisimamia Wizara na kuishauri Serikali ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa uamuzi wake wa kufanya ziara katika Wilaya ya Masasi ili kusikiliza kero za Wananchi na kujionea matatizo yaliyopo katika mpaka wa Hifadhi ya Msenjesi na Vijiji vya Chungulungulu, Namatembo na Chiwale.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni la muda mrefu sana, lakini namshukuru Mheshimiwa Waziri, ameonesha nia ya kutatua mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amekuwa Kiongozi wa Kitaifa wa kwanza kufika Kijiji cha Chungulungulu toka mwaka 1963, alipotembelea Hayati Waziri Mkuu, Ndugu Rashidi Mfaume Kawawa; hongera sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kaonesha mfano mzuri, kwa kuahidi kusaidia Sekta ya Maji na Barabara. Huu ni mfano wa kuigwa na Mawaziri wengine. Naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri, ashirikiane na Waziri wa Ardhi katika kutatua mgogoro huu kwa kuwaandalia mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vinavyozunguka hifadhi hii na kurekebisha mpaka kama Wananchi walivyoomba ili kumaliza kero hii.

Mheshimiwa Spika, tunaomba kazi hii ifanyike haraka ili kuleta maana halisi ya ahadi ya Waziri kumaliza mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Masasi kuna vijiji ambavyo vilianzishiwa mpango wa Miradi ya Ufugaji Nyuki lakini hadi sasa haijakamilika na kuna vikundi vya ujasiriamali ambavyo wanahitaji kupata elimu ya ufugaji nyuki. Ombi langu kwa Wizara, ione umuhimu wa kupeleka Mradi huu katika Jimbo langu la Masasi.

Mheshimiwa Spika, natumaini maombi niliyoomba Wizara itayatekeleza kwa manufaa ya Wananchi na Serikali kwa ujumla. Ahsante. Naunga mkono hoja.

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii ni muhimu katika kuleta maendeleo na kukuza uchumi wa Tanzania na pia ni uti wa mgongo wa maisha wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imejaliwa kuwa na Maliasili nyingi katika sehemu zake zote kuanzia Kata hadi Taifa. Tanzania ina wanyama, mabonde na maporomoko ya maji. Yote haya ni moja kati ya kulifanya Taifa hili kupata fedha za ndani na nje/kigeni, lakini la kusikitisha ni kuona mali hii inafisadiwa na baadhi ya watu wachache ambao ni walafi na kuwafanya Wananchi wa Tanzania hii kuendelea kudidimia katika dimbwi la umaskini.

Mheshimiwa Spika, utalii ni uchumi mzuri katika nchi na asilimia kubwa ya pato la nchi linaletwa na utalii, lakini Serikali ya Tanzania inapoteza asilimia fulani ya pato kwa sababu Watalii wanakuja kutembea tu na fedha yote wanaiacha kwao, Tanzania inaambulia fedha ya *Airport Tax;* itabidi Serikali ibadilishe mwelekeo ili fedha ipatikane kwa wingi. Hata hivyo, Serikali inapoteza pato lake lingine kwa kuiachia Nchi ya Kenya kujitangaza kuwa Mlima wa Kilimanjaro upo kwao na Watalii wengi hushukia Kenya na kuanza safari zao.

Mheshimiwa Spika, hakuna kizuri kisichokuwa na athari, utalii unaleta athari kwa vijana wa kike ambao mila na tamaduni za nchi zinabadilika.

Mheshimiwa Spika, utoroshaji wa wanyama kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), uliopo Wilaya ya Hai ni kuhujumu uchumi kwa kusafirisha na kuuza nje ya nchi wanyamapori hao, ambao ni nyara za Serikali ya Tanzania kinyume na Sheria ya Uhujumu Uchumi, Namba 57, Kifungu cha (1) na (60).

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona wanyama kama Twiga, wanapakiwa ndani ya ndege na kusafirishwa hadi Doha Qatar bila Serikali kulizungumzia suala hili. Uwanja wa Ndege kuna Uhamiaji na Usalama wa Taifa; wote hawa hawakuona? Hapa inaonesha kuna jambo linafichwa.

Mheshimiwa Spika, kuna wanyama kama Tembo, Twiga, Simba, Nyati, Faru na Viboko ni vivutio vya utalii, lakini utaona kwamba watu huuwa Tembo na kusafirisha pembe nje ya nchi, huku ikiachwa Tanzania kwenda na maji.

Mheshimiwa Spika, kuna hoteli nyingi ambazo zimetofautiana daraja (*stars).* Hoteli hizi zinatofautiana hata kimapato. Je, ni hoteli ngapi za Daraja la Tano, Nne, Tatu, Pili na Kwanza; na mapato yake ni kiasi gani kwa mwaka kwa kila kiwango? Naomba Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, alieleze Bunge hili. Pia ni vizuri Waziri angeainisha viwango vya kila hoteli angalau ikajulikana mapato yake, ingewezekana kuongeza mapato kama ni kidogo. Baadhi ya hoteli utoaji wa *tax* ni wa kusuasua na huwa siyo rahisi kukupa kiwango/idadi kamili ya wageni wanaoingia katika hoteli kwa siku. Wizara ipange mipango mizuri ya mikakati ya kukusanya fedha na hata ikiwezekana, kuwe na sheria itakayowabana wenye hoteli kubwa na ndogo.

Mheshimiwa Spika, sababu mojawapo ya kuwa na hoteli ni kuwapatia vijana wetu kazi, lakini hoteli kubwa kubwa wafanyakazi hutoka nchi za jirani kama Kenya, Malawi na Zambia na hawa huwa ni Mameneja au wanashika Idara mbalimbali za hoteli na vijana wetu ni *waiters* au *house keepers*. Hii haina maana kwamba hawajasoma, lakini kuwadhalilisha na kutaka siri zao zisitambuliwe. Wizara ichunguze hili ili ipate undani wake.

Mheshimiwa Spika, kuna mchezo unaochezwa na wawekezaji wa hoteli wa kukimbia malipo; mfano, hoteli moja inabadilishwa majina mara tatu; Sheraton, Helsinki, Movenpick; je, Serikali haioni kwamba inawekwa kama boya? Wawekezaji wanachukua fedha na kujitajirisha wao na Serikali zao, Serikali inakula hasara kwa kutajirisha nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa, misitu ina umuhimu wa kipekee katika maisha ya kila siku ya viumbe hai hususan binadamu. Tunapata mahitaji ya msingi na hasa nishati, vifaa vya ujenzi, samani, madawati, asali na kubwa zaidi ni kuwa misitu ni chanzo kikuu kabisa cha mvua, kwa hiyo, tutaepuka jangwa. Lawana kutoka vizazi vijavyo ni kuwakosesha urithi wa misitu ambayo ni moja kati ya haki zao za msingi kabisa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe na utaratibu wa kuwashirikisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi katika zoezi la kupanda na kutunza miti. Serikali ipitishe sheria ndogo ndogo, zitakazomtaka kila Mwananchi bila kujali uraia wake, kupanda miti angalau kumi kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, ninashauri yafuatayo:-

- Rasilimali hii tuliyopewa na Mungu ya Maliasili hatujaitumia vizuri na kikamilifu katika kuondoa umaskini. Ninaishauri Serikali ipange mipango na mikakati juu ya kutambua nguvu yetu, udhaifu wetu, fursa zetu na tishio kwa nchi jirani.

- Misitu tuliyonayo itumike kutengeneza madawati ya shule na samani za Serikali ili kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima na kuagiza vifaa kutoka nje.

- Uchumi unaotokana na *National Park* uwasaidie Wananchi. *National Parks* zizidi kutangazwa ili Watalii waje kwa wingi na kuleta maendeleo ya nchi.

- Miundombinu ya mbuga itengenezwe vizuri ili iwe rahisi kufika.

- Wananchi wa Tanzania wahamasishwe kwenda kuangalia na kutembelea mbuga mbalimbali zilizopo nchini, hii inatokana na kuwa hakuna tabia ya kuthamini kilicho chetu.

- Jamii ya Tanzania hawajui mali iliyopo nchini pao, ni vizuri Wizara itangeze kwa kutumia vikundi vya uhamasishaji na kwenda sehemu mbalimbali na kutoa huduma za umuhimu wa mbuga zetu.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Napenda kujua; kwenye Mkoa wa Tanga kulikuwa na Chifu na Kabila la Wasambaa, Chifu Kimweri, ambaye kuna wakati alipita Mto Ruvu, kati ya Msambiazi na Kiloza; mpaka leo hii Mto haujapanuka; kwa nini pasiwekwe mahali pa kumbukumbu ya Watalii waje waone eneo la historia?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa mimi nitaunga mkono Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ni kwa sababu tu nafungwa na Kanuni ya Bunge ya *Three Line Wheels* na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imejaa madudu ya kutisha, haina dhamira ya kweli kulisaidia Taifa hili, si kwa Watendaji Wakuu wala Wakurugenzi, wanachukua maneno ya wahenga waliosema "na lizame tugawane mbao." Hii inadhihirika pale ilipofika Watendaji wakalisaliti Taifa

hili kwa kuona na kubaini utoroshwaji wa wanyamapori 116 na ndege 16, wenye thamani ya zaidi ya shilingi 170,570,500 tokea tarehe 24 Novemba, 2010 mpaka hivi leo hakuna hatua na dhamira ya kweli ama kwa Waziri kuwajibika au Watendaji Wakuu!

Mheshimiwa Spika, hata pale Kamati ya Ardhi wanapotaka kupata ufafanuzi wa suala hili, kubwa zaidi ni kubabaishwa na kupigwa danadana, hakuna mashiko kwa Watendaji wa Wizara wala kwa Waziri mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, hili ni zito, haiwezekani Ndege ya Kijeshi ya Qatar iingie nchini na (Nchi Huru), ituwe Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa washuke askari wapakie wanyama siyo mmoja; pana askari nchini, usalama wa uwanja wa ndege, pana ulinzi, pana maafisa wa kiwanja chenyewe, pana Watendaji na *Management* ya Kiwanja cha Ndege; haya yote yatendeke hivi hivi bila ya kuwa pana mpango makini na kabambe umeandaliwa! Hii ni hatari na hata kuieleza kwa watu (Wananchi) ni aibu. Yaelekea kwamba, Serikali haikuwepo pale na la ajabu hakuna hatua za kinidhanu zilizochukuliwa. Hii ni *Entebe Raid*. Waisraeli walipoingia Uganda miaka ya sabini, wakawaokoa watu wote Ndege ya Ufaransa ilipotekwa nyara na Wapalestina.

Mheshimiwa Spika, katika hali hii kwa nini usiamini kuwa jeshi la kigeni linaweza kuvamia nchi hii na kuiteka wakati wowote wanaotaka? Hili ni kosa kubwa na si la Wizara hii kama Wizara bali linaingiza Wizara nyingi. Hapa Wizara ya Ulinzi inahusika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inahusika, Wizara ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa inaingia, lakini zaidi Ofisi ya Waziri Mkuu ya Usalama wa Taifa. Ninajiuliza kwa nini hatua hazikuchukuliwa! Je, Wizara hizi zimejulishwa; na hatua gani zilichukuliwa?

Je, wameandikiwa au kufuatilia ndege ya kijeshi iliyoingia bila ya idhini ya nchi nini kimejibiwa? Je wahusika katika saga hili wamechukuliwa hatua gani!

Je, Wafanyakazi wa KIA wamewajibishwa au wameachiwa kwa taratibu za mipango kwa kuwa suala hili lipo mahakamani?

Kweli tunakubali kuna sheria na haki za watendaji, lakini vilevile kuna sheria za wanaotendewa; nini Serikali inatuambia Bunge hili kwa niaba ya Wananchi?

Mheshimiwa Spika, huu ni udhalilishaji wa hali ya juu; mimi kwa mawazo yangu, Uongozi wa Wizara hii ama wawajibishwe wao au wawajibishwe Watendaji wao. Ahsante.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Pori la Liporamba ni maarufu kwa Tembo na Nyuki. Kuna mgogoro wa mpaka kati ya Pori hilo na Wananchi, ninaiomba Wizara itatue hili.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa maliasili ndani ya Ziwa Nyasa umeonesha kuwa kuna samaki wa mapambo, fukwe zenye mandhari nzuri na matumbawe ya kuvulia samaki. Waziri aje kuona kinachosemwa hapa.

Mheshimiwa Spika, tuvumbue maeneo mapya ya utalii badala ya kutegemea yale ya Kaskazini tu. Kusini ni *stable* kwa utalii mpya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja. Pamoja na hayo, ni vyema nikazungumzia yafuatayo kwa ajili ya kupata maelezo ya kina, *hence* kuboresha:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, sijaelewa ni kwa nini Mamlaka ya Wanyamapori inasuasua kuanzishwa mpaka sasa wakati ni nyenzo muhimu sana na sababu za msingi zinaeleweka kwa nini ianzishwe? Naomba maelezo ya kina tafadhali.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Utalii, naipongeza Bodi ya Utalii angalau kwa sasa wameanzisha kipindi maalum kwenye TV (runinga), lakini hata hivyo Sekta ya Utalii wa Ndani, izingatie uwiano wa Kikanda/Kimkoa kuliko kuwekeza tu Kaskazini. Kaskazini iendelee, lakini pia mkazo utiliwe kwenye Mikoa mingine ambayo vyanzo vya utalii vipo kama vile Mkoa wa Mbeya kuna vivutio vingi sana lakini havizingatiwi/kufuatiliwa. Idara husika iweke mikakati ya uendelezaji/urutubishaji huo.

Mheshimiwa Spika, katika Utalii wa Nje, *package tour* inafanyika *booking* huko huko nje, Watalii wanakuja tu nchini na kuacha pesa huko huko nje, huku Tanzania wanalipia pesa ndogo sana; kwa mantiki hii, nchi inapoteza pato kubwa sana la Taifa.

Mheshimiwa Spika, *consession fee* iwepo na iongezeke, inayotolewa sasa ni *peanuts* kabisa. Tanzania siyo shamba la bibi; inakuwaje gharama za maisha na hoteli zinaongezeka na *fee* hii inabakia tu hapo hapo? Nani walihusika na kwa nini?

Mheshimiwa Spika, Sheria Na. 5 ya Wanyamapori iangaliwe upya kwa kuangalia mazingira tuliyonayo na ya nchi za nje. Tukumbuke kuwa tasnia ya uwindaji ni tofauti na nyingine, hii inahitaji uwekezaji mkubwa, hivyo kutokana na Sheria ya Wanyamapori/Uwindaji ya asilimia 25 kwa wazawa waliowekeza vya kutosha *highly* na kuwa na *track record* nzuri, wapewe kipaumbele katika vitalu walivyokuwa wanavimiliki na wameviomba tena kuliko kunyang'anywa kwa sababu ambazo haziko *logical.* Kwa hali hii, kama nchi na Wizara/Serikali, itapata lawama nyingi kwamba kuna *something fishy along the line.* Waziri na timu yake inabidi watende haki na busara pia itumike, maana haya makampuni *I am sure* yaliyowekeza *highly with good track record* yatakuwa yalishapewa *TIC Protection Guarantee*. Hili jambo Wizara iliangalie kwa kina; *should not personalized issues, otherwise, the implication will be negative.* Siyo haki wala halali wawekezaji wa kigeni katika tasnia ya uwindaji tuwaone kama wabia, iko *complicated*. Zaidi tuwe na *win - win situation environment*.

Mheshimiwa Spika, *integrity* kwa watendaji ni finyu sana. Nyaraka za Serikali hazina usiri; uchunguzi ufanyike na hatua zichukuliwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, biashara ya uuzwaji wa wanyama hai ni lazima iwepo? Tunaminywa sana kama nchi, *rate/price given* pia ni ndogo sana; kwa nini wanyama hai wauzwe nje ya nchi? Kwa mantiki hii, hatutakuwa na *hunting business* wala utalii wake maana wataanzisha 2000 huko huko nchini mwao, watakuja kufanya nini kama wanyama wetu wameshawachuka? Hii biashara ya wanyama hai nje ya nchi ikome!

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Uranium* usitishwe; kwanza, kwa sababu haukuhusisha Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira; vile vile ya Madini. Pia Bunge Zima halikuhusishwa. Hakuna anayelielewa jambo hili tunazungumzia nini, sasa kwa nini tujadili jambo ambalo halijulikani na halijahusisha vyombo vyetu husika? Kwa nini Wizara ilianza mazungumzo na *UNICEF* na kadhalika bila kuhusisha vyombo husika?

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Ngorongoro Hoteli isijengwe kabisa kwa sababu ipo karibu na Faru ambao ni wanyama adimu Duniani huko ni *rim* ya *Crater.*

Mheshimiwa Spika, katika misitu; *Tanzania Forest Fund* ni ya nini wakati kuna Mfuko huo? Mifuko luluki haileti tija. Misitu ya asili isivunwe. Vibali vya misitu ni tatizo na vina walakini; mfano, kule Mbeya, waombaji wanapewa kibali cha mwaka mmoja lakini mgao wa miezi miwili; inakuwaje? Isitoshe, mgao unatolewa kinyemela hata kwa wasiokuwa na vibali hivyo. Hii ni nini? Wahusika wote wawajibishwe iwe fundisho kwa wengine pia.

Pia kuna uvunaji wa miti ya mturunga na uchomaji wa mkaa katika Msitu wa Asili wa Mporoto Mbeya ambao ndiyo unazunguka Ziwa Lyosi kule Isyonje na hiki ndicho chanzo cha Mito yote inayoingia Mto Ruaha.

Mheshimiwa Spika, naomba nipatiwe majibu/maelezo ya kina.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, mimi naomba nichangie jinsi ninavyoona juu ya Wizara hii muhimu kwa mustakabali wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko makubwa yanahitajika katika Wizara hii ili kuifanya Tanzania kuwa na mapato makubwa yanayotokana na utalii. Mfumo uliopo sasa bado haulinufaishi Taifa katika kuinua uchumi wa nchi. Kinachoonekana sasa ni mfumo ambao inaonekana ni kama mfumo wa kikoloni mamboleo, ambao unahamisha uchumi wa Taifa la Tanzania kwenda nchi nyingine; tukiachwa na uchumi duni na kunufaisha wageni na wajanja wachache. Tumejaliwa utajiri huu mkubwa, Mwenyezi Mungu ametujalia; lakini hadithi inabaki ile ile ya aliyenacho huongezwa.

Mheshimiwa Spika, sioni sababu za msingi kwa nini tuuze wanyama hai nje ya nchi; tena kwa bei ya kutupa! Kwa kufanya hivyo, hatuoni kwamba tunaua utalii ndani ya nchi yetu? Hivi kama wanyama watauzwa huko Ughaibuni, nao wakaweka *zoo* huko; hatuoni kuwa Watalii waliotarajia kuja kuona wanyama Tanzania baadhi wataishia kwenye *zoo* hizo na hivyo kuikosesha nchi yetu mapato yatokanayo na utalii? Nashauri biashara ya kuuza wanyama hai iachwe na ninaomba tamko la Wizara.

Mheshimiwa Spika, nataka kujibiwa na Mheshimiwa Waziri ni lini atafika Mbarali kuonana na Wananchi ili kutatua mgogoro wa mpaka ambao kwa sasa tumefikia hatua nzuri?

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa pia kuwa ni katika Bunge lililopita Mheshimiwa Waziri aliahidi kuwa, angefika Wilayani Mbarali, akishirikiana na mimi Mbunge, kwenda kuwasikiliza Wananchi na kuondoa utata uliokuwepo, lakini hilo halikufanyika. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari mara baada ya Bunge hili afike Wilayani Mbarali? Kama yeye hatakuwa na nafasi kutokana na majukumu ya Kitaifa; je, yupo tayari kutuma Uongozi wa Wizara ili kuja kushirikiana nami katika kuondoa mgogoro wa mpaka pamoja na kesi zilizopo mahakamani ambazo Wananchi wapo tayari kuziondoa lakini upande wa Wizara bado hawajafika kuonana na Wananchi?

Naomba Mheshimiwa Waziri anijibu ili Wananchi wasikie na waone nia ya Serikali *(TANAPA)* ya kutaka kushirikiana nao katika kulindi na kuhifadhi maliasili zetu. Vinginevyo, itakuwa vigumu kuunga mkono hoja kama sitajibiwa.

Mheshimiwa Spika, wanyama na mbuga zetu za Tanzania ni sehemu ya rasilimali zetu za Taifa. Kitendo kinachofanywa na wageni wanaojihusisha na ununuaji wa wanyama hai hasa baadhi ya njia zinazotumika kuwakamata wanyama hawa, havivumiliki kabisa; kwa sababu huwafukuza kwa magari kwa muda mrefu hadi wachoke ndipo wawakamate. Kitendo hiki ni cha kinyama mno; kinatia uchungu; kinafanywa na wageni hawa wasio na huruma! Huwatesa sana wanyama, kitendo hiki ingalikuwa ni kwa binadamu, ingelifananishwa na biashara ya utumwa. Naomba na mimi niwasemee wanyama hawa; tafadhali biashara hii ya utumwa kwa wanyama wetu iachwe, Mungu hakukosea kuwapa maisha wanyama hawa kuishi Tanzania, tuwalinde utalii ufanyike hapa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia picha za wanyama wanaokamatwa zinatia uchungu, tutaua biashara ya utalii, nchi hii hatuna viwanda vya magari, meli na kadhalika. Mungu katupa uchumi huu kwa sababu alijua namna tutakavyoshindana na Mataifa makubwa; kwa kutupa rasilimali nyingi ndani ya nchi yetu, hii ikiwa ni pamoja na madini tuliyonayo kwenye ardhi yetu. Upo ujanja wa Mataifa yaliyoendelea, kuja kujichukulia madini kwa kutuachia faida kidogo. Nashauri tusiwe wajinga hata katika hili; madini yasichimbwe kwa masharti yenye manufaa makubwa kwa wageni. Uwepo utaratibu wa wazi wa kueleza Mikataba inayofanywa na Serikali dhidi ya wawekezaji wa uchimbaji wa madini. Hii itasaidia kujua manufaa ya Mikataba hiyo kwa Taifa; kukiwa na usiri inatia shaka kuwa huenda kuna maslahi binafsi kwa baadhi ya watendaji wasio waadilifu. Nataka kujua tatizo linalofanya kuwe na usiri kwenye Mikataba. Kuwapa taarifa Wabunge ni rahisi tu kwani Vikao vya Bunge vipo karibu karibu; kila baada ya miezi miwili; naomba nijibiwe.

**MHE. BRIG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nilikwishaonana na Mheshimiwa Waziri kuhusu kibali cha kujenga barabara kupitia Msitu wa Asili Shaghayu, itakayounganisha Kata ya Mbalamo na Kata ya Mlalo katika Jimbo la Mlalo. Suala la *Environmental Impact Assessment, NEMC* walitaka shilingi milioni sitini; Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto haina pesa hizo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, wakati wa Kampeni za Uchaguzi wa 2010, alitoa ahadi hatika mkutano wa hadhara, Mjini Lushoto kwamba, barabara hiyo lazima itajengwa *with or without EIA.*

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mbaramo, barabara hiyo ni ukombozi wao. Tayari Wananchi wa Mbaramo na Mlalo, kwa msaada wa Halmashauri yao, wamekwishachimba barabara mpaka kwenye mipaka ya Msitu wa Shaghayu. Kisingizio cha kulinda vyanzo vya maji siyo sahihi kwa sababu barabara zote katika Wilaya ya Lushoto zimepita katika misitu. Kwa hiyo, Wanachi wanaona kuwa hoja ya *EIA* ni njia ya kuwakosesha haki yao ya kupata mawasiliano ya barabara.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Jimbo la Mlalo wanaomba wapatiwe kibali cha ujenzi wa barabara hiyo kupitia Msitu wa Asili wa Shaghayu.Nawasilisha.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayofanya katika suala la uhifadhi wa wanyamapori, misitu na maliasili nyingine. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imeandaliwa vizuri na pia iliwasilishwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara hii ni makubwa na maeneo ya nchi yetu ni makubwa kwa kuwa maliasili zipo kila mahali. Inashangaza sana kuona Wizara nyingine karibu zote zina Naibu Waziri lakini Wizara nzito kwa majukumu (Maliasili na Utalii), ina Waziri tu bila Naibu.

Mheshimiwa Spika, suala la wanyanya walioibiwa na kusafirishwa nje ya nchi linashangaza na watu wote wanajiuliza maswali; walisafirishwa vipi; toka pori lipi au hifadhi ipi! Je, Uwanja wa KIA hauna vyombo vya ulinzi na usalama; Polisi, Uhamiaji, Usalama wa Taifa na kadhalika? Walioshiriki katika kashfa hii, wanastahili kushtakiwa kama wahaini.

Mheshimiwa Spika, kuna uharibifu mkubwa sana wa mazingira katika misitu iliyohifadhiwa. Watu hujipenyeza katikati ya misitu na kuweka makazi, wanalima, wanachoma mkaa, hivyo miti huteketea ingawa kwa pembezoni msitu unaonekana upo salama.

Mheshimiwa Spika, je, walinzi wa misitu hawapo *(forest rangers)*? Kutokana na hali ya uharibifu wa misitu na mapori; ni muhimu sana kwa Wizara kuhimiza upandaji wa miti ya asili na isiyonyonya maji ardhini.

Mheshimiwa Spika, namtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri katika utekelezaji wa Bajeti hii. Naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu sana wa kutangaza vivutio vya utalii nchini. Je, Serikali inaona umuhimu huu? Kama inaona kuna umuhimu; je, ina mikakati gani?

Mheshimiwa Spika, kuna Watalii wanaoingia nchini kwa kupitia nchi jirani . Je, hii haiathiri nchi yetu kimapato?

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nimpongeze Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa kazi nzuri anayoifanya akiwa peke yake bila ya Naibu Waziri. Mimi napenda niishauri Serikali kuwa, ihakikishe Wananchi wetu wanafaidika na Sekta hii ya Utalii. Unaweza ukaona hoteli za kitalii zimezungukwa na Wananchi lakini ajira katika hoteli hizo wanaajiriwa watu kutoka nchi jirani kama Kenya, Botswana na nchi nyingine. Pia hifadhi za wanyama, Wananchi wa maeneo yanayozungukwa na hifadhi hizi hawafaidiki. Naomba sana Serikali iwafikirie watu hawa wanaoishi jirani na hifadhi hizi.

Mheshimiwa Spika, misitu yetu inavunwa kiholela, hakuna uhifadhi maalum, miti inakatwa bila ya kupanda mengine. Pawekwe sheria ndogo ndogo katika vijiji vyetu, anayekata mti basi apande mti mwingine na kuwe na utaratibu wa kuangalia kuwa haya yanatendeka.

Mheshimiwa Spika, watu wetu wanapanda miti lakini hakuna taaluma wanayoipata ili waishughulikie miti ikue. Wafugaji wetu hata watu wakipanda miti basi wao wanailisha wanyama, kuwe na utaratibu wa kutoa mafunzo kwa watu wetu namna ya kupanda miti. Pia Serikali yetu itoe taaluma ya kuhifadhi na kuishughulikia baada ya kwisha kuipanda miti hii ili isiharibiwe na wafugaji au watu wengine.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii juu ya madhara yatokanayo na uharibifu wa wanyama wakali watokao katika Hifadhi ya Serengeti kwa Wananchi wa vijiji vizungukavyo Hifadhi, ambapo huharibu mazao, hudhuru watu na hata kupelekea kuuwa binadamu; kitu ambacho kinatia fedheha na kutoa maswali mengi kwa Wananchi hawa kwamba, Serikali inathamini maisha ya wanyama zaidi kuliko binadamu.

Fidia inayotolewa kama kifuta machozi ni finyu sana. Pili, kuna tatizo la *game rangers* kuwauwa na kuwanyanyasa Wananchi wa maeneo yaliyo kandokando na Hifadhi za Wanyama. Mfano halisi, kwenye Bunge la Aprili au Februari niliuliza swali kuhusu Wananchi sita wa Gibaso waliouwawa au kupotea katika mazingira ya kutatanisha tangu mwaka jana hadi leo na ukizingatia kuna vijana wawili walinusurika na wangekuwa watu muhimu katika kutoa msaada ili kujua hatima ya watu wale sita. Naomba katika majumuisho, Waziri anipe majibu katika hili jambo ikiwa ni pamoja na mauaji ya watu kwa wanyamapori Tarime na Serengeti.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu *TANAPA*; imekuwa inalalamikiwa kutotenda haki kwa kiasi kikubwa pale inapotoa maeneo ya uwekezaji wa hoteli kwa usiri mkubwa bila ya Watanzania kujua, yaani bila ya kuweka kwenye gazeti na hivyo kuwapa wageni. Hili ni dhahiri hasa kwenye Hifadhi ya Serengeti, ambako kuna makampuni ya kigeni yanayoendesha shughuli za kitalii (*Tour Operators*), ambao wanapewa ardhi na kujenga *Permanent Tented Lodges* hasa maeneo ya Grumeti River, Kaskazini Mashariki ya *Serengeti National Park*, bila kufuata Sheria ya Utoaji wa Zabuni kwa Umma. Makampuni ya kigeni yaliyopewa ardhi ni sokwe asilia, *Lewala Tented Camps, Tree Tops* na Nomad. Nataka majibu ya kwa nini *TANAPA* wanafungua mdomo kwa rushwa na kushindwa kufuata masharti ya *Public Procurement Act,* inayoelekeza *tender* kutangaza. Hii ni fedheha kuona *TANAPA* hawatoi fursa hii kwa kampuni za kizalendo, maana hii ni rasilimali zetu. Wanakuwa wagumu kwa hili; *why?* Watoe kwa wote; wageni na wenyeji. Kwa nini Serikali imekuwa kimya badala ya kuinyooshea kidole na kuikemea TANAPA? Nashauri Bodi hii ivunjwe.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine hai ni kuhusu shughuli za *Balloon Safaris* ndani ya Hifadhi ya Serengeti. *TANAPA* walimpatia *Serengeti Balloon Safaris* hati ya kuendesha *Central Serengeti* kwa ku-*operate Baloon* moja tu kwa eneo hilo. Cha ajabu, kampuni hii iliendelea kupewa vibali vya kuendesha shughuli zake awamu kwa awamu bila ya kutangaza *tender* na sasa wana kibali cha kuendesha shughuli kwenye hifadhi yote ya Serengeti. Ikizingatiwa makampuni ya wazawa yakiomba yanaambiwa hakuna nafasi. Nataka kujua wamiliki wa hii kampuni; na kwa nini wahodhi mbuga nzima? Nataka Waziri aniambie kwa nini hakuna hata kampuni ya wazawa iliyopewa fursa yoyote ya kuwekeza iwe hoteli; *Permanent Tented Camps; na Balloon Safaris*. Katika kunipa majibu kwa hili, vilevile upo uozo kwenye Hifadhi ya Tarangire, ambapo Kampuni ya *Mada Hotels* hurusha *Ballon Safaris.* Hii nayo ni dhahiri kama kuna mkono wa rushwa kwa *tender* hazikutangazwa.

Mheshimiwa Spika, suala la *concession fees* limezungumzwa sana. Hivyo, natoa rai Serikali ifuatilie na kuhakikisha *concession* hailipwi kama ilivyoelekezwa; ni aibu kuona wenye hoteli wanakiuka lakini hawachukuliwi hatua.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu kuhusiana na madhara ya wanyama kwa Wananchi na fidia kiduchu inayotolewa, kuhusu mustakabali wa watu wale sita waliopotea baada ya

kutuhumiwa na *game rengar* na risasi kusikika tangu Oktoba 2010 kuhusu *TANAPA* kukiuka masharti ya kuitangaza *tender* ya kuwanyima wazawa maeneo ya kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na kuweza kufika katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukue fursa hii, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri, ambayo imejaa matumaini kwa Watanzania ambao wana hamu na maendeleo ya nchi yao ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii, nichangie Hotuba hii katika upande wa Utalii. Utalii ndiyo chanzo cha kuingiza fedha katika nchi yetu. Utalii ni Sekta ambayo bado hatujaipa kipaumbele, kwani bado nchi yetu hatujaweza kuitangaza vizuri katika Soko la Dunia, kwani tumekuwa tukipokea Watalii ambao bado siyo wa kiwango ambacho kinaendana na mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imepata bahati kubwa ya kuwa na vivutio vingi vya utalii, ukilinganisha na baadhi ya nchi jirani, lakini nchi kama Kenya, Watalii ambao wanatembelea katika nchi hiyo wanachajiwa fedha nyingi kutokana na walivyojipanga vizuri katika kujitangaza.

Mheshimiwa Spika, wenzetu hawa wanakuwa wakijaribu kutangaza hata baadhi ya vitu vyetu na kuvifanya vyao na kuweza kujipatia mapato.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuwa, Mheshimiwa Waziri aanze kujipanga vizuri katika sekta hii muhimu katika nchi yetu; kwanza, azidishe matangazo ndani ya nchi na nje ya nchi; pili, hata bei za kiingilio cha kwenye mbuga zetu ziongezeke, lakini mazingira yaboreshwe ili Watalii hao waweze kuvutika zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wabunge wengi wamechangia kwenye Sekta hii, naomba niunge mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri na Watendaji wake wote, kwa kuandaa Hotuba hii na kuleta Bungeni ili tuijadili.

Mheshimiwa Spika, mchango wa Wizara hii muhimu sana hapa nchini kwenye Pato la Taifa bado ni mdogo sana, haulingani na rasilimali za wanyamapori, misitu, mambo ya kale na nyuki tulizonazo hapa Tanzania. Mchango wa asilimia 17.2 ya Sekta Ndogo ya Utalii bado ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ikisimamiwa vizuri kwa kuondoa mianya ya rushwa kwenye sekta zake zote, kuwepo na watumishi waadilifu, kuvitumia vivutio vyetu kikamilifu na kutokulindana watendaji wabovu, Wizara hii pekee inaweza kupunguza umaskini kwa kiasi kikubwa na hata kuinua sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, misitu ya asili hapa Tanzania kwa kiasi kikubwa imeharibiwa vibaya sana na hakuna upandaji wa miti unaoendana na uharibifu.

Mheshimiwa Spika, Viongozi na Watendaji katika ngazi ya Wilaya, Tarafa, Kata na Vijiji, wanachochea uharibifu mkubwa wa misitu na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ieleze ni hatua gani zinachukuliwa za haraka kuokoa Misitu ya Hifadhi ya Mamiwa North na Mamiwa South iliyoko Morogoro, ambapo Watendaji wa Serikali wa Wizara hii ndiyo wameweka mashine za mbao katikati ya msitu na wanasafirisha mbao.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kutoa *OC* kwa Idara ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwenye Halmashauri zetu ili Afisa Maliasi wapate uwezo wa kusimamia uondoshaji na

uhifadhi wa misitu katika Halmashauri. Maafisa Maliasili wamekuwa wanakaa ofisini na kulindwa kwenda kwenye *field.*

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe maelezo kuhusiana na Kampuni ya *TH – CITIES* inayokusanya mapato yatokanayo na Hifadhi za Jamii *(WMA)* zilizoko Arusha. Hii kampuni ipo kwa utaratibu gani na mapato hayo yanakwenda Mfuko gani? Hifadhi hii inasimamiwa na Wananchi kama Sheria inavyosema na Kanuni za WMA za 2002. Serikali itatoa miongozo na wataalam pale watakapohitajika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mikakati gani endelevu ya kuokoa misitu ya Mkoa wa Tabora inayotekelea kutokana na uchomaji/ukaushaji wa Tumbaku. Tumbaku inaingiza pato kubwa kwa Taifa hili na Serikali inajua miti inayoteketea.

Mheshimiwa Spika, tani moja ya tumbaku inakaushwa kwa kuni tani kumi. Pamoja na Serikali kutambua mchango wa Zao la Tumbaku kwenye Pato la Taifa, lakini wameshindwa hata kuweka Programu Maalum kwa Mikoa yenye tumbaku kupanda/kurudishia misitu inayoteketea.

Mheshimiwa Spika, kuanzisha Wakala wa Misitu *(TFS)* ni jambo jema sana; ikiwa itasimamiwa vizuri, itaweza kuokoa misitu yetu kwa kiasi kikubwa ila lazima lengo la kwanza/jukumu lake la kwanza liwe ni kulinda misitu na siyo kuvuna. Tatizo kubwa ninaloliona ni Watendaji hawa hawa wa misitu kukosa uaminifu. Hivyo ili *TFS* iweze kufanikiwa, lazima kuwepo na *reform* (mabadiliko ya watumishi – wezi waondolewe). Pia Wizara itoe semina na mafunzo kwa watumishi wake wafuate sheria, kanuni na miongozo, kulinda Maliasili waliyokabidhiwa na siyo kushiriki kuharibu.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utalii cha Taifa – Dar es Salaam, kuna tatizo kubwa la uongozi na usimamizi. Mkuu wa chuo anaongoza watumishi wengine kidikteta; hashirikishi watumishi kwenye maamuzi yoyote. Kwa miaka 2008 – 2011, watumishi zaidi ya 20 wa kada mbalimbali wameacha kazi na wengine wako mbioni kuondoka. Huyu Mkuu wa Chuo haambiwi lolote na mtu yeyote. Afisa yeyote wa Wizara akitaka kujua tatizo la pale lazima aondolewe, aidha kwa kuhamishwa au kuachishwa kazi.

Mheshimiwa Spika, tunazo taarifa kwamba, analindwa na bosi mmoja wa Ikulu na ndiyo maana pamoja na kuwepo na tatizo kubwa kwa muda mrefu, yeye bado haguswi. Naiomba Serikali iunde Tume ikamhoji mtumishi mmoja mmoja, bila kuingiliwa na *Management* ili kujua tatizo lililopo.

Mheshimiwa Spika, Waziri aeleze kama anajua tatizo lililopo na kama anajua ni hatua gani zinachukuliwa kukiokoa Chuo hiki na fedha za umma zinapotea kwa kuajiri watumishi kila leo?

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Maliasili imeshindwa kushughulikia tatizo la Wananchi wa Vijiji vya Mpanda, Mlohoka, Shela na Upele katika Kata za Usinge, Igunzi na Igagalo, Wilaya ya Urambo. Wananchi hawa wamekuwa wanasumbuliwa, wananyang'anywa mifugo yao, kuchomewa nyumba zao na hata kuuawa na polisi mara kwa mara kwa sababu wapo hifadhini.

Mheshimiwa Spika, Vijiji hivi vimesajiliwa, vipo kisheria, vina mipaka yake, vina Serikali zao na Uongozi wa Kisheria. Wamekaa maeneo yao tangu miaka ya 1970, leo wanaambiwa wako hifadhini. Naomba Serikali itoe maelezo hapa leo; kwa nini Wananchi hawa wanakuwa wakimbizi ndani ya nchi yao? Nini hatima ya tatizo hili ambapo Viongozi wa Wilaya ndiyo wanaotuma Polisi, Afisa Wanyamapori na Mgambo kunyanyasa?

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuanza kwa kumpongeza Waziri wa Maliasili, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa maandalizi mazuri ya Hotuba ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuchangia Hotuba hii, napenda kuzungumzia mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, hakuna atakayeshindwa kuelewa kuwa misitu yetu hasa ya asili na mapori, yanazidi kuangamia kwa watu kuamua kuingia ndani ya misitu hiyo na kukata miti ovyo ili kupata magogo, mbao na kadhalika au kuchoma moto ovyo bila kuangalia athari zake kama nchi kimazingira. Sioni juhudi kubwa ya Viongozi wote Kitaifa, Kimkoa na ngazi za chini, wakikemea suala hili na kuchukua hatua kali. Tunajimaliza wenyewe kama Taifa. Napenda kuishauri Serikali ihakikishe kwamba, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS)*, inapewa mamlaka ya kutosha, nyenzo au vitendea kazi vya kutosha ili waweze kufanya kazi na kuweka mipango mizuri ya kuiokoa misitu yetu. Si kuiokoa iliopo tu, bali pia kuiendeleza na kusimamia upandaji wa miti mingi katika maeneo mbalimbali ya wazi hapa nchini. Dalili za kuibuka kwa jangwa hapa nchini zimeanza kuonekana; ni lazima hatua za haraka zichukuliwe.

Ajenda ya Hifadhi ya Misitu iwe ni ya kudumu kwa Sekta zote zinazotumia Ardhi kama Rasilimali kubwa kama Kilimo, Nishati, Madini, Maji na kadhalika. Viongozi katika ngazi zote, wahamasishwe kuzungumzia suala la uharibifu wa misitu na mapori na kulikemea. Miaka ya zamani, Wananchi waliruhusiwa kumiliki misitu na mapori yanayowazunguka vijijini na kuhakikisha inahifadhiwa kwa kutungiwa sheria za kimila. Kwa njia hiyo, hakuna mtu aliyethubutu kuingia katika misitu na kuiharibu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba ni kweli Sekta ya Utalii hapa nchini inaiingizia uchumi wake kwa asilimia 17, lakini ninaamini kama hatua za kuongeza eneo kubwa linaloendelezwa kwa utalii, asilimia hii ingeongezeka. Naelewa Wizara inajitahidi sana kutangaza vivutio vya utalii wa Tanzania kwa nguvu kubwa ndani na nje ya nchi, lakini haisaidii sana iwapo miundombinu katika maeneo hayo yenye vivutio ni mibovu. Kwa mfano, nchi hii inahitaji utalii katika Mikoa ya Kusini na Kusini Nyanda za Juu kama Mbuga za Ruaha, Kitulo na kadhalika. Maeneo hayo hayana barabara za kuaminika, sioni namna ambayo Watalii watatembelea maeneo ya Kitulo, ambalo ni eneo lenye vivutio vizuri sana, lakini halipati Watalii wa kutosha kutokana na ubovu wa barabara. Kuna umuhimu wa Wizara hii kupewa fedha za kutosha ili kutengeneza barabara ziendazo katika mbuga hizo. Hali ni mbaya sana. Wizara hii pia iwe na mawasiliano ya karibu na Wizara ya Ujenzi ili kuainisha barabara zinazopewa kipaumbele katika matengenezo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo mfupi, naunga mkono hoja hii.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa Hotuba nzuri. Pia bila kumsahau Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara. Wizara ya Maliasili ni muhimu sana, kwa sababu inagusa vitu asilia ambavyo ni vya muhimu sana. Nikichukulia vyanzo vya maji, vinatetgemea uwepo wa uoto asilia wa miti.

Katika Wilaya ya Geita, miaka ya 80 kulikuwa na uwepo wa uoto asilia wa mapori *(heavy forest*), lakini leo hii kuna ukataji wa miti wa hali ya juu sana, kiasi kwamba hali ya hewa imebadilika sana, mvua zimepungua ukilinganisha na miaka ya nyuma. Hali ikiendelea hivi, kuna hatari kubwa mbele ya kuwa na ukame mkubwa sana kutokana na shughuli za uchimbaji wa madini. Kwa hali hii, ninaiomba Wizara iangalie utaratibu maalum ili kunusuru hali hii.

Katika Msitu wa Hifadhi ya Taifa Geita, ipo kasi kubwa sana ya kukata miti kwa ajili ya kupasua mbao na pia kwa ajili ya mkaa. Wizara ya Maliasili itusaidie kupata njia mbadala na kupata nishati hii muhimu kwa ajili ya kupikia. Hata kwa kupata teknolojia bora ya kutumia *bio-gas* itasaidia jamii kuacha kukata miti ovyo kwa ajili ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara itoe elimu ya mara kwa mara kwa jamii kuhusu umuhimu wa kutunza mazingra na pia kusisitiza upandaji miti katika maeneo ya wazi. Hii itasaidia sana kuboresha mazingira yetu tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara ifanye mambo matatu muhimu: Kwanza, kuwepo Programu Maalum ya Utunzaji wa Mazingira katika sehemu za machimbo; pili, kuwepo na mpango mbadala wa nishati; na tatu, elimu ya mara kwa mara ya utunzaji mazingira itolewe.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, kero kubwa iliyopo katika Majimbo yetu na Wilaya zetu ni migogoro kati ya vijiji vivyopakana na Hifadhi za Taifa kwa wakulima na wafugaji (makazi, malisho na mashamba).

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ichukue hatua za haraka, kuainisha/kupima mipaka hiyo katika maeneo yenye migogoro kipekee; migogoro ya Vijiji vya Lositete, Mbulumbulu, Tloma, Mang'ola juu na Endamaghan vinapakana na Hifadhi ya Ngorongoro. Ufumbuzi unatakiwa haraka.

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Chemchem, Endallah, Kansay na Buger, vinavyopakana na Hifadhi ya Manyara; kero hii inatakiwa kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu. Ni vyema Serikali iwashirikishe Wananchi katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na usumbufu mkubwa sana wa wanyamapori kuvamia mashamba ya Wananchi na kuharibu mazao yao na mara nyingine watu kuuawa. Serikali ihakikishe kunakuwepo askari wa kutosha katika maeneo yote ya Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, biashara ya wanyamapori kimsingi haina tija kabisa kwa nchi yetu. Hii ni rasilimali ambayo Tanzania tumejaliwa na Mwenyezi Mungu; siyo vyema kuhamisha rasilimali hii kwenda kwingineko na tena kufanyika kwa namna ya wajanja wachache wasio na uzalendo kwa nchi yao. Wanyama wanahamishwa nchini na Serikali ikidai kwamba hawana habari, mnyama anapakiwa toka hifadhini hadi uwanja wa ndege bila kufahamika! Nafiriki Serikali haikuwa makini; huu ni mchezo mchafu; inatia mashaka kuhusu ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali inapata kigugumizi katika kutatua matatizo hayo? Hii inaashiria ushiriki wake katika kutorosha/kuibwa kwa wanyama hao. Wahusika wote wawajibike na wawajibishwe.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kupitia Wizara hii na Idara zake, kutoa huduma ya jamii kama ujenzi wa Zahanati/Shule na kadhalika. Pamoja na pongezi hizo, bado mchango wake ni mdogo sana ukilinganisha na inavyopasa kufanya kwa maendeleo ya nchi. Hifadhi tulizonazo na kama mapato yake yatasimamiwa vizuri, nchi hii haina sababu ya kulia kila siku juu ya umaskini. Serikali iwe makini kwa rasilimali zake kwa maendeleo ya watu wake.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri pamoja na Kamati yake ya Kudumu ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia machache kuhusu usimamizi wa ulinzi wake. Inashangaza kuona jinsi shughuli nzima ya usimamizi na ulinzi wa wanyamapori; kwanza, sehemu zingine za hifadhi hizi zipo jirani na makazi ya watu; kama ni jirani na makazi ya watu ni wazi kwamba, kuna mashamba pia ambayo huwa yanaharibiwa na wanyama hawa kama vile tembo na hata Nguruwe, ambao huwa waharibifu sana wa mazao mashambani. Inapotokea wanyama hawa kuharibu mazao, wakulima wanathirika na uharibifu huo, watu wenye dhamana wapewapo taarifa, huwa hawatilii maanani, badala yake majibu yatolewayo siyo ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, kama mtu atabahatika kupata fidia huwa siyo kiasi cha kuridhisha. Ikitokezea mkulima kukasirika kwa kuharibiwa mazao yake na kupewa majibu mabovu au kutojaliwa, akachukua sheria mkononi akamuua mnyama mmoja tu, askari hao huwa wakali sana na hata kuweza kumuua mtu huyo. Sasa ina maana mnyama ana thamani zaidi kuliko mtu na mazao yake. Naiomba Serikali ilizingatie hili ili haki itendeke.

Mheshimiwa Spika, vilevile usimamizi wa uvunaji wa magogo una utata mkubwa sana, kwani baadhi ya askari huwasumbua sana wanyonge ambao hukata miti michache kwa matumizi madogo kama vile mbao labda kwa matengezo ya kitanda ili kujipatia riziki tu. Atanyang'anywa na kuuza yeye kwa wenye pesa wakati vigogo hukusanya magogo, mbao na boriti, kwa magendo kutoka hata ofisini. Serikali iliangalie sana hilo kwani hali hii inaleta dhuluma na uonevu kwa watu wa chini.

Mheshimiwa Spika, vilevile wavijiji/vijiji vinavyozungukwa na hifadhi hawanufaiki na hifadhi hizo zaidi ya hasara tu. Ni vyema pakiwa na viliwazo fulani fulani ili kupunguza makali ya uharibifu na uonevu unaofanywa na askari husika na hifadhi hiyo.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kulinda maliasili tulizonazo hapa nchini. Kipekee, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kufanya kazi kubwa ya kusafiri kwenda Delta ya Mto Rufiji na baadaye kwenye Bahari ya Hindi hapo mwezi Mei ili kuangalia rasilimali za Maliasili, zilizopo kwenye Kanda hii. Kutembelea eneo hili kunahitaji si tu ujasiri, bali pia uzalendo wa hali ya juu, kwani unakabiliana na matatizo makubwa ya mawimbi pamoja na hatari mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, eneo hili la Delta ambalo ni maarufu kwa miti ya mikoko, lina changamoto nyingi sana. Changamoto hizi ni pamoja na kuzuiliwa kulima katika eneo la kapa (*mangrove swamps*).

Mheshimiwa Spika, Wananchi wanaoishi katika maeneo haya, wapo kwa zaidi ya miaka 400 iliyopita. Wakati wa biashara ya *Wind Trade* baina ya Persia na Afrika Mashariki, Waarabu walikuwa wanakwenda kwenye maeneo haya ya Delta ili kununua miti hiyo ya mikoko. Tangu wakati huo hadi sasa, watu wa maeneo hayo wanaendelea kufanya biashara ya mikoko.

Mheshimiwa Spika, pamoja na eneo hili kuwa na mikoko mingi pia eneo hili lina rutuba nyingi kutokana na matope yanayotokana na *deposition* inayosababishwa na mafuriko ya Mto Rufiji. Kutokana na hali hiyo, Wananchi kwa kiasi fulani, wamefyeka miti hii na kutumia ardhi kwa kilimo cha mpunga. Kitendo hiki cha kukata miti na kutumia ardhi hiyo kwa kilimo ni makosa kutokana na Sheria za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza ni kitendo cha Serikali kung'ang'ania sheria bila ya kutatua matatizo yanayowakabili Wananchi hawa. Sheria hii ni ya hivi karibuni, lakini Wananchi wanaishi katika maeneo hayo kwa zaidi ya miaka 400. Je, nani ni mvamizi; sheria au Wananchi hawa?

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kuwa, Serikali ikae na Wananchi wa maeneo haya na kuweza kuwatatulia tatizo hili kwa busara na si kwa jazba kama ilivyo sasa. Lazima Serikali iweke mkakati endelevu si wa kuzuia tu, bali pia namna ya kuwaendeleza Wananchi hawa wasio na makosa wanaoishi huko. Kitendo cha Serikali kuwaambia wasilime ni sawa na kuwaambia Wananchi hao wafe, kwani hakuna kazi yoyote inayowapatia Wananchi hao riziki (chakula) chao cha kila siku.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ikae na Wananchi hawa kuanzia sasa hadi mwezi wa Oktoba ili kuweka mikakati ya pamoja bila ya kubaguana na kwa kuzingatia haki za binadanu ili Wananchi hawa waendelee kulima katika maeneo hayo. Si rahisi Wananchi wa maeneo hayo wakaenda kulima nje ya Delta ambako watatumia zaidi ya saa kumi kusafiri na mitumbwi na baadaye kuendelea kutembea kwa miguu kwa zaidi ya saa mbili ili kuyafikia mashamba hayo. Aidha, hakuna miundombinu yoyote ya kilimo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, eneo hili la Delta pia ni zuri sana katika Sekta ya Utalii. Eneo hili lina *beach* nzuri sana, zenye mchanga mweupe, zenye zaidi ya km 40; ni vizuri sana Serikali itangaze eneo hili ili litumike kwa ajili ya utalii. Kwa sasa tayari *flying doctors* wametengeneza Kiwanja cha Ndege katika KIjiji cha Jaja, ambako kila mwisho wa mwezi wanafika na kutoa matibabu kwa Wananchi hawa wa Delta na Vijiji vyake jirani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Madaktari hawa wameshatoa mwelekeo kuwa Delta kunafikika; ni vizuri basi na serikali ikaendeleza eneo hili kwa kuzitangaza *beach* zake ambazo ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ni mchapakazi na ameanza vizuri, isipokuwa katika Wizara hii kumeharibika kuna mambo hayaendi vizuri, nashauri wasafishe kwa utaratibu ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kama watabaki bila mabadiliko basi waondolewe ili kulinda rasilimali za nchi pamoja na *integrity* ya Wizara yenyewe na kama wanaweza kuja na mabadiliko, wasimamiwe kwa karibu na wao wakubali kusimamiwa kwa mtindo wa kasi zaidi ya Mheshimiwa Jakaya, vinginevyo watapitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Nkasi Kusini kuna Hifadhi ya Wanyana ya Lwanfi, Halmashauri ya Wilaya wamekwisha kubali kuipa *TANAPA* Pori hili ili liweze kulindwa kikakamavu zaidi kwa makubaliano kuwa pawepo kurekebisha mipaka ili mahitaji ya Wananchi jirani wa vijiji vinavyozunguka Pori, waachiwe walau kilomita tano ili wazitumie kwa kilimo na kupata nishati za kuni kwa kupikia, hakuna namna. Vijiji vya Mtapenda, Kakoma, Isale, Ntuchi China, Kitosi, Kate na Kasapa, vimebanwa sana na hifadhi hii. Vilevile vijiji vyote vya Kando ya Ziwa Tanganyika wamebaki hawana maeneo ya kulima na kutafutia nishati ya kuni. Nataka maelezo ya Wizara; hili la mipaka wamelizingatia vipi?

Mheshimiwa Spika, Nkasi Kusini ina Ziwa Tanganyika; ni Maliasili inayotusaidia lakini bado Wananchi hawajawezeshwa vya kutosha kiuchumi ili rasilimali hii iwasaidie vilevile elimu juu ya matumizi bora ya Ziwa. Waliopo, kazi wanazofanya ni faini tu kwa Wananchi na wanakuwa watu maalum kwa wakazi wa maeneo. Rushwa na faini ndiyo kitu watu wanachofahamu. Mabwana Samaki, Mabwana Nyama, wanafanya ukatili. Maafisa Wanyamapori wanauwa watu kila mara, hakuna hatua wanayochukuliwa. Nchi hii ni ya utawala wa kisheria na si mauaji tu na vitendo vya kikatili kupita kiasi. Tafadhali, Mheshimiwa Waziri ajaribu kumaliza jambo hili. Nchi siyo ya kitumwa.

Mheshimiwa Spika, usafirishaji wa wanyama nje ya nchi ni aibu nyingine; nashukuru Waziri Mkuu ametuahidi kuwa linaangaliwa upya, lakini nashauri kuwa hata wale wanyama waliosafirishwa bila kufuata utaratibu, hatua zichukuliwe kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, ni kigezo gani mnataumia kiasi kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi imekuwa ikipata fedha kidogo sana za mapato yatokanayo na maliasili wanyamapori na zimekuwa zinapungua badala ya kuongezeka; hili halijajenga kielelezo cha kuridhisha maana na faida ya kulinda Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi hii inakabiliwa na wafugaji wakubwa kuchungia mifugo yao ndani ya Hifadhi hii na Maofisa wanaonekana wanapewa visenti kidogo na wanawaacha. Hii inabagua; mbona wakulina hawaruhusiwi kulima ndani?

Mheshimiwa Spika, mwisho, uvunaji wanyamapori unafanywa na majangili na nadhani kuna mkono pia wa Maafisa Wanyamapori kwani suala hili linafanywa na watu wenye fedha pekee na hakuna hatua zozote na Wananchi wanashangaa kulikoni. Litazamwe tafadhali.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayofanya kutumia maliasili ya nchi hii pamoja na Watalii wa ndani na nje kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii inaweza kuwa chanzo kizuri cha kukusanya mapato kama zilivyo nchi nyingine. Idadi ya sasa inaweza kuongezeka ikiwa tutaboresha sehemu zetu za kitalii ziwe za kuvutia zaidi. Kwa mfano, utalii wa bahari unaweza kutuvia sana kama tutaboresha fukwe zetu na tutalinda mazingira ya bahari zetu ili Watalii wapende kuzitembelea. Sekta ya Utalii ina changamoto zake; nazo ni kumong'onyoa maadili ya Watanzania. Sijui ni kwa namna gani tutaweza kuendesha utalii wenye tija bila ya kuathiri mila na desturi zetu?

Mheshimiwa Spikanchi yetu ilikuwa inapoteza rasilimali za misitu (magogo), kwa kuuza nje ya nchi kwa bei ndogo. Fursa hiyo pia ilitumiwa na walanguzi kusafirisha magogo bila kibali; hivyo, kuikosesha Serikali mapato. Naomba Serikali ipunguze kwa kiasi kikubwa, usafirishaji magogo nje ya nchi ili badala yake isafirishe samani.

Mheshimiwa Spika, Zao la Asali limepanda bei hapa nchini na linaweza kusaidia MKUKUTA. Naomba Serikali iwe na Programu Maalum nchi nzima ya kuhamasisha ufugaji nyuki. Kuna tetesi kwamba, asali ya Tanzania sasa inakataliwa katika soko la nje, kwa sababu imegundulika kuwa nyuki wanachukua asali katika maua ya Tumbaku. Je, suala hili lina ukweli gani?

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la Tembo (Ndovu), kuvamia mashamba ya kilimo na kuharibu mazao ya wakulima. Pamoja na juhudi za Serikali za kutenga mifugo, lakini bado sehemu nyingi zinaharibiwa na Ndovu na jambo hili linaweza kusababisha njaa hapa nchini.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, naomba nijitambulishe kuwa niliwahi kufanya shughuli za ku-*promote* utalii wa Tanzania nchini Marekani.

Mheshimiwa Spika, utalii siyo kuleta watu wa kuangalia Mlima Kilimanjaro, wanyama na maziwa. Utalii ni fani kubwa na inahusisha shughuli nyingi sana zinazoangukia chini ya aina nyingi za utalii zikiwemo *Ecotourism, Cultural Tourisim* na *Voluntour.*

Mheshimiwa Spika, kuna faida nyingi zitokanazo na utalii zikiwemo faida za kiuchumi, faida za maendeleo ya jamii na upatikanaji wa ajira. Katika suala la ajira, Watanzania wengi wanashindwa kunufaika kwa sababu ya kiwango cha elimu kisichokidhi mahitaji ya Utalii wa Kimataifa. Sababu nyingine inayowafanya Watanzania wasinufaike na ajira itokanayo na utalii ni kukosa *exposure* ya Kimataita.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali badala ya kujikita kutoa elimu ambayo ni *academic,* ikazanie kutoa elimu katika *life skills, human relations, protocol* na vilevile kuna haja kubwa ya kutambua na kuzifahamu tamaduni za wageni wetu kutoka nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba nitumie takwimu nilizokuwa nimezifanyia kazi mwaka 2000 wakati natafuta *feedback* ya Watalii 457 waliokuwa wametoka Tanzania. Kati ya Watalii 457, Watalii 398 walioneshwa kukerwa na mambo yafuatayo: Watanzania hawawezi kutenganisha mambo binafsi na biashara; Watanzania wengi wanakosa *professionalism,* hili ni tatizo Watanzania wengi hawaandaliwi; na Watanzania wengi siyo waaminifu. Katika hili kuna mama mmoja alidai kuibiwa heleni hotelini; hii ni aibu.

Mheshimiwa Spika, lakini kati ya Watalii 457 niliofanya nao mahojiano, Watalii 439 walisema bei za malazi, chakula na vinywaji zipo juu sana ukilinganisha na Kenya.

Mheshimiwa Spika, tukitaka mapato yaongezeke kwenye Sekta ya Utalii, ni lazima tukubali kubadilika ili tuweze kuingia kwenye ushindani wa Utalii wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie usemi kutoka *converstone* kama ifuatavyo, nanukuu: *"Developmental stages of motivated person recognizes desire, faces fears, moves out of comfort zone, sets goals in life, becomes highly disciplined."*

Mheshimiwa Spika, endapo Serikali itarekebisha mambo madogo madogo yanayowafanya Watalii wasirudi tena nchini; ni imani yangu kuwa nchi yetu itapata ongezeko kubwa sana la mapato yatokanayo na utalii. Naomba kuwasilisha.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa jitihada zake za kuleta mabadiliko katika Wizara na hasa katika kuwezesha wazawa kushiriki katika uwindaji wa kitalii kwa kuvifanya vitalu kuwa wazi kwa ushindani.

Katika kusimamia mashirika yaliyoko chini ya Wizara, hatua ya kwanza iwe ni kuwateua Wakurugenzi wa Bodi, ambao wana sifa kielimu na kiuzoefu, lakini pia wawe ni watu wenye *good track record,* uadilifu na uzalendo. Ukishateua watu wa aina hiyo, wapatie *terms of reference* zinazoeleweka na baada ya hapo uwe na imani nao. Hatua ya tatu ni kuwapa uhuru wa kusimamia Menejimenti, Wizara isiwaingilie sana. Tutumie *principle ya eyes on hands off,* tuachane na *micro-management* ya mashirika. Nimetoa ushauri huo kama mtaalamu wa masuala ya Menejimenti.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Wizara kwamba, baadhi ya Wabunge wanaweza waka-*develop* kuwa watu wanaopenda rushwa. Katika hali hiyo ni muhimu Waziri kuwa anakutana na Wakurugenzi wa Bodi kuwakumbusha wajibu wao, lakini kubwa zaidi kuwepo na *system* ya Wizara kupewa taarifa kila *quota* au nusu mwaka.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu Wizara hii ni muhimu sana kwa uchumi wetu. Utalii ni sekta muhimu sana. Tunatakiwa kuboresha vivutio vyetu na hasa miundombinu katika vivutio hivyo kama hoteli na barabara ili Watalii wanapokuja wasipate *cultural shock* wapende kurudi tena.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kwa Serikali kuhakikisha tuna ndege kubwa za kuwaleta Watalii *directly* kutoka nchi zao kuja Tanzania kuliko kupitia Nairobi.

Wakurugenzi wa Bodi za Mashirika yaliyoko chini ya Wizara wanatakiwa washiriki katika *promotion* ya utalii. Wakurugenzi hao ndiyo wanaotoa maamuzi kuhusu *promotion* ya utalii; ni vyema wakahudhuria Maonesho ya Kitalii ili waone *what is on the ground,* lakini pia wapate fursa ya kuzungumza na kuwahamasisha *potential* Watalii waje kututembelea. Wakurugenzi wakishateuliwa ni sehemu muhimu ya Shirika; kama Wakurugenzi hao ni *competent na high committed* kwa maendeleo ya utalii, watafanya kazi nzuri. *There will be value for money.*

Mheshimiwa Spika, tuwalinde wanyama wetu ambao ni kivutio kikubwa wasitoweke, huo ndiyo utajiri wetu. Idara ya Wanyamapori iwe *manned by highly committed people* ikiwa ni pamoja na *Managements* za Mashirika.

Mheshimiwa Spika, misitu inatoweka; *afforestation* ni mkakati muhimu sana wa kuhimizwa na Wizara. Wizara iwe na doria dhidi ya uharibifu wa misitu yetu.

Mheshimiwa Spika, *TTB* haina *capacity*; ni vizuri *TTB* kufanywa Kiongozi katika Masuala ya Utalii, lakini inahitaji kusaidiwa na Wataalam wa Ngorongoro na *TANAPA;* katika Maonesho ya Kitalii huwezi kuacha kutumia Wataalam wa Mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusisitiza kwamba, utalii, madini na kilimo, ndiyo ukombozi wa wanyonge wa Tanzania.

Namtakia kila la heri Mheshimiwa Waziri na Mungu ambariki.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebaini uwepo wa urani *(uranium)* Kiteto, Pori la *Selous* na Namtumbo. Hivi sasa Serikali imo katika juhudi ya kutaka eneo la *Selous* katika hiyo sehemu iliyogundulika urani huitoa katika sehemu ya Pori la Akiba hili kwa vile Pori la *Selous* ni urithi wa Dunia. Ushauri wangu; ni vyema uchimbaji huo ukaanza katika maeneo ya Kiteto na Namtumbo. Kutokana na utekelezaji huo, tutaweza kujua athari za mazingira kikamilifu kabla ya kwenda katika eneo la Selous ambapo ni urithi wa Dunia.

Mheshimiwa Spika, inavyoonekana Wizara hii katika kutangaza biashara ya utalii, nguvu kubwa wamezielekeza kwa Watalii wa Kigeni. Unapotembea nchi nzima, huoni matangazo yanayowatangazia Watanzania nchini. Makampuni mbalimbali yakiwemo ya simu za mkononi ni weledi wa kutangaza makampuni yao. Leo hii unaposhuka Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Nyerere Dar es Salaam, hakuna tangazo linalowahamasisha Wananchi kuanzisha utaratibu wa kutembelea maeneo ya utalii. Ipo haja Wizara ianzishe matangazo ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ninayo taarifa, aidha, ni kampuni au watu 180 wamepewa leseni za kukamata wanyama hai kibiashara. Hali hiyo inaweza ikasababisha wanyama wengi kukamatwa kwa vile wafanyabiashara wa tasnia hiyo ni wengi mno. Ni vyema tasnia hiyo iangaliwe upya, faida na hasara ya biashara yenyewe.

Mheshimiwa Spika, wakati wa msimu hasa wa utalii (*high season*), eneo la Mbuga za Kaskazini linazidiwa na wingi wa Watalii. Hilo hutokezea kwa sababu bado vivutio vya utalii Kusini Magharibi mwa Tanzania havijatangazwa ipasavyo. Kubwa kuliko yote ni kuwa, miundombinu ya maeneo hayo ni hafifu ikiwemo usafiri wa ndege. Je, Wizara kwa kupitia *TANAPA* haiwezi kuanzisha safari za ndege kwenda maeneo ya Kusini na Magharibi? Nia ya kuanzishwa safari hizo iwe ni kuanzisha tu, badaye wafanyabiashara binafsi wanaweza na wao kuanzisha safari hizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina Taasisi ya *TAWIRI* na *TAFORI* kwa ajili ya utafiti. Ninavyoamini mimi, bila utafiti itakuwa hakuna uhifadhi endelevu. Taasisi hizi za utafiti kila mwaka fedha wanayopewa kwa ajili ya utafiti ni kidogo mno. Hali hiyo inasababisha kukwama kwenye tafiti zao. Ninaiomba Wizara kuwa, mwakani fedha ya utafiti iongezwe.

Mheshimiwa Spika, umefika wakati Mapori ya Akiba kuharakishiwa uundwaji wa Mamlaka ya Mapori ya Akiba badala ya kuendelea chini ya Idara ya Wanyamapori. Mamlaka hiyo itawezesha uwepo wa ufanisi kama kwa hiasi fulani ulioko *TANAPA.* Ahsante.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia yafuatayo:-

Kwa kuwa ndani ya Mbuga ya Katavi kuna makazi ya Askari wa Wanyamapori yaliyopo Mlele, ambayo ni ya kisasa na yana miundombinu ya uhakika kwa maana ya nyumba, shule na zahanati; na kwa kuwa eneo hili lipo mbali na makazi ya watu wengine (wanakijiji) hivyo kuwafanya askari kuwa kama kisiwani; je, Serikali inasema nini kuhusu matumizi mbadala ya eneo hilo kama kufanya kuwa Chuo cha Wanyamapori?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inasema nini kuhusu mauaji ya mara kwa mara yanayotokea au yanayofanywa na Askari Wanyamapori kwa raia wanaoishi karibu na mbuga?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inasema nini kuhusu wawekezaji wenye vitalu ambao licha ya kutochangia shughuli za maendeleo katika eneo husika wamekuwa pia wakiwanyanyasa Wananchi ikiwemo kuwapiga? Nini msimamo wa Serikali kuhusiana na hilo?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jana tarehe 17 Agosti, 2011 ndani ya Bunge lako Tukufu imeripotiwa kwamba, tariban wanyama 126 ndani ya nchi yetu, wakiwemo Twiga wanne walikuwa wanasafirishwa kinyume cha sheria. Serikali imefanya au imechukua hatua gani kwa wote waliohusika?

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Malialisi na Utalii, kwa kuwasilisha hotuba yake nzuri na ndiyo leo Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuchangia kwa nguvu zote na kuweza kumsaidia Mheshimiwa Waziri jinsi ya kujipanga kwenye matumizi ya Wizara yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaiomba Wizara iweke wataalam wenye fani zinazolingana na nyadhifa zao ili kuondoa udhaifu w watendaji, pamoja na utata uliojitokeza katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, utoroshwaji wa wanyamapori na ndege kupitia Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro *(KIA),* hili lilikuwa jambo la aibu. Maafisa Wanyamapori, Usalama na Viongozi wa Serikali walikuwa wapi na hata Wizara baada ya kupata taarifa hiyo imechukua hatua gani? Je, sheria ya nchi inaruhusu wanyama hao kurejeshwa nchini?

Mheshimiwa Spika, hali ya ujangili nchini ni mbaya sana; je, Wizara imejipanga vipi ili kuzuia suala hili kwa kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais Kikwete ya kuiongezea nguvu na fursa ili Wizara iweze kutokomeza tatizo hilo la ujangili katika mapori yetu nchini?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, kwani ni hoja muhimu sana na ndiyo hasa roho ya Watanzania. Maliasili ni eneo pana sana na ambalo linashirikisha Wananchi wa hali zote.

Mheshimiwa Spika, ni bora Askari wa Wanyamapori wawe watu wenye mkono, watende haki kwa Wananchi. Pia Maafisa Wanyamapori nao waache kufanya maeneo yanayopakana na hifadhi kuwa ndiyo mtaji kwao, kwa kuwanyanyasa wakazi hao. Katika eneo la Urambo katika Kata ya Usinge katika Kijiji cha Shera, Afisa wa Maliasili pamoja na Askari Polisi waliingia kijijini Shera na kupora ng'ombe wakidai wamewakuta eneo la Hifadhi. Walimpiga Mwenyekiti wa Kijiji alipohoji. Mimi mwenyewe nilikwenda huko na kuoneshwa ng'ombe walipochukuliwa na pia nilioneshwa mpaka ambao unatenganisha Kijiji na Hifadhi. Nilipoombwa nioneshwe risiti, nilioneshwa risiti ambazo zinaonesha ng'ombe wamekamatwa eneo la Mpanda Line, ambapo huko na Kijiji cha Shera Kati kuna mto mkubwa sana, ambapo mtu hawezi kuwavusha ng'ombe, kwani kuvuka hapo panahitaji boti na lazima isombe zaidi ya mara tatu au nne.

Mheshimiwa Spika, tuliambiwa na Afisa Maliasili, Bwana Msusa, kuwa ng'ombe wanachukuliwa lakini risiti hazitolewi na ndiyo tulikuta mtu anachukuliwa ng'ombe sabini lakini risiti inayolipwa na ng'ombe waliochukuliwa ni tofauti. Ng'ombe sabini lakini inaonesha ng'ombe thelathini au arobaini; hii ni dhuluma kubwa.

Mheshimiwa Spika, pia tulimshauri Bwana Msusa kuwa ni wakati mwafaka sasa kufuatilia mipaka halali na kuitisha vikao vya wanavijiji na kutoa mafunzo na kuwaelimisha zaidi. Kama hivyo sivyo, basi Wizara na Serikali kwa ujumla, mvihamishe vijiji hivyo kwani vipo kisheria, vimesajiliwa na vina viongozi wa kuchaguliwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iangalie Watendaji wake ambao siyo waaminifu na wanaoamua kuwasumbua Wananchi kwa manufaa yao binafsi. Kisingizio bajeti mliyopangiwa haijafikia, yaani kiwango manachotakiwa kukusanya hakijafikia, huu siyo uungwana kabisa.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kuwa, kukata miti kuna athari kubwa na hivyo siyo vizuri kutata miti hiyo. Kama siyo kukata miti ili kutafuta nishati ya matumizi ya nyumbani hasa kupikia; ni nini watu hawa wafanye; kufa na njaa au kukaa na chakula kibichi nyumbani? Nadhani sote tunaona ambavyo umeme ni gharama kubwa, hata sisi wa mijini hatumudu, Wananchi wako hoi, uchumi kwa mtu mmoja mmoja ni duni sana, hebu nanyi Maliasili kaeni mfikirie kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Spika, pale wanaposema mkaa ukamatwe, mtu anapokutwa na gunia kama tatu anasafirisha alipe, hii siyo dawa ila ni kuongeza bei ya mkaa toka shilingi 8,000 mwaka 2009 hadi shilingi 18,000 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangi ni kuhamasisha na kuwalazimisha Watanzania wote kupanda miti na Wizara nayo iongeze mashamba ya miti. Pia ni muhimu kuongeza uhamasishaji wa upandaji wa miti mkishirikiana na Wizara ya Mazingira ili kunusuru nchi kuwa jangwa na pia kuwanusuru Watanzania ambao ni dhaifu sana kifedha, kwani ndiyo wengi katika nchi hii. Lazima tukae tufikirie na tuamue kuwasaidia Wananchi wetu kwa umaskini uliokithiri. Ahsante.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia kwenye Hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ana mpango gani juu ya kufufua utalii na kutangaza utalii Mikoa ya Magharibi husuan Kigoma kama inavyotangaza Mikoa ya Kaskazini?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa Mkoa wa Kigoma una maeneo ya kumbukumbu kama *Livingstone Memorial* na Mbuga za Gombe na Mahale, ambapo kuna wanyama/viumbe adimu kama Sokwe mtu ambao ni adimu maeneo mengi Duniani. Licha ya hilo, kuna maporomoko ya Kakombe na Mkenke, ambayo nayo ni vivutio tosha, lakini pia ni mbuga ambayo ipo *on the shore of Lake Tanganyika*. Cha kusikitisha, Mkoa huu unaingiza Watalii 1,000 tu kwa mwaka; wa ndani na wa nje. Hii ni aibu kwa Taifa lenye miaka 50 ya Uhuru. Je, Waziri ana mikakati gani ya kukuza utalii Mkoa wa Kigoma ili vijana wetu wapate ajira na Pato la Taifa likue?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR**: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na kazi nzuri anayoifanya katika kuiongoza Wizara hii kwa uadilifu mkubwa sana, akiwa hana Naibu Waziri wa kumsaidia lakini kwa hakika anaweza. Kwa maana hiyo, nampongeza kwa dhati na ndiyo maana naunga mkono hoja hii leo na napenda kuwashauri Wabunge wenzangu waunge mkono hoja hii ili tuweze kumpa nguvu ya kufanya kazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali itoe elimu kwa wakazi wanaozunguka Mlima Kilimanjaro waweze kusaidia Pato la Taifa kupitia watalii wanaoutembelea Mlima huu, wautunze Mlima huu na waepukane na kukata miti sambamba na kuchoma moto msitu unaozunguka Mlima huu. Utalii ni chachu ya mapato ya nchi yetu; endapo theluji *(ice)* itapungua katika Mlima huu kutokana na uharibifu wa mazingira, Tanzania itakosa Soko la Utalii katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, naomba Serikali iutangaze Mlima huu nje ya nchi kwamba upo Tanzania na siyo Kenya.

Mheshimiwa Spika, kuna tabia ya nchi jirani ya Kenya kuutangaza Mlima huo kwamba upo Kenya, jambo ambalo siyo kweli; endapo hatutachukua *seriousness* ya kuutangaza Mlima huu, basi wenzetu ambao hawana nia safi ya maendeleo ya nchi yetu, watapata nafasi ya kupotosha zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Chuo cha Wanyamapori MWEKA kina uongozi mzuri sana; na kwa kuwa wakufunzi na wanafunzi wanaheshimu Mamlaka iliyopo kwa maana hiyo wanasoma kwa utulivu bila kupambana na Serikali iliyopo madarakani; na kwa kuwa Chuo hiki kina wanafunzi wa Kitanzania na wa nje ya nchi yetu, kinahitaji makazi, nyumba za kutosha ili wanafunzi wasiwe wanaishi nje ya *Campus* ya Chuo ili kuleta ufanisi katika masomo yao; naishauri Serikali iwajengee majengo ya ziada katika eneo lao ili waepukane na kuishi nje ya *Campus* ya Chuo. Naishauri Serikali iwe inawatengea fungu kubwa zaidi ili Chuo hiki kiweze kufanya vizuri zaidi kwa sababu hivi sasa kinafanya vizuri, lakini kikipata nguvu zaidi basi nacho kitafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Chuo hiki ni cha kupigiwa mfano dhidi ya Vyuo vyote hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR**: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kuchangia leo hii kwa maandishi. Naiomba Wizara hii izidishe kuitangaza nchi yetu ili kuvutia watalii wengi, Pato la Taifa liongezeke kwa sababu tuna vivutio vingi sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uharibifu wa mazingira, naiomba Serikali ipange mkakati endelevu kwa kuwahamasisha Wananchi kulinda vyanzo vya maji na kupanda miti kila kaya iwe ni lazima.

Mheshimiwa Spika, pia naishauri Serikali iongeze adhabu zaidi kwa wale wote wanaohujumu Maliasili yetu kama Wanyama na misitu kwa wale wote wanaokata miti ovyo na kuchoma misitu bila kuzingatia utaratibu.

Mheshimiwa Spika, pia naiomba Serikali ifuatilie uharibifu wa Msitu wa Hifadhi ya Miyenze katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Pori hilo limevamiwa na wachoma mkaa na wakata magogo na mbao. Pori hili linateketezwa kwa kasi kubwa sana hata Mheshimiwa Waziri nimewahi kumtaarifu yote yanayojiri katika Hifadhi hiyo ya Miyenze.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kuleta Hotuba nzuri. Napenda kuchangia eneo moja tu ambalo ni migogoro inayotokana na mwingiliano wa mipaka ya mashamba na Hifadhi za Taifa. Mifumo ni mingi lakini nitaje michache tu:-

Kwanza, mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Taifa na Shamba la Umwagiliaji la Igomelo.

Pili, Mradi wa Umwagiliaji kujengwa ndani ya Hifadhi ya Taifa huko Sikonge.

Tatu, Wanyamapori hasa Tembo kula mashamba ya wakulima yanayopakana na Hifadhi. Kwa mfano, Miradi ya Mpunga huko Kanyonza (Kibondo), Mwega (Kilosa), Mto wa Mbu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka mwaka 2009, mimi mwenyewe nilipokuwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji na Mheshimiwa Ezekiel Maige wakati huo akiwa Naibu Waziri, tulitumwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutafuta ufumbuzi wa mgogoro wa Sikonge.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, ziunde kikosi kazi kitakachojumuisha Wataalamu wa Kilimo, Maliasili na Utalii na Wanasheria ili watafute suluhisho la kudumu kwa faida ya Wananchi wote na kuwaelimisha Wananchi kuhusu rasilimali za Taifa na wajibu wa Wananchi kuzilinda.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo pia inaweza kuangalia maeneo mengine na kuyaboresha kwa kuweka miundombinu ya umwagiliaji kama ikionekana inafaa. Mfano, Mradi wa Umwagiliaji wa Mwendamtitu huko Mbarali, ambapo mwaka 2010/2011, Serikali imetenga shilingi milioni 500 kuuboresha kwa ajili ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Utalii. Aidha, namshukuru Mungu ambaye amenipa baraka kubwa kwangu hata niweze kupata nafasi ya kuchangia hoja hii. Hata hivyo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Utalii Mheshimiwa Maige kwa moyo wake wa kujitolea kuwatumikia Watanzania. Sambamba na pongezi hizo nampongeza Katibu Mkuu wa wizara na timu yake yote kwa kazi ngumu ya kuendeleza utalii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mkubwa katika Wizara hii utaelekea katika sehemu kubwa mbili kama ambavyo zimeainishwa hapo chini:-

Kwanza kwa kuwa *TANAPA* wameshindwa kabisa kutatua kero ya Wananchi wa Kata ya Ilungu katika kuwafidia maeneo yao ambayo *TANAPA* ilifanya tathmini na hatimaye kuchukua maeneo yao bila fidia; naomba Waziri aje mwenyewe na nikiwapo na mimi ili aweze kuongea na Wananchi wa Ilungu kwa ajili ya kumaliza kero hii.

Mchango wangu wa pili katika hoja hii ya Wizara ya Utalii ni kuhusu maeneo ya Milima ya Uporoto yanayozihusu Kata ya Igoma na Ilungu, ambayo pia yalichukuliwa na Serikali *(TANAPA),* kama Hifadhi ya Taifa. Maeneo haya yameathiri sana wafugaji ambao kwa miaka mingi walifugia mifugo yao katika milima hiyo. Baada ya Serikali kuyatumia maeneo hayo, Wananchi hawana tena mahali pa kupeleka mifugo yao. Mwaka jana, Serikali iliahidi kwamba, itawapatia maeneo mengine ya kufugia mifugo yao lakini mpaka leo hii hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iwapatie majibu mazuri Wananchi katika maswala hayo mawili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja tena.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wananchi walikwishaomba mchakato wa Uanzishwaji wa *WMA* – Litumbandyori – Mbinga lakini mpaka leo sijaona hatua zozote kuwasaidia Wananchi kuanzisha *WMA*. Wizara inaanza lini na kumaliza lini mchakato huu? Wilaya imeomba lakini kimya mpaka leo. Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, suala la mipaka ya Pori la Uhifadhi la Litumbandyori ni lazima lifahamike mapema. Wizara imetangaza kugawa vitalu, lakini mambo ya mipaka bado hamjatatua. Tatueni kwanza hili.

Mheshimiwa Spika, nilipata majibu ya Mheshimiwa Waziri kuhusu kuanzisha utalii wa kiutamaduni Mbinga na alisema shughuli hii imeanza. Mimi ni Mbunge wa kule na nafahamu jambo hili halijaanza. Wizara itoe wataalamu, aidha, Bodi ya Utalii tukae pamoja na kuona ni vipi tutaanzisha utalii wa Wanambinga kuvutia watalii.

Mheshimiwa Spika, nimesoma katika Hotuba ya Bajeti jinsi Wizara ilivyosaidia kuhamasisha upandaji miti. Hali ya hewa Mbinga ni nzuri sana kwa miti. Naomba Wizara ije ifanye semina za uhamasishaji.

Mheshimiwa Spika, Mbinga inayo mapori mazuri kwa ufugaji wa nyuki, mwamko ni mdogo sana; semina za uhamasishaji zitasaidia sana. Nipo tayari kushiriki katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Ezekiel Maige (Mb), Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa Hotuba nzuri ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2011/2012 ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika na taarifa iliyopo ukurasa wa 67 wa Hotuba ya Waziri kuwa, Wizara kupitia Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB)*, itaendelea kuboresha tovuti yake kwa kuongeza Lugha za Kimataifa kama Kijerumani, Kifaransa, Kihispaniola na Kiitaliano. Napenda kuitia moyo Wizara na *TTB* kuwa, tusiishie kuongeza lugha hizo bali vilevile *TTB* ianze kuandaa *directory* ya Watanzania wenye uwezo wa kuongea Lugha hizo za Kimataifa pamoja na Kirusi ili pale tunapopata mwitikio mkubwa kutoka nchi inayotumia zaidi lugha Fulani, tuwe na uwezo wa kuwatumia katika kuwapokea hata kuwapa taarifa muhimu za nchi yetu kwa lugha yao. Hii inawapa *comfort* zaidi watalii.

Mheshimiwa Spika, aidha, nimepata faraja kuona Wizara itafungua Ofisi za Utalii katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa ili kuwawezesha wafanyabiashara ya utalii kupata huduma kwa karibu na urahisi. Pendekezo langu Mheshimiwa Naibu Spika ni kwamba, mbali na hatua hii nzuri, Halmashauri zetu zihamasishwe katika maeneo yao kukuza na kuendeleza utalii, kuongeza kasi ya utangazaji wa vivutio na huduma za utalii.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri na kuunga mkono hoja.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kushiriki shughuli za Bunge leo.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, Naibu Waziri,

Katibu Mkuu na Watendaji wake wote, kwa kazi nzuri wanayofanya kulijenga Taifa, lakini kwa Hotuba nzuri iliyoandaliwa.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa una hazina kubwa ya maporomoko ya Mto Kalambo yaliyoko Wilaya Mpya ya Kalambo. Maporomoko hayo ni vivutio vya kipekee na ni mojawapo ya mazao ya utalii.

Mheshimiwa Spika, maporomoko haya yako mpakani mwa Tanzania na Zambia. Kwa upande wa Zambia, eneo la maporomoko limehifadhiwa vizuri sana na kuwekewa ngazi vizuri sana. Kwa hali hii Zambia inajipatia mapato mengi kupitia maporomoko hayo, mapato ambayo Tanzania hatupati kwa vile eneo la maporomoko yameachwa bila kuwa *maintained.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa Rukwa inapata barabara ya kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga, kutoka Sumbawanga mpaka Mpanda, kutoka Sumbawanga kupitia Matai kwenda Kasanga Bandarini (Wilaya ya Kalambo) kwa kupitia Matai kwenda Kasesya, kwa kiwango cha lami; ni wazi kuwa sasa tutapata watalii kwa wingi sana Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, natoa rai yangu kuwa, sasa ni wakati mwafaka kwa Serikali kupitia Wizara hii ya Maliasili na Utalii, itupie jicho kwenye hayo maporomoko ya Mto Kalambo, yafanywe matengenezo ya kuvutia, yanayohitajika kiutalii ili basi tuwateke watalii wote wanaotembelea maporomoko hayo kwa kupitia Zambia.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa ungeweza kusonga mbele kimaendeleo kama tungeweza kupata watalii na fedha zao kama ilivyo maeneo mengine hapa nchini kama Moshi Mkoa wa Kilimanjaro, kwa watalii kuupamba Mlima Kilimanjaro na kutuachia Dola zao.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Waziri ameyatambua na kuutambua umuhimu wa maporomoko ya Mto Kalambo; hivyo, natoa rai kwa Waziri kuyazingatia na kuyafanyia kazi mapendekezo yangu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABAS Z. MTEMVU**: Mheshimiwa Spika, tatizo la mara kwa mara la ukosefu wa malighafi Kiwanda cha *Afri Mech Co. Ltd* cha Vibiriti chapa Kasuku Mbagala Temeke; inasikitisha Kiwanda hiki mara kwa mara kinakosa malighafi. Kiwanda hiki kimeajiri wafanyakazi 600, akinamama, cha kusikitisha Mkurugenzi wa Misitu jinsi alivyokuwa na upendeleo; naomba maelezo kwa nini Kiwanda hiki kinakosa malighafi?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. BETTY E. MACHANGU**: Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa juhudi kubwa inayofanya katika Wizara hii, inayolinda maliasili ya Taifa. Kipekee, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Maige na timu yake, kwa ufuatiliaji kiasi ya kuwa Wizara mojawapo inayochangia pato kubwa la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ninashauri Serikali iendelee kufuatilia kero zitakazoweza kuathiri upatikanaji wa Pato la Taifa. Yapo mambo mengi yanayoweza kuathiri upatikanaji wa Pato la Serikali kama migogoro ya wanakijiji na Hifadhi za Taifa, uvamizi katika Hifadhi za Taifa wanaovamia kulima na kufuga.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iwe na mkakati wa Wizara hii kuajiri Maafisa Misitu wenye ujuzi na uzalendo, ambao watakuwa wanatembelea misitu mara kwa mara kuondoa wavamizi hawa, lakini pia kukamata wezi wa mbao, magogo na kuchoma mkaa, vyema wawezeshwe na bunduki na risasi kujihami. Wavamizi wanakuwa na silaha.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali (Wizara hii), imtake Waziri wa TAMISEMI atoe agizo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya kulinda Hifadhi za Halmashauri za Wilaya na pia

Hifadhi za Taifa. Wakurugenzi hawa wanao uwezo huo na kama Serikali ikiweka agizo hilo kama *one of the performance indicators* ya kumpima Mkurugenzi yeyote wa Halmashauri ya Wilaya, hakika watafanya na misitu yetu italindwa.

Mheshimiwa Spika, misitu inaweza kulinda vizuri pia kama wanakijiji wanaozunguka hifadhi watashirikishwa katika mpango mzima wa kulinda msitu. Muhimu kuwe na fungu la *Participatory Forest Management*. Vyema fungu hili liwepo lifanye kazi. Fungu hili likiwepo, *District Forest Officers* wahakikishe wanashirikisha wanakijiji; mara nyingi *District Forest Officers* wanaongea na wafanyabiashara wa mbao na kutoa vibali bila kuwashirikisha Wanavijiji/ Serikali za Vijiji).

Mheshimiwa Spika, hatua hii itafanikiwa kwa urahisi kama Serikali (Wizara yenyewe), itakwenda vijijini kutoa elimu hii kwa vijiji vyote vinavyozunguka Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, ipo haja pia ya kila anayepewa leseni ya kupasua mbao/kuchoma mkaa, picha yake na kibali chake, kopi yake itangulizwe katika ofisi za kijiji/kitongoji husika ili wanakijiji waweze kumtofautisha na mvamizi mwingine yeyote; yaani Mwananchi ambaye atakwenda kukata/kuranda mbao au kuchoma mkaa, ambaye kijiji hakina nakala ya picha na kibali chake basi wasimkubalie kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko mengi kutoka kwa Wakazi wa Kilimanjaro ya kuwa, fedha ya leseni za utalii ni vyema asilimia kidogo ikabaki katika Halmashauri ya Wilaya husika kwa maagizo kuwa fedha hiyo itumike kusaidia kuulinda Mlima Kilimanjaro (kwa *case* ya Kilimanjaro). *Fees* za Utalii *(TALA)* za $2000 nazo wanalalamikia zipo juu, lakini kama *retention* kidogo itabakia katika Halmashauri za Wilaya za Kilimanjaro, yasingekuwepo malalamiko. Ninaomba Serikali iliangalie hili.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Moshi ulitangazwa kuwa Mji wa Kitalii *(Millenium Town)* tangu mwaka 2000 na aliyekuwa Waziri wa Utalii, Mheshimiwa Zakhia Meghji. Mpaka leo hakuna maendeleo/uwekezaji wowote uliofanywa na Serikali katika Mji huo. Je, Serikali inasemaje kuhusu hili?

Mheshimiwa Spika, upo umuhimu mkubwa wa kuongeza Wanyama katika Hifadhi ya Mkomazi katika Wilaya ya Same. Hii itasaidia Hifadhi hiyo kutembelewa na watalii na hivyo uchumi wa vijiji vinavyoizunguka Hifadhi ya Taifa kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa Serikali ikatafuta aina nyingine ya nishati ya kupikia kwa wakazi walioko karibu na Hifadhi za Taifa, lakini pia hata mijini. Mfano, kuanzisha miradi ya *biogas,* gesi asilia na majiko poa, ambayo itapunguza kasi ya Watanzania kukata miti ili kuchoma mkaa.

Mheshimiwa Spika, familia zinazoishi karibu sana na Hifadhi za Taifa/Halmashauri za Wilaya wamekuwa wenyeji na wavamizi/wezi wa mbao katika Hifadhi hizo. Nashauri Serikali familia zinazozunguka Hifadhi zipewe elimu *(advocacy)* kuhusu athari hizo. Ipo sheria inayoelekeza kuwa, makazi ya watu yawe umbali wa kilomita 70 kutoka Hifadhi hizo. Ninashauri Serikali ilifuatilie ili kuendelea kulinda Hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali kupitia upya mfumo wa kugawa vitalu vya uwindaji ili Watanzania nao wapate nafasi. Naishauri Serikali isirudi nyuma katika hili na naipongeza sana. Hata hivyo, yapo manung'uniko kuwa Dola za Marekani elfu thelathini kama *Block fee* kwa kitalu cha kawaida ambacho hakina wanyama wengi ni ghali.

Mheshimiwa Spika, manung'uniko ni kuwa hali itakuwa mbaya zaidi hasa pale ambapo eneo la uwindaji linatumiwa pia na wafugaji na wanakijiji wengine. Nashauri Serikali iliangalie hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza, nianze kwa kumshukuru Mungu, mwingi wa neema, kwa kuniwezesha afya na uzima.

Mheshimiwa Spika, ili utalii ukue na kutangazika, kunahitajika barabara, viwanja vya ndege, reli na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ambayo tumejaliwa neema ya vivutio vingi, ambavyo vikitumiwa vizuri vitawavutia watalii wengi na kuliingizia pato Taifa. Ninaposema vivutio, nina maana milima, mabonde, mito, maziwa, bahari na mbuga za wanyama pia maporomoko ya maji.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa, Wilayani Mpanda, kuna Mbuga ya Wanyama iitwayo Katavi; ina vivutio vingi na wanyama wengi wakubwa ambao huwezi kuwalinganisha na wanyama wa hifadhi nyingine Tanzania; mfano, Simba, huwezi kumlinganisha na Simba wa Mikumi. Vilevile Tembo, Twiga na Nyati wa Katavi, huwezi kuwalinganisha na wa Mikumi au wa Hifadhi nyingine.

Mheshimiwa Spika, watalii wa kutosha hawafiki mkoani humo kwa wingi, kwa sababu ya ubovu wa miundombinu kama barabara, viwanja vya ndege na reli. Sasa nataka kujua Serikali imejipanga vipi kuhusu suala hili ili kuruhusu watalii wengi kuingia katika Hifadhi hii ya Katavi?

Mheshimiwa Spika, vivutio ni vingi lakini hatuna faida navyo. Mfano, Mkoa wa Rukwa tuna Maporomoko ya Karambo, yanayovutia sana, lakini wanaoingia kutalii ni wageni wanaotoka Zambia, Malawi na wachache wanaopitia nchi hizo jirani, lakini Tanzania haifaidiki na maporomoko hayo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ivae sura ya ubunifu kwa kuweka kipaumbele katika maporomoko hayo na kwa kufanya hivyo kuna faida tutakazopata; mfano, tutakuwa tumeongeza idadi ya vivutio vya utalii Tanzania. Pili, tutaongeza pato kwa Taifa na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla, lakini pia tutakuwa tumetengeneza fursa ya ajira kwa Vijana wa Mkoa wa Rukwa, ambao wanalia na maisha magumu kwa kukosa ajira.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwa kusema siungi hoja hii mkono mpaka haya mambo yote niliyoongelea yapatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya Mwaka 2011/2012. Pia nachukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuandaa Bajeti nzuri, yenye kuainisha namna ya kulinda, kuhifadhi, kudumisha na kuvuna Maliasili zetu kwa manufaa ya nchi yetu, kuimarisha na kuongeza mianya na fursa zilizoko katika Sekta ya Utalii kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Nchi yetu ina bahati ya kuwa na hazina kubwa ya maliasili ambayo ni pamoja na misitu ya asili, wanyamapori wa kila aina, mapango ya asili, maporomoko ya maji katika mito mbalimbali, maeneo ya kihistoria kama njia kuu iliyopitisha Watumwa enzi za biashara ya utumwa, majengo yaliyobeba hazina ya kihistoria, zana za kivita za watawa na viongozi wa jadi wa makabila mbalimbali hapa nchini, nyanda zenye maua ya asili, milima na hasa Mlima Kilimanjaro ambao ni mrefu kupita yote hapa Afrika na una kilele chenye barafu. Hazina hii inaipa nchi yetu umaarufu wa kujulikana ulimwenguni kote. Kwa maana hiyo, tunahitaji kuzilinda na kuzihifadhi kwa faida yetu na ya kizazi kijacho. Pamoja na faida ya umaarufu mkubwa unaotokana na maliasili zilizoko hapa nchini, bado kuna Wananchi ambao kwa ubinafsi wanahujumu maliasili hii ikiwepo uvunaji ovyo wa misitu ambapo wanakata miti ovyo na kusababisha aina ya miti ya asili kama mikoko inayohifadhi kingo za bahari, mipingo na kadhalika kupotea. Kufungua mashamba katika mbuga za wanyama na kuingilia vyanzo vya maji, uwindaji haramu wa wanyamapori na uharibifu wa mazingira kama kuchoma moto ovyo katika mbuga za wanyama, misitu na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa jitihada zake za kukabiliana na vitendo vya hujuma na ukatili kwa kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na misitu. Aidha, kwa kutambua kuwa waharibifu hawa ni miongoni mwa Wananchi wachache wenye ubinafsi na kwamba, wanaishi na kujumuika katika vijiji vilivyozunguka mbuga hizi, Wananchi hawa wameshirikishwa katika ulinzi. Jambo hili limewapatia fursa za kuweza kujikimu kimaisha kama kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo katika misitu hii kama ufugaji wa nyuki unaowapatia mazao ya asali na nta ambayo kwa sasa hivi mazao haya yana soko kubwa duniani. Mwananchi huyu ananufaika kwa kupata pesa za kujikimu kimaisha; hivyo, anawajibika kuacha kufanya shughuli za kijangili za kuhujumu maliasili hizo. Kadhalika, nchi yetu inapata pesa za kigeni. Pamoja na mikakati hii, lakini kuna askari ambao wameajiriwa na Serikali kulinda mali hizo. Napenda kwa dhati kabisa kuiomba Serikali kuhakikisha askari hawa ambao wanaishi katika mazingira magumu ikiwa ni kuishi katika maskani ya wanyama wakali na pia kukabiliana na majangili ambao wamejipanga na silaha kali, kuhakikisha walinzi hawa wanaboreshewa maslahi yao na mazingira ya kufanyia kazi kama kuwapa vitendea kazi ambavyo ni silaha, magari, mavazi ya kinga na makazi bora.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali kushirikisha wadau wote ili waweze kunufaika na rasilimali hizo, kama kuwapa mamlaka wilaya kuunda Kamati za Usimamizi wa Uvunaji wa Mazao ya Misitu na Utoaji Leseni za Uvunaji wa Misitu, lakini bado inaonekana hujuma nyingi zinafanyika. Kuna malalamiko mengi sana kwa Wananchi kuhusu namna leseni zinavyotolewa na ni kwa watu gani. Mamlaka na Kamati hizi badala ya kutoa vibali na leseni kwa kutumia haki inasemekana vibali na leseni zinatolewa kwa wenye pesa au walanguzi ambao wanapanga na wanakamati kwa mapatano fulani fulani. Watu hawa badala ya kuvuna miti iliyokomaa mara nyingi huvuna miti yote hata michanga ambayo haijakomaa ilimradi wanajua watapata pesa. Naiomba Serikali iweke mkazo katika maeneo yote ambayo yana misitu ya asili iliyoruhusiwa kuvunwa. Sheria ya kukata mti panda miti nayo izingatiwe ili tusitengeneze nchi ambayo ni jangwa.

Nasema hivi kwa kujali kabisa maliasili na misitu yetu na sijui tunakokwenda tunawaachia watoto na wajukuu wetu mazingira gani kwani siku za nyuma kwa mfano, ukiwa katika Mkoa wa Morogoro, ulikuwa unaona maji yakitiririka katika Milima ya Uluguru, mito yote ilijaa maji na misitu ilifunga miti kabisa. Leo hii ukiangalia Milima ya Uluguru iko uchi, vumbi tupu na ukame, kwa kuwa miti imekatwa ovyo. Uchomaji wa mapori na misitu ovyo umekithiri. Mioto ya hapa na pale inawashwa na kuteketeza maliasili na wanyamapori bila sababu na ukiuliza utaambiwa ni msimu wa wenyeji kuwinda ndezi. Wanachoma majani ili waweze kukamata vijinyamapori hivyo, moto huu unasambaa kwa kasi kwani hushindwa kuudhibiti. Kweli inasikitisha sana, kuna haja ya Serikali kuendeleza juhudi za makusudi kuelimisha Wananchi manufaa yanayotokana na maliasili na misitu yetu ili wapate kushiriki katika kuhifadhi hazina hii.

Mheshimiwa Spika, nina uhakika nchi yetu ina hazina kubwa ya kuvutia watalii na hata wawekezaji. Nashauri Serikali ifanye mikakati ya kutangaza vivutio vya asili, kwa mfano, Mapango ya Amboni Tanga, maeneo yaliyo na nyayo za watu wa kale, magofu, maeneo waliyotoka Watawala na Machifu wa zamani ambako kuna mambo mengi ya kihistoria, maeneo yaliyopiganiwa vita na kadhalika. Maeneo haya yakitangazwa na kupata wawekezaji ambao watajenga hoteli kubwa kubwa zenye hadhi ya kimataifa, yanaweza kuiingizia nchi pesa nyingi sana. Sambamba na uwekezaji huu, Serikali inatakiwa kujipanga vyema katika kutoa elimu ya mambo ya hoteli na upishi kwa kuboresha vyuo vyake vya utalii hapa nchini. Aidha, somo la kiwango cha huduma kwa wateja kwa wafanyakazi wa hoteli kiwekewe mkazo kwani kimeporomoka sana kiasi cha wanaowekeza katika biashara ya mahoteli kuajiri wafanyakazi kutoka nchi za jirani kama Kenya na Uganda. Kwa kweli inasikitisha sana kwani Watanzania wengi hatujawa na mwamko wa kujituma, kuwajibika na kujali kwamba “Mteja ni Mfalme” kwa maana usipotoa huduma nzuri na kumridhisha mteja, utakosa biashara, hivyo mteja anatakiwa ahudumiwe vizuri, aheshimiwe ili akiridhika na huduma, aje tena kwako au awashawishi na wengine waje kutumia huduma zako. Hii ni sababu moja inayowafanya wenye hoteli kutowaajiri wataalamu wengi wenye taaluma ya hoteli hapa nchini kwa kuwa hawapo tayari kupoteza biashara kwa maana ya wateja.

Mheshimiwa Spika, wakati huu wa utandawazi na soko huria, Wizara inatakiwa ijitahidi kufanya utafiti kupata maeneo mengine yenye vivutio vya utalii badala ya kutegemea maeneo machache yaliyopo sasa. Nchi yetu imejaliwa kuwa na pwani na fukwe salama; hii inaweza kuwa fursa nyingine ya kupanua wigo katika biashara ya utalii. Pwani zetu ambazo ni salama kwa maana ina vina vyenye maji masafi na hakuna wanyama hatari kama Mamba na Samaki wakali, inaweza kutumika kwa michezo ya kuogelea, mbio za mitumbi, majahazi na madau kufuatana na asili za jadi katika Pwani zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuchukua fursa hii kutoa kilio cha Wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini kuhusu wingi wa Mamba waliojaa katika Mto Ruvu, ambao mpaka sasa wanahatarisha maisha ya Wananchi wa Kata ya Ruvu na Kata za jirani. Mamba walioko katika Mto Ruvu ni wengi sana kiasi kwamba wanawafuata Wananchi hadi mashambani. Wananchi wanaoishi kando ya Mto huu wengi ni wakulima wa mpunga, nyanya na mbogamboga. Pia wanafanya shughuli za uvuvi wa samaki wa aina ya Kambale ambao wanapatikana kwa wingi katika Mto Ruvu. Nasikitika kusema kwamba, kuna Wananchi wengi wanaoishi kando ya Mto Ruvu, ambao wamepoteza maisha yao kwa kuliwa na mamba hawa na wengine wamejeruhiwa vibaya na kupoteza viungo vyao. Kwa mfano, kuna Wananchi ambao wamekatwa miguu na wengine wamekatwa mikono na kupata ulemavu wa maisha. Watu hawa kwa kuwa wanaishi vijijini, hawafahamu sheria wala haki iliyopo kama kupata fidia au kupatiwa matibabu na Wizara. Naomba sana sana Serikali itoe elimu kwa Wananchi wafahamishwe haki zao. Mimi naamini kabisa kuna sheria ya kuwapa fidia wahanga wa maafa ya kudhuliwa na mamba au wanyamapori. Sheria na haki hizo zipo katika makabrasha na mafaili ya Ofisi za Maliasili na Utalii. Wananchi hawazielewi na hawajui wakipatwa na maafa wafuatilie wapi kupata haki ya fidia.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mamba wengi katika Mto Ruvu ni kubwa na kwa kuwa Wananchi hawaruhusiwi kuua au kuvuna mamba hawa, naomba Serikali ifanye mipango ya haraka kuweza kuvuna mamba walioko katika Mto huu kwa madhumuni ya kuwapunguza ili wasiendelee kuwa tishio kwa Wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini. Mpaka sasa kuna Wananchi wengi wanaoogopa kufanya shughuli za maendeleo kama kilimo, ufugaji na uvuvi, kwa kuhofia kupoteza baadhi ya viungo vyao katika Jimbo la Kibaha Vijijini ili waweze kuwalipa fidia haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kwanza, kumshukuru Mwenyezi Mungu na Wananchi wa Jimbo la Babati Vijijini. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda na Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri kwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara, kwanza kabisa, kuweka vipaumbele na ifanywe kazi ya ziada ili kufanikisha malengo. Tuna maliasili nyingi ndani ya nchi yetu, namna ya kusimamia maliasili zote zilizopo nchini na changamoto zilizopo, wahusika katika ngazi ya Wilaya, Mkoa hawana usafiri, nyenzo nyingine ya kufanyia kazi, kama elimu ya juu ya maliasili yetu ingetolewa kwa Wananchi na katika Shule zetu za Sekondari na Vyuo Vikuu, uelewa wa Wananchi wengi zaidi ungesaidia kutunza maliasili yetu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara iangalie namna ya kumaliza mgogoro wa Vijiji vya Ayamango, Gedamar na Gidejabong. Leo Waziri ametamka kuwa mgogoro umekwisha, naomba Wananchi hao wapewe maeneo mbadala mapema na pia suala la fidia wanayolipwa iangaliwe upya imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, pia tunaomba Hifadhi za Tarangile na Manyara waangalie namna ya kuweka *electric fence* kuzuia wanyamapori hasa Tembo kuingilia Wananchi na mazao yao kwa wanaoishi jirani na hifadhi. Pia tunaomba utaratibu wa fidia au kifuta jasho/machozi uangaliwe upya, pamoja na hasara kubwa Mwananchi anayopata bado inakuwa adha ya kupata hicho kifuta jasho kidogo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara iangalie namna ya kufungua mageti ya kudumu katika hifadhi kwa upande wa Nagara – Mayoka na Mamire – Mwinkantsi ili Wananchi wa maeneo hayo wapate unafuu kiuchumi. Mageti hayo yakifunguliwa, maeneo hayo yatanufaika kiuchumi na pia itafungua maeneo au *circuit* mpya ya utalii Babati. Tunaomba *TANAPA* watupe ushirikiano wa karibu ili tukae nao na kuwajulisha mipango yetu na faida Wananchi na hifadhi itakayopata.

Mheshimiwa Spika, pia tunaomba Wizara ianzishe bustani ya miche Babati Vijijini na eneo la kuuza mbegu za miti ili tuweze kuboresha hifadhi ya maeneo yetu na tuwe katika orodha na mpango wa kupata elimu na uwezeshwaji wa ufugaji wa nyuki. Itasaidia kupunguza uharibifu wa misitu yetu na maeneo ya hifadhi, ambapo Wananchi watapata mapato ya mazao ya nyuki badala ya kukata miti na kuchoma mkaa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba pia Wizara iangalie na kutusaidia kuboresha Sekta ya Utalii Babati na kusaidia kutangaza maeneo yetu ya utalii.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara iangalie namna ya kufanya semina na kutupa elimu Halmashauri ya Babati juu ya utalii, maliasili na namna ya kushirikiana ili tukuze uchumi na ujirani mwema.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninaamini Wizara itatupa ushirikiano wa karibu.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, niruhusu nimpongeze Waziri wa Maliasili na Utalii, yeye binafsi, Katibu Mkuu wake na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pia nawapongeza kwa kuleta Hotuba hii Bungeni. Pamoja na pongezi hizi, ninayo machache ya kuchangia. Nami nitaanza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wanyama waharibifu hasa Tembo (Ndovu), wameendelea kuwa kero kwa Wananchi wa Vijiji vya Rugera, Katanda, Kibwera, Mlamba na Mshabaiguru, Kata za Kihanga na Rugera Wilayani Karagwe. Kagera pia tatizo hili lipo Vijiji vya Nyakasimbi, Ruhita, Kibogoizi, Nyakakika na Chamuchuzi, Kata za Nyakakika, Rugu, Bweranyange na Ihembe Wilayani Karagwe. Naipongeza Serikali kujenga Kituo cha Wanyamapori Kijiji cha Nyakakika Wilayani Karagwe. Naomba tupatiwe watumishi wa kutosha, magari, silaha na mafungu yafike kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nalipongeza Shirika la *TANAPA* kwa kutangaza utalii wa ndani. Pia nawapongeza Marubani wa Ndege za *Precission Air* kwa kutangaza utalii wa nchi yetu kwa abiria wote wanaosafiri na ndege zao. Naomba Marubani wa ndege nyingine waige mfano huu na wahamasishwe kufanya hivyo. Ili utalii wa ndani ufanikiwe, napendekeza *TANAPA* (Wizara), itenge magari kila mkoa kwa ajili ya kuwapeleka na kuwarudisha watu wanaotaka kwenda kutalii kwani hivi sasa gharama za usafiri ni ghali; mfano, gari kutoka *Mlimani City* kwenda Mikumi National Park na kurudi, inakaribia au kuzidi shilingi 200,000; fedha hizi ni nyingi kwa Mtanzania wa kawaida na hasa ukizingatia kuwa watu wengi wanapenda kwenda kutalii na familia zao. Hivyo, gharama hizi hazimuwezeshi hata kidogo Mtanzania tunayemlenga kufanya utalii katika nchi yetu. *TANAPA* inunue magari mazuri na ya kisasa na Wananchi wachangie gharama za kawaida.

Mheshimiwa Spika, Mapori ya Akiba Kimisi na Burigi yamemega mipaka ya vijiji vifuatavyo; Ruhita, Kahanga, Nyakasimbi, Nyakakika, Chabuhora, Kaiho na Chamuchuzi, Kata za Rugu, Nyakasimbi, Nyakakika, Nyakabanga na Bweranyange Wilayani Karagwe.

Kitendo cha mapori haya kumega ardhi ya vijiji hivi kimeleta kero kubwa sana kwa Wananchi kwani wamekosa eneo la kufanyia shughuli zao za maendeleo ikiwemo kilimo na ufugaji. Wananchi wanapopeleka mifugo yao katika maeneo haya yaliyomegwa na Mapori ya Hifadhi, hukamatwa na Maaskari wa Wanyamapori na kutozwa faini kubwa kati ya shilingi 500,000 - 1,000,000 au zaidi. Hivyo, mfugaji hulazimika kuuza mifugo yake yote.

La kusikitisha, hata risiti ya kukiri kupokea fedha hizi huwa haitolewi na ikitolewa inakuwa ni chini ya fedha zilizotolewa kutokana na hali hiyo. Ninaomba na kuisihi Serikali (Wizara), irekebishe haraka mipaka ya Mapori ya Akiba ya Kimisi na Burigi kwani tatizo hili ni la muda mrefu sana. Kwa nini Serikali inawanyanyasa Wananchi wa vijiji hivi. Katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri,

naomba atupe majibu ya lini mipaka hiyo itarekebishwa. Hatua hii ianze na kukamilika ndani ya mwezi mmoja.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali ifuatilie na kurudisha wanyamapori waliotoroshwa kwenda nje ya nchi kwa kutumia Ndege ya Mizigo ya Shirika la Qatar. Pia wahusika wa ndani na nje wakamatwe na wafikishwe katika vyombo vya sheria na Serikali itueleze (Bunge), hatua zote zilizofikiwa.

Mheshimiwa Spika, ugawaji wa vitalu vya uwindaji uwe na uwazi wa hali ya juu sana na uwalenge wazawa wa kawaida na hata kama uwezo ni mdogo basi wajiunge katika umoja ili Mtanzania wa kawaida naye afaidike na vitalu vya uwindaji.

Mheshimiwa Spika, Mapori ya Akiba Kimisi na Burigi hayana *open space* kwa ajili ya uwindaji. Wananchi wanaozunguka maeneo hayo, wanaomba wapatiwe maeneo ya uwindaji.

Mheshimiwa Spika, mauaji tunayoshuhudia na manyanyaso yanayofanywa na Askari Wanyamapori yakomeshwe. Yeyote atakayevunja sheria, afikishwe katika vyombo vya sheria ili sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, yeye binafsi na Naibu Waziri. Baada ya pongezi hizi, naomba sasa nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi iliyojaliwa mambo mengi yanayoweza yakaongeza mapato ya utalii, lakini bado hayajashughulikiwa ipasavyo. Mikoa yote ya Kusini mwa Tanzania haijatambulika kama inaweza kuchangia katika utalii pamoja na utajiri iliyonayo katika mambo yafuatayo: Hali ya hewa na hali ya kijiografia; uzalishaji wa mazao ya kilimo; *natural vegetation;* na maliasili ya misitu, madini na wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara/Serikali inasema nini juu ya kuboresha utalii *(Strategic repositioning)* katika Mikoa yote ya Nyanda za Juu (Iringa, Mbeya, Songea na Rukwa)?

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali haina Mpango Mkakati Kitaifa kuboresha miundombinu katika Mikoa ili kuboresha Sekta ya Utalii katika nchi hii? Je, Mtalii atafika vipi mbuga za wanyama kama *Ruaha National Game Reserve* Iringa bila kuboresha viwanja vya ndege kama Nduli kilichopo Iringa; barabara kutoka Iringa – Kalenga – Ruaha National Park bila kuweka lami na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, Serikali inashauriwa kuwa wazi katika mambo yenye maslahi Kitaifa na iwe shirikishi katika kutunga Sheria, Sera na Kanuni zinazohusu upatikanaji, uchimbaji, usafirishaji na uuzaji wa maliasili zote za nchi hii kama madini na wanyamapori. Je, kwa nini ushirikishwaji Wananchi ni duni sana na kuzua migogoro?

**MHE. NASSIB S. OMAR**: Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumekuwa tukisikia na kuona migogoro mingi ya mipaka baina ya vijiji vyetu na Hifadhi za Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, migogoro hii imelitia hasara kubwa Taifa kwa uharibifu mbalimbali kama kuteketeza maeneo kwa moto na hujuma nyingine. Pia baadhi ya wakati Wananchi wamekuwa wakihamishwa kwa nguvu. Hatua hii husababisha mali na makazi ya Wananchi hao kupotea na kuharibika. Hivyo ni vyema Wizara iwashirikishe kikamilifu Wananchi katika kuweka mipaka ya Hifadhi zetu. Pia pawe na eneo la *no mans land* katika Hifadhi zote ili kupunguza uharibifu wa Hifadhi. Mipaka iwekwe kwa alama zilizokuwa wazi, zenye kuonekana kwa urahisi katika kuweka mipaka hii njia za kisasa zitumike za kutumia *GPS.*

Mheshimiwa Spika, mwisho, Wizara ijipange vizuri ili migogoro ya mipaka ipungue na kama ikiwezekana kwisha kabisa.

Mheshimiwa Spika, ingawa matangazo ya biashara yamekuwa yakitoka kidogo katika vyombo vya nje vya habari lakini hayatoshi; mfano mzuri ni Nchi ya Kenya ambayo imekuwa ikitoa matangazo ya kuvutia watalii katika *CNN, BBC* na Mashirika mengine ya habari pamoja na majarida mbalimbali ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ili utalii uweze kuongezeka kwa kiwango kikubwa na kufikia Mpango wa Taifa 2011/2016, lazima Wizara ichukue hatua za makusudi kujitangaza katika vyombo mbalimbali nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri, ameeleza kuwa tangazo moja tu litatolewa katika Ligi ya Uingereza. Hii haitoshi kabisa; atakaporudi Waziri katika majumuisho lazima atueleze kuwa, matangazo mengi zaidi yatatolewa katika vyombo vya habari na katika Majarida ya Kimataifa.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Maige (Mb) na Katibu Mkuu, Bibi Maimuna Tarishi, kwa hotuba nzuri na yenye mwelekeo unaotia matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda kutumia nafasi hii kuelezea wasiwasi wangu kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali zetu na hususan misitu kwa sababu zifuatazo:-

- Urithi huu wa misitu unazidi kutoweka kwa haraka sana na nchi inachakaa.

- Mwaka 1961 Tanganyika (Tanzania) ilikuwa na hekta za misitu 48 milioni, lakini leo 2011 tuna eneo la hekta 33 milioni tu za misitu na ifikapo 2025, Tanzania itakuwa na eneo la misitu lenye hekta 29 milioni tu.

- Eneo la misitu linalokatwa *(deforestation)* kwa mwaka ni hekta 400,000.

- Asilimia 95 ya watu waishio vijijini hutumia kuni kama nishati na asilimia 75 ya waishio mijini hutumia mkaa. Kwa mfano, Dar es Salaam pekee hutumia magunia 30,000 (@30 Kgs) za mkaa kwa siku, sawa na magunia 10,950,000 ya mkaa kwa mwaka, sawa na mita za ujazo 365,000. Mita hizo za ujazo hutokana na kukata hekta 10,400 kwa mwaka kwa Dar es Salaam pekee!

- Tatizo ni kubwa zaidi kwa nchi nzima!

- Idadi ya watu kufikia 2025 itakuwa ni milioni 65 na hivyo mahitaji ya Nishati kuwa makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, je Wizara ina mkakati gani endelevu wa kunusuru hali hii?

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Wilaya ya Kilolo hususan Kata za Mahenge, Udekwa, Ibumu na Image, wamekuwa katika ulinzi shirikishi katika Hifadhi za Udzungwa na Image pamoja na kuzima moto, kuzuia majangili na kadhalika, lakini Kata hizi hazinufaiki na ushiriki huu kama ilivyo katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inasema nini kuhusu hili?

**MHE. DIANA M. CHILOLO**: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi ya awali kabisa, kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige (MB). Pamoja na kuwa Mheshimiwa Maige hana Naibu Waziri, lakini ameonesha uwezo wa juu sana katika kutekeleza majukumu yake katika Wizara ikiwemo kuwashirikisha Watendaji wote wa Taasisi zote ambazo zipo chini ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mwenyezi Mungu, aendelee kumpa afya, nguvu na kuendeleza tabia yake ya uzalendo wa kuipenda nchi yake na jamii inayomzunguka. Vilevile niendelee kuwapongeza Katibu Mkuu, Mama Maimuna Tarishi, ambaye alifanya kazi kubwa na

nzuri alipokuwa Katibu Mkuu TAMISEMI. Matumaini yangu ni kuwa, ataendeleza juhudi zake za utendaji kwa kumsaidia Waziri. Nimalizie kwa kuwapongeza Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii ambayo imeainisha wazi utekelezaji wake na ukweli Hotuba ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuitaarifu Serikali kuwa, Wilaya ya Manyoni inayo tatizo la kupungukiwa sana Askari wa Wanyamapori kwa kuwa Wilaya hii ndiyo pekee katika Mkoa wa Singida yenye Kitengo cha Wanyamapori na inapotokea tatizo kwenye Wilaya zingine hasa Wilaya jirani ya Singida Vijijini hulazimika kwenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiojificha, matatizo yanayohusu Kitengo hiki ni mengi na hujitokeza katika Wilaya hizi. Matatizo hayo ni: Tatizo la kujitokeza wanyama wakali wanaohatarisha maisha ya Wananchi na mali zao; kuna fununu kuwa majangiri huvamia vitalu vya uwindaji na huondoka bila kukamatwa; wapo majambazi ambao hugeuza misitu ya hifadhi kuwa maficho yao kwa vile hakuna Askari wa Wanyamapori; na tatizo linapojitokeza, Serikali huchelewa kuleta huduma, mfano, Simba wanaokula watu, Simba mmoja hajapatikana hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, nina hakika utaungana na mimi kuwa, Wilaya ya Manyoni na Wilaya ya Singida ni Wilaya kubwa sana na ndizo ambazo huwa zinakumbwa na matukio ya Simba kula watu, kuvamiwa na majangiri au majambazi kugeuza maficho yao kwenye misitu ya akiba au vitalu vya uwindaji. Jambo la kusikitisha, Wilaya ya Manyoni haina gari la Askari wa Wanyamapori ili angalau lifanye kazi na Wilaya zingine endapo dharura inajitokeza kama ilivyojitokeza wakati Simba walipoanza kula watu. Napenda kujua kilio hiki Serikali itakisikia na kukitekeleza lini? Naomba Waziri anipe majibu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, napenda kuijulisha Serikali kuwa karibu kila Mkoa unavyo vivutio vya watalii ingawa vivutio vingi havijulikani. Ninapenda kuiomba Serikali ifanye utafiti upya kubaini vivutio mbalimbali ambavyo havijulikani ili kuvijua na kuvitangaza kwa wageni wanaokuja kutalii kwa njia mbalimbali; mfano, kwa kupitia televisheni, magazeti, *internet* na kadhalika ili watalii wanapokuja Tanzania, wawe wanajua wanakwenda kutembelea nini.

Mheshimiwa Spika, nitafurahi endapo Serikali itatambua mambo mazuri yaliyopo Singida ambayo ni vivutio vya watalii mfano:-

(i) Alama ya Center ya Tanzania iliyowekwa na Wajerumani katika Kijiji cha Sukamahela, Kata ya Sorya, Tarafa ya Kilimatinde, Wilaya ya Manyoni.

(ii) Picha ya mtu ambayo ipo juu ya jiwe kubwa huko Manyoni, Tarafa ya Nkonko, Kata ya Iseke.

(iii) Makumbusho ya vitu vya asili ya Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali haya yafuatayo:-

(i) Mheshimiwa Waziri akubali kuongozana na mimi pamoja na Wabunge wa Majimbo kwenda kuona vivutio hivyo.

(ii) Kwa kuwa *Center* ya Tanzania ni Manyoni Tarafa ya Kilimatinde na Kata ya Sorya, Kijiji cha Sukamahela, basi itambulike rasmi na siyo Dodoma.

(iii) Serikali kuajiri Afisa Maliasili na Utalii ili kusimamia makumbusho ya Mkoa wa Singida na kusaidia kuendelea kuibua vingine.

(iv) Kutoa fedha za kununua samani za makumbusho.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Ezekiel Maige, Waziri mwenye dhamana, wakati alipokuwa Naibu Waziri waliongozana na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho

Kikwete kwenye ziara yake Mkoani Singida. Nimepata taarifa kuwa, mizinga hii ilishaletwa bali sikupata taarifa, matokeo yake Mkuu wa Mkoa alivigawa kwenye taasisi zake nami naendelea kudaiwa na wanawake wajasiriamali wanajishughulisha na ufugaji wa nyuki kwa njia za kisasa Wilaya ya Manyoni. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kuondoa kero ya kudaiwa na wanaweke niliowaombea kwenye mkutano wa hadhara kwenye Uwanja wa Namfua Singida Mjini, kwani siwezi kudai kwa Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mtaalam wa Nyuki wa Wilaya ya Manyoni, kwa kazi zake nzuri za kutoa elimu ya ufugaji wa nyuki kwa vitendo. Hivyo basi, naomba juhudi zake zitambuliwe na aongezewe nguvu kwa kupewa fedha na mizinga ya kutosha ya kisasa ili kazi zake ziweze kuwa na tija kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Askari wa Wanyamapori cha Kanda ya Kati kilichopo Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kumpongeza Kamanda wa Kikosi cha Askari wa Wanyamapori, Afande Paschal Murina wa Kikosi cha Kanda ya Kati, kilichopo Wilayani Manyoni, kwa uongozi wake uliotukuka. Nimeamua kumpongeza kwa vile anawashirikisha askari wake vizuri na wanafanya kazi nzuri sana, kwani wanawakamata majangiri mara kwa mara na shughuli zote zilizoko kwenye Kanda hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi yake nzuri na askari wake wote, lakini wanakabiliwa na upungufu wa magari kwani yapo magari matano; magari ya doria ni matatu tu, gari moja la Kamanda na lingine ni bovu. Vilevile askari waliopo kwenye Kikosi hiki ni 23 tu ambao hawatoshi kabisa kulingana na ukubwa wa Kanda hii na kulingana na mfululizo wa matukio ya ujangili, wanyama wakali kushambulia Wananchi na mali zao, wanyama kula mazao yaliyolimwa na hata kuingia kwenye makazi mfano Ndovu, Simba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo hapo juu, napenda kuitaarifu Serikali kuwa, kuna haja sasa kuongeza askari ili kuboresha utendaji wa kazi katika Kanda hii ya Kati. Nina matumaini makubwa, Mheshimiwa Waziri, atatoa jibu lenye kuwatia moyo askari hao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuikumbusha Serikali kuwa, zipo nyumba tano tu za Askari wa Wanyamapori katika Kituo cha Manyoni. Hivyo, askari wachache wanakaa kwenye nyumba hizi na Kamanda wa Kikosi hiki anakaa nyumba ya Halmashauri kwa mahusiano mazuri na askari 17 wanapanga uraiani; kitendo ambacho kinawafanya kuishi maisha ya wasiwasi kwani wahalifu nao wapo uraiani.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua Serikali ina mpango gani wa kuwajengea askari hawa nyumba ili waweze kufanya kazi zao vizuri na kujilinda na maadui. Nitashukuru endapo Mheshimiwa Waziri atapokea ombi langu.

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kuwapongeza Askari wa Kituo cha Manyoni, kwa kazi kubwa wanayofanya kwa kuwakamata wahalifu na vitu walivyoiba pamoja na usafiri wanaotumia. Mfano, Manyoni kuna baiskeli zaidi ya 60 ambazo zina miaka zaidi ya sita. Napenda kuishauri Serikali kuwa kama wahusika wamezitelekeza basi ziuzwe ili fedha hizo ziweze kufanya kazi za ujenzi wa Miradi ya Maendeleo; mfano, kununua madawati ya Shule za Sekondari za Kata.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii akitoa ufafanuzi atakapojibu hoja za Wabunge leo jioni. Nashukuru vitu kama mbao na mkaa, huuzwa baada ya siku 30 na fedha hupelekwa Wizarani.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia mchango wangu kwa kurudia kumpongeza Mheshimiwa Ezekiel Maige, Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa kazi zake nzuri, akisaidiwa na Katibu Mkuu, Mama Maimuna Tarishi na Watendaji wote wa Wizara hii. Nawaombea Mungu awape afya, nguvu na ushirikiano udumu ili Wizara hii iendelee kuwa na tija katika kuzalisha na kuongeza Pato la Taifa.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuendeleza Sekta ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwomba Waziri na Wizara yake kusaidia uvunaji wa Mamba Mto Ruvuma katika Kata za Mahurunga, Kitaya, Namtumbuka, Kilambo, Tangazo na Madimba kwani sasa hivi Mamba katika maeneo hayo ni wengi na wanahatarisha sana maisha ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu kuwa ni fidia ipi inatolewa kwa Wananchi wanaopoteza maisha na kujeruhiwa na Mamba pamoja na wanyama kama Boko na Tembo.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu Wizara ina mpango gani wa kukuza utalii katika Mikoa ya Kusini hasa Mtwara na Lindi kwani kuna vivutio vya kutosha vya utalii.

Mheshimiwa Spika, Pwani ya Msimbati Mtwara Vijijini ndiyo pekee ambayo unaweza kuendesha gari maji yakipwa bila matatizo yoyote. Pia ni eneo zuri kwa wapiga mbizi kwani kuna bustani nzuri sana ya matumbawe chini ya bahari.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA A. CLEMENT**: Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa Hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia suala la vijiji vinavyochukuliwa na Serikali na baadaye vikatengwa kuwa eneo la Mbuga za Wanyama. Baadhi ya vijiji huchukuliwa wakati tayari wanakijiji wameshapewa hati ya kijiji na wameshaishi muda mrefu; hii inasababisha sana ugomvi na malalamiko kwa wanavijiji na pia kutokuwa na imani na Serikali kwa kuwahamisha hamisha.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ilifikirie kwa kina suala la wanyamapori wanaowafuata wanakijiji na kuwavamia kwa kuwaathiri na kuwauwa na pia kuwaharibia mazao na mali zao; iwape fidia zao haraka au kifuta machozi kifikiriwe sana kuongezwa kwani kilichopo hivi sasa ni kidogo mno hasa ukilinganisha na ukali wa maisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PEREIRA AME SILIMA**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nikushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja ya Waziri wa Maliasili. Nampongeza sana Waziri na Wataalamu wake, kwa Hotuba nzuri. Pamoja na pongezi hizo, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inakabiliwa na tishio kubwa la kukosa huduma na mazao ya misitu ikijumuisha mbao, miti na huduma za mazingira na kilimo. Upoteaji wa misitu tayari umetufikisha mahala ambapo kwa vyovyote vile inatupasa tubadilike, vinginevyo maafa makubwa yatalikumba Taifa.

Mheshimiwa Spika, tayari kilimo chetu cha kutegemea mvua kinashindwa kutupatia mazao na sasa mvua hazinyeshi za kutosha wala kufuata wakati. Mabwawa yetu ya kuzalisha umeme hayatimizi malengo ya kujengwa kwake na hivyo kuleta tatizo kubwa la upatikanaji wa nishati ya umeme nchini. Aidha, hali ya maisha ya Wananchi ambao wengi wanategemea nishati za miti wanalipa gharama kubwa kwa nishati ya kupikia chakula kuliko gharama ya chakula chenyewe.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuanzisha na kusimamia zoezi la tathmini ya misitu chini ya *NARFOMA.* Naiomba Wizara kutumia matokeo ya tathmini hiyo kujipanga zaidi hasa katika matumizi ya rasilimali hii.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 95 ya Wananchi wa Tanzania wanategemea nishati ya miti (kuni na makaa). Kwa sababu hiyo, misitu iliyopo inalazimika kutimiza mahitaji *(demand),* kwa hali yoyote ile na hili linapelekea misitu mingi kupotea. Hivi karibuni, Tanzania imeelezewa kuwa na rasilimali nyingi za gesi. Ugunduzi huu ni nyenzo muhimu ya kuhifadhi misitu yetu kwa matumizi mengine. Nashauri utafiti na jitihada zifanywe ili Wananchi waelimishwe na hatimaye wafikishiwe *LPG* ili kaya zibadilishe aina ya nishati wanayotumia kwa kupikia. Hili siyo jambo la baadaye kwani tayari tumeshachelewa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nchi yetu kuwa na vivutio vingi vya watalii yakijumuisha mambo ya kale, wanyamapori na rasilimali nyingine nyingi; pamoja na rasilimali hizo, Watanzania hawajapata fursa ya kuzifaidi rasilimali hizo kwani hawana utamaduni wa kutembelea maeneo ya mbuga na pia kwa sababu ya gharama kubwa zinazohitajika.

Mheshimiwa Spika, zipo jitihada za kuwafanya Watanzania watambue rasilimali zao, lakini juhudi hizi bado hazitoshi na ni budi mbinu na mikakati mipya inahitajika ili Watanzania watambue na kustarehe na rasilimali za nchini kwao. Jambo hili ni muhimu pia kama mbinu ya uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, matumizi makubwa ya misitu yetu hadi leo ni ya uvunaji *(extractive)* hata kama mahitaji ni kipato na siyo bidhaa *(products)* za misitu.

Mheshimiwa Spika, misitu tuliyonayo inao uwezo wa kutupatia kipato bila ya kuiangusha. Hata hivyo, bado tumejikita sana katika matumizi ya kiuvunaji. Naomba tuchukue hatua za makusudi kubadilika na kuwawezesha Wananchi wapate na kutumia fursa zilizopo.

Mheshimiwa Spika, hapa nakusudia kutumia rasilimali za misitu ya juu na ya pwani (mikoko) katika utalii kama *kayaking, bird viewing* na kadhalika. Hii itasaidia kulinda miti na bado tutapata kipato.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo linaweza kutupatia kipato bila ya kuangusha miti ni ufugaji wa nyuki. Nchi yetu inazo rasilimali za misitu ya aina nyingi pamoja na rasilimali kubwa ya nyuki.

Mheshimiwa Spika, kinachotakiwa na ambacho ndiyo nakipendekeza ni kutoa elimu na kuanzisha programu kubwa ili zisaidie kuhifadhi misitu na kusaidia juhudi za kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI**: Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake, kwa kazi nzuri na Hotuba nzuri iliyowasilishwa kisayansi na vielelezo vya picha za matukio mbalimbali. Pamoja na hayo, napenda kupata ushauri, kutoa maoni na maombi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mfumo wa upangaji wa madaraja ya hoteli nchini unapaswa kulindwa kisheria na hivyo kutoa elimu kwa wawekezaji katika maeneo hayo, kufahamu vigezo muhimu kabla ya kuanza ujenzi wa hoteli ili kujiwekea lengo la daraja la hoteli mwekezaji anayojenga.

Mheshimiwa Spika, bado majengo mengi ya hoteli yasiyokidhi vigezo vya madaraja ya juu Kitaifa yameendelea kujipachika majina makubwa yasiyostahili. Je; ni lini usimamizi wa madaraja ya Hoteli Kitaifa utaanza kutekelezwa na kusimamiwa kwa dhati?

Kuachia wanyamapori hai kusafirishwa nje ya nchi kuna lengo la kudhoofisha utalii. Sehemu nyingi duniani hazina aina ya wanyamapori kama waliopo katika Hifadhi za Tanzania na hivyo kuwa kichocheo kwa watalii kuja kuwaona hapa Tanzania. Wanaochukua wanyama hao hai, wanaanzisha vituo vyao nje ya nchi na kujitangaza ili wageni waende huko kuona wanyama pengine kwa gharama ndogo lakini kunaathiri utalii nchini. Je, Wizara inashindwa kutambua jambo hilo na kuzuia ili kuboresha utalii badala ya kudhoofisha utalii?

Mheshimiwa Spika, uvunaji wa mitiki unaoendelea mfululizo katika Shamba la Lunguza Muheza unatishia Hifadhi ya Mazingira katika eneo jirani la Hifadhi ya Msitu wa Amani na Mto Ziggi na vyanzo vya maji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, hata kama Taifa linapata fedha kwa mauzo ya miti, siyo busara kuchangia kuharibu mazingira na kuhatarisha maisha ya baadaye ya Wananchi wa Wilaya ya Muheza. Vipimo vya hali ya hewa kwa sasa vinaonesha kuongezeka kwa joto katika eneo la Hifadhi ya Msitu wa Amani, hali inayoashiria janga kubwa katika miaka michache ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri sasa tusimamishe uvunaji ili kutoa nafasi ya kukua kwa miche mipya iliyopandwa na inayoendelea kupandwa katika maeneo yaliyovunwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatari za athari ya mazingira kutokana na uvunaji mitiki Shamba la Lunguza, matatizo yafuatayo yamejitokeza:-

(a) Barabara kutoka Shamba la Lunguza hadi Muheza inayosimamiwa na *TANROADS* imekuwa inaharibiwa na magari mengi makubwa yanayobeba magogo ya mitiki kila siku, kila mwezi na kila mwaka mfululizo. Gharama za matengenezo ni kubwa sana kuliko mapato yanayoingizwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

(b) Wageni wanaonunua magogo ya mitiki wameanzisha viwanda eneo lote la barabara kutoka Lunguza hadi Muheza Mijini kwa kupasua magogo hayo na kutengeneza mbao, kukwepa utaratibu wa kusafirisha nje magogo ya mazao ya misitu. Matokeo yake ni kurundikana kwa maganda na maranda ya mbao, kuziba maeneo ya mashamba na kuwezesha madhara makubwa ya vumbi kwa Wananchi wanaoishi jirani na viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, viwanda hivyo pia vinapokea magogo ya mitiki kutoka Mashamba ya Morogoro na magari yao kuchangia uharibifu wa barabara.

Mheshimiwa Spika, licha ya mfumo huo wa viwanda kuhusu Wizara ya Viwanda na Biashara, bado Wizara ya Maliasili na Utalii inapaswa kuwajibika kwani mbao zinazozalishwa hazilipiwi ushuru wala kodi kwa kisingizio cha kodi iliyolipwa kama miti toka Shamba la Lunguza. Nini ushauri wa Wizara juu ya mfumo huu?

Mheshimiwa Spika, pamoja na madhara niliyoyaainisha hapo juu, Meneja wa Shamba la Lunguza amejitahidi kusaidia katika ujenzi wa Ofisi, maeneo ya Kata jirani na Msitu wa Lunguza. Tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naomba rasmi sasa Wizara ya Maliasili na Utalii isaidie kupitia Miradi ya Ujirani Mwema, isaidie ujenzi wa madarasa mawili katika shule mpya ya Kata Mpya ya Tongwe inayopakana na Shamba la Lunguza. Kwa kuwa Kata ya Tongwe ipo jirani na Shamba la Lunguza, basi Meneja wa Ujenzi apewe jukumu la kusimamia ujenzi wa vyumba hivyo viwili na Serikali ya Kijiji iendeleze ujenzi wa vyumba vingine kwa Mfuko wa MMES na nguvu za Wananchi. Nitashukuru kupata jibu la ombi hili.

Mheshimiwa Spika, eneo la Hifadhi ya Msitu wa Amani lina vipepeo wa aina yake duniani. Vipepeo wamekuwa kivutio cha utalii na Wananchi wanashiriki kusafirisha nje ya nchi vipepeo na mayai ya vipepeo hao. Je, Wizara inasimamia vipi maliasili hii na biashara hiyo?

Mheshimiwa Spika, upo mti wa maajabu ambao una ndevu kama za binadamu; kwa nini Wizara isitumie chombo chake cha utafiti kuona hali asilia ya mti huo uliopo katika eneo la Hifadhi ya Msitu wa Amani Wilayani Muheza?

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Mbunge, mimi mdau mkubwa katika Sekta ya Utalii kwa kuwa mfanyakazi wa *Tanzania Association of Tour operators*

*(TATO),* kama Katibu Mtendaji kwa takriban miaka 20 sasa. Kwa uzoefu huo, naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mapato makubwa katika Sekta ya Utalii yanapatikana kutoka kwa Wageni wa Kitaifa US$ 1.5 bilioni katika mwaka 2010, yaani asilimia 25 ya mapato ya biashara ya nje. Wageni hawa walikuja kutokana na kazi kubwa waliyofanya Kampuni za Binafsi. *Tour operators* wale siyo *TANAPA* wala *MCAA* kama Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilivyosema kwenye taarifa yake. Naunga mkono hatua ya Serikali ya kusisitiza Taasisi hizo kufanya *marketing* ya vivutio vya utalii kwa sababu *TANAPA* na *MCAA* hawana bei ya *tourist products.* Vivutio vya utalii vya Tanzania siyo wanyamapori tu viko vingi; *Cultural Tourism, Beach Holidays, Site Seeing* na kadhalika na kadhalika. Kazi hii iachiwe *TTB* na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kufanya *destination marketing, component* muhimu ni usafiri wa ndege kuanzia kwenye *Source Market* hadi kwenye *destination.* Bila nchi kuwa na ndege yake *(National Career), destination* inakosa asilimia 60. Nashauri Serikali ishirikiane na Mashirika makubwa ya ndege yaliyoingia ushirikiano wa kuwa na *National Airline* au Mwekezaji mahiri atafutwe haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa vile biashara ya utalii inahitaji uzoefu na utaalam (uweledi), nashauri Serikali katika kuunda Bodi za *TTB, TANAPA, MCAA* na Kamati zingine, Wadau wa Sekta wateuliwe kwa uwiano wa nusu ya Bodi nzima. Kuwateua wanasiasa, kunazifanya Bodi hizi kuwa dhaifu. Ninaomba niishauri Serikali kuwa, hii Sekta ni ya Biashara ya Kimataifa; jazba za kisiasa na uzalendo wa ukereketwa usipewe nafasi.

Mheshimiwa Spika, Watumishi wa Wizara chini ya Katibu Mkuu, wategemee maamuzi ya kitaalamu ambayo yanatolewa *timely* na *professionally.* Uzoefu unaonesha kuwa, Idara zote katika Wizara hii pamoja na Taasisi zake, zina tabia ya kuchelewesha kutoa maamuzi kuhusu matatizo yanayoletwa na kutegemea Vikao vya Bodi kwa mambo mengi. Wataalam waheshimiwe, Bodi zisiwe zinaingilia wataalamu.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa migogoro ya mipaka/misitu na Hifadhi Taifa, naomba ahadi ya Waziri iliyoko kwenye Hotuba itekelezwe hasa kuhusu mpaka wa Hifadhi ya Manyara na Kata za Daudi, Marangu, Bargish na Gehandu katika Wilaya Mbulu iharakishwe hasa kuhusu *Buffer Zone* ili kuwawezesha wakazi hao kupata maeneo ya malisho ya mifugo yao pamoja na akina mama wapate kuni. Nashukuru.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU**: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara, Taasisi na Wafanyakazi wote wa Wizara, kwa kazi nzuri mnayofanya. Naamini kwa ushirikiano, tutapiga hatua haraka.

Mwaka 1973, Tanzania iliongoza duniani kwa ku-*export* kiasi kikubwa zaidi cha nta (tani 275). Tanzania pia ni moja kati ya nchi kumi duniani zenye *potential* kubwa zaidi katika ufugaji nyuki. Kwa hali hii ufugaji nyuki ni moja ya maeneo muhimu sana na yenye uhakika wa kupunguza umaskini na kuongeza kipato cha Watanzania iwapo tutajipanga vizuri. Ukuaji wa mapato ya Serikali umekuwa ukipungua mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara kwa kutenga fedha kwa ajili ya utafiti wa chawa au kupe wanaojulikana kama *Varroa Species or Destructor*, ambao wameenea katika Wilaya 25 katika Mikoa 12 ya Tanzania Bara. Sijui Wizara imetenga kiasi gani cha fedha kufanya kazi hii? Najua *TAWIRI* wameomba shilingi 178,022,670; nitapenda kujua Wizara imetenga kiasi gani.

Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, aliitembelea *TAWIRI,* Alhamisi, tarehe 31 Machi, 2011 ili kukagua shughuli za utafiti. Katika ziara hiyo, Mheshimiwa Pinda alionesha masikitiko yake jinsi ambavyo Serikali imeshindwa kutoa kipaumbele kinachostahili juu ya mchango wa Sekta ya Ufugaji Nyuki katika mchango wa maendeleo hapa nchini. Mambo mengine aliyosisitiza ni:-

(i) Kuanzisha Idara ya Nyuki; je, hili litafanyika lini?)

(ii) Kituo cha Njiro kinachoshughulikia utafiti wa nyuki ni dhaifu sana kiuwezo wa vitendea kazi na bajeti kiasi kwamba hakikidhi matakwa; je, Wizara imechukua hatua gani kuhusiana na hali hii?

(iii) Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa agizo iandikwe Miradi inayohusu uchavushaji *(pollination services)* kwa kutumia nyuki. Alitoa mfano, mwaka 2006/2007 mchango wa Sekta ya Ufugaji Nyuki katika huduma za uchavushaji mazao katika Nchi ya Marekani peke yake zilikisiwa kufikia Dola za Kimarekani bilioni mia mbili. Mkazo maalum uanze wa kuelimisha wakulima nchini ili waanze kuthamini huduma za uchavushaji ili uhifadhi wa nyuki ukue, lakini pia mchango wake katika Pato la Taifa ujulikane kwa kuthamanishwa katika fedha.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Misitu ya Sayaka Jimboni Magu, imekuwa ikifuga wanyama wakiwemo Tembo, Nyati na kadhalika, ambao huleta uharibifu mkubwa wa mara kwa mara wa mashamba ya Wananchi na pia kuua watu:-

(a) Je, Wizara ina taarifa na suala hili?

(b) Je, Wizara inaweza sasa kutoa maelekezo ili wanyama hawa waharibifu waliozaliana kwa wingi katika miaka ya hivi karibuni wavunwe wauliwe nyama yao wagawiwe/wauziwe kwa bei ndogo katika kipindi hiki cha sasa ambapo Wananchi wana njaa ili kupunguza utapiamlo na kunusuru maisha ya Wananchi? Hali hii pia ipo sawa na *crocodiles* katika mialo ya Kata za Kongolo, Lutale na Nyanguge katika Jimbo la Magu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PINDI H. CHANA**: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Lini vibali vya kupasua miti katika Shamba la *Sao Hill* vitatoka? Mimi ni miongoni mwa walioomba vibali na sifa na vitendea kazi ninavyo; je, nitapata kibali cha kupasua mbao *Sao Hill*?

Mheshimiwa Spika, Mbuga ya Kitulo Makete ipewe kipaumbele na uwezeshaji na *Ruaha National Park* Iringa ili watalii waweze kufika katika mbuga hizo za wanyama kwa wingi sana.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI**: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kidogo kwenye bajeti hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kimondo cha Mbozi ni moja ya vivutio na eneo la kujifunzia hasa kwa Wanasayansi wanaopenda kujifunza mambo ya vimondo *(Meteorite),* vilivyoanguka/vilivyodondoka kutoka angani. Vimondo pamoja na kile cha Mbozi, vinaweza kuwa chanzo kizuri sana cha mapato ya Serikali kama vikisimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema kwamba, kimondo cha Mbozi kimetelekezwa! Pamoja na kulisema jambo hili kwa muda mrefu humu Bungeni nikiomba kimondo kitunzwe vizuri, kitangazwe, kijengewe vizuri, kuwepo machapisho ya kutosha yanayoelezea historia ya kimondo hicho; hadi leo hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua ni lini sasa Serikali kupitia Wizara hii itafanya hayo niliyoyataja hapo juu. Je, kwa mwaka huu wa fedha ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya kuanzia kukiwekea kimondo hicho mazingira mazuri?

Mheshimiwa Spika, Makumbusho ya Taifa ni muhimu sana hasa kwa vizazi vya mbeleni. Katika historia au tunapotoa maana *(definition)* yake, tunasema historia ni somo linalohusu mambo yaliyopita ya sasa na yajayo. Ili tuelewe tulipo na tunakokwenda ni lazima tujue tulikotoka. Hapa ndipo umuhimu wa Makumbusho ya Taifa yanapokuwa na umuhimu mkubwa sana. Nashauri mila na utamaduni wa makabila yote nchini kwetu ziwekewe kumbukumbu nzuri kwa faida ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia kwamba, Makazi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (Hayati), Rais wa kwanza wa nchi yetu, yawe Kumbukumbu ya Taifa. Nasema hivyo kwa sababu hapo ndipo palikuwa makazi rasmi ya Mwalimu Nyerere; ni muhimu vizazi vinavyokuja vije kuona mahali ambapo Mkombozi na Mwasisi wa Taifa hili aliishi. Hata hivyo, Shirika hili lipewe pesa za kutosha ili liweze kufanya kazi vizuri. Nawasilisha.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA**: Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji husika, kwa kuandaa hotuba vizuri na pia kuiwasilisha vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza pia kwa kuendesha na kusimamia vizuri shughuli za Wizara na Mashirika yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wanyama hasa Tembo, wanaendelea kuharibu mashamba ya Wananchi na taarifa itolewapo inachukua muda mrefu Askari wa Wanyamapori kufika kutoa msaada kwa kuwafukuza, ninashauri yale maeneo yanayoathiriwa na wanyama hasa Tembo, wapangwe Wanamgambo kadhaa, wapewe mafunzo kiasi ili Tembo wanapovamia wasaidie wakati Afisa Wanyamapori wanasubiriwa kwa msaada zaidi kama ikibidi.

Mheshimiwa Spika, silaha za mgambo hawa ziwekwe kwenye Ghala la silaha la Polisi Kata au vituo vingine vya polisi.

Mheshimiwa Spika, Askari wa Wanyamapori wafanye kazi yao vizuri. Wajenge mahusiano mazuri na wanavijiji vinavyopakana na Hifadhi. Watambue hawa wanavijiji ni washirika katika uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, uharibifu wa misitu kwa uchomaji moto umeendelea katika maeneo mengi. Wizara iweke mkazo katika uhifadhi wa misitu na upandaji miti. Mkazo uwekwe kuzuia uchomaji moto.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, nianze kuipongeza Wizara, Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Asasi zote zilizo chini ya Wizara hii, kwa hotuba nzuri na kazi nzuri inayoendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii kwa kiasi kikubwa inaweza kuchangia kuinua uchumi wa nchi hii. Naipongeza Wizara kwa mipango mizuri iliyopo. Naomba msirudi nyuma ongezeni kasi.

Mheshimiwa Spika, nasikitishwa sana na kasi iliyopo ya kuvuna miti, huku tukisahau kuwa miti imeota/imeoteshwa na kutunzwa kwa miaka mingi na sasa inavunwa kwa kasi ya kutisha. Misitu mingi ya asili hasa kati ya Kahama na Biharamulo, inayoonekana ukiwa barabarani, ukweli ni kuwa miti imebaki kando kando ya barabara, humo ndani miti mingi mno imekatwa. Wataalam wamesema, ifikapo mwaka 2016 miti ya kuvuna itakuwa imekwisha Tanzania.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara ina mipango gani ya kuweka mpango wa uvunaji endelevu ili kuhifadhi misitu yetu? Je, Serikali ina mipango gani Mkoani Kagera ya kuelimisha na kuanzisha vikundi vya uoteshaji miche/miti?

Mheshimiwa Spika, nawapongeza *TANAPA*, Ngorongoro na Bodi ya Utalii, kwa kazi nzuri ya kutangaza vivutio vilivyo nchini ili kuwavutia watalii wengi kuja nchini na kuongeza kipato cha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitueleza mwaka jana kuwa mambo ya utalii yataendelea kupanuliwa katika mikoa mingine tofauti na ile mikoa ya kawaida ya Kaskazini. Je, ni lini Serikali itaendeleza na kutangaza vivutio vya utalii vingi vilivyopo Mkoa wa Kagera?

Mheshimiwa Spika, tatizo la wanyamapori hasa Tembo kuingilia mashamba ya wakulima limekuwa kubwa hasa katika maeneo yanayozunguka Hifadhi. Mkoani Kagera katika Wilaya ya

Muleba, Wilaya ya Bukoba Vijijini, Karagwe hasa Kata ya Kihanga na Biharamulo hasa Kata za Lusahunga, wanyama wameharibu mali na mashamba ya wakulima. Tatizo hili limezungumziwa na Watanzania na Wabunge wengi. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kumaliza tatizo la wanyama (Tembo) kuingilia watu na mashamba yao Mkoani Kagera?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA**: Mheshimiwa Spika, naomba kujua yafuatayo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri:-

(i) Ni lini Wizara itatoa kwa Waheshimiwa Wabunge Kanuni za Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori?

(ii) Waziri alipokuwa akijibu swali hapa Bungeni kwenye Mkutano wa Nne alisema fidia kwa Wananchi walioharibiwa mazao yao ni shilingi 100,000 kwa heka moja. Je, Serikali ipo tayari kuongeza mara tano zaidi ya kiwango hicho cha sasa?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. JOYCE J. MUKYA**: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2011/2012, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchimbaji katika maeneo ya Hifadhi au Mbuga za Wanyama; suala hili limenigusa kwa kiasi fulani, kwa kuwa kuna harakati za kutaka kuhalalisha shughuli za uchimbaji wa madini katika Hifadhi au Mbuga zetu za Wanyama. Sheria zetu hivi sasa zinapinga shughuli hizi za uchimbaji, lakini kwa kipindi kirefu kumekuwa na harakati na kampeni za kutaka mabadiliko ili uchimbaji uhalalishwe.

Mheshimiwa Spika, napinga harakati hizi kwani zinalenga kuharibu juhudi za uhifadhi zilizofanywa na Waasisi wetu. Mfano, Marehemu Baba wa Taifa, alikuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha mbuga hizi zinatunzwa kwa ajili ya vizazi vya baadaye.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya wajanja wameshagundua kuna utajiri mkubwa wa madini katika mbuga hizo kwa kutumia utaalam na vifaa vya kisasa vya utafiti na ndiyo maana wameanza kampeni hizo.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri kama Taifa tuseme hapana, kwani hatufaidiki na utajiri wa madini tuliokuwa nao sasa sehemu mbalimbali nchini halafu tunataka tuanze kupunguza hifadhi zetu tuwape wageni wachimbe madini yetu na faida yote wahamishie kwao. Mfano, *Tanzanite* yetu ambayo inachimbwa Arusha – Tanzania, huko soko la nje inaonekana inatoka Kenya.

Mheshimiwa Spika, hata kama tunaruhusu uchimbaji huo, tutumie busara alizotumia Hayati Baba wa Taifa, kwa kuhifadhi maeneo kwa ajili ya vizazi vijavyo. Hivi sasa tufanye kazi kuwaandaa na kuwawezesha Watanzania kumudu uchimbaji mkubwa na wa kisasa ili baadaye tukija kuruhusu uchimbaji huo, basi faida ibaki hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumeibuka wimbi la utoroshaji wanyama hai na nyara za Serikali kwenda nje ya nchi kinyume cha sheria. Baadhi ya Watumishi wa Idara mbalimbali za Serikali, wametuhumiwa kufanikisha biashara hii haramu na tukio la karibuni ni lile la kusafirisha wanyama kupitia Uwanja wa Ndege wa KIA, ambapo walisafirisha ndege 16 na wanyama 120, tarehe 26 Oktoba, 2010 kwa ndege ya *Qatar Airforce C-17* na lingine ni lile la kutorosha Twiga kumi.

Mheshimiwa Spika, licha ya suala hili kuripotiwa na vyombo vya habari ambavyo ndivyo vilifichua hujuma hii, lakini Serikali ilichukua zaidi ya miezi miwili kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya wahusika, ambapo baadhi ni wageni kutoka nje, walioshirikiana na wenyeji na majina ninayo. Hii inatia mashaka kuwa, pengine vyombo vya habari visingepigia kelele uhalifu huu hadharani, jambo hili lingefunikwa funikwa bila wahusika kuwajibishwa.

Mheshimiwa Spika, sasa kama wanyama hai tena wakubwa wametoroshwa kupitia Uwanja wa KIA, ambao una kila aina ya ulinzi, kwa kutumia vyombo mbalimbali pamoja na Idara za Ulinzi za Serikali zenye wajibu wa kusimamia ulinzi wa rasilimali zetu, sasa sijui hali ikoje huko katika viwanja vidogo vidogo vilivyopo ndani ya mbuga au hifadhi zetu mfano, Tarangire – Arusha, Serengeti – Mara na kadhalika, ambako hakuna ulinzi wa kutosha? Hali hii inatoa taswira kwamba, wanyama wengi wamekuwa wakitoroshwa kila kukicha kupitia viwanja hivyo vidogo ambavyo baadhi havina ulinzi wa kutosha na vingine vinamilikiwa na wawekezaji wa kigeni.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri akija kutoa majumuisho hapa, aeleze utaratibu unaotumika kudhibiti utoroshaji wa wanyama katika viwanja vidogo hivyo vya ndege kama kile cha Kampuni ya *Klains Camp* kule *Loliondo Game Controlled Area* katika Wilaya ya Ngorongoro Mkoani Arusha.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu zilizopo zinaonesha kuwa, Uwanja huo uko umbali wa kilimita tatu tu kutoka mpaka wa nchi yetu na nchi jirani ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, najua Serikali kupitia kwa Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, ilitangaza kuufunga Uwanja huo kutokana na sababu kadhaa ikiwemo kuwa mpakani na kukosa vyombo vya ulinzi na usalama vya kutosha kama Polisi, Uhamiaji na Idara zingine muhimu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo sasa zinasema kuwa, kuna juhudi zinafanyika kuhakikisha Uwanja huo unafunguliwa na kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho atueleze kama sababu zilizopelekea Uwanja huo kufungwa zimepatiwa ufumbuzi hadi wahusika wafanye kampeni za kuufungua.

Mheshimiwa Spika, wakati ipo hivyo, kuna taarifa kuwa Kampuni ya *MWIBA Holdings* ya Mjini Arusha inayofanya biashara ya utalii wa picha katika Pori la Hifadhi la Makao Wilayani Meatu Mkoani Shinyanga, imeanza harakati za kujenga uwanja wake mdogo *(Airstrip)* eneo la Kijiji cha Makao km 15 tu kutoka uwanja mdogo ulioko Pori la Hifadhi la Maswa.

Mheshimiwa Spika, kinachodhihirisha kiburi na pengine kujiamini kupita kiasi, Kampuni tayari imeshapeleka zana za ujenzi eneo la Mradi hata kabla ya kupata vibali kutoka mamlaka husika. Hivi sasa ndiyo imeandika barua Wilaya ya Meatu kuomba isaidie upatikanaji na kibali. Sasa najiuliza; wana uhakika gani wa upatikanaji wa kibali hadi wapeleke vifaa *site?*

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Serikali kwa kushirikiana na Wadau, ifanye jitihada za makusudi za kutangaza vivutio vya utalii tulivyonavyo ili kuongeza Pato la Taifa kwa fedha za kigeni na shilingi yetu. Mfano, Mlima Kilimanjaro umekuwa ukijulikana upo Nchini Kenya kwa baadhi ya maeneo huko nje na wakati upo nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, muda umefika sasa wakulima wadogo wadogo wawezeshwe kupata utaalamu na hata fedha kumudu kuzalisha mboga ajili ya kuuza katika hoteli za kitalii hapa nchini badala ya kuagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo wafugaji wawezeshwe kufuga kwa kiwango stahiki ili waweze kuuza mazao ya mifugo, mfano, maziwa na nyama katika hoteli zetu badala ya bidhaa hizo kuendelea kuagizwa nje.

Mheshimiwa Spika, katika hili, nadhani Wizara hii inabidi ishirikiane na Wizara zingine kama vile Uvuvi na Mifugo, Kilimo, Chakula na Ushirika na Taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja. Naunga mkono hoja kwa sababu maliasili za nchi hii ni chanzo kikubwa cha ukuaji wa uchumi na mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, mchango wa Wizara hii upo wazi kutokana na ukweli kwamba, nchi yetu imejaaliwa kuwa na utajiri wa kutosha wa maliasili zikiwemo mbuga za wanyama, mambo ya kale, tamaduni zetu, misitu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa bahati mbaya upo upungufu unaojitokeza kutokana na vitendo vya uhujumu uchumi; kwa mfano, utoroshaji wa wanyama hai uliofanywa kupitia Kiwanja cha Kimataifa wa Kilimanjaro. Utoroshwaji wa wanyama hawa ni ukiukwaji wa sheria na kulikosesha Taifa mapato yake halali.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara kwa kuja na wazo la kuongeza maeneo ya kukuzia utalii hasa Kanda ya Ziwa Viktoria katika Jiji la Mwanza, ambapo kutakuwa na hatua za makusudi za kuongeza hoteli za kitalii na kuiomba Serikali kuupandisha hadhi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwanza na kuboresha huduma za kitalii katika Jiji hili zuri la Mwanza, ambalo lipo jirani kabisa ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Ngorongoro pamoja na Rubondo.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ukurasa wa saba, aya ya 14, inazungumzia kuhusu uendelezaji wa miundombinu katika Mapori ya Akiba ikiwemo Mapori ya Akiba ya Moyowosi, lakini cha kushangaza ni kwamba; Kigosi ni Pori la Akiba, halina miundombinu. Naishauri Wizara ichukue hatua za haraka kuhakikisha Pori la Akiba la Kigosi ambalo halina miundombinu ya uhakika, limeifanya huduma ya shughuli za kitalii kuzorota na zaidi kuwapatia nafasi majangiri kuua wanyamapori katika Pori la Akiba la Kigosi, ambalo lipo katika Jimbo la Mbogwe.

Mheshimiwa Spika, watu wa Mbogwe na mimi mwakilishi wao, tunaiomba Wizara ihakikishe kwamba, Pori la Akiba la Kigosi linapandishwa hadhi na kuwa Hifadhi ya Taifa ya Wanyamapori *(TANAPA).* Jambo hili lifanyike haraka.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii ilizuia Wananchi wa Kijiji cha Nsango kunywesha mifugo yao katika mito iliyomo katika Pori la Akiba la Kigosi. Nashukuru Wizara ilikubali kugharimia uchimbaji wa lambo kwa ajili ya unyweshaji mifugo. Wizara ilitanguliza shilingi milioni ishirini na tano, lakini cha kushangaza ni kwamba, tangu Oktoba mwaka jana wizara ilipotoa fedha hizo, lambo hili halijachimbwa. Naomba Wizara ifuatilie na ikiwezekana iongeze kiasi cha fedha ili uchimbaji wa bwawa hili ukamilike, kwani makadirio yaliyotolewa kitaalam ni kwamba, zinahitajika zaidi ya shilingi milioni sabini na tano.

Mheshimiwa Spika, niiombe Wizara kwa dhati, iongeze fedha zaidi kusaidia ukamilishaji wa Bwawa katika Kijiji cha Nsango.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja, naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, naomba niipongeze Wizara kwa kutambua uwepo wa vivutio vingine katika nchi yetu, ambavyo bado havijatangazwa kiasi cha kutosha. Naipongeza Wizara kwa kutambua uwepo wa Kivutio cha Maporomoko ya Kalambo na kuthubutu kuweka kwenye *cover* ya kitabu chake cha bajeti.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kwa namna ya pekee, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Ezekiel Maige, kwa kuweza kutembelea Maporomoko ya Kalambo. Naishauri Wizara iwe na

mkakati wa kulitangaza eneo hili la Kalambo ikiwa ni pamoja na Ngome ya Bismark, iliyoko Ziwa Tanganyika, Mji Mdogo wa Kasanga.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara ijielekeze katika kuyatangaza maeneo mengine kuliko kuendelea na Mikoa ya Kaskazini tu; mfano, Mikoa ya Kusini Nyanda za Juu, yaani Mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Katavi, kama inavyofanya sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko kutoka kwa Wananchi, juu ya ukabila uliokithiri Wizarani, kwa maana ya kuwa na watu wa kabila fulani kuanzia ngazi ya juu mpaka chini; ni vizuri Wizara ikalifuatilia jambo hili na kuhakikisha kwamba, kunakuwa na uwiano wa makabila.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa maoni yangu kuhusiana na Sekta ya Utalii na namna bora ya kuiendeleza Sekta hii ili iweze kuchangia katika maendeleo ya Taifa hususan kuongeza Pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Bodi yetu ya Utalii ina dhamana kubwa ya kutangaza utalii ndani na nje ya nchi; ni vyema, Bodi ya Utalii iongeze jitihada zake ili kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea nchi yetu; na ni vyema watumie *Digital Media* ili kuhamasisha watalii wengi zaidi. *TTB* waanzishe *free online travel Guide,* ambayo itawawezesha wageni na watalii ku-*download* taarifa mbalimbali za utalii wa nchi yetu ili kujipa uelewa wa sehemu muhimu za vivutio vya kitalii vya nchi yetu ili kuwezesha ziara zao za kitalii kuwa zenye furaha na kuwavutia watalii wetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye *Guide* hiyo tunaweza kuweka kimakundi, vivutio vya aina tofauti mfano: Utalii wa mijini, milima, kitamaduni, bahari na kadhalika. Vilevile Hoteli mbalimbali pamoja na gharama zake, ziainishwe kwenye mwongozo huo ambao unapaswa kurejewa mara kwa mara ili taarifa na takwimu zake ziendane na wakati.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kuwa na Mpango Mkakati wa kuongeza idadi ya hoteli zetu ili kuwa na idadi kubwa ya vitanda, kwani hivi sasa ikitokea tukiletewa Mkutano mkubwa wa Kimataifa inakuwa vyumba havitoshi. Tunapoteza mapato mengi sana kwenye hili; kazi zitaongezeka endapo tutaongeza idadi ya hoteli zenye ubora wa Kimataifa. Kwa kufanya hivyo, ajira zitaongezeka, Pato la Taifa litaongezeka na mauzo yetu ya ndani yataongezeka.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuna haja ya kuangalia ni namna gani pia Sekta hii ya Utalii inaweza kushirikiana na Sekta ya Kilimo. Tunawezaje kufanya vizuri zaidi; tunawezaje kuwa shindani; ni vizuizi gani vinavyozuia uwekezaji mkubwa katika Sekta hii ya Utalii; na ni vitu gani vinaweza kufanyika au kuboreshwa ili kuhamasisha utalii zaidi? Yote haya ni muhimu yakatafutiwa majibu katika mpango mkakati huo.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa huduma ya usafiri wa anga ni tatizo lingine linalopelekea utalii wa nchi yetu kutokushamiri. Suala hili linahitaji kupatiwa ufumbuzi haraka iwezekanavyo. Nchi yetu imejaaliwa vivutio vingi vya utalii, ambavyo vina uwezo wa kutuletea si chini ya watalii milioni kumi kila mwaka, lakini ni watalii milioni moja tu ndiyo huweza kufika nchini.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kuruhusu ndege nyingi na zenye bei nafuu kuja nchini kwetu ili kuchochea kuingia kwa watalii wengi nchini. Vilevile tunahitaji kulegeza bei za *visa* ili Wamarekani wengi na watalii wetu wa jadi, waweze kuja nchini kwetu zaidi. Tunapaswa kuwa na utashi wa kisiasa na kuchukua hatua za kiuchumi ili kuongeza *tourism base* yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Utalii inapaswa pia kuandaa mwongozo/kanuni ambazo zitawezesha upangaji wa bei ambao haubadiliki mara kwa mara, zenye unafuu na ambazo zitapangwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu hasa kwa kujielekeza katika misitu.

Mheshimiwa Spika, misitu yetu hasa ya mbao na mazao ya misitu, nasikitika sana kuona takwimu za idadi ya tani za magogo zilizofikishwa nje ya nchi na zilizopo Serikalini, hazilingani kabisa na idadi ya magogo yaliyopokelewa huko nje.

Mheshimiwa Spika, Rasilimali za Tanzania yaonesha wazi kabisa hazilindwi tena na siyo rasilimali za Taifa tena, bali ni mali za wajanja wachache.

Mheshimiwa Spika, sipingi upelekaji wa magogo nje kama utaalamu wa uvunaji na sheria unafuatwa, lakini bado pia kuna mahitaji makubwa sana ya mazao ya mbao na misitu yanahitajika ndani, hasa kwa kutengeneza madawati kwa shule zetu za sekondari na msingi.

Mheshimiwa Spika, napenda kurudia; rasilimali zetu hazilindwi tena; inasikitisha kuona sisi wenyewe tumeamua kuwazuia watalii kuja Tanzania kwa kuwapelekea wanyama huko huko. Hili ni kosa kubwa sana ambalo tunalifanya.

Mheshimiwa Spika, hapa tunajaribu hata kumkosoa Mungu, Mungu hakukosea kutupa wanyama na wengine akawapa mafuta na utaalamu. Kwa nini tumkosoe Mungu; tunatoa rasilimali zetu (wanyama) na kuwapa watu ambao Mungu amewapa rasilimali mbadala huko?

Mheshimiwa Spika, kodi au tozo ambazo zinatozwa kwa kitanda alaliacho mtalii ni lazima zirudishwe na zisimamiwe kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, siyo tu kutasaidia sana kujenga miundombinu ya mbuga zetu, bali pia kuongeza Pato la Taifa na hadhi na heshima ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kurudia tena; wanyama waliopelekwa nje, hupunguza kabisa kuleta watalii ambao wangekuja Tanzania kuona wanyama hao.

Mheshimiwa Spika, taratibu zilizotumika kuwachukua wanyama hawa kwenda nje pia zitumike tena kuwarudisha wanyama hao Tanzania.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri na ninampa pole kwa kupambana na hali iliyopo.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie na alitolee ufafanuzi wa kina suala la mipaka ya vijiji kama nilivyomweleza. Ningefurahi sana kama wangeamua kuwaruhusu Wananchi wanaoishi kwenye vijiji vilivyosajiliwa na Serikali miaka ya 70 kwa kuwa wamewekeza humo na halikuwa kosa lao.

Nawashauri mkubali kupunguza ukubwa wa Hifadhi na *officially* mkubaliane na kupunguza kero kwa Wananchi ili waendelee kuishi kwenye vijiji vyao halali, kwa amani, furaha na bila wasiwasi. Leo hii Wananchi wa Kata za Nkiniziwa, Puge, Magengati, Millambo Itobo, Mwakashanhala, Utwigu, Muhugi na Mizibaziba, wanaishi kama wakimbizi kwenye nchi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali iliweza kuwapa ardhi ya Hifadhi ya kuishi wakimbizi kule Lugufu, Mishamo na Katumba na inataka kuwafukuza Wananchi maskini kwenye vijiji vyao halali ambapo wana vibali?

Mheshimiwa Spika, naomba kujua hivi mna mikakati gani katika Wizara ya kuzuia *capture* ya wanyama kutoka kwenye Hifadhi zetu? Wanaowakamata wanyama wetu wanakwenda kutengeneza *Zoo*; sasa wakishakuwa na sehemu za kuangalia wanyama huko huko kwao watakuja huku kufanya nini?

Mheshimiwa Spika, *the major competitive advantage we have over them is the presence of Wildlife* kwetu na kukosekana kwao; kwa nini tunawapa faida na unafuu wa kuona rasilimali yetu?

Mheshimiwa Spika, hivi mna-*link* vipi *marketing* yenu ya *Tourism* na uwepo wa *National Carrier* (Ndege ya Taifa)?

Mheshimiwa Spika, Wizara inanuka rushwa na ubadhirifu, pia utendaji mbovu wa baadhi ya Watendaji hususan katika utoaji vibali vya kuvuna misitu na vibali vya kujenga hoteli huko kwenye Hifadhi; kwa nini Mheshimiwa Waziri anakubali kuchafuliwa na kuharibiwa kazi? Hebu washughulikie hawa.

Mheshimiwa Spika, nashauri Watendaji wabovu wote wafukuzwe; na vibali vyote vya wawindaji, wakamata wanyama na wanaojenga hoteli kinyume cha taratibu vifutwe. Vilevile Mheshimiwa Waziri aisafishe Wizara; duniani tutamtambua, tutamtukuza na peponi ataingia!

Mheshimiwa Spika, hivi kwa nini Wizara inalazimisha kujenga barabara ya lami kule Mbugani Serengeti; hamwoni mtaua wanyama na kuharibu uasilia wa *movement* za wanyama?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, lakini yafuatayo yazingatiwe:-

Mheshimiwa Spika, mapato yanayotokana na Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro; asilimia saba inayotolewa na *KINAPA* kwa ajili ya ujirani mwema haitoshi; Halmashauri za Siha, Moshi Vijijini, Hai na Rombo zinazozunguka Mlima Kilimanjaro zikutane na *TANAPA* kuangalia jinsi ya kuboresha mapato; na ianzishwe Tozo ambayo haipungui asilimia 30 ya mapato ya *TANAPA* ili yaende kwenye Halmashauri zinazozunguka Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, Wafanyakazi wanaofanya kazi ya kuhudumia watalii wananyonywa na Makampuni ya kitalii. Kutokana na *guideline* za 2009, malipo ya wafanyakazi wanaohudumia utalii ni kama ifuatavyo; Guide dola 20; Wapishi dola 15; na abeba mizigo dola kumi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ya Kazi ikishirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na *TANAPA*, ihakikishe hawa wafanyakazi wanalipwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, tangu zamani Wananchi wanaozunguka Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro walipewa Ukanda wa Nusu Maili *(Half mile strip),* ambapo Wananchi waliweza kupata majani ya ng'ombe na kuni zilizokauka. Ninashauri eneo hili lirudishwe kwa Wananchi ili Wananchi walitumie.

Mheshimiwa Spika, nashukuru jitihada za Serikali za kutengeneza kwa kiwango cha lami Barabara ya Marangu Mtoni - Kilema Kaskazini - Kirua Vunjo Magharibi - Kawawa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, ikishirikiana na *TANAPA,* wafungue Barabara ya Maua Kilema Kaskazini kwenda katika Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake, ambayo imegusa maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nami nichangie kuhusu mambo muhimu yafuatayo; Misitu, Mazingira na Hifadhi ya Wanyama.

Mheshimiwa Spika, misitu ni kitu muhimu sana popote duniani. Misitu ndiyo inayoleta taswira nzuri ya Taifa letu na kuweka hali ya hewa vyema.

Mheshimiwa Spika, kama misitu itahifadhiwa vizuri, italeta faida kubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nchi zenye misitu kama vile Msumbiji, zimewekeza sana ndani na kusaidia zaidi uchumi wa Taifa. Ni vizuri kuzingatia uhifadhi wa misitu na hii ni Sera ya Kimataifa ya Kuhifadhi Misitu.

Mheshimiwa Spika, mazingira huimarika zaidi kama kutakuwa na Hifadhi za Misitu yetu na hii ndiyo inayoleta mvua na kuboresha kilimo. Ninashauri mazingira yaimarishwe kwa kuitunza misitu.

Wanyama ni viumbe ambavyo vinaishi bila gharama yoyote huko porini, lakini wanyama hawa wanahujumiwa na kuangamizwa.

Mheshimiwa Spika, wanyama wanaingiza mapato Serikalini, kwa maana hiyo, uhifadhi wao uwe mzuri sana ambapo watalii wana uwezo mzuri na mazingira mazuri ya kuweza kuwaona wanyama hao.

Mheshimiwa Spika, lengo kubwa sana la kuwahifadhi wanyama liwe hasa kwa malengo ya baadaye, yaani vizazi vinavyokuja ili waelewe vyema umuhimu wa wanyama na kuwatunza kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mkazo zaidi ufanywe kuepukana na ukataji miti ovyo ovyo.

Mheshimiwa Spika, wanyama walindwe na kuenziwa lakini pia watafutwe wanyama wengine ambao hawapo katika Hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, nazipongeza Hotuba zote zilizotolewa kuhusiana na Wizara hii. Nampongeza Waziri kwa hotuba yake, Hotuba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge pamoja na ile iliyotolewa na Msemaji Mkuu wa Upinzani. Ninaiomba Serikali izingatie sana maoni yaliyotolewa na Kamati pamoja na yale ya upande wa Upinzani, kwa ajili ya ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, Maliasili na Utalii ni Sekta ambayo inao uwezo mkubwa sana wa kuliingizia Taifa pato la fedha za kigeni nyingi pamoja na fedha za ndani. Pamoja na hayo, bado imekuwa ni Sekta isiyothaminika kwa manufaa ya Wananchi wazawa wa nchi hii, bali kwa wajanja wachache ambao wangeuza utajiri asili wa nchi hii kuwa mali ya watu wachache.

Mheshimiwa Spika, ujangiri, wizi, uharamia katika maliasili zetu umeshamiri. Misitu inachomwa moto ovyo, wanyama wanauawa ovyo sambamba na kuibiwa kupelekwa nje ya nchi. Wamiliki wa hoteli wanakwepa kulipa kodi. Kwa hiyo, Serikali inapoteza mapato mengi na makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tunamtaka Waziri awe jasiri kwa kusimamia sheria ili mapato ya maliasili zetu yapatikane na Watanzania waweze kufaidi rasilimali zao, kwa kupata huduma bora za kijamii za msingi, kwani kupitia pato la maliasili na utalii, Tanzania inaweza kupiga hatua kubwa sana ya kimaendeleo, hata kufikia ile ndoto ya maisha bora.

Mheshimiwa Spika, Serikali pamoja na juhudi zake za kukuza utalii ni lazima pia iangalie mazingira ya biashara hiyo kama sehemu ya kivutio. Baadhi ya maeneo yameachwa bila kufanyiwa matengenezo, hii inaweza ikakimbiza watalii. Mfano, Mlima Kilimanjaro, miundombinu yake imekuwa mibovu kwa maana ya vyoo na hii imepelekea kinyesi kutiririka kwenye mito, ambayo Wananchi wanaitumia kwa matumizi ya maji ya kunywa, kupikia na shughuli nyingine za kibinadamu. Hii ni aibu sana kwa Taifa hili, inaweza kuwakimbiza watalii ambao tunawategemea sana katika Sekta hii ili kuongeza kipato.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, tunamtaka Waziri alieleze Bunge lako Tukufu, watu waliohusika katika kutorosho wanyama kwa maana ya Tembo, wachukuliwe hatua kwa maana

ya kushtakiwa lakini pia wanyama hao warudishwe nchini mara moja tena wakiwa hai. Naomba kuwasilisha.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Kwanza, napenda kupewa majibu kwani nilikwishauliza swali Bungeni; kwa nini Wananchi wanakatazwa na hawapewi vibali vya uvuvi na urinaji wa asali katika Pori la Moyowosi Wilayani Kibondo?

Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu inakuwaje wageni wanufaike na Pori hili la Moyowosi wanyimwe vibali vya uvuvi; wanyimwe vibali vya urinaji asali na uwindaji katika pori hili?

Mheshimiwa Spika, pia napenda kupata majibu kwa nini mapato yamepungua yanayotoka kwenye Pori la Moyowosi kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo; mfano mwaka 2009/2010 shilingi 10,713,025; mwaka 2010/2011 shilingi 6,467,113.17; je, hakuna Mikataba?

Mheshimiwa Spika, pia napenda kupata majibu kwamba ni utaratibu gani unafaa ili Wananchi nao waweze kuwinda katika Pori hili bila kubughudhiwa?

Ninapenda kupata majibu ni lini Serikali itaanza kutoza fedha, yaani kodi kwenye hoteli zilizoko kwenye Hifadhi na Mbuga za Wanyama kwani tumekuwa tukipoteza zaidi ya shilingi bilioni 20 mfano mwaka jana pekee?

Tatu, wizi wa wanyama; siungi mkono hoja mpaka nijue kwa nini wanyama wamekuwa wakiibiwa ndani ya nchi na kupakiwa kwenye ndege wakiwa hai. Je, nani anahusika na ni lini wanyama hawa watarudishwa?

Nne, Sheria za Maliasili, *Natural Resource Laws;* Wataalam wa Sheria za Maliasili wanasema sheria hizo zitakuwa ni bora endapo zitatunza rasilimali za Taifa. Kwa kuwa Sheria ya Wanyamapori ya 2009 imempa Waziri mamlaka ya kuteua watu mbalimbali, ningependa kushauri Sheria hii ifanyiwe marekebisho ili baada ya uteuzi, Bunge liweze kuthibitisha watu hao. Je, Kanuni za Sheria hii zimeshapitishwa?

Tano, napenda kupewa majibu na Serikali kwa nini nchi kama South Africa wanatoza pesa nyingi kwa watalii wanaowinda ndani ya Hifadhi zetu wakati wanyama wetu ni bora na ni wa asili kuliko wa South Africa wanaofugwa kwenye mashamba tofauti na wetu wanaokuwa kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kupewa majibu.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza mchango wangu kwa kuunga mkono Hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Mambo mengi yaliyoko kwenye Hotuba ni ya kweli.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono, napenda kuchangia baadhi ya mambo kama ifuatavyo:-

Kwanza, napenda kuchangia kuhusu ulinzi wa wanyamapori. Jambo hili lisipozingatiwa, wanyama watamalizika nchini. Ulinzi huu hautafanikiwa kama Wananchi wasiposhirikishwa. Ujangili huu hasa unafanyika kwenye maeneo ya vitalu vya uwindaji na maeneo ambayo yanahifadhiwa na Serikali. Ni vyema ulinzi uwekewe mkazo mkubwa na ushirikiano mkubwa kati ya Wananchi na Serikali kwa ujumla wafanye ulinzi kwa nguvu kubwa.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa wanyamapori katika maeneo ya Halmashauri ni mdogo sana, jambo ambalo ni kikwazo kwa ulinzi wa wanyamapori. Bora iwekwe bayana kukutana na Viongozi wa Halmashauri ili nao washiriki kwenye ulinzi wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu maeneo ya *WMA*; Wizara isiwe mbali na *WMA* ili wanyama wasiwindwe kupita kiasi kwa ajili ya biashara; wasijali fedha na kumaliza wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Wizara kusaidia uanzishwaji wa *WMAs,* naomba *WMA* ya Lake Natron ambayo imetajwa na Waziri kuanzishwa, kwani Wananchi wapo tayari kuwa na Hifadhi ili waweze kulinda wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, napenda kuupongeza Mfuko wa Wanyamapori *(TWPF)*, kwa msaada mkubwa kujenga vituo kwa ajili ya kulinda wanyamapori kwa maeneo mbalimbali kwenye Kituo cha Longido. Jengo limemalizika, lakini bila gari hakuna uwezekano wa kulinda wanyama kwani eneo ni kubwa mno. Kuanzia Rombo mpaka Lake Natron ni eneo la mpakani, majangili toka Kenya wanakuja kuwinda huko.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la wafugaji jamii ya Wamasai, kuna uuwaji wa Simba kwa wingi kutokana na kula mifugo nao huwatafuta Simba hao mpaka kuwauwa. Huwezi kuwazuia kuwauwa baada ya Simba kuwauwa ng'ombe au mifugo wanaofugwa; kwa ajili hiyo naomba mifugo wafidiwe kama wenzetu wa Kenya wanavyofanya.

Mheshimiwa Spika, ombi langu lingine ni kuhusu maeneo yaliyotengwa kama ardhi oevu *(Ramsar Sites)*; Wananchi wanaishi huko na kulisha mifugo tangu enzi na enzi; inafaa kutoa elimu kwa maeneo yote ambayo ni makazi ya watu mfano Lake Natron ni Kijiji ambacho watu wanaishi na kufuga hapo kutakuwa na migogoro zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwenye ukurasa wa nane, Ibara ya 17, Mheshimiwa Waziri ameelezea kwamba, Wananchi wa Vijijini watapimiwa ardhi; kwenye matumizi bora ya ardhi hili liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kurudia kuupongeza Mfuko wa Wanyamapori *(TWPF),* Hifadhi ya *TANAPA* Wananchi wanafaidika kwa ajili ya mchango wao mkubwa; kwenye Mradi wa Hifadhi wanachangia asilimia 70; huu ni mchango mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, napongeza na naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA A. NYWAYO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri yafuatayo:-

Kwanza, ni vyema Wizara ikaangalia upande wa Kusini mwa nchi yetu, vivutio na malikale zilizopo kama chanzo kingine cha maliasili na utalii. Maeneo kama Mikindani na Kilwa zina magofu, fukwe na utalii wa kiutamaduni, ambao haujaendelezwa. Kwa nini utalii wa kihistoria, makumbusho na malikale zilizopo huko haziwekewi mkakati ili uwe chanzo cha mapato ya nchi yetu? Hivi sasa maeneo ya Kusini yana mawasiliano rahisi kwani barabara ipo; tatizo nini tena?

Pili, nchi kama Afrika ya Kusini hifadhi yake ya Kruger Park inawaleta watalii wengi sana toka kila pembe duniani. Inakuwaje sisi Watanzania wenye mbuga, hifadhi na maeneo mengi yenye sifa za kipekee duniani; tusikamate soko la utalii? Serikali ihakikishe mazingira ya utalii yanaboreshwa zaidi ili pato la nchi yetu likue.

Tatu, Rasilimali ya Nta na Nyuki ipo sana katika Mikoa ya Kusini lakini Wananchi hawajahamasishwa kuitambua na kuielewa ambapo ingeweza kuwa zao mbadala la kiuchumi badala ya Korosho na ufuta. Serikali ichukue hatua za makusudi kuiendeleza Sekta hii. Aidha, kuwepo na Chuo kingine cha Nyuki au Misitu kwenye Mikoa ya Kusini.

Nne, Mji wa Mtwara una wageni wengi sana, wanaongezeka kila kukicha kutokana na utafiti wa gesi na mafuta. Wageni hao hulazimika baadhi yao kulala Dar es Salaam na kuwahi kazini Mtwara kwa ndege asubuhi. Aidha, kutokana na uwezo wao, huduma za hoteli na nyumba

za Mtwara huonekana si za viwango vyao. Kwa nini basi Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii isijenge hoteli moja ya kisasa ili kukidhi haja hiyo na kuongeza pato la nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MURTAZAR A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako, mchango wangu katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara yake kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Ezekiel Maige, Waziri, kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili, nampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana katika utendaji wake wa kila siku.

Mheshimiwa Spika, katika uwasilishwaji wa hotuba, tumeona kuwa, Wananchi wanasisitizwa kuwatunza wanyamapori, lakini pia uhifadhi wa mazingira. Hapa pana tatizo kwa maana Wananchi bado hawajanufaika na rasilimali husika, kwa maana hata gawio la mapato inachukua muda mrefu sana kupatikana. Kwa mfano, Wilaya ya Kilwa haijapokea gawio toka mwaka 2008. Kwa nini tusibadilishe mfumo kwa kuweka tozo husika zikalipwa na kubaki wilayani au kwa ngazi za vijiji ili kuondoa usumbufu kwa Wananchi?

Malipo yawiane pia na uhalisia huku ikizingatiwa kuwa ukubwa wa eneo la Kilwa kama Wilaya ni sawa na Mkoa mzima wa Kilimanjaro mathalani. Pia ni vyema Wananchi wakashirikishwa kulinda misitu na wanyamapori badala ya kuleta askari ambao mara zote wanajenga uhasama na Wananchi. Ifike wakati sasa miti na rasilimali zote ziingizwe kuwa ni mali ya Taifa na ziwe zinakabidhi kwa Uongozi wa Vijiji kama *(assets)* ambazo zinafanyiwa *inventory* kila mwaka au kila baada ya muda fulani ambao utapangwa. Kila viasilia hivyo vipewe namba maalum; mfano *barcode* na pale itakapogundulika haipo mahala pake, basi viongozi wahusika wanawajibika mara moja kama vile wanavyokabidhiwa dhamana nyinginezo za Serikali.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya uvuvi yamepewa kipaumbele ila napenda Serikali ichukue hatua zaidi kuimarisha ulinzi baharini kwa kuwa mpaka sasa hali ni mbaya na Wananchi wazuiwa kuvua katika baadhi ya maeneo huku wengine (wageni) wanavua na kuondoka na rasilimali hizi bila kuzingatia malipo au athari zozote ambazo zinajitokeza baadaye. Wananchi wanaozuiwa kuvua wapewe mbinu mbadala ili kujiendesha katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, nakubali ufugaji wa nyuki ni njia bora katika kuimarisha uchumi ila tatizo kubwa ni elimu kwa wakulima. Tatizo lingine kwa maeneo yetu ni migogoro isiyokwisha baina ya Wananchi na Viongozi kuhusu matumizi ya misitu, ukizingatia kuwa eneo letu limezungukwa na *Selous Game Reserve.*

Mheshimiwa Spika, suala la maeneo ya Hifadhi na mipaka ya Vijiji ni mgogoro usiokwisha na unastahili sasa kuchukuliwa hatua za makusudi kumalizika. Mazingira yaliyo karibu na mbuga yaboreshwe kwa kuweka miundombinu na huduma ili Wananchi wanufaike na rasilimali hizi na kuondoa dhana ya kutoona manufaa ya wanyamapori na pia misitu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo katika uhifadhi wa mikoko na wazalishaji wa chumvi, ambao kila mwaka wanalipa shilingi laki tatu lakini Serikali inashindwa kuwalinda wazalishaji hawa katika soko kwa kuweka mfumo huria kwa chumvi kuagizwa nje ya nchi huku iliyopo hapa nchini haina soko.

Mheshimiwa Spika, Hotuba pia imezungumzia uhifadhi wa malikale, lakini kuhusu mapango sijasikia wakizungumzia Mapango ya Kipatimu wala mpango wa uhifadhi wake hali ya kuwa wamezungumzia Mapango ya Amboni. Jitihada ifanyike ili kubaini maeneo mapya ya utalii na kuyaboresha, ikumbukwe Waziri wa Maliasili wa zamani, Mheshimiwa Zakhia Meghji, alitoa ahadi kwa Wananchi wa Kilwa kuimarisha miundombinu na kuyaweka mapango haya katika ramani ya vivutio vya utalii nchini. Tuna makanisa na misikiti ambayo ina uhai wa zaidi ya miaka mia moja pia.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru na kuipongeza Serikali kwa kutangaza vivutio vya nchi vikafahamika katika maeneo mengi zaidi duniani na hatimaye kuliongezea Taifa pesa za kigeni zipatazo Dola za Kimarekani 1987.5 milioni. Naishauri Wizara iongeze jitihada katika kuongeza na kupanua wigo wa aina za utalii kuhusisha utamaduni, mazingira, historia, makumbusho na michezo. Naishauri Serikali iangalie upya namna ya kutangaza vivutio vya utalii nchini hasa kwa kuitisha mkutano wa wadau ili tuishauri Serikali namna bora ya kutangaza hasa katika Nchi za Mataifa ya Ulaya, Asia na Amerika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya yote mazuri, nadhani lipo tatizo katika Sekta ya Utalii nchini kwa maana ingeweza kufanya zaidi ya hayo. Tukiangalia kwa jicho la tatu na kwa undani, utaona changamoto nyingi sana na kubwa. Changamoto hii ipo katika mgawanyo wa kile kinachokusanywa baina ya Mawakala wa Utalii na Serikali. Sina uhakika kama Wizara au Idara inazo takwimu sahihi za wageni wanaoingia Tanzania na viingilio vyao na kama kweli tunaweza kuzidisha idadi ya wageni na viingilio tukapata mapato yanayotolewa Wizarani.

Mheshimiwa Spika, hapa kuna tatizo kubwa kwa maana watalii wanaingia wakiwa tayari wamelipia kila kitu (visa, viingilio, hoteli, usafiri na kadhalika), baadaye wakala analipa kwa kuieleza Serikali na kutaja tarehe ambazo walileta wageni. Sijui kama kunakuwa na uangalifu *(cross checking)* kwa idadi ya wageni na taarifa zao ni sahihi kiasi gani na hata kodi anayotakiwa kulipa inakuwa hivyo hivyo. Hivi kwa nini wasije kulipia tozo hizi zote hapa nchini na kuongeza mzunguko wa fedha za kigeni hapa nchini? Ukweli ni kwamba, mzunguko wote wa ada, *visa,* hoteli na usafiri, zinabaki watokako na sisi tunaambulia vumbi tu na makombo tu ya watokako huku ajira kwa vijana wetu ikiwa shakani.

Mheshimiwa Spika, nalitolea mfano hili; mwezi Januari, 2011 meli kubwa ya kitalii inayoleta watalii kutoka Nchi za Ulaya ilipita Mombasa, Tanga, Zanzibar na kuja Dar es Salaam ilielekea Afrika ya Kusini. Kati ya wageni waliokuwa katika meli ile, walikuwa wamekata tiketi ya kutembelea Bagamoyo na Dar es Salaam, kila mmoja alitoka kwenye meli na tiketi yake na kupanda gari kuelekea sehemu aliyochagua.

Mheshimiwa Spika, kilichofanyika, walitafuta wakala hapa nchini kwa kuwalipa kiasi kidogo na kufanya kazi ya kuwatembeza bila kujua huko kwao wametozwa kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, mfano wa pili ni ule wa wageni ambao wanatoka katika Nchi za Amerika na Ulaya na kuingia kwa kutumia Uwanja wa Ndege Mdogo wa Soronera, wanatembelea Mbuga za Serengeti na Ngorongoro na kukaa hotelini kisha kuondoka. Wote hawa wanakuja wakiwa wameshalipa kila kitu kwao. Wageni hawaendi hata Arusha Mjini kulala kwenye hoteli za ndugu zetu na wala hawapiti kwenye maduka kununua vitu mbalimbali vya kitalii ili wanufaishe biashara zetu. Matokeo yake makampuni yanayowaleta yanapiga hesabu na kuja kuwasilisha Serikalini viingilio na kodi baada ya safari zao. Kama watu wa *National Park* wanalinganisha idadi ya wageni na pesa wanazolipa baadaye ni kidogo sana ukilinganisha na hali halisi. Hili utalishuhudia kama nilivyofanya utafiti niliposafiri kutoka Soronera kuja Ngorongoro kwa gari ndogo. Baada ya kuona watalii wengi wakishuka kwenye ndege na kuanza safari za kutembelea vivutio vya utalii, nikaamua kufanya utafiti usio rasmi.

Niliamua kuhesabau magari ya watalii kutoka *gate* la kutokea Sorenera mpaka *gate* la kutokea Ngorongoro ili kufika Olduvai Gorge, Laetoli, Crater au kwenye maboma kwa muda wa saa nne (saa tatu hadi saa saba. Nilihesabu magari niliyokutana nayo uso kwa uso yalifikia 633, mengine makubwa na madogo ambayo yanabeba wastani wa watu kumi hadi kumi na mbili na mengine madogo ambayo yanaweza kubeba watu wanne hadi sita.

Nilikadiria wastani wa watu watano kila gari, hivyo kupata idadi ya wageni takriban 3,165 kwa muda wa saa nne, ikimaanisha ni wastani wa wageni 792 kwa kila saa. Wakati huo Ngorongoro walikuwa wanaruhusu wageni kuingia kuanzia saa mbili mpaka saa kumi na mbili. Kama saa kumi zinatumika kwa wageni kutembelea mbuga, kwa hiyo, wageni takriban 7,920 wanatembelea mbuga kwa siku moja; si haba. Kimsingi, inatulazimu kuangalia upya mfumo wa malipo kwa watalii wanaoingia nchini na hasa wanaolipia gharama katika maeneo ya nchi wanazotoka kwa maana hatuna *proper mechanism* katika ukusanyaji wa tozo hasa zile

zinazofanywa kielektroniki kama *credit cards, debit cards, check cards* na kadhalika; ni njia ipi inayotujulisha kama wamelipa kiasi gani na kodi zetu na stahiki nyingine tunazipataje.

Mheshimiwa Spika, Sera na Sheria za Maliasili zilenge kumnufaisha Mwananchi wa kawaida, ikizingatiwa kuwa wao ndiyo washiriki wakubwa katika kulinda na kuhifadhi rasilimali hizi; hivyo, wanastahili kunufaika nazo. Wawindaji wanalipa mirabaha sawa na asilimia 30 ya faida zitokanazo na pato (biashara ya uwindaji), kwa ajili ya maendeleo kupitia Halmashauri zao kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, jitihada za makusudi kabisa zifanyike kuhakikisha kila Mwananchi anashirikishwa katika upandaji wa miti na ni vyema kila Kata au kila Kijiji kikawekewa lengo ama kiwango maalum au idadi ya miti ambayo wanatakiwa kuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba nikushukuru kwa kunipokelea maoni yangu kwa kuamini kuwa, yatafanyiwa kazi stahiki. Nakutakia kila la kheri, namwomba Mungu atulinde sote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja. Kwanza, lazima tuthamini na kuwa na uchungu na rasilimali zetu tulizopewa na Mwenyezi Mungu. Tusitoe au kuacha watu kutuibia wanyama wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara idhibiti jambo hili. Sheria kali ziwekwe na utekelezaji wake ufuatiliwe kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwenye *TANAPA* kama ifuatavyo:-

Ninavyojua Shirika la *TANAPA* linashughulika na Mbuga za Wanyama za Taifa *(National Parks)*. Kwa nini *TANAPA* wanatoa *incentives* kwa Wananchi wanaozunguka Mbuga za Wanyama tu hawatoi kwa nchi nzima? Mfano, wanaweza wakatoa hata vitabu na madaftari katika shule za msingi kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ifanye utaratibu *TANAPA* iweze kupanua wigo wake ili kila Mwananchi afaidi matunda ya Mbuga zetu. Watakuwa na hamasa ya kutembelea Mbuga zetu. Waige mfano wa *NMB* wanaosaidia popote katika shule zetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nampongeza Mheshimiwa Waziri; awe shupavu na afanye kazi yake bila woga.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa bajeti nzuri na uwasilishaji mahiri. Pia nawapongeza Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Watumishi wa Wizara, kwa uandaaji mzuri wa Bajeti.

Upangaji madaraja ya Hoteli: Mheshimiwa Spika, naipongeza wizara kwa juhudi kubwa ya kuboresha uhifadhi wa maliasili na kuboresha utalii nchini mwetu. Mikakati wanayoitekeleza inazaa matunda mazuri. Napenda kusema jambo moja ambalo Wizara inafaa ilisimamie kwa umakini nalo ni upangaji madaraja ya hoteli *(Classification)*. Hili litaongeza ufanisi katika Sekta ya Utalii. Watalii wetu wanapokuja wajue wategemee nini katika hoteli watakazofikia. Katika kufanikisha hili, Wizara iongeze juhudi ya kusimamia uzalishaji wa wataalamu wa huduma za hoteli; wapatikane wataalam wengi zaidi wa ndani watakaofanya kazi katika Sekta hii. Tupunguze uhitaji wa watumishi wa sekta kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa kutenga pesa na kuweka mikakati ya kutangaza vivutio vya utalii vya nchi yetu. Wizara iendelee na mikakati hii, lakini eneo la utalii

wa ndani bado linahitaji msukumo mkubwa. Watanzania wengi bado hawatembelei vivutio vya nchi. Mkakati wa *NCAA* wa kuwabeba Wananchi toka Arusha kwa ada nafuu uimarishwe na uigwe na Mamlaka zingine na Wizara itoe maagizo maalum. Tupandishe kwa kiwango kikubwa utalii wa ndani ili utalii huu uchangie mapato ya sekta. Nchi nyingi zinachangiwa sana na utalii wa ndani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na rekodi ya mafanikio, Wizara inatakiwa ishughulikie kero za Wananchi; moja ya kero hizo ni mipaka ya Hifadhi na ardhi ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Bagamoyo, hivi karibuni kumezuka mgogoro mkubwa wa ardhi katika Kijiji cha Kitame, baada ya *SANAPA* kabadili mipaka yake bila ya ushiriki wa Wananchi wa Kitame! Mheshimiwa Waziri atoe kauli kwa nini *SANAPA* inafanya taratibu hizi zisizokuwa za haki kwa Wananchi wa Kitame? Namwomba Waziri alitafiti tatizo hili na kuingilia kati ili mipaka mipya iwekwe baada ya mashauriano na Wananchi na kama Wananchi wataridhia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, hivi karibuni nilikuwa UK na sikuona matangazo ya utalii kwenye mabasi ya Lowdham kama wanavyofanya Kenya; bila matangazo hatutaweza ku-*capture* soko hili kama Kenya.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wataalam, kwa Hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara izingatie uhifadhi wa wanyama zaidi na hivyo uwindaji na kusafirisha wanyama hai nje ya nchi upigwe marufuku.

Mheshimiwa Spika, mipaka yenye migogoro kati ya hifadhi na vijiji ihakikiwe, lakini kila mara Wananchi husika wasikilizwe zaidi wakibainisha maeneo ardhi ya vijiji inapoishia ndipo hifadhi ianzie pale.

Mheshimiwa Spika, wanyama waliotoroshwa warudishwe nchini na warudishwapo Taifa zima lihabarishwe.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuchimba *Uranium* uanze upya. Kamati mbili za Bunge; Nishati na Madini na Ardhi, Maliasili na Mazingira, zihusike ili ajenda iwe ni ya Serikali na Kamati za Bunge. Mwekezaji anayefahamika sasa awekwe pembeni ili mpango ukikamilika aweze kuja naye ashindanishwe sawa na wenzake watakaojitokeza wakati huo kama wawekezaji wengine.

Mheshimiwa Spika, *WMA* ya endema Wilayani Kiteto sasa wapatiwe *User Rights* ili jamii zianze shughuli zao za kutunza na kuhifadhi wanyama. Pori la Akiba la Mkungunero liishie mipaka ya Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Spika, mwindaji aliye makini aitwaye *Big Game Safaris* adhibitiwe vizuri. Amefukia visima vya maji vya jadi na kujenga kiwanja cha ndege eneo lenye mgogoro na Kijiji cha Makame. Wizara isimamie mgogoro huu uishe.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, Utalii kama Sekta muhimu kwa uchumi wa nchi yetu, umeelemea sana Kaskazini. Mara nyingi *TANAPA* hutangaza utalii kupitia Balozi zetu kwa njia ya vipeperushi, ambapo *TANAPA* inafanya shughuli zake katika maeneo ya Kaskazini zaidi.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Kusini mwa nchi yetu vipo vivutio vingi vya utalii hususan utalii wa kihistoria na kijiografia. Je, Serikali ina mpango gani wa kutangaza vivutio hivi nchi za nje ili kupunguza msongamano kule Kaskazini?

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa juhudi kubwa ambazo amezionesha tangu apate nafasi hiyo hasa ikizingatiwa kwamba, hana Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, wanawake/vijana wengi sasa hivi ni wajasiriamali kwa kutengeneza shanga, vinyago, mavazi mbalimbali ya kiasili ambayo huwavutia sana watalii. Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia kupitia Wizara hii ili waweze kuuza mali zao huko nje badala ya nafasi za kwenda kwenye maonesho kutumiwa na Maafisa wa Wizara wakienda huko bila vifaa vyovyote.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara hii haioni ni wakati mwafaka umefika kuwasaidia vijana walioko kwenye hoteli za kitalii kuwanufaisha kundi hili kwa kuwapatia nafasi za mafunzo ili waweze kukidhi haja ya kuwahudumia watalii vizuri zaidi na kuleta mvuto katika kutoa huduma ya kiutalii?

Mheshimiwa Spika, Wizara ina mpango gani kwa Jamii ya Kimasai ambao wapo ndani ya Hifadhi, kuwaruhusu kulima mboga mboga kuzunguka vibanda vyao kama vile matembele, majani ya maboga, majani ya kunde, maharage, mchicha na kadhalika kwa masharti maalum kwani Serikali inawasaidia kupata mahindi na mchele bila mboga?

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, MBOMIPA isaidiwe hata kwa ruzuku ili ifanye kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Spika, Wataalam wa Idara ya Wanyamapori waongeze ari ya kuzisimamia *WMA* na baadhi yao waache kushirikiana na wale wanaovuruga. Naomba MBOMIPA isaidiwe ili kesi zake ziishe.

Mheshimiwa Spika, Taasisi za Wizara zisaidie sana Jimbo la Ismani ambalo kwa sehemu kubwa ndilo linalozunguka *Ruaha National Park*. Wizara na yenyewe ihimize ujenzi wa barabara ya lami kwenda Ruaha badala ya kuachia Wabunge.

Mheshimiwa Spika, viwango vya uchangiaji kwa Miradi ya Maendeleo ya Jimbo la Ismani ni vidogo ukilinganisha na ukubwa wa kazi na ukubwa wa Mbuga *(Ruaha National Park)* na ukilinganisha na viwango vya misaada inayotolewa katika vijiji vinavyozunguka Mbuga nyingine za Kaskazini. Hii haifai kuendelea kwani sisi pia tunafanya kazi kubwa na tumejitolea sana kulinda na hasa kwa kuzingatia eneo letu ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara, *TANAPA* na Mfuko wa Wanyamapori, watusaidie kujenga Vituo vya Polisi Idodi na Pawaga ili kuimarisha ulinzi wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, naomba *TANAPA* na Mfuko wa Wanyamapori watusaidie kujenga Zahanati Kinyika - Pawaga, kuweka umeme wa jua Zahanati, Vituo vya Afya na Shule za Sekondari za Pawaga, William Lukuvi, Mlowe na Idodi; na Zahanati za Mlowa, Isele, Kisenga, Usolenge, Magozi, Ilolo mpya, Nyamehene, Mahuninga, Tangamalenge, Idodi na Kitisi.

Mheshimiwa Spika, ni lini mpango wa kujenga eneo jipya la *Ruaha National Park* Kijiji cha Kitisi utaanza?

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Wizara ichangamkie matatizo ya Wananchi wanaozunguka Mbuga badala ya kusubiri kuombwa ombwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa, idadi ya Watanzania wanaotembelea maeneo ya utalii ni wachache sana. Napendekeza kuwa, Wizara na Taasisi zake zijitahidi kuhamasisha Watanzania hasa wa kada ya kati na chini, waone umuhimu wa kuhudhuria na kutembelea kwenye maeneo yetu ya utalii.

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya *CAG* inaonesha kuwa, Wizara hii ina matatizo makubwa katika suala zima la fedha. Ningependa kujua tatizo ni nini hasa na je, hatua gani zimechukuliwa kwa wote waliosababisha Wizara hii kuwa na upungufu huu?

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua *Project* ya Vyura wa Kihansi imefikia wapi? Napenda kujua hatima ya vyura hawa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilombero imebarikiwa kuwa na Milima ya Udzungwa, ambayo ni kivutio kizuri kwa watalii, lakini cha kusikitisha ni kuwa hakuna barabara ya lami kuelekea kwenye milima hii; hivyo, kusababisha watalii wengi kutotembelea milima hii na kuikosesha fedha/mapato Serikali yetu. Napendekeza Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi hasa kwenye bajeti ijayo, Wilaya hii ipate barabara ya lami ili kuongeza idadi ya watalii kwenye Milima ya Udzungwa na Mbuga ya Wanyama ya Selous.

Mheshimiwa Spika, wanyama wamekuwa kero kwa Wananchi wa maeneo yanayozunguka mbuga. Wizara imejipangaje kuzuia wanyama hawa hasa Tembo kuingia kwenye vijiji?

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la mipaka kati ya Wananchi wanaoishi katika Kata za Kidatu, Sanje, Mkula, Mang'ula, Mwaya, Kisawasawa, Kiberege na maeneo mengine yanayozunguka Milima ya Udzungwa. Wananchi wanalalamika kuwa, *TANAPA* wameinga kwenye maeneo yao. Napendekeza Wizara ilifanyie kazi suala hili kule Wilayani Kilombero.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Kilombero wengi wao wanatumia kuni kama chanzo chao muhimu cha nishati ya moto, lakini cha kusikitisha ni kuwa, Wananchi hawa wamezuiliwa kuokota kuni bila kuandaliwa mazingira mbadala ya kupata nishati.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itoe kauli kuhusiana na suala hili; hivi ni sahihi kweli kuokoa miti wakati Wananchi hawana nishati mbadala?

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. ABDULSALAAM SAMEIR:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Yafuatayo ni malalamiko yangu kuhusu mipaka ya Kihelelo, Ruhemba na Msindani:-

Mheshimiwa Spika, sehemu ambayo Hifadhi imeingia naomba ibaki kama ilivyo ili kufidia eneo ambalo Kijiji cha Ruhembe kimeingia kwenye Hifadhi. Eneo ambalo wanakijiji wameingia kwa kweli Wananchi hawa kama mtawatoa, tutawaletea umaskini wa kudumu. Eneo hilo lote limelimwa miwa na miaka yote ndiyo tegemeo lao katika kutoa umaskini. Takriban zaidi ya asilimia 25 ya wakulima wa miwa katika Kijiji hicho wanalima hapo.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri azingatie maombi yangu kwa niaba ya Wananchi na Wakulima wa Miwa katika Kijiji cha Ruhembe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa maandishi. Awali ya yote, naunga mkono hoja hii ili atekeleze wajibu wake pamoja na yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Mpanga, Jimbo la Njombe Magharibi, walihamishwa na kupelekwa Mpanga A, baadhi walilipwa fidia na wengine bado wanadai mpaka leo na wengine wamefariki bila kulipwa fedha zao; kuna malalamiko mengi na namna zoezi zina lilivyoendeshwa; na ramani ya awali haina mgogoro na Wananchi waliikubali japo hawakulipwa wote.

Mheshimiwa Spika, *TANAPA* wamekuja na hoja mpya ya kurekebisha mpaka na kutaka Wananchi wa Vijiji vya Mpanga A, Malangali, sehemu ya Ludinga wahamishwe tena baada ya kufanya uthamini wa mali zao ili kupanua eneo la Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, jambo hili halikubaliki kabisa na Wananchi pamoja na Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Njombe; kwanza, hakuna kwa kuwapeleka hata kama unataka kuwalipa fidia; na pili, wanyama wanaolengwa kuhifadhiwa hawapo.

Watumishi wa *TANAPA* wanawanyanyasa sana wanavijiji tajwa, kwa kutumia ubabe hata yale maeneo ambayo yahajafidiwa kila mara wanawatishia kuwa watahamishwa. Wananchi hawa hawana raha hata kwenye nchi yao.

Mheshimiwa Spika, mimi nikiwa Mbunge wao, sikubaliani na namna *TANAPA* wanavyokwenda moja kwa moja kwa Wananchi bila kuwashirikisha Viongozi wa Serikali na Chama, ikiwa ni pamoja na mimi ambaye ni Mbunge wao au Diwani wa Kata ya Ludinga. Wananchi kwanza na wanyama baadaye. Naamini Waziri atalishughulikia hili haraka na naomba atutembelee ili ajionee mwenyewe hali halisi ilivyo. Kesi ya Mpanga inafanana sana na ile ya Mbarali.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko mengi ya namna Wizara inavyotoa vibali vya kuvuna Msitu wa Sao Hill. Inaonesha utaratibu uliopo haupo wazi sana *(transparent system)* ya vigezo vinavyotumika kupata kibali. Ninao Wananchi wameomba kwa zaidi ya miaka mitatu hawajawahi kufanikiwa. Nashauri utaratibu uliopo uelezwe vizuri zaidi kwa Wananchi.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Spika, dhima kubwa ya maliasili ni kutunza mali kale zikiwemo wanyama, misitu na mabaki ya mapango au masalia ya nyumba za kale ili viwe endelevu. Hivyo basi, maeneo ambayo yana misitu ya asili yanalazimika kuitunza ipasavyo, kwani leo hata watalii wa ndani hawawezi kuitembelea.

Mheshimiwa Spika, *museums* zimesahaulika kabisa, si wazawa wala watalii wa nje, hawafikirii kutembelea sehemu hizi za kumbukumbu. Katika *covering paper* ya kitabu chako imeonesha kumbukumbu ya Nyayo za Laetol; je, ni watalii wangapi wa ndani na nje wametembelea sehemu hiyo?

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine kama hiyo ipo Halwego Handebezyo katika Kisiwa cha Ukerewe Mkoani Mwanza, leo imesahaulika limekuwa pango la wavuta bangi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na udhibiti hafifu wa uvunaji wa mazao ya misitu ya asilia, tatizo kubwa linajitokeza wale wanaopewa dhamana ya kulinda na kusimamia uvunaji ndiyo wanaohujumu zoezi zima. Misitu midogo midogo ya asili imeteketezwa kwa kuvunwa bila mpangilio.

Mheshimiwa Spika, wanyamapori waishio majini hasa Ziwani (Ziwa Victoria), wamekuwa wakiharibu mazao na kujeruhi watu. Pale wanapoharibu mazao, Wizara yako haichukui hatua yoyote lakini mnyama mmoja akiuawa Wizara yako inahoji!

**MHE. MOHAMED G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mkuu wangu wa Mkoa, Mheshimiwa Dkt. Parseko Kone, kwa ubunifu wake wa kuanzisha Makumbusho ya Mkoa wetu, ambayo yako Jimboni kwangu. Makumbusho haya yamesaidia sana kutunza vitu vya asili; mfano, vifaa vya ngoma, uwimbaji, mavazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha makumbusho haya, naomba yafuatayo:-

(i) Ninaomba Serikali itenge fedha za kununulia samani ili vitu vya asili viweze kuhifadhiwa vizuri kwani ni kumbukumbu za vizazi vijavyo na italeta heshima hata wageni (watalii), wanapokuja watavutiwa kutembelea mara kwa mara.

(ii) Ninaishauri Serikali iajiri mtaalam mwenye kusomea fani ya utalii ili aweze kusaidia kuendelea kutafuta vitu vya asili vijijini mapema kabla wazee wa zamani hawajafa wote. Ninasubiri jibu kwa Mheshimiwa Waziri wakati akijibu hoja hapo kesho.

(iii) Napenda kuitaarifu Serikali kuwa bado kuna tatizo la Wananchi kukata miti kwenye Misitu ya Hifadhi iliyoko Mwankoko na Unyamikumbi kwa ajili ya kuchoma mkaa. Hii inaharibu hifadhi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ikemee swala hili.

**ABDULKARIM I. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Watumishi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, azidi kujizatiti na kuhakikisha Sekta hii ya Utalii inazidi kuchangia katika pato la nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba yale yote yaliyopendekezwa na Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ayachukue na kuyafanyia kazi. Naomba Mheshimiwa Waziri, akaze buti na asikubali kudhalilishwa na watu kwa niaba ya watu wengine wanaofanya madudu ndani ya Wizara au Idara zake.

Mheshimiwa Spika, naomba sana katika utangazaji wa utalii muikumbuke Mafia jamani; kuna fukwe nzuri, mandhari ya bahari nzuri, magofu yapo tena ya zamani katika maeneo ya Juam, Chole, Kismani Mafia na sehemu ya Kijiji cha Kange, tuna Potwe (Whale Shark), samaki mkubwa anayecheza na binadamu tuna Hifadhi ya Bahari yenye kila kivutio ndani ya maji; ni nzuri na ni namba moja katika Pwani yetu ya Afrika Mashariki. Jamani tutangazieni maeneo ya Kisiwa chetu.

Mheshimiwa Spika, sina zaidi ila ni kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii nitoe mchango wangu juu ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii, ambayo ni chachu ya uchumi na maendeleo ya nchi yetu juu ya unyanyuaji wa Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Upinzani siyo tu kupinga kila kitu ambacho kitawasilishwa na Serikali, bali ni kuwa na sababu za msingi ambazo zitathibitisha ukweli wa hoja zitakazotolewa na Upinzani kwa misingi ya kuielekeza Serikali ili iendelee kuifanyia vyema jamii wanayoiongoza.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba, Hotuba hii iliyowasilishwa na Mheshimwia Waziri, imeonesha mwanga na imeandikwa kwa umakini mno licha ya kasoro ndogo ndogo zilizojitokeza na ambazo kuna uwezekano mkubwa wa kuweza kuzirekebisha; mfano, kima kidogo ambacho kimeidhinishwa kwa ajili ya kutolea matangazo Sekta hii ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, Sekta hii ya Utalii ni muhimu sana na ni Sekta ambayo wenzetu walio nchi jirani siku zote wanachukua mapato ya Watanzania kwa mlango wa nyuma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na udugu na ujirani tulionao baina ya Tanzania na Kenya, lakini ndugu zetu Wakenya wanautumia Mlima Kilimanjaro kana kwamba ni sehemu ya ardhi yao. Wanathubutu kuwatangazia watalii kutoka sehemu nyingine za duniani kwamba, wafike Kenya kuuona Mlima Kilimanjaro. Katika hili naiomba Serikali iweze kutoa kauli juu ya majirani zetu hawa ili waheshimu uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi pekee iliyojaliwa maliasili zenye kuvutia, Tanzania imejaliwa kuwa na kijani kibichi kwa asilimia 70; pia ina Mito, Maziwa na Bahari yenye fukwe za kutosha ambazo ni kivutio pia kwa watalii wanaoingia na kutoka nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, umoja na mshikamano wa ngazi ya juu ya Wizara pamoja na kada za chini ya Wizara hii umedhihirika mbele ya Bunge hili, kwani hata kama wapo wanaosema kwamba, kuna tatizo hili katika Mbuga au Hifadhi ya wanyamapori, lakini hakuna aliyepingana na utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika hifadhi ya wanyamapori kuna mambo lazima yapangiwe sheria upya juu ya utekelezaji wa baadhi ya migogoro na matatizo yanayojitokeza katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu na hata katika hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii na Waziri Maige wameisitiri sana Serikali kutokana na utendaji wao ulio makini mno, jambo ambalo litakuwa ni changamoto kubwa kwa Wizara nyingine za Serikali; na hapa Serikali itathibitisha kwamba, siyo kweli kwamba Upinzani unapinga kila kitu.

Mheshimiwa Spika, suala zima la uchomaji misitu ovyo na ambalo haliangaliwi kwa upana wake, linachafua moja kwa moja mazingira ya nchi yetu. Siyo vyema suala hili la uchomaji miti ovyo likaachiwa Wizara peke yake; suala hili ni la ulinzi wa kila mmoja wetu kwani uchafuzi wa mazingira hupelekea kuleta janga kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina mazao yatokanayo na misitu kama vile uvunaji wa mbao zitokanazo na misitu. Katika hili kuna sheria zinazotumika katika kuwapatia vibali Wananchi wanaoomba vibali na usajili wa ukataji wa mazao ya misitu. Ninaomba Wizara iwatendee haki wale wote ambao waliomba wapatiwe usajili wa uvunaji wa mbao zitokanazo na miti ya misitu, ingawa ninaamini kwamba, haki itatendeka kwa wale wote walioomba usajili wa uvunaji wa miti ya mbao itokanayo na misitu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uhifadhi wa wanyamapori lakini napenda niseme kwamba, tunaheshimu sana hifadhi ya wanyama hao pamoja na usalama na uhai wa maisha yao. Hata hivyo, uhifadhi wa Wananchi wetu walio pembezoni mwa Hifadhi ya Wanyamapori ni suala la kulizingatia ipasavyo; vinginevyo ni kuhatarisha maisha ya Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kundi ambalo linaipatia Tanzania mamilioni ya dola ni la wageni. Hata hivyo, wageni hao wanaoingia nchini mwetu kwa nia ya utalii ni lazima wazingatie mila na desturi za nchi yetu. Mwanaadamu ni mwanaadamu ni tofauti na wanyama.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi wa tano, katika Hoteli ya White Sand iliyoko nje kidogo na Jiji la Dar es Salaam, waliingia watalii ambao walikuwa wakitembea kama wanyama! Sasa utalii wa aina hii hatuna haja nao, Watanzania tunataka watalii wenye heshima zao na siyo wahuni. Kwa kuwa Waziri anayeongoza Wizara hii ni mfuatiliaji, naamini kwamba, wale wote ambao watakwenda kinyume na sheria za nchi yetu, watachukuliwa hatua za kufaa.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, naomba niungane na wenzanugu katika kuchangia Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Katavi ni kubwa na yenye wanyama wakubwa na wenye afya nzuri sana na ukizingatia hifadhi hii ina msitu mkubwa unaofanya wanyama mbalimbali waishi vizuri sana. Tatizo kubwa la Hifadhi hii ni kutokutangazwa vya kutosha na Wizara, kwani matangazo mengi yanaelekezwa kwenye Hifadhi za Mikoa ya Kaskazini kuliko Mikoa mingine hasa ya Nyanda za Juu Kusini ambako nako kuna Hifadhi za Kitulo, Ruaha, Gombe, Mahale na Mbuga ya Katavi ambako mimi natoka. Jitihada za dhati za kutangaza Hifadhi zetu bado hazijafanyika. Naiomba Serikali ifanye juhudi kubwa za kufanya matangazo ya kuitangaza Mbuga ya Katavi ili iweze kupata watalii wa kutosha, ambao watasaidia kukuza uchumi wa eneo la Mpanda.

Mheshimiwa Spika, bado Wizara haijaweka utaratibu wa kuwaelimisha Wananchi wa nchi hii waweze kushiriki na kutembelea mbuga za wanyama zilizoko karibu nao. Tukiishirikisha jamii, taasisi mbalimbali kama mashule, Watumishi wa Serikali, Viongozi wa Dini na Viongozi wa Kisiasa wanaweza sana kuiimarisha Sekta ya Utalii wa Ndani ukakua kwa kiwango kikubwa sana na kuchangia Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, upanuzi unaofanywa na Hifadhi lazima uwashirikishe Wananchi wa maeneo husika. Wananchi wakishirikishwa, tutapunguza migogoro inayojitokeza kati ya Wahifadhi na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wananchi kwa sasa wanakuwa watumwa katika nchi yao kwa kukosa maeneo ya kufanyia shughuli za kilimo. Niwaombe Serikali waangalie upya maeneo ambayo yana migogoro kati ya Wananchi na Wahifadhi iangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa Mradi wa Vijiji kumi na *UBENDE Group* ni mkubwa sana na hautaweza kupata ufumbuzi kama Wizara haijatoa maamuzi ya kuliacha eneo hili, kwani ukweli halisi wa Mradi huu ni wa kitapeli kwa baadhi ya Watendaji wa Halmashauri ya Wilaya wa Kitengo cha Msitu, kujimilikisha eneo hilo kwa maslahi yao binafsi ambayo haiwasaidii Wananchi hao wanaoishi katika Vijiji vya Kakese, Kabage, Mwamkulu, Nkungwi, Sibwesa, Kasekese, Matena, Kapalamsenga Itenka. Naishauri Serikali kupitia Wizara waje waone maeneo hayo na ukweli utaonekana. Haiwezekani Wananchi waporwe ardhi yao kwa kudanganywa kwa kupewa nyama. Kitendo hicho ni cha kuwadhalilisha Wananchi, nami mwaskilishi wao sikubaliani. Naomba Wananchi hawa wawe huru na ardhi yao.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tabia mbaya sana ya kutokutoa huduma kwa jamii zinazozunguka Hifadhi na maeneo ya uwindaji. Jamii itanufaika vipi na rasilimali zilizopo? Tunaomba sasa wawindaji na wahifadhi wawe wanawashawishi wawekezaji wanapokuja wahakikishe wanatoa huduma kwenye maeneo ya wanakijiji.

Mheshimiwa Spika, naomba Mhifadhi wa Mbuga ya Katavi ashirikiane na Wizara kuhakikisha wanaomba msaada wa Serikali kuokoa wanyama aina ya viboko na mamba walioko Mbuga ya Katavi, wanaokufa kwa kukosa maji. Wizara iandae Mpango Mkakati wa kuchimba mabwawa ili kuwahifadhi wanyama hao ambao wapo katika hali ya kutoweka.

Mheshimiwa Spika, endapo nitapata majibu, nitaunga mkono.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanywa katika kuimarisha mapato ya Serikali. Naomba yafuatayo yaweze kufanyika:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhakikisha *concession fees* inalipwa kwa kiwango kunacholingana na thamani halisi ya fedha wanazopata wawekezaji. Napendekeza isiwe chini ya dola 50. Kwa wawekezaji watakaoshindwa kufuata taratibu za nchi ni bora waache na wenye nia njema ya Taifa hili watakuja kuwekeza.

Pili, naomba Wakazi wa Wilaya ya Kisarawe katika Vijiji vya Vikumburu, Kihare, Dololo na Gwata, wanaopakana na Hifadhi ya Selous, wawezeshwe kwa shughuli mbalimbali za uchumi ili kuleta tija kwa Hifadhi na Wananchi.

Tatu, naomba Serikali inijulishe ni jinsi gani Wananchi wa Kitongoji cha Mwambisi Kisarawe imepatikana hatima yao. Ikumbukwe kama nilivyoeleza awali kwamba, Kitongoji hiki kilitambuliwa rasmi kwa Tangazo la Serikali Na. 205. Naomba Wananchi hawa wanaotangatanga mpaka sasa, Serikali itoe ufumbuzi wa Wanakitongoji hawa nini hatima yao. Naiomba Serikali itafute ufumbuzi wa kuwasaidia Wananchi hawa ambao Kitongoji chao halali kimevunjwa kwa kuwa wamevamia Hifadhi ya Msitu wa Pugu.

Kwa nini Serikali isione sasa kuna makosa yamefanyika hivyo kuwalipa fidia Wananchi hawa au kuwaacha katika Kitongoji chao kinachotambuliwa rasmi na Serikali? Kitongoji hiki kina uongozi wake rasmi.

Nne, naomba Wizara ikomeshe mauaji ya Wananchi kwenye maeneo ya Vijiji vinavyopakana na Selous kwani yanaweza kupunguza imani ya Wananchi kwa Serikali yao.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja hii. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara hii, kwa kutoa hoja hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, naanza kuchangia kuhusu Askari wa Wanyamapori. Askari hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu, kwa hiyo, ninashauri wawezeshwe kwa vifaa, waongezewe mishahara na pia wawekewe Bima wakati wanapopata madhara wakiwa kazini.

Mheshimiwa Spika, kifuta machozi kizidishwe kwa wanaopata matatizo au kuuawa na wanyamapori kizidishwe kwa sababu uhai haununuliwi, kwa hiyo, kutoa kifuta machozi kidogo siyo vizuri.

Mheshimiwa Spika, nazidi kukushukuru tena kwa kuniruhusu na naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, Serikali haijasema ni vipi itaendeleza utalii katika Ukanda wetu wa Bahari. Nashangaa Mheshimiwa Waziri ametaja mipango yote ya nchi katika mbuga na misitu, lakini hakuna maelezo yoyote katika bahari zetu. Je, Serikali haioni au haijui kama Tanzania kuna bahari na watalii wanapenda zaidi maeneo ya fukwe za bahari. Naiomba Serikali itoe tamko juu ya jambo hili na nisipopata maelezo ya kuridhisha sitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Nchi hii ina ukanda mkubwa wa fukwe za bahari kutoka Tanga, Pangani, Bagamoyo, Dar es Salaam, Mafia, Kilwa, Lindi, Mtwara na kadhalika, lakini mipango ya kuendeleza utalii katika maeneo haya haukuguswa kabisa; matokeo yake yamekuwa misitu, mapori na milima. Kwa namna hii, inaonesha Serikali inawasahau watu wa Kanda ya Bahari ya Hindi. Huu ni ubaguzi unaoonesha dhahiri Serikali haijali maendeleo ya wakazi wa maeneo hayo. Leo unapozungumzia utalii katika Tanzania usiongelee suala la bahari; kweli Serikali ina nia ya kuongeza mapato?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali inipe jibu la kuridhisha juu ya hoja hii au mpango wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2010 – 2015); hauwatambui watu wa Ukanda wa Bahari ya Hindi?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie Ukanda huu wa Bahari ya Hindi kuhusu utalii kwani kuna vyanzo vikubwa vya mapato.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuvitambua visiwa vidogo vilivyomo katika Bahari ya Hindi, kuwekeza kwa ajili ya utalii. Hii ni hidaya kubwa katupa Mungu, wenzetu katika nchi nyingine, huvitumia visiwa kama vile kwa kuingizia mapato ya nchi kwa asilimia 60 au zaidi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na usalama mdogo kuhusu watalii wanaoingia nchini mwetu; wamekuwa wanasumbuliwa na wezi na watu wanaojifanya mapapasi na wamekuwa na wakati mgumu hasa katika maeneo wanapowasili Dar es Salaam. Kwa hiyo, naishauri Serikali iweke utaratibu mzuri juu ya usalama wa watalii ili kuondoa kero zinazowakumba hivi sasa.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu kuchangia Wizara hii. Ninamshukuru *Allah* kwa kutufikisha siku ya leo katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mradi wa HADO ulizinduliwa mwaka 1973, lengo kuondokana na uharibifu wa mazingira. Mradi huu uliweza kuwapatia vijana ajira na kuendeleza jamii zao mbalimbali kwa upandaji miti na uoteshaji kwa kuajiriwa na kuchezea timu mbili hizi na HADO na Maliasili. Kwa sasa hali hiyo imetoweka na kupoteza dira ya matumaini.

Mheshimiwa Spika, Mradi umekutwa na changamoto ya kutokuwa na fedha za kuuendesha tokea mwaka 2004 haujaletewa fedha. Matokeo yake wafanyakazi wa Mradi wa HADO hawana kazi ya kufanya na wamekuwa wakipewa mishahara bure kwa kuwa Mradi hautengewi fedha za kuwawezesha kuuendeleza.

Mheshimiwa Spika, vilevile ofisi haipo kiutendaji kwani vifaa muhimu vya ofisi hakuna, hata usajili wanaotegemea kuendeleza shughuli zao haufanyi kazi zao kwa kukosa mafuta.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kutoelewana kati ya Askari wa Maliasili na Wananchi katika Jimbo la Kondoa. Wananchi wengi wa Wilaya ya Kondoa, wanategemea nishati ya kuni na mkaa kama njia kuu ya nishati kwa matumizi ya majumbani na biashara pia.

Mheshimiwa Spika, kwa kutofuata utaratibu, askari wamekuwa wakiwanyanyasa Wananchi; wanawapokonya mali zao na kuwapiga bila hata kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria kama kweli wametenda kosa husika. Hali hii inaleta manung'uniko na malalamiko kwa Wananchi kwa Serikali yao kwani kuwakataza Wananchi kuvuna mkaa au kuni bila ya kuwapa njia mbadala ni uonevu hasa kwa kuzingatia kuwa, gesi na umeme ni ghali kwa Wananchi wa Kondoa, pia maeneo mengi umeme hakuna kabisa.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa Askari wa Maliasili, Askari wa Wanyamapori nao wamekuwa wakiwakamata sana Wananchi wanaozunguka maeneo ya Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, hali hii imefikia badala ya askari kuthamini binadamu wenzake kwa utu, anathamini zaidi wanyama.

Mheshimiwa Spika, Sheria zipo wazi zinasema mtu fulani akitenda kosa aadhibiwe na Mahakama, lakini wafungua mashtaka ni wao wenyewe na watoa hukumu ni wao wenyewe. Huu siyo utaratibu kwani inaleta mateso kwa Wananchi, kitu ambacho kama wangetoa uadui, ulinzi shirikishi kwenye Mbuga za Kondoa ungekuwa mkubwa na kulinufaisha Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la Tembo kuvamia maeneo ya raia, lakini ni jambo la ajabu hali hiyo ikitokea askari wanakosa hata risasi. Suala la Maliasili Kondoa limo chini ya Halmashauri yenyewe na Hifadhi za Wanyama Songasonga, lakini kuna ufinyu wa bajeti kwa ujumla kuziwezesha ili zifanye kazi kama zinavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Kondoa umetengewa shilingi milioni tisa tu kwenye mazingira; fedha hizi ni kidogo sana kwa ukubwa wa majukumu ya mazingira mfano, kupanda miti, kuielimisha jamii na kutunza wanyama. Majukumu haya ni mengi, fedha zilizotengwa ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, elimu ya wanyamapori itasaidia kuondoa migogoro kati ya Wananchi na Askari Wanyamapori au Askari wa Maliasili. Elimu pia itasaidia kuzuia ukataji miti kwenye maeneo yaliyotengwa na Serikali kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kondoa imebahatika kuwa na vivutio vya utalii katika nchi yetu. Mji kama Mji hauwezi kujitengeneza kutokana na sababu nyingi ikiwemo uhaba wa fedha, lakini kama Serikali itasaidia kutangaza vivutio vya utalii Kondoa, itakuwa imeusaidia sana Mji ule kimaendeleo. Kondoa, ukiondoa Mbuga, imebahatika kuwa na michoro adimu, ambayo imepelekea kuingizwa kwenye sehemu ya urithi wa dunia.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie jinsi ya kuvitangaza hivi vivutio ili Wananchi wa Kondoa wafaidike na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Siungi mkono hoja hii.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, natoa pongezi kwako kwa kuendesha na kusimamia vizuri sana Vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa hongera sana kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige, kwa kazi nzuri na nzito anayoifanya. Pia natoa pongezi nyingi kwa Katibu Mkuu, Bibi Maimuna Tarishi na Naibu Katibu, Bibi Nuru Millao, Wakurugenzi na Wakuu wa Idara zote za Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kazi wanazozifanya. Misitu ni jambo muhimu katika maisha ya binadamu ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, misitu inayo faida sana; nishati, mvua tunayoipata, hewa, kivuli, uhifadhi wa ardhi, dawa, uhifadhi wa vyanzo vya maji, udongo mzuri kwa kilimo, utajiri wa familia

mpaka Taifa, matunda ya ndege, wanyama na binadamu, maji kwa matumizi ya ndege, binadamu na wanyama, vyote vinategemea misitu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara mara inapokuwa inatenga bajeti, jambo la kwanza liwe upandaji miti katika mikoa, miji na penginepo. Fedha hizo zinapotengwa zinakuwa kidogo sana na wakati mwingine hakuna kabisa.

Mheshimiwa Spika, ni kuwa utalii wa nchi yetu, Wizara imeangalia Mikoa ya Kaskazini na Zanzibar. Naishukuru Wizara kwa bajeti hii, nimeona angalau kutakuwepo Ofisi za Utalii katika Kanda ya Juu Kusini na Kanda ya Ziwa, kwani utalii unaweza ukakua zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Spika, ifahamike kuwa kila mkoa unao vivutio, ambavyo nashauri Wizara ifanye jitihada ya kuvitambua. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunaboresha utalii/vyanzo vya utalii nchini. Kwa kuvitambua vivutio hivyo vya kila mkoa na kuvitangaza, tutakuwa tumepanua na kuimarisha utalii wa nchi yetu. Namna hiyo tutakuwa tumekuza pato la nchi.

Mheshimiwa Spika, miti inachukua miaka mingi kukua hasa ya asili. Nashauri Wizara, licha ya kuwa Wilaya/Mkoa ndiyo kazi yao kusimamia misitu hii na upandaji miti, wawe wanakwenda mikoani mara kwa mara kutembelea misitu hiyo pamoja na hifadhi ya misitu.

Mheshimiwa Spika, ufugaji nyuki ni jambo ambalo linamweka na kumwezesha Mwananchi/Mkulima kupata kipato kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, nashauri elimu ya ufugaji nyuki isisitizwe na kutolewa kwa Wananchi.

Tunaajiri watu wa nje ya nchi yetu ya Tanzania kufanya kazi kwenye hoteli za kitalii. Ukweli ni kuwa, jambo hili siyo zuri kabisa. Ushauri ni kuwa, tupanue vyuo vyetu hivyo vichache vya utalii tulivyonavyo nchini.

Mheshimiwa Spika, elimu ya utalii itolewe kikamilifu chuoni kusudi vijana wetu wa Kitanzania wafanye kazi hizo katika hoteli kubwa na za kitalii hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa, kutoelewa wanyama waliosafirishwa nje ya nchi, bila mtu yeyote kufahamu, hili ni jukumu la wafanyakazi wa Wizara/Hifadhi, kutatua tatizo hili kwa kuhabarisha ni akina nani walihusika. Jambo hili ni baya, waliohusika na tendo hili inabidi wawajibishwe.

Mheshimiwa Spika, ni vyema wanyama wetu warudishwe nchini kwa namna yoyote ile. Napenda kuwaweka sawa Wananchi kuwa, utafiti wa *uranium* Wilayani Namtumbo, Mkoa wa Ruvuma, mpaka sasa hakuna Mwananchi aliyepata madhara, kwani kulikuwepo uvumi kuwa, Wananchi wamepata matatizo kuhusu maisha/miili yao. Nashauri Wizara ifanye kazi nzuri, kwa uadilifu, tutazidi kusonga mbele.

Mheshimwa Spika, napenda kusema kuwa, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii nyeti, kwa kazi nzuri anayoifanya. Ameonesha uzalendo katika kulinda rasilimali za nchi. Nashauri aendelee na msimamo wake huo hususan katika kupambana na Watendaji wezi na wabadhirifu na pia wanaowanyanyasa Wananchi kwenye mipaka ya Hifadhi na vijiji.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa kuwa, Wizara hii ni kubwa sana kiutendaji, pamoja na kwamba, Mheshimiwa Waziri anamudu vizuri majukumu yake, lakini majukumu ya Wizara hii ni mengi hususan katika kutembelea maeneo yaliyo chini ya Wizara hii, Hifadhi na Mbuga za Akiba na vijiji vinavyozunguka maeneo hayo. Wananchi wanahitaji kutembelewa mara kwa mara ili kutoa maelekezo na ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili Wananchi kama vile wanyama waharibifu, wanyama wakali, watendaji wabovu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iliangalie hili kwa kumpatia Mheshimiwa Waziri msaidizi wake, yaani Naibu Waziri. Mfano, tulimtumia sana Mheshimiwa Maige, alipokuwa Naibu Waziri wa Wizara hii na alitembelea sana maeneo yetu ya Mbuga za Hifadhi za Rungwa, Kizigo na Mhesi na alitoa ufumbuzi wa matatizo mengi. Sasa hivi siyo rahisi kumtumia Waziri kama tulivyofanya kwa sababu yuko pekee na matatizo ni lukuki.

Mheshimiwa Spika, kama haiwezekani kuwa na Naibu Waziri, basi alipwe mishahara miwili. Hivi ni kwa nini Wizara kama vile ya Kazi na Ajira, na ile ya Viwanda na Biashara ziwe na Manaibu Waziri wakati Viwanda vyetu vingi vimekufa?

Mheshimiwa Spika, wanyama waharibifu wa mali na mazao ni kero kubwa sana na ni kikwazo kwa maendeleo ya Wananchi. Naishauri Serikali iwalipe Wananchi thamani halisi ya uharibifu wa mali kama vile mifugo na mazao badala ya kulipwa kifuta jasho, kama Serikali inavyofanya wakati na kufidia malipo ya nyumba wakati wa kupitisha barabara mpya.

Mheshimiwa Spika, Kijiji kipya cha Lulanga kimetokana na Kijiji cha Itagata. Kwa bahati mbaya, Kijiji cha Lukanga kipo ukingoni mwa mpaka wa Mbuga ya Akiba ya Mhesi na kuna mgogoro wa kila mara na Watendaji wa Hifadhi. Kibaya zaidi, Kijiji cha Lulanga hakiwezi kufanya shughuli za maendeleo kama kilimo na ufugaji kwa sababu hakina ardhi ya kutosha. Pia kero ya wanyama wakali na waharibifu ni kubwa kwa sababu hifadhi ipo ukingoni kabisa mwa kijiji.

Mheshimiwa Spika, nashauri mpaka huu usogezwe nyuma kama ilivyofanyika kwa Kijiji cha Doroto, ambako Wananchi wa Doroto sasa wapo huru kufanya shughuli zao bila bughudha ya wanyama waharibifu. Naomba jibu kwa Kijiji cha Lulanga.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iweke utaratibu wa Wananchi kupatiwa kitoweo cha nyamapori kama ilivyokuwa zamani, ambapo Wizara ilikuwa na utaratibu wa kutoa fursa kwa Wananchi kununua nyama ya pori. Inaonekana kitoweo hiki cha nyamapori wanaofaidi zaidi ni wageni na viongozi; hii siyo vyema, wakati Wananchi wa maeneo husika hushiriki kwa namna moja ama nyingine katika ulinzi wa uhifadhi wa wanyamapori. Naomba ufafanuzi juu ya suala hili; ni kwa nini utaratibu ulisitishwa?

Mheshimiwa Spika, Utalii wa Tanzania bado haujatangazwa vizuri, kuna nchi kadhaa kama vile Israel, Wananchi wake wengine wana habari potofu kwamba, Mlima Kilimanjaro upo Afrika ya Kusini na wengine Kenya.

Mheshimiwa Spika, mapato yanayotolewa kwa Wananchi wanaozunguka Mbuga za Wanyama, yawekwe wazi kwa vijiji vinavyohusika ili yawekwe kwenye makisio ya vijiji husika kwa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii ihusishe utalii wa asili, vijiji na Wananchi wahusishwe kwa watalii; wafike waone utamaduni wa maeneo hayo, ngoma na kadhalika; siyo Wamasai tu.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa bajeti ya Wizara hii, ambayo ni sekta muhimu kwa maendeleo ya Taifa.

Napenda kujua kwa nini Wizara haina pesa za maendeleo zilizotengwa kama Wizara nyingine?

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumejaliwa vivutio vingi vya utalii na hata Wazungu wakasema *Tanzania The Land of Kilimanjaro, Serengeti and Zanzibar*. Tulitegemea vivutio hivi vitatangazwa katika kila sehemu muhimu kama Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere, bandarini na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, cha aibu na cha kusikitisha, katika sehemu kama hizo kuna mabango ya kibiashara ya makampuni ya simu na hoteli.

Mheshimiwa Spika, ninashauri mabango yote yaondolewe katika sehemu muhimu na yawekwe mabango ya vivutio vyetu vya utalii.

Mheshimiwa Spika, Wizara haijawafahamisha Watanzania nini maana ya vitalu, kwani sheria zake wala kanuni hawazifahamu na ndiyo maana matatizo ya wawindaji na mabwana pori katika mbuga za wanyama hayaishi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Tanzania bado hatujautangaza utalii wetu kwa kiasi kikubwa, kwani kwa wenzetu wamefanikiwa; unapopanda ndege tu basi unakuta vipeperushi vinavyotangaza utalii wao na vivutio vingine.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Tanzania na Wizara hii isiandae utaratibu mpya wa kutangaza vivutio vya utalii wetu kwa namna mbalimbali kwa kuweka vivutio ambavyo vitakuwa endelevu. Tuna milima, tuna mbuga za wanyama na fukwe za kuvutia kwa watalii na tukifanya hivyo basi utalii wetu utakua na Serikali itapata mapato makubwa sana kutokana na utalii wetu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna vivutio vingi lakini tegemeo letu hasa ambalo ni kivutio kikubwa ni wanyama; hivyo basi, Serikali iwahimize Wananchi jinsi ya kutunza wanyama wetu ambao ni rasilimali yetu, tuitumie kikamilifu ili kuingizia mapato Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, pamoja na Wizara hii kuwa si ya Muungano, lakini nataka Mheshimiwa Waziri anifahamishe kama Wizara Zanzibar mnaitangaza vipi katika Sekta hii kwani nayo ina vivutio vingi vya utalii. Mfano kuna Msitu wa Jozani; fukwe za kuvutia; kisima cha chini kwa chini; pango la Mkama Ndume; Kanisa la Mkunazini lililokuwa linatumika kuuzia Watumwa; Beitil Rais; Beitil Jaaibu; na Beitil Maali na vingi vingine.

Mheshimiwa Spika, ninataka kufahamu wale wanyama waliosafirishwa na Ndege ya Tanzania kwenda Arabuni watarejeshwa lini na nani waliohusika? Lazima wachukuliwe hatua za kisheria na pia wanyama hao warejeshwe haraka sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naomba kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake Wizarani, kwa bajeti nzuri iliyowasilishwa. Naomba nichangie hasa kwenye matatizo yaliyojitokeza, ambayo nadhani yanachangia sana katika kupunguza sana mapato toka Sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, watalii wanaokuja wanalipa kila kitu nchi za nje kwenye Wakala wao; hivyo, Tanzania hupata mapato kidogo sana. Kwa nini Serikali haitoi Sera ya Fedha kiwango cha chini ambacho mtalii lazima atumie akija nchini?

Mheshimiwa Spika, kwa nini biashara ya kitalii hasa vitalu na hoteli zilizoko mbuga za wanyama zisiwe na sura ya Kitaifa? Hali ilivyo sasa wenye biashara hii kwa asilimia siyo chini ya 80 ni watu wenye asili ya Kiasia; kwa nini isiwe ni sharti kwamba biashara hii isiwe na sura ya kizawa?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na taarifa ya *tarrif* zilizobadilishwa na naipongeza Wizara kwa hilo. Kwa nini *tarrif* hizo hazikutumika toka mwaka 2007 mpaka kuanza kutumika mwaka huu wa 2011? Nani aliyezikalia hadi hii mwaka huu? Je, fedha kiasi gani zimepotea kwa suala hilo?

Tunayo taarifa kuna makampuni yamekwenda Mahakamani; kwa nini makampuni hayo yasichukuliwe kama wahujumu uchumi na kufilisiwa? Serikali imekuwa laini sana na kudhaniwa ni mshiriki wa hujuma hizo.

Mheshimiwa Spika, hainiingii akilini kwamba, wanyama kama Twiga wanne na swala 66 wanachukuliwa bila hifadhi husika kujua na watumishi wa viwanja vya ndege kujua. Lazima kuna mtandao mzima wa uhalifu huu; Serikali imechukua hatua gani kuchunguza tukio hili kwanza kwa wale waliohusika na hatua gani imechukuliwa kwa wale waliokuja kuchukua wanyama hao? Inashangaza kuona muda mrefu umepita tokea suala hilo kutokea na Wananchi wanahoji ni vipi

Serikali mpaka leo iwe kimya kwenye suala hili na waliohusika wanaendelea kana kwamba hakuna kitu kilichotokea!

Mheshimiwa Spika, Mbuga za Kusini na hasa Selous, haina usimamizi mzuri na hivyo basi huvamiwa na majangili waliokuwa kwenye Mbuga za Kaskazini mwa nchi. Tembo ambao walikuwa wengi sana, wanatishia kutoweka kwa sababu wanauwawa kila siku na biashara ya magendo imeshamiri kutumia Pwani za Mkoa wa Lindi ikiwa ni pamoja na Pande, Lihimalyao, Kivinje, Somanga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, siyo pembe za tembo tu, lakini hata samaki; kumekuwa na biashara kubwa sana ya magendo kwa samaki kuuzwa baharini. Inaeleweka kuwa pwani hii ina samaki wengi, ambao sehemu nyingine nyingi za Pwani ya Afrika wametoweka. Haiwezekani kama haya yote yanafanyika kukiwa na mamlaka zote. Sina hakika kama Wizara yako ina ofisi kwenye mikoa hii muhimu, lakini pia haiwezekani kuwa hata Wizara ya Maliasili isilijue hilo.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika kwa Waziri na Wizara kuwa wakali na kutowaonea huruma wote ambao wanahujumu uchumi wa nchi. Wizara hii ikisimamiwa na watu ambao ni waadilifu, inaweza kusaidia sana kuongeza mapato ya Serikali na kuchangia katika maendeleo ya nchi. Namwomba Waziri atoe maelezo ya hatua atakazochukua ili kuhakikisha anasafisha Wizara hii na wafanyakazi wote ambao siyo waadilifu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nampongeza Waziri na naunga mkono hoja.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza sana Waziri, kwa kazi nzuri ya kuisimamia Wizara. Nawapongeza Wafanyakazi wote chini ya Katibu Mkuu, kwa pamoja na Asasi zote zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa kuchukua maamuzi mazito ya kubadili viwango vya malipo ya *concession fees.* Huo ni ujasiri wa aina yake; ni uzalendo wa kujali maslahi ya nchi na si ya mtu mmoja; hongera sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Sheria za Uwindaji. Zamani katika eneo la Mloka kulikuwa na wanyama wengi sana, leo hata Nyani hakuna; hii ni kutokana na ujangili. Wanaopewa leseni za uwindaji, wanapewa leseni ya kuuwa mnyama mmoja mmoja wanaua zaidi. Usimamizi hakuna, naomba usimamizi uimarishwe zaidi.

Mheshimiwa Spika, huu utaratibu wa kuwinda usiku, kitu ambacho sheria hairuhusu lakini wawindaji wanawinda usiku na hakuna mtu anayewazuia hasa kule Kidunda (Mlandizi), ambapo wawindaji wamekwishaanza kuingia *Selous.*

Mheshimiwa Spika, hapo awali katika Kambi ya *Rufiji Basin River* kulikuwa na wanyama wengi sana, lakini kwa utaratibu wa kutokuwa na usimamizi, tukiacha utaratibu kama ulivyo, kwa miaka 5 – 10 ijayo hapatakuwa na wanyama kabisa.

Mheshimiwa Spika, Sheria inasema katika suala la uwindaji inawataka wawindaji kuuwa wanyama majike badala ya madume. Mfano, ukikuta majike kumi na madume matano ukiyaua madume yote matano hao majike yatazalishwa na nani? Serikali itamke na kusimamia sheria zake.

Mheshimiwa Spika, nakuomba katika kusimamia yote hayo, pamoja na upungufu wa wafanyakazi kama ulivyokiri kwenye hotuba yako, lakini usimamizi wa yote hayo unahitaji wafanyakazi, motisha, vitendea kazi kama magari na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi kwenye vituo ufanyike kwa wale wote wanaopewa leseni kama leseni hiyo inasema ni wanyama wangapi waliouawa kwa kuwindwa.

Mheshimiwa Spika, naomba askari wa wanyamapori (*game attendant*), wawezeshwe, wapewe *insentive* ili kupunguza vishawishi kwa wawindaji. Hawa askari wa wanyamapori wakimotishwa wataisaidia sana Serikali kusimamia hifadhi zetu nchi nzima. Bila wao watalii wakati mwingine hutupa takataka, huacha uchafu katika makambi.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza wafanyakazi wote wanaosimamia Hifadhi zetu ambao ni tunu tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, wapewe motisha.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, katika eneo la Tambasi, Kata ya Sumbawanga, lipo eneo la Hifadhi ya Mazingira ambalo linamilikiwa na Halmashauri ya Sumbawanga Vijijini; mpaka sasa hakuna miti ambayo inahifadhiwa, bali limezungukwa na makazi ya Wananchi na lipo katika Manispaa ya Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, je, Waziri mwenye dhamana anaonaje kama sasa eneo hilo litakabidhiwa kwa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ndiyo wawe wamiliki kwa sababu lipo katika Manispaa yao na ili kuondoa mvutano uliopo sasa wa kuwa kila Halmashauri inasema ni eneo langu?

Ninaiomba Wizara ifanye maamuzi ya dhati kwani eneo hili linaashiria kuleta uhasama pande zote mbili; upande wa Sumbawanga Vijijini na Kata ya Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya hitimisho; naomba tamko rasmi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri la Hifadhi hii ibaki wapi leo.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali hii kuwaongezea uwezo Maliasili na Utalii ya Rukwa hasa kifedha, kwa sababu utendaji wa kazi kijiografia ni mgumu, ukizingatia Mkoa wa Rukwa watu ni maskini kupindukia.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ielekeze ufugaji wa nyuki Sumbawanga Vijijini na Wilaya ya Nkasi. Kitu cha muhimu Serikali izingatie kuwawezesha Watu wa Maliasili na Utalii Mkoani Rukwa, wawe na nguvu kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SEIF S. RASHID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii ya kuchangia. Napongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali katika kuendeleza uhifadhi wa maliasili na kukuza utalii nchini lakini kuna changamoto za msingi za kuonesha udhaifu mkubwa wa kutekeleza kazi hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhifadhi wa misitu iliyoko nje ya maeneo ya uhifadhi na ile iliyo ndani ya uhifadhi ni dhaifu sana, kutokana na ukweli kuwa miti imekuwa ikipungua kwa kukatwa kwa kasi na kwa bahati mbaya hata watumishi wa Wizara yenye dhamana pia baadhi yao wanahusika.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa jumuiya za uhifadhi wa wanyamapori katika Kata za Ngarambe, Utete, Ngorongo, Ndundunyikanza na Mwaseni, zinasuasua na inashangaza kuona kwamba Serikali inategemea ufadhili wa kutekeleza kazi hii muhimu na kusababisha muda mrefu kupita zaidi ya miaka mitatu bila ya kukamilisha kazi hii. Huu ni udhaifu usiokubalika hata kidogo. Naunga mkono hoja kwa matumaini ya kuona Serikali itakamilisha zoezi hili ndani ya mwaka huu bila ya visingizio.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mipaka. Tumeshuhudia kutanuka kwa mipaka ya uhifadhi wa Selous ambao umeingiliana na ukuaji wa vijiji vyetu na kusababisha kero nyingi na mwingiliano usio na tija, sana ni kuongeza madhara kwa wananchi wanaofariki au kudhurika katika maeneo yetu kuongezeka kwa mfano Kata ya Mwaseni, Kijiji cha Mloka ikifika jioni basi Tembo (Ndovu) wanaingia Kijijini wananchi wanaishi kwa shida. Mashamba yetu yanaliwa na wanyama hao na fidia ni shida. Cha msingi katika uendelezaji wa matumizi ya misitu na uhifadhi wa wanyamapori na kuendeleza utalii naitaka Serikali tena kwa makini sana ifanye yafuatayo:-

(a) Kukamilisha zoezi la uundwaji wa Jumuiya ya Uhifadhi – Rufiji Kata nilizozitaja.

(b) Kupitia mipaka na kuongeza eneo la wazi kwa ajili ya Warufiji kunufaika na maliasili yao.

(c) Ugawaji wa vitalu vya utalii utolewe kwa Warufiji ili wanufaike na utajiri wao.

(d) La msingi ni Serikali kuanza kutengeneza barabara ya kutokea Ikwiriri – Mkongo hadi Mloka kwanza kabla ya barabara ya kutokea Kisarawe hadi Vikumburu kwenda Mloka. Lisipozingatiwa hili naitahadharisha Serikali kwamba Warufiji hawataruhusu watalii kuingia Selous upande wa Mloka haitatengenezwa tena ya Mkongo hadi Mloka haitatatengenezwa tena kwa kiwango cha lami. Warufiji waliopoteza maisha na mali zao kutokana na wanyama kwa miaka mingi wakishuhudia Serikali ikipata mapato yanayotokana na utalii bila ya mrejesho wa tija kwao. Wakati umefika ukandamizaji huu unakwisha, hatupo tayari kuendelea kuona haya ya maeneo fulani kuwa bora zaidi kuliko wengine.

(e) Naitaka Serikali kuandaa utaratibu ili Warufiji wanufaike na mito, mabwawa yaliyopo ndani ya maeneo ya uhifadhi yaliyo karibu na vijiji na hasa vile ambavyo vilikuwa nje ya mipaka ya mwaka 1938 – 1958.

Mheshimiwa Spika, naitaka Serikali kuangalia juu ya wafanyakazi wao hasa wale ambao hawajalipwa mishahara yao na haki zao nyinginezo Wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nashukuru kupata nafasi hii, ni matumaini yangu kwamba, Serikali itatekeleza kazi kubwa ya uhifadhi. Naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA N. MAKILLAGI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mawazo yangu juu ya hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nianze kwa kumpongeza Waziri, Katibu Mkuu na wale wote walioshiriki kutayarisha Randama ya Bajeti hii muhimu kwa uchumi wa Taifa letu. Baada ya pongezi, naomba nitoe mawazo yangu katika vipengele vichache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pili, naipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuhakikisha sekta hii ya utalii inaimarika siku hadi siku na kuchangia pato la Taifa. Pamoja na pongezi naishauri Serikali kujieleza zaidi katika masuala yafuatayo:-

(a) Kuhamasisha Watanzania wapende kufanya utalii katika vivutio vyetu vya ndani.

(b) Serikali ijitahidi kudhibiti baadhi ya watendaji na wananchi wanaohujumu nyara za Serikali.

(c) Jitihada za kudhibiti ukataji miti hovyo ziendelezwe ikiwa ni pamoja na wizi wa magogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vitalu. Nashauri Serikali ifanye kila linalowezekana kuhakikisha wanawake pia wanapewa fursa ya kuendesha biashara ya uwindaji katika vitalu vyetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa nia na juhudi zake katika kusimamia sheria na taratibu katika sekta za maliasili na utalii. Anapaswa kuongeza juhudi kwa kuwa sekta hizi zimekumbwa na ufisadi na ukiukwaji wa sheria kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na rai kwamba sekta za maliasili na utalii zinaweza kuliingizia Taifa kipato kikubwa sana kama tukiwa makini zaidi na tukijipanga vizuri na tukiziba nyufa zote za ufisadi na ukwepaji tozo. Hakuna sababu kwa nini Tanzania, iliyo na misitu ya hifadhi na mbuga za wanyama kubwa kupindukia na maeneo mengi ya makumbusho, izidiwe sana kimapato na Kenya ambayo haikubarikiwa sana kwa maliasili wala maeneo ya makumbusho!

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu nitachangia katika maeneo yafuatayo:-

(i) Ukiukwaji wa taratibu katika ugawaji wa vitalu vya uwindaji.

(ii) Shughuli za maliasili Bukombe.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze na suala la ukiukwaji wa taratibu katika ugawaji wa vitalu vya uwindaji. Kuna taarifa za ukiukwaji wa taratibu katika ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii, ambazo zinasema kuwa maafisa wakuu wa Wizara wamewabeba Wazungu. Taarifa hizi zimesemwa mahali pengi, lakini ziliripotiwa rasmi katika magazeti, (mfano Mtanzania, toleo No. 5614 la tarehe 21 Juni, 2011).

Mheshimiwa Spika, Waziri, katika majumuisho yake, ajibu maswali yafuatayo kuhusiana na kadhia hii:-

(a) Ni kweli kuna makampuni ya kigeni yamepewa zaidi ya 15% ya vitalu, kitu ambacho ni kinyume na taratibu?

(b) Kuna tetesi kuwa vitalu vyote vinono wamepewa wageni. Hii ni kweli? Wageni wamepewa vingapi na wenyeji vingapi?

(c) Ni kweli ugawaji wa kitalu cha Maswa Mbono haukufuata taratibu?

(d) Kwa nini utangazaji wa mgawo wa vitalu ulicheleweshwa mwaka huu?

(e) Wizara itachukua hatua gani ili ugawaji vitalu wa baadaye uwe wa haki na wazi?

Mheshimiwa Spika, sasa nichangie kuhusu shughuli za maliasili Bukombe. Mada hii nitaizungumzia kwa kuigawa katika mada ndogo zifuatazo: Hifadhi na mazao ya misitu, mifugo katika hifadhi, utafiti wa madini katika hifadhi na ufugaji wa nyuki.

Mheshimiwa Spika, hifadhi na mazao ya misitu. Sehemu kubwa ya Wilaya ya Bukombe imepakana na Hifadhi ya Kigosi. Licha ya hifadhi hii kubwa, Bukombe ina hifadhi ya Halmashauri. Hifadhi hizi zinafaa sana kwa mazao ya miti, mazao ya nyuki na kadhalika na hifadhi ya Kigosi inafaa kwa uwindaji.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kwa Waziri. Kwa nini shughuli za maliasili za Bukombe bado zinasimamiwa na Kahama? Bukombe kuna Afisa wa Maliasili. Kwa nini shughuli hizi zisihamishiwe Bukombe? Wananchi wa Bukombe wamenituma kuishauri Serikali ihamishie shughuli hizo Ofisi ya Bukombe ili Halmashauri ya Bukombe ianze kunufaika na shughuli hizi badala ya kuendelea kuinufaisha Kahama.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine linahusu mbao zinazokamatwa na Halmashauri. Kwa nini mbao hizi zisitumike kutengenezea madawati ya shule zetu?

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nitaongelea Hifadhi ya Halmashauri ya Bukombe. Naongea kwa masikitiko makubwa kuhusu jambo hili. Hifadhi hii imeharibika kabisa, imevunwa miti kwa ajili ya mbao na mkaa na waliofanya uhalifu huu ni Maafisa wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Waziri atueleze, je, ni nani anawajibika kusimamia hifadhi za Halmashauri? Iwapo Maafisa wa Halmashauri wanaposhiriki katika uhalifu wa kuvuna miti ya hifadhi, nani atawawajibisha? Kwa nini Wizara isikague Hifadhi za Halmashauri mara kwa mara?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifugo katika hifadhi. Wafugaji wa ng'ombe hufugia mifugo yao katika hifadhi zote mbili. Hii ni kwa sababu mifugo imeongezeka na Serikali haijatenga maeneo kwa ajili ya mifugo. Pia inasemekana baadhi ya mifugo inatoka nchi jirani hasa katika Hifadhi ya Kigosi.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wengi kwa kuwa wanafahamu kuwa wanavunja sheria kuchungia katika hifadhi, wako tayari kuwahonga "Magemu" (Askari wa Maliasili).

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri ashirikiane na Waziri wa Ardhi ili waharakishe zoezi la kutenga maeneo ya malisho katika Wilaya ya Bukombe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufugaji wa nyuki. Shughuli hii ni muhimu sana kwa wananchi wengi wa Bukombe. Ikiwa Serikali itawasaidia wafugaji hawa, ni wazi wataondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaomba wasaidiwe mambo yafuatayo:-

(a) Vibali/Leseni za uvunaji mazao ya nyuki vitolewe katika Halmashauri ya Bukombe na siyo Kahama.

(b) Wasaidiwe utaalam wa kutengeneza mizinga ya kisasa na mashine za kusafishia na kufungashia asali.

(c) Leseni za uvunaji wa asali zitolewe mara moja kwa mwaka tu na zihusike na kipindi cha Juni – Disemba.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Kwanza kabisa nataka kutoa pongezi kubwa kwa Kitengo cha Makumbusho kwa jitihada zao za kuleta makusanyo mbalimbali kutoka Kenya, kuleta sanamu (mdimu) kutoka Ufaransa iliyoibiwa katika makumbusho ya Taifa, Dar es Salaam. Hongera sana. Sasa tunaiomba Serikali iongezee fedha Kitengo hiki cha Makumbusho ili waendelee kurudisha vitu vingine vilivyopo Ulaya. Kwa mfano, kuna mabaki ya wanyama ya mjusi (*Dainasoo*) ambaye ana uzito wa Kilo 80, urefu wa mita 22 na upana wa mita 11. Inasemekana alichukuliwa Lindi mwaka 1906. (*Fossils)* Mifupa ya mijusi hiyo ilipelekwa Ujerumani ya wanyama watano (5) na mingine ipo Uingereza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba mturudishie mjusi wetu nchini Tanzania kwani ni mali yetu, ni urithi wetu, ni utamaduni wetu, ni elimu kwa vizazi vyetu. Hii ni mojawapo ya kuongeza wigo wa utalii nchini. Mjusi yule aliyetoka Lindi huwaingizia Wajerumani Sh. Bilioni tatu na zaidi kwa kuingiza Watalii laki tano (500,000) kwa mwaka. Je, sisi Tanzania tunapatiwa nini? Naiomba Serikali leo ituambie sisi tunapata nini?

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la kukaimu kazi ya Ukurugenzi wa Bodi ya Makumbusho kwa muda mrefu. Tangu Mkurugenzi wa Makumbusho afe, Mr. Norbert Andrew Kayombo 30/11/2010 mpaka leo, hakuna mpya aliyewekwa, anakaimu tu Mr. Jackson Kihiyo. Kwa nini asiwekwe huyo huyo awe Mkurugenzi kwani ana sifa zote za kuwa Mkurugenzi. Ana *masters.* Wakati huu si wakati wa kukaimu nafasi kwani tunakwenda kwa wakati na tusingoje wakati utubadilishe.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie suala la kupanua wigo wa utalii nchini. Watalii sasa wanataka utalii wa utamaduni. Utalii wa utamaduni yaani *Culture Tourism*. Wamechoka sasa kuona wanyama na kuona Mlima Kilimanjaro. Inabidi sasa Wizara ibadilishe kisahani au mtindo wa aina ya utalii. Watalii sasa wanataka kuona utamaduni wa mtu, vitu, sehemu, mazingira.

Kwa mfano, utalii wa Zanzibar watu wanakwenda kule kuona watu wamevaa kanzu na kofia na kushika fimbo mkononi au akinamama kuvaa buibui. Kwa hiyo, tamaduni hizo zipo kila mahali ili mradi kuelekeza na kuendeleza tu, watu waende huko. Sisi Lindi kuna vivutio zaidi ya 20 vya (*Culture Toursim)* utalii wa kitamaduni kama ifuatavyo:-

(1) Kuna kumbukumbu za vita vya Majimaji katika Kijiji cha Kinjeketile huko Kipatimu, Kilwa; ukoo ule mzima upo pale Kipatimu Kilwa.

(2) Kuna mapango kadhaa Kilwa na pango kubwa kuliko mapango yote Tanzania, lipo Kilwa linaitwa Mang'omes. Lilikuwa linatumika wakati wa vita ya I na vita ya II ya dunia mwaka 1905 – 1907 na mwaka 1939 – 1945.

(3) Kuna Pori la Selous Liwale, Lindi, mbuga za wanyama kwa ajili ya uwindaji wa kitalii, *Selous Game Reserve.*

(4) Kuna eneo la Tendeguru Lindi Vijijini, eneo ambalo walitolewa mijusi watano (5) na zaidi *(Dainasoo*) wanyama waliishi miaka 200 iliyopita na kupelekwa katika *Museum* ya Ujerumani. Watalii wenyewe anakuja kufuata kuona kama kuna mifupa mingine ya mijusi hiyo, mabaki yapo mengine.

(5) Kuna fukwe za bahari (*White sand*) inayofaa kwa kujenga hoteli, kuogelea na kutoka Lindi hadi Dar es Salaam = Kilometa 449 zinafaa, na Kituo cha Mitema Beach ni eneo la *Divers of the World,* huja kila mwaka kuogelea, wanapozunguka duniani.

(6) Kuna magofu ya Waarabu Kilwa, Kilwa *Ruins*, Kilwa na Songo Mnara ni urithi wa Dunia sasa.

(7) Kuna Mji Mkongwe Kilwa ambao ulikuwa na utaratibu wao wa maisha ya juu, ni hati ya Miji mikubwa Mikongwe ya Afrika Mashariki tangu *Anno Domino* 900 – 1,700, Kilwa ni mmojawapo.

(8) Kuna uwanja wa ndege una *run ways* sita. Uwanja ambao ulitumika wakati wa Vita ya Pili 1939 – 1945 na vile vile uwanja huo ulikuwa unatumika katika ukombozi wa Afrika, vita vya Afrika ya Kusini, Msumbiji, Zimbabwe na Seychelles.

(9) Kuna mashamba ya kutengenezea chumvi asili (*White salt*).

(10) Kuna Bahari Kuu itokayo Msumbiji kupitia Lindi kwenda Dar es Salaam yenye *Beach* nzuri na samaki kwa wingi, wakubwa wakubwa inafaa kuwa na Kiwanda cha Minofu ya Samaki.

(11) Kuna Boko 500 wanaotii binadamu katika Mto Nyange, Kilwa. Ni historia.

(12) Kuna Makonde *Culture, Carvings* and Makonde *Plateu*.

(13) Kuna asali na miti ya mbao mpingo, mvinje, mbambakofi, mninga, msufi, mvule na kadhalika.

(14) Kuna Mjusi (*Dainasoo*) yupo Ujerumani anakuja, wa Lindi. Ana uzito wa Kilo 80, urefu mita 22 na upana mita 11. Alichukuliwa mwaka 1906, mijusi mitatu na kuwekwa *Museum* ya Ujerumani na kuwa kivutio kikubwa Ujerumani, ambako watalii 500,000 (laki tano) huja pale kuona kila mwaka na kuingiza Sh. Bilioni tatu, mia mbili na thelathini na nne milioni. Ni nchi tatu tu wanyama hao walionekana mifupa yao duniani, Tanzania, Lindi; Marekani (*Califonia*), na Afrika ya Kusini. Turudishiwe Lindi.

(15) Kuna boma la Liwale la Ujerumani lililokuwa linatumiwa na Wajerumani katika kuta za boma hilo kwa ndani kuna picha za watu ambao wanasadikiwa kuwa, watu hao waligandishwa wakiwa wazima ukutani na kugandishiwa na *cement.*

(16) Kuna Kisiwa cha Popo Kilwa.

(17) Kuna Kilimo cha Korosho, ufuta, mbaazi, mtama, mpunga, mahindi na mhogo.

(18) Kuna mabonde yapatayo 15 yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, mboga mboga.

(19) Kuna Gesi ya Songosongo Kilwa, Lindi na *Gypsum*.

Mheshimiwa Spika, siwezi kusema yote, kwani ni mengi zaidi ya vivutio 20. Tunamwomba Waziri aje Mkoa wa Lindi angalie vivutio hivyo, kisha aweze kuandaa utalii Lindi. Kwa nini Lindi tuwe kila kitu wa mwisho, wakati nyenzo zote za uchumi tunazo. Tusaidieni, sisi maskini, mikoa ya pembezoni, lakini kuna kila fursa ya kuwa matajiri. Jamani mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Lindi tupeni utalii.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, P/S Lindi Vijijini, tatizo la ardhi. Kuna eneo kubwa ambalo lilikuwa linatumiwa na Wakoloni zamani kwa ajili ya kupanda mkonge. Eneo hilo limeombwa na wananchi kwani sasa halitumiki. Tunaiomba Serikali ifute hati ile miliki ili wananchi wapewe. Eneo la Navanga na jirani zake huko Lindi Vijijini njia ya kwenda mpakani Mtwara. Tumeshaiomba Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Ezekiel Maige kwa kazi nzuri anayoifanya. Hotuba yake ni makini na inaonesha alivyojipanga tayari kwenda kwa kasi zaidi kutekeleza ilani ya CCM na malengo yake.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini nimwulize Mheshimiwa Waziri atueleze ni utaratibu gani ameweka kuboresha usalama katika pori la Rwiga, Biharamulo na Burigi. Pori hilo la hifadhi limekuwa kero kwa wananchi maana badala ya kuhifadhi mazingira na wanyama, pori hilo ni hifadhi ya majambazi na watu wengi wanatekwa na kunyang'anywa mali zao wanapovuka kutoka Muleba kuenda Biharamulo. Wafugaji kutoka nchi jirani wanachunga katika pori hilo bila kubugudhiwa lakini cha ajabu wananchi raia wanasumbuliwa wanapojaribu kuiga wageni. Je, Mheshimiwa Waziri ana habari ya ubaguzi huo? Naomba aunde timu ya kuchunguza kinachojiri katika hifadhi hiyo ambayo sasa wananchi wa Kata za Kasharunga, Nyakabango, Kimwani, Kyebitembe na Burigi wanaiona kama kero na chanzo cha kuwanyanyasa na kuwabambikiza kesi zisizo na msingi wanaporipoti wageni walio katika hifadhi hiyo.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia afya njema inayoniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya Kibunge.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kuwapongeza Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kutekeleza mpango kazi wa mwaka 2010/2011 iliyopelekea uandaaji wa hotuba hiyo ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajielekeza katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, migogoro ya mipaka/misitu na hifadhi za Taifa. Mkoa wa Pwani umezungukwa na mbuga ya wanyama Selous, katika maeneo ya Wilaya ya Kisarawe, Rufiji na Hifadhi ya Saadani iliyopo Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo hayo tumeshuhudia migogoro ya mipaka kati ya vijiji vinavyozunguka mbuga/hifadhi hizo hasa maeneo ya Kata za Mwajeni Wilaya ya Rufiji na Vikuburu, Wilaya ya Kisarawe. Migogoro hiyo inatokana na uamuzi wa Wizara/Hifadhi kuongeza mipaka ya hifadhi hizo. Badala ile mipaka iliyokuwepo awali na uongezwaji wa mipaka hiyo haikushirikisha wananchi wa vijiji vinavyozunguka hifadhi hizo. Tatizo hili la migogoro ya mipaka limesababisha kuwepo kwa tuhuma za watu kuuawa/kulima na askari wa wanyamapori pindi wanapoingia kwenye maeneo ya hifadhi hizo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kujipatia riziki.

Mheshimiwa Spika, kutokana na migogoro hiyo, Askari wa Wanyamapori Wilaya ya Kisarawe wameua watu wawili, ilichukua muda mrefu sana ili kufunguliwa mashtaka na mtu

mmoja amejeruhiwa vibaya na hata Wizara haikuweza kuhudumia. Je, Wizara imejipangaje katika mkakati wa kumaliza migogoro hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi?

Pili, Shirika la Hifadhi la Taifa (*TANAPA*). Kwa mujibu wa kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri Ukurasa wa 17 inaonesha hadi Mei, 2011 Shirika lilikusanya kiasi cha bilioni 99.014.

Mheshimiwa Spika, Shirika lina wajibu wa kuchangia maendeleo ya wananchi wanaozunguka hifadhi kupitia mpango wa ujirani mwema. Hata hivyo, kwenye hotuba hiyo aya ya 37, kiwango cha pesa kinachotumika kwenye miradi hiyo hakikutajwa wala hakuna kiambatanisho cha kuonyesha ni aina gani ya miradi na wapi ilipotekelezwa na kwa kiasi gani ili wawakilishi wa wananchi (Wabunge) wa maeneo hayo tujiridhishe kwani kuna malalamiko kuwa, mapato mengi yanayokusanywa na *TANAPA* yanatumika kwenye matumizi ya kawaida hasa posho za vikao na safari za nje zisizokuwa na tija yoyote.

Mheshimiwa Spika, naomba orodha ya miradi ya maendeleo iliyochangiwa iandaliwe kwa mfano, Kata ya Mkange, Kijiji cha Gongo, Matipwili ambavyo vimepakana na hifadhi ya Saadani, Wilaya ya Bagamoyo ina changamoto nyingi ikiwemo kukosa kituo cha Afya, Mabweni katika Sekondari ya Matipwili, changamoto hizi ni za muda mrefu lakini *TANAPA* haijaonesha jitihada za makusudi za kusaidia maeneo hayo katika kutatua changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, tatu, *TANAPA* na Ngorongoro kulipa gawio kwa Hazina. Naunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuyataka Mashirika hayo kulipa Serikali gawio la asilimia 10% kutoka katika mapato yake. Naunga mkono uamuzi huu kwa vile ni ukweli usiopingika kuwa mashirika haya yanakusanya pesa nyingi, pamoja na kazi ya uhifadhi lakini matumizi ya kawaida safari, posho, *Gratuity* na kadhalika, Pia kiasi kikubwa sana kutokana na Serikali kutokuwa na vyanzo vya kutosha vya mapato ni vema mashirika haya yakachangia ili kuondoa utegemezi na bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nne, uvunaji holela wa misitu na uvamizi wa maeneo ya misitu. Katika Mkoa wetu wa Pwani kuna tatizo kubwa la uvunaji holela wa misitu na pia uvamizi wa wananchi kwenye maeneo ya misitu. Tatizo hilo kwa kiasi kikubwa linachangia uharibifu wa maeneo ya misitu na uvunaji holela wa misitu hiyo ambayo inachangia sana mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Spika, Misitu ya Ruvu Kusini, Ruvu Kaskazini, Kazimzumbwi, Pugu, Masanganya na Mtita katika Mkoa wa Pwani, tumeshuhudia misitu wanafanya biashara ya mbao, naiomba Wizara isimamie sana maadili ya Maafisa Misitu na kuwachukulia hatua kali.

Mheshimiwa Spika, tano, malipo ya Tozo (*Concession fee*). Nimesikitishwa sana na kitendo cha Kampuni zinazofanya biashara ya utalii cha kugomea viwango vipya vilivyopendekezwa na *TANAPA*. Malipo ya dola kumi kwa kila mtalii anayelala katika hoteli tangu 1990 mpaka sasa haizingatii hali halisi.

Mheshimiwa Spika, upotevu wa bilioni 19 kwa mwaka wa fedha 2008/2009 kwa mujibu wa taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani hauvumiliki hata kidogo. Naiomba Wizara, isimamie viwango vipya vya malipo ya *concession fees* bila ya kutetereka na iwachukulie hatua kali za kisheria wamiliki wa hoteli hizo za kitalii.

Mheshimiwa Spika, sita, nimalizie kwa kuiomba Wizara isimamie vizuri rasilimali fedha na kuhakikisha zinatumika kama ilivyokusudiwa. Ripoti ya *CAG* ya mwaka 2009/2010 inaonyesha upungufu mkubwa katika usimamizi wa rasilimali fedha. Hoja nyingi katika ripoti hiyo inaonesha kuna matumizi mabaya ya pesa za Wizara na uzembe uliokithiri unaochangia upotevu wa mapato kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri, atuletee taarifa hatua gani zimechukuliwa kutokana na yaliyoanishwa katika ripoti ya *CAG* ya mwaka 2009/2010?

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. CELINA O. KOMBANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza sana Wizara kwa kazi nzuri. Mimi ni mdau katika Mbuga ya Selous. Tatizo kubwa wale wananchi wa Ulanga hawafaidiki na mbuga hii. Wanalinda maliasili za mbuga hii, ikiwemo misitu na wanyama, lakini cha kushangaza ni kwamba hafaidiki hata kupata kitoweo ingawa kanuni zinawaruhusu. Halmashauri hawapati 25% ya mapato ya uwindaji kwa wakati wa miaka mingine hawapati kabisa. Naomba Mheshimiwa Waziri suala la 25% lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni baadhi ya wawindaji kutosaidia masuala ya maendeleo katika vijiji husika, wawindaji hao ni jeuri hatujui jeuri hii inatoka wapi, ni vyema na busara wakachangia kwenye masuala ya maendeleo kama anavyofanya Mama Bomani nampongeza.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, Wizara ilituahidi gari mwaka 2008 kwa ajili ya kuzuia ujangiri. Lakini baada ya ufuatiliaji wa karibu mimi mwenyewe, Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi kwa muda wa mwaka mzima tukaambiwa aliyekuwa Katibu Mkuu Ndugu Blandina Nyoni alilipeleka katika Wilaya nyingine. Ni vyema mkaangalia kumbukumbu zenu na kutupatia gari kwa ajili ya kumwezesha Afisa Wanyamapori ili aweze kufuatilia kwa karibu majangiri wanaoiba nyara za Serikali kule Ulanga.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2011/2012 hayakidhi mchango na sekta husika kwa uchumi wa nchi na maisha ya wananchi miaka 50 ya uhuru. Maliasili ni urithi wa Taifa na utalii ni fursa ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia kujikwamua katika umaskini. Hivyo, Serikali iipe uzito wa kibajeti na kiusimamizi wa ufanisi kama Wizara ya kimkakati kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naungana na wengine kutaka Serikali ihakikishe viwango vya *concession fees* vinapanda kwa kuanza kutekeleza kiwango cha dola 40. Pia, hatua zichukuliwe kwa wote waliolitia hasara Taifa.

Aidha tukio la wizi wa wanyamapori hai 130 la Novemba, 2010 ni dalili ya mianya katika mifumo yetu ya muda mrefu, hivyo pamoja na kuchukua hatua kuhusu kashfa hiyo vyombo vya ulinzi na usalama vifanye uchunguzi mpana katika maeneo mbalimbali ya nchi yenye biashara ya wanyamapori ili kulinda maliasili za nchi na kuongeza mapato ya Serikali, taarifa ya uchunguzi husika iwasilishwe Bungeni. Pia Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009 ifanyiwe mapitio kupunguza mamlaka ya Waziri na pia kanuni za ugawaji wa vitalu ziwekwe hadharani.

Mheshimiwa Spika, hatua hii iambatane na kushughulikia kasoro zote zilizojitokeza katika ugawaji mpaka sasa Serikali ieleze mkakati wa kukabiliana na upotovu wa mapato kwenye utalii unaotokana na ujazo yazingatie bei halali ya Sh. 29,000/= badala ya 10,000/=, lakini pia mapato yetu kwenye misitu yazingatie bei ya sasa ya soko la dunia. Kwa ujumla, mapato yaliyotajwa na Serikali kwenye kitabu cha kwanza kutokana na maliasili na utalii hayaendani na fursa zilizopo hivyo, Serikali iwasilishe makadirio ya nyongeza ya mapato na fedha zote zitakazopatikana zielekezwe kwenye kitabu cha nne cha miradi ya maendeleo ambayo miradi yote kwenye Fungu 69 vifungu 1001 mpaka 4002 havijatengewa fedha zozote.

Mheshimiwa Spika, Wizara ieleze hatua za haraka ambazo itachukua kufufua Kiwanda cha Tembo *Chipboards Limited* ambacho Wizara ya Maliasili na Utalii ina taarifa kuwa kimefungwa toka 30 Juni, 2008 wakati malighafi ya misitu inapatikana kwa wingi *Shume Plantations*. Katika kuchukua hatua, Wizara ishirikiane na Mamlaka nyingine kuhakikisha mafao ya wafanyakazi ambao mpaka sasa wamekuwa katika Kijiji cha Mkumbwa yanalindwa malipo hayo ni salio la mafao takriban milioni 52, nauli za mizigo na familia, michango ya *PPF*. Vielelezo vyote vipo Wizarani na vimeletwa kwa nyakati mbalimbali 2008, 2009, 2010 na 2011.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam lina fursa ya kuongeza mchango kwenye pato la Taifa kutokana na maliasili na utalii. Pamoja na fursa ya bahari na mahoteli ya kitalii, Jiji la Dar es Salaam lina nafasi pia ya kuchangia pato la Taifa kutokana na utalii wa kihistoria na pia idadi kubwa ya watu wenye kuweza kuchangia utalii wa ndani na urahisi wa mawasiliano kwa watalii wa nje. Dar es Salaam pia ni soko la maliasili na mazao yake ikiwemo misitu na wanyama. Hivyo,

Wizara ishirikiane na Halmashauri kuwa na mpango wa mkakati maalum. Katika kufanya hivyo, Wizara irejee barua yangu ya mwezi Mei, 2011 ya kutaka pori la Hifadhi ya Msitu wa Pande katika Jimbo la Ubungo liendelezwe kuwa Kituo Maalum cha Utalii wa Mjini (*Gadrens and Animal Park*). Program hiyo maalum iandaliwe na Wizara kwa ushirikiano na taasisi zake hususan Chuo cha Taifa cha Utalii, *TAWIRI, TANAPA, TAFORI, TTSA, TTB, NCT, NMT* na *TFS*. Hivyo, pamoja na kuhitaji nyongeza ya ruzuku kwenye taasisi zisizokuwa na mapato ya kutosha lazima kuongeza pia ufanisi kwenye matumizi ya kifungu 2001 (Kasma 27030, 27100, 410200) kifungu 2001 (Kasma 270300 na 270600), kifungu 4001 (Kasma 270300, 270500, 290700) na kifungu 4002 (Kasma 270800).

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, naomba nipongeze Wizara kwa hotuba nzuri na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu watumishi. Wizara ipewe Naibu Waziri, watumishi Wilayani hawatoshi hasa Kasulu.

Pili, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, wanaomba Idara ya Maliasili, wapewe bunduki imara lakini wana tatizo kubwa la risasi.

Tatu, ni kuhusu Watalii. Utangazaji na uhamasishaji wa utalii inabidi ubuni mbinu mpya zaidi:-

(i) Kutoa tamasha kwa wafanyabiashara na kuwapa motisha maalum kwa shirika linaloleta watalii wengi.

(ii) Bajeti ya utangazaji iongezwe.

Nne, ni kuhusu misitu. Ombi langu kwako ni kuomba uhamasishaji na upandaji miti katika Jimbo la Manyovu, kwani misitu imeharibiwa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba uamuru maliasili Kasuli ili miti iweze kupandwa kwa kiasi kikubwa na tunatoa wito kupata mbegu za miti ambazo ni rafiki kwenye vyanzo vya maji

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nimechoka, wananchi wamechoka na wanapoteza imani juu ya Serikali ambayo inachelewa kutekeleza na kutoa maamuzi juu ya yale ambayo yanatakiwa kuamuliwa, kero ya Ubende *WMA* ambayo wananchi hawakushirikishwa lipo tatizo la mipaka na hususan nisemee Kata ya Kakese katika Jimbo langu ni lini Serikali itamaliza tatizo hili. Naomba jambo hili lipatiwe ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, kwa nini mnasita kumaliza jambo hili au ni kwa sababu ya majina ya watu wanaojiita viongozi wa Ubende *WMA* ndio mnawaogopa na kupuuza maslahi na matakwa ya wananchi. Wizara ijisahihishe na kutoa maamuzi.

**MHE. SAIDI R. BWANAMDOGO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba nishauri katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Mabucha ya nyamapori. Kwa kuwa wananchi huwathamini wanyama kwa kuwalinda, ni vizuri Serikali ikaweka utaratibu wa kuwa na mabucha yatakayotoa nyama ya pori angalau mara moja kwa miezi sita, hususan katika maeneo yaliyo karibu na hifadhi za wanyama.

Pili, kumaliza migogoro ya mipaka baina ya vijiji na maeneo ya hifadhi. Kuna maeneo mengi nchini ambayo kuna migogoro ya aina hiyo. Mfano, katika Hifadhi ya Saadani kuna mgogoro mkubwa sana baina ya Kijiji cha Saadani na Hifadhi hiyo. Ni vema Wizara ikaingilia kati ili kuona haja ya kuondoa utata huo.

Tatu, usafirishaji wanyamapori nje ya nchi. Ni wakati muafaka sasa kuachana na utaratibu huu ambao unaleta aibu na kudhoofisha uchumi wetu.

Nne, tatizo la wachukua chumvi katika Kiwanda cha Chumvi *Sea Salt* huko Saadani *National Park*. Kuna mgogoro wa watu wanaochukua chumvi eneo hili na kudaiwa kutoa Sh.100,000/= kama ushuru. *TANAPA* Saadani na *Seasalt* Saadani wote ni wadau katika eneo moja, iweje leo *Seasalt* walipe fedha kwa *TANAPA*?

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii imetelekeza Wilaya ya Chunya ambayo inachukua asilimia 46% ya Mkoa mzima wa Mbeya, kwa kuwa na pori kubwa lenye wanyamapori wengi wanaouliwa hovyo na wenyeji wenye bunduki za Gobole.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya ina rasilimali asilia kama vile Ziwa Rukwa, misitu yenye miti ya mninga, mturunga kwa ajili ya mbao, miti ya kuzalisha kuni na kadhalika. Lakini hakuna usimamizi mzuri kwani Idara ya Maliasili, Wilaya haina gari kwa maafisa hao ili watembelee Jimbo langu la Songwe.

Mheshimiwa Spika, Ziwa Rukwa ni miongoni mwa Maziwa matatu yanayoongoza kuwa na mamba majini. Je, Serikali ina mpango gani wa kuvua mamba Ziwa Rukwa wakati wananchi wanaoishi kando kando ya Ziwa wanauliwa na mamba hawa? Takwimu zinaonesha, wananchi zaidi ya 30 kwa kila mwaka wamekufa kwa kifo cha mamba.

Mheshimiwa Spika, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri ufanye ziara Wilaya ya Chunya na uone pori la maliasili lilivyo na upeleke gari kwa watendaji wa Wilaya hii.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya, Jimbo langu la Songwe kuna mlima wa utalii uitwao Kwimba, Mlima huu ni wa maajabu sana ambapo kama Wizara ingefika na kuona maajabu yaliyoko pale tutapata utalii utakaotuingizia fedha za kigeni na Taifa tukafaidika. Njooni muutazame Mlima Kwimba, Chunya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Ezekiel M, Maige, Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba yake nzuri na yenye uchambuzi wa kina ambayo ilitolewa jana asubuhi. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa wananchi wa Wilaya yangu ya Siha wamekuwa wakivamiwa na tembo jambo ambalo limesababisha uharibifu mkubwa kwa mazao yao na hivyo kuwaletea hasara kubwa na njaa.

Mheshimiwa Spika, nimewasiliana na Mheshimiwa Waziri pamoja na Katibu Mkuu kuhusu kifuta machozi kwa wananchi walioathirika bila mafanikio. Ninayo maelezo toka kwa Mheshimiwa Waziri kuwa Wizara imeyapitia malalamiko hayo na vifuta machozi hivyo na kwamba ni wale tu wenye ekari moja na zaidi ndio wanaostahili kifuta machozi.

Mheshimiwa Spika, nimetoa maoni yangu kwa Waziri, kwamba kama kigezo hicho kitatumika kwa Mkoa wa Kilimanjaro hakuna atakayepata kifuta machozi. Hakuna mtu mwenye ekari moja katika Mkoa wa Kilimanjaro kule kuna kihamba (kihamba *system*) kama ile "Nyarubanja *system*" ya Kagera.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ambao nilimpatia Mheshimiwa Waziri ni kwamba, tujumlishe ekari zote zilizoathirika na msingi huo ndio utumike kama kifuta machozi. Wakati wa kugawana hicho kifuta machozi ndipo tuangalie *size* ya eneo la mtu na kumpatia mhusika kama mtu ana nusu, robo au robo tatu ya eka basi mtu apewe kwa msingi huo.

Mheshimiwa Spika, bado nasubiri kauli ya Serikali kuhusu suala hili. Kwa upande wetu tunaahidi tutaendelea kuwalinda wanyama wetu kwani ni rasilimali kubwa kwa Taifa letu, kitu ambacho kinakuza utalii na hivyo kutuingizia mapato ya hali ya juu nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho tunaomba Serikali itupelekee maafisa wanyamapori ambao watatusaidia kukabiliana na wimbi la wanyamapori hasa wakati huu ambao eneo la Kaskazini la nchi yetu na nchi jirani ukame wa kutisha. Tunahitaji *manpower* risasi magari na kadhalika kwa ajili ya zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi iliyojaliwa maliasili na rasilimali nyingi sana na ina nafasi nzuri sana kijiografia lakini cha kusikitisha bado Tanzania ni nchi maskini sana. Hii inatokana na kuwa na viongozi wasio waadilifu.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kuona kwamba pamoja na rasilimali zetu na sheria zinazotawala lakini wanyamapori wanauzwa! Aibu. Naipongeza sana Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa taarifa yao kuhusu mazingira ya rushwa na ufisadi yaliyofanywa katika Uwanja wa Ndege wa *KIA*. Haiingii kichwani eti wanyama 116 wavunwe, wasafirishwe kwa magari na kuingia *Airport* bila Mamlaka husika kujua!

Mheshimiwa Spika, ni wazi katika vivutio vya nchi hakuna kinachoingiza fedha nyingi kama Mlima Kilimanjaro na Ngorongoro *Crater*. Lakini pamoja na fedha nyingi zinazopatikana bado miundombinu hususan katika hifadhi ya Mlima vikiwemo vyoo hakuna. Hali inayowafanya watalii wajisaidie vichakani ustaarabu ambao hawajauzoea kabisa. Pia hali hii itapunguza idadi ya watalii.

Mheshimiwa Spika, suala la misitu nalo ni muhimu sana kwani makaa yanatokana na miti. Kwa mfano, kwa nchi nzima tunakata hekta 162,000 za miti kwa mwaka huku tukipanda hekta 130,000 tu, lakini kwa Dar es Salaam peke yake tunatumia magunia 30,000 kwa siku, kwa mwaka ni magunia 10,950,000 sawa na mita za ujazo 365,000 ambazo ni sawa na hekta 10,400 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatari sana na wataalam wanasema ifikapo mwaka 2017 misitu yetu itakwisha. Wote tunatambua umuhimu wa misitu kwamba ni chanzo cha mvua na wote tunaona mabadiliko ya tabia nchi na ukame uliokithiri. Naomba Serikali ihakikishe wanasimamia ukataji miti na kupanda miti mingi zaidi ili nchi yetu isiwe jangwa.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Maige kwa kazi nzuri anayoifanya ya kusimamia utekelezaji wa sera, mipango na Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2010 katika sekta hii muhimu kwa uchumi na maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kuwa Wizara iandae *strategic plan* itakayoonesha ni vipi sekta ya utalii itakuzwa na kuendelezwa. Kwa sisi wananchi wa Wilaya ya Tanga Mjini tungependa kujua ni mikakati gani Wizara inayo ya kuboresha mapango ya Amboni, ili kuvutia watalii wa nje na ndani?

Mheshimiwa Spika, naishauri pia Wizara ishirikiane na Jiji la Tanga na Halmashauri za Wilaya ya Mkinga na Pangani katika kujenga, kuendeleza na kuhamasisha utalii katika ukanda wa pwani ya Bahari ya Hindi kuanzia mpakani Horohoro hadi Pangani na Bagamoyo. Hivi ni kwa nini watalii waishie Mombasa tu na siyo kuingia katika upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mikakati mahususi inahitajika. Ni vizuri Wizara ikaliangalia suala hili ili kukuza uchumi si tu wa wakazi wa Mkoa wa Tanga ila Tanzania kwa ujumla?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

kwanza, ni kuhusu Askari wa Wanyamapori, limekuwepo tatizo la Maaskari Wanyamapori, waongezwe. Tunalo tatizo la wanyama waharibu kupatiwa ufumbuzi, wananchi wanahimizwa kulima, lakini mazao yao yanaliwa na wanyama waharibifu. Askari wamo kuhudumia Wilaya

nzima, katika Wilaya ya Missenyi kuna Askari Wanyamapori mmoja, ana bunduki lakini hana risasi, hivi kweli kuna uwezekano wa uadilifu? Kwa kuwa Wilaya ya Missenyi inasumbuliwa sana na wanyama waharibu, tunaomba kuongezewa Maafisa Wanyamapori na kupewa risasi za kutosha kwa kuwa katika hotuba ya Waziri ni kwamba mtaajiri watumishi lakini tunaomba hata kuleta wafanyakazi (Afisa Wanyamapori) toka maeneo yenye ziada.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Mbegu za Miti, Wilaya ya Missenyi ni Wilaya inayopata mvua mwaka mzima na yenye udongo wa rutuba, tunaomba uwepo mkazo wa kupanda miti na hata kuwepo sehemu za kupata mbegu na pia tuwe na mikakati ya kampeini ya kupanda miti na hata kutumia viongozi wa Serikali za vijiji kuwekewa malengo kuwa kila kijiji kiwe na msitu ili tuweze kuvuna mazao ya miti. Wilaya ya Missenyi ni eneo zuri sana la kuangalia na likitumiwa vizuri litaleta tumaini hata kusaidia kwenye badiliko la hali ya hewa. Kiwango cha miti iliyopandwa mwaka 2011 hakitoshi jitihada ziongezwe.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kupitia maandishi nachangia sekta ambayo kwa imani yangu ikisimamiwa vizuri kwa zaidi ya asilimia arobaini, sekta hii ni muhimu lakini sekta hii haitunzwi kadri inavyopashwa kutunza na kuvunwa kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, eneo langu la kwanza ni hifadhi na misitu ya Serikali zipo hifadhi na misitu mingi Mkoani Kagera. Wote tunatambua kuwa huu ni urithi wa Taifa letu lakini matumizi yake yanatia masikitiko. Hifadhi zetu zimekuwa ni sehemu za wahamiaji haramu kuchunga ng'ombe wao maelfu kwa maelfu. Wananchi waliokuwa watiifu wa sheria za nchi baada ya kuona hivyo nao wakaanza kuchunga mifugo yao katika hifadhi.

Mheshimiwa Spika, mbali na kuharibu uoto wa asili na mazingira, vitendo hivyo vimepelekea wanyamapori hasa tembo kukimbilia kwenye mashamba na makazi ya binadamu. Wanyama hawa wameleta uharibifu mkubwa katika Wilaya za Muleba, Kata za Ngengena, Rutoro, Wilaya ya Bukoba Vijijini na Karagwe. Mashamba ya migomba yameliwa na wananchi kuachwa bila chakula.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuwa Wizara iongoze Wizara nyingine husika kwa kuhakikisha wavamizi wa hifadhi wanaondolewa ili wanyama watulie sehemu zao na wakulima wapate amani. Pia Wizara iwe mstari wa mbele kama msimamiaji wa hifadhi kuwanyooshea kidole na kuwatia adabu watendaji wa ngazi ya Wilaya na Mkoa ambao maeneo ya hifadhi zilizoko katika himaya zao yanavamiwa bila wao kuchukua hatua yoyote.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la utendaji wa Wizara ambalo limekuwa gonjwa sugu na bahati mbaya viongozi wanaelekea kulizoea tukiwemo sisi Wabunge. Suluhisho la utendaji ni kuwaondoa. Iwapo hakuna ushahidi wa kuwafukuza wapelekwe sehemu ambako watakuwa na madhara kidogo lakini pia wataweza kujirudi.

Mheshimiwa Spika, ili kujenga tabia ya kuwajibika wale watendaji wengine wapewe malengo na Kurugenzi na idara ziendeshwe kwa malengo *performance management programmes* (*PMP*). Chini ya utaratibu huu anayoshindwa kutimiza malengo anaondoka mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inaendesha shughuli zake bila *PMP*. Tuanze na Wizara hii ambayo ikisimamiwa vizuri inaweza kusimamia uchumi wa Taifa letu kwa kiasi kikubwa sana.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na nchi yetu kuwa na rasilimali nyingi za maliasilia, lakini ukienda kwa Mwananchi wa kawaida hasa wanaoishi karibu na mali hizo. Sana utakuta hawaoni faida ya moja kwa moja ya wao jinsi zinavyowanufaisha, sana utawasikia wanalalamika jinsi viongozi wa Serikali wanavyoshindwa kutatua migogoro kati ya hifadhi na wanavijiji kwa muda mrefu na kupelekea madhara, usumbufu na kuleta umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Morogoro ni kati ya mikoa iliyopo nchini ambao umebahatika kuwa na maliasili nyingi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wilaya ya Kilombero kuchangia pato la Taifa kutokana na maliasili zilizopo, Wananchi wa wilaya hiyo hawafaidiki moja kwa moja na maliasili hizo ingawa yapo mapato ya 25% yanayopewa Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, miaka ya sabini hadi 80 Serikali ilikuwa ina utaratibu wa kila wiki, mwezi, kuwinda nyati, swala na kuwauzia wananchi kitoweo, hivyo ilionesha wazi jinsi Serikali inavyowajali wananchi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo ulipunguza uwindaji haramu na wananchi kuona wanyama ni mali yao na kutoa ushirikiano kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilombero ina wakulima na wafugaji, wakulima wa Kata ya Ifakara Vijiji vya Mbasa, Kikwawila, Mahanyika, Mikuyuni, Vipingu na kadhalika, wanapata hasara kubwa kwa wanyama kama tembo, nyati, boko na kadhalika wanakula mpunga na mazao mengine. Hivyo, ni jukumu la Wizara kuandaa mazingira ya kulinda wananchi na mazao yao, wananchi wanazidi kuwa maskini kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Chita na Mofu wapo wawekezaji waliomiliki vitalu vya uwindaji, lakini vijiji vinavyozunguka havipati faida yoyote, matokeo akionekana mwananchi kwenye maeneo hayo, hupewa mateso ya kuchunwa ngozi ya nyayo na mikono ili asiweze kuondoka alipo, labda itokee raia mwema amepita na kumwona na kumwokoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii haivumiliki raia wanateseka ndani ya nchi yao. Wizara inapotoa vibali iwe inafuatilia utekelezaji wa wawekezaji hao kuhusu mahusiano na wanavijiji.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia hoja hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi ngumu wanayoifanya. Lakini pia naomba nimpe pole Waziri kwa jukumu kubwa alilokabidhiwa ambalo ni gumu, Mungu amsaidie.

Mheshimiwa Spika, uvunaji wa misitu yetu ni jambo la kuangalia sana kwa misitu inavunwa kiholela, magogo yanasafiri siku hadi siku malighafi inaondoka nchini, yanabakia majangwa na Serikali inaendelea kukosa mapato.

Mheshimiwa Spika, hata viwanda vyetu vya mbao vya wazawa vinaendelea kubaki hivi hivi tu kutokana na tatizo hili la usafirishaji wa magogo. Hivi Serikali inajua kwamba mti wa msandali unatoweka kwa nguvu kubwa kutokana na kusafirisha magogo ya mti huu na sasa wanachimba hadi mzizi wake kutokana na magogo kuisha. Wanasafirisha magogo yanakwenda kusagwa na kutolewa mafuta mazuri ambayo bei yake ni kubwa sana kwa sababu ni mali sana. Hivyo, wanafaidi watu wengine rasilimali za Watanzania, kwa nini wasiwezeshwe wazawa ili malighafi zisitoke nje ya nchi? Kwa nini tusiweke usimamizi mzuri ili mti uendelee kuwepo kwa kupandwa pale unapokatwa? Kwani Serikali haiwajui wanaofanya biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Watanzania asilimia kubwa hawamiliki hata shilingi mia tano (500) kwa kutwa kwa msingi huo basi si Watanzania wengi wenye uwezo wa kutembelea vivutio vyetu vya utalii kutokana na bei ambayo imewekwa. Hivyo, wazawa hawajui katika Tanzania yao kuna nini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ipunguze bei hiyo iliyopo kwa wazawa.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nataka nishangae sana kwa namna ambavyo Mwenyezi Mungu ametujalia rasilimali ambazo hazipatikani popote duniani halafu tunasikitika kwamba nchi (Tanzania) ni maskini sana.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumejaliwa kuwa na vivutio vyote ambavyo kila nchi duniani wanatambua kwamba vitu hivyo mambo hayo yanapatikana Tanzania mfano, misitu mikubwa sana, maziwa makubwa sana, Mlima mkubwa sana na wanyama na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, maajabu na inashangaza kwamba vivutio vyote hivyo ambavyo ni vyanzo vya mapato lakini nchi inajinamia kwa umaskini, kama hilo halitoshi ni kwamba ni rasilimali ambazo kwetu sisi hatuna gharama yoyote katika kulea hizo kwani ni majaliwa ya Mungu tu, ile kwetu kama nchi ni kujipanga vizuri tu na tukaongozwa na uzalendo wa dhati wa kulihurumia Taifa hili kwa kuwa wakweli na waaminifu kwa watendaji pamoja na viongozi wa Serikali, kwani watendaji tu hawawezi kuihujumu nchi bila ya sapoti au ushirikiano mkubwa na viongozi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kama hakuna ushirikiano wa dhati na viongozi wa Serikali, inawezekanaje wanyama kama Twiga na kadhalika wakaweza kusafirishwa kupitia uwanja wa ndege?

Mheshimiwa Spika, kama kwetu tunafanya kazi kwa uzalendo, tusingeweza kukosa fedha za kutosha kuendesha nchi yetu kutokana na maeneo hayo tu ya utalii, ni ajabu nchi ambayo inaongozwa kwa misingi ya utawala bora lakini hatuna mpango mkakati na unaosimamiwa kwa uzalendo ili nchi hii tukajikwamua.

Mheshimiwa Spika, kwa namna nchi yetu ilivyo na neema ya wanyama wa kila aina ambao wanafaa kuliwa pamoja na bahari na maziwa yenye samaki watamu kuliko maeneo yote duniani, kama tungekuwa na mipango mizuri na ya kizalendo, basi tungekuwa tumejipanga vizuri tukawa na ndege za kusafirisha minofu ya samaki pamoja na nyama, jambo ambalo lingeweza kuliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Askari Wanyamapori wanathubutu kuua Watanzania kwa kuua mnyamapori apate kitoweo na Serikali inaliridhia hilo, lakini wapo ambao wanasafirisha wanyama kupitia uwanja wa ndege kweupe mchana na hao hawaonekani kutenda hujuma kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, katika jambo hili la kuenzi uchumi huu wa Taifa, bado hatujawa wakweli na kuna kiini macho kwa Wizara na watendaji wake na inaonekana wazi kwamba wanahusika katika kuhujumu uchumi unaotokana na utalii!

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** *Honourable Speaker, briefing paper on the operation and implementation of The New Wildlife Law, The Wildlife Conservation Act, 2009. The Wildlife Conservation Act (the Act) is a law which was enacted in 2009 to make better provisions for the conservation management, protection and sustainable utilization of wildlife and wildlife products and to provide for other related matters. This law came into effect on the 13th day of March 2009.*

*Honourable Speaker, first, is about shortcoming and impracticability of Section 21 of the Act on grazing rights. Section 21 of the Act restricts any person to graze any livestock in any game controlled area save with written permission of the Director of Wildlife previously sought and obtained. The section further provides that non compliance of the above requirement is an offence and the person shall be liable on conviction to a fine not exceeding five hundred thousand or imprisonment for a term not exceeding five years.*

*Section 21(1) Any person shall not, save with the written permission of the Director previously sought and obtained, graze any livestock in any game controlled area.*

*(2) Any person who contravenes this section commits an offence and shall be liable on conviction to a fine of not less than one hundred thousand shillings but not exceeding five hundred thousand shillings or imprisonment for a term of not less than one year but not exceeding five years, or both.*

*Honourable Speaker, before the coming into effect of this Act and declaring certain areas game controlled areas, there were certain communities living within these areas conducting their daily economic activities (livestock keeping). It is therefore impractical, cumbersome and*

*unrealistic to require a local villager of a certain village located within a game controlled area to seek for a written permission from the Director of Wildlife to be allowed to graze his cattle within a game controlled area.*

*This requirement might result in chaos and conflict between the indigenous communities living within the game controlled areas and the Government. This is a general land use planning matter which the government seemingly overlooked when drafting the Act. The preparation of Land Use Management Plans over these areas is of paramount importance as a means to clearly identify, demarcate and pinpoint the economic activities to be carried thereon.*

*Honourable Speaker, second, limitations of Section 38 of the Act on Transparency and Good Governance in allocation of Hunting Blocks. Under the above Act, hunting blocks are allocated to applicants by the Minister after consultation by the Hunting Block Allocation Advisory Committee under section 38(6) of the Act. Under section 38(3) of the Act, the Hunting Block Advisory Committee consists of members appointed by the Minister including the Director General of Tanzania Wildlife Research Institute, the Director General of Tanzania National Parks; a representative of the Attorney General, the principal of College of Wildlife Management; any other five persons appointed by the Minister; and the Director of Wildlife who shall be the Secretary.*

*Further section 38(4) requires the Minister when appointing the five persons as stated above, shall have regards to the needs of gender balance, knowledge and experience in business administration, environmental conservation matters relating to economic empowerment. The Act also imposes an obligation on the Minister to ensure that any modality or system used in allocation of hunting blocks is transparent and is inline with the principles of good governance as provided under section 38(11) of the Act.*

*Transparency under the Oxford English Dictionary generally means openness, communication and accountability.*

*Good governance is an indeterminate term used in development literature to describe how public institutions conduct public affairs and manage public resources in order to guarantee the realization of human rights. Good governance is a form of governance that embodies eight specific characteristics, and can be seen as an ideal of governance. Good governance embodies processes that are participatory, consensus oriented, accountable, transparent, responsive, effective and efficient, equitable and inclusive, and which follow the rule of law."*

*The Minister under the Act has been given vast powers in the entire process of allocation of hunting blocks. The current appointmtent of the five persons sitting under the Hunting Block Advisory Committee is not transparent and does not encompass the ethos of good governmance. This is due to the fact that the criteria of appointment stated under the Act which needs to be taken into account by the Minister, were not put to the public for scrutiny as a means to justify such appointments.*

*Section 38(3) The Hunting Block Allocation Advisory Committee shall consist of following members to be appointed by the Minister:-*

*(a) The Director General of Tanzania Wildlife Research Institute;*

*(b) The Directsor General of Tanzania National Parks;*

*(c) A representative of the Attorney General;*

*(d) The principal of College of Wildlife Management;*

*(e) Any other five persons appointed by the Minister; and*

*(f) The Director of Wildlife who shall be the Secretary.*

*(4) In appointing persons referred to in paragraph (e) of subsection, (3), the Minister shall have regards to the need for gender balance, knowledge and experience in business administration, environmental conservation matters relating to economic empowerment.*

*Section 38(6) The Minister shall, upon advice by the Committee, allocate a hunting block to the applicant.*

*Section 38(11) The Minister shall ensure that any modality or system used in allocation of hunting blocks is transparent and is inline with the principles of good governace.*

*Honourable Speaker, third is about conflict of section 39(3)(a) of the Act with Section 22(b) of the Tanzania Investment Act, 1997.*

*Section 39(3)(a) of the Act provides that a minimum of 25% of the shares in a foreign hunting company shall be owned by Tanzanians in order for the company to be eligible for allocation of hunting blocks. The requirement has thus forced the existing foreign hunting companies which have secured their investment under the Tanzania Investment Centre, to sell 25% of their shares to nationals so as to meet the requirement of the Law. This requirement of the law conflicts with section 22 of the Tanzania Investment Act,1997 which guarantees all investors who own, whether wholly or in part, the capital of any business enterprise not to be compelled by any law to cede his/its interest in the capital to any other person.*

*Section 39(3) of the Act the Minister may make regulations prescribing for shares to be owned by citizens in any hunting company, the number of hunting blocks to be owned by a company, criteria, size and value of hunting blocks but in any case.*

*(a) The shares to be owned by the citizens shall not be less than twenty five percent of subscribed shares;*

*Section 22(b) of the Tanzania Investment Act Subject to subsection (2) and (3) of this section.*

*(a) No person who owns, whether wholly or in part, the capital of any business enterprise shall be compelled by law to cede his interest in the capital to any other person.*

*This provision of the Act therefore conflicts with the Tanzania Investment Act as it contravenes the investment guarantee given to foreign investors by forcing them to cede part of their capital to other persons.*

*The anomaly can create disputes between the Government of the United Republic of Tanzania, the Tanzania Investment Centre and foreign investors. Section 23(2) or the Tanzania Investment Act gives three options to foreign investors to pursue should a dispute arise between them, the Tanzania Investment Centre and the Government of the United Republic of Tanzania where amicable settlement has failed.*

*The foreign investors may submit their disputes to arbitration forums in accordance with arbitration laws of Tanzania for investors; or in accordance with the rules of procedure for arbitration of the International Centre for the Settlement of Investment Disputes; or within the framework of any bilateral or multilateral agreement on investment protection agreed to by the Government of the United Republic and the Government of the Country the Investor originates.*

*Section 23(2) of the Tanzania Investment Act reads: "A dispute between a foreign investor and the Centre or the Government in respect of a business enterprise which is not settled through negotiations may be submitted to arbitration in accordance with any of the following methods as may be mutually agreed by the parties, that is to say:-*

*(a) in accordance with arbitration laws of Tanzania for investors;*

*(b) in accordance with the rules of procedure for arbitration of the International Centre for the Settlement of Investment Disputes;*

*(c) Within the framework of any bilateral or multilateral agreement on investment protection agreed to by the Government of the United Republic and the Government of the Country the Investor originates".*

*Section 39(3) of the Act empowers the Minister to make regulation prescribing for shares to be owned by citizens in any hunting company among others. To rescue the above anomaly, the Minister needs to make regulations prescribing ownership of shares in hunting companies to be 50% citizens and 50% foreign investors. The doctrines of Internationsl business are rooted in the philosophy of risk sharing. Risk sharing promotes more investment as the burden of capital is not solely borne by one person. In turn this shall encourage many Tanzanian citizens to invest in the hunting sector.*

*Section 39(3) of the Act The Minister may make regulations prescribing for shares to be owned by citizens in any hunting company...*

*Honourable Speaker, four is about Section 39(3)(b) of the Act is unconstitutional as it contravenes Article 13 of the Constitution of the United Republic of Tanzania on equality before the law.*

*Section 39(3)(b) of the Act provides that, the percentage of foreign owned companies allocated hunting blocks shall not exceed fifteen percent of the total hunting companies at any particular time. This provision of the Act is unconstitutional as it discriminates against those Tanzanian citizens who own 25% of shares in the foreign hunting companies as allocation of hunting blocks to such companies is restricted by the Act to only 15% of the total hunting companies. This implies that a Tanzania citizen owning shares in a foreign company is treated differently from Tanzania citizen owning shares in a local company which contravenes Article 13 of the Constitution of the United Republic of Tanzania.*

*Article 13 of the Constitution of United Republic of Tanzania advocates that all persons are equal before the law and are entitled without any discrimination, to protection and equality before the law. The Article also is to the effect that, no Law enacted by any authority in the United Republic of Tanzania shall make any provision that is discriminatory either of itself or in its effect. For the purpose of this Article the expression discrimination means to satisfy the needs, rights or other requirements of different persons on the basis of nationality, tribe, place of origin...*

*Article 13(1) All persons are equal before the law and are entitled, without any discrimination, to protection and equality before the law.*

*(2) No law enacted by any authourity in the United Republic shall make any provision that is discriminatory either of itself or in its effect.*

*(3) For the purposes of this Article the expression "Discriminate" means to satisfy the needs, rights or other requirements of different persons on the basis of their nationality, tribe, place of origin, political opinion, colour, religion, sex or station in life such that certain categories of people are regarded as weak or...*

*Currently there are 30 foreign hunting companies which have been operating in the hunting business for the past 25 years and have applied for allocation of hunting blocks for the period from 2013 to 2018. Only nine foreign companies which represent 15% of the total foreign companies will be allocated hunting blocks as required by the Law and leaving out 21 companies to close down their operations.*

*The implication of the above mentioned closures will result in the government of Tanzania losing direct taxes of up to Tshs. 50 billion from these companies. Records have proven that these foreign companies have been complying with the obligation to pay the required taxes as well as Wildlife Division Fees.*

*It is well known that these foreign hunting companies have heavily invested in research and monitoring of the hunting blocks. They possess enormous knowledge, skill, information and data of all the animal species and related features within wildlife econsystems in Tanzania. This is the key element in the hunting business and Tanzanians are still building the capacity, skill and knowledge to conduct such research as we still rely on foreign donors to fund and conduct such research.*

*Furthermore, up to 5,200 employees will lose their jobs due to the foreign companies closing down their operations in Tanzania. This will also occasion loss in taxes paid to the Government such as SDL, PAYE et cetera.*

*It has been observed that certain laws encourages foreign Investors to invest in our country and grants Investment guarantees to them and at the same time the government enacts laws which discourages foreign Investments and contravenes on the investment guarantees.*

*The Minister responsible should address the apparent fundamental predicaments caused by the above mentioned provisions of the Wildlife Conservation Act and start process to amend the said provision to comply with the Constitution of the United Republic of Tanzania and the Tanzania Investment Act so as to boost and stimulate economic growth through the hunting business and to honour its Investment guarantees to foreign Investors.*

*The laws making process is dynamic that means any law can be changed at any point in time. Most of the problems with enacted laws are usually noticed and observed during the implementation of the laws. The responsible Ministers have been given powers to rectify such abnormalities found in the laws.*

*For example the Land Act, No.4 of 1999 under section 20(3) provided that, all land acquired prior to the enactment of the Land Act shall be deemed to have no value. This meant that all the land in Tanzania had no value and therefore could not be mortgaged in Banks for certain values.*

*This section was later discovered not to be economically sound and in 2004 through the Land (Amendment) Act under section 4 which is to the effect that all the land in Tanzania has value save for the land acquired by non citizens prior to the enactment of the Land Act except for unexhaused improvements.*

*Section 20(3) of the Land Act stipulates that, all lands acquired prior to the enactment of this Act shall be deemed to have no value save for unexhaused improvements.*

*Section 4 of the Land (Amendment) Act stipulates that for the purpose of compensation made pursuant to this Act or any other written law, all lands acquired by non-citizens prior to the enactment of this act shall be deemed to have no value except for unexhausted improvements...*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukirudi mchana, Waziri mhusika ataanza kujibu hoja zenu. Kwa hiyo, wale ambao hawakupata nafasi ni bahati mbaya, waliitwa walikuwa hawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kigwangalla, mbona unasimama nikiwa mimi nimesimama! Kulikuwa na nini? Enhee, nakuita Dokta Kigwangalla.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi siku ya Alhamisi wiki iliyopita wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu, nilipata fursa ya kuuliza swali la nyongeza kuhusiana na posho za madaktari. Swali hili lilijibiwa na Mheshimiwa Dokta Lucy Nkya, Naibu Waziri wa Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na nilimuomba mimi afute kauli yake kwamba Madaktari hawapewi posho ya nyumba na kwamba imefutwa kinyume cha Sheria. Yeye alisema kwamba wanapewa! Lakini mimi leo hii nilisema kwamba kauli hiyo haikuwa ya ukweli.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba Mwongozo wako kama ili kuweka kumbukumbu sahihi, Mheshimiwa Waziri atakubali sasa kufuta kauli yake, kurekebisha na hatimaye kuwachukulia hatua Wakuu wa Vitengo, Idara na sehemu mbalimbali za Serikali ambapo Madaktari wameajiriwa na hawalipwi posho za nyumba, lakini vilevile hawapewi nyumba, kinyume cha *Standing Order* ya Serikali ya mwaka 1994 na pia *Standing Order* ya Serikali ya mwaka 2009 na pia Sera ya Utumishi wa Umma. Naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mara nyingi mkikuta kama kuna tatizo la namna hii mnafika pale ofisini, tuna ofisi yetu nzima kabisa ya ushauri wa namna ya kuendesha mambo kama haya. Kwa hiyo, kwa maana ya suala hilo wewe ungekuwa umefanya hilo, sisi tungekupa kwenye *adjoinment motion,* unasimama kwamba juzi Waziri alisema hivi na hivi na mimi nimefanya utafiti wangu hivi na hivi; inakuwa imekuwa kwa utaratibu. Maana sasa ukimwambia ajibu huyu, hawezi kujibu kwa sababu, hakujua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nakuomba ufanye utaratibu wa namna hiyo. Tunao utaratibu kabisa wa Kanuni. Kama ulijibiwa hapa kitu chochote ambacho wewe ulikuja kuamini baadaye sio sahihi alivyosema, una uhuru wa uwezo kabisa wa kutumia Kanuni zetu kui-*refeer back.* Lakini kile Kitengo chetu cha Ushauri wa Kisheria, mkitumie vizuri. Kwa hiyo, unafika hapa haupotezi muda unapata muda kabisa, unajieleza na wenyewe wanaohusika itabidi wajibu kadiri inavyostahili. Nilikuona Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kutumia Kanuni ya 48, inayohusu Jambo la Dharura na Kifungu cha 3(a), (b) na (c) kwa ruhusa yako.

**SPIKA:** Na wewe unataka nini sasa? Mwongozo wa kwangu? Hakuna ku-*discuss* chochote; kuhusu nini? Eleza kitu unachotaka kuongozwa.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, kuna jambo la dharura. Kutatokea tatizo kubwa sana hali ya sukari nchini itazidi kuwa mbaya kiasi kwamba licha ya agizo la Rais, kwamba...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, suala la sukari haliwezi kuwa la dharura. Dharura aliyozungumza asubuhi, ni kama alivyosema Mheshimiwa Wenje, sasa umeme hauwaki. Sasa naomba utafute utaratibu mzuri zaidi wa kuliendesha suala lako hilo. Naomba utafute utaratibu mzuri wa Kikanuni na kama umeshindwa tafuta ushauri kwa Idara yetu ya Sheria, utapata maelezo zaidi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mambo ya kidharura ni dharura kweli kweli! Kwa mfano lile swali alilouliza Mheshimiwa Wenje, inawezekana watu hospitali wanakufa! Wapo kwenye *operation* wanakufa! Ndio maana tukamwambia, alivyoeleza ni dakika tano, tumeshaagiza hapa tutapata majibu saa 10.00 jioni ikiwezekana. Sasa mengine tusifanye kila kitu ni dharura, hatutaweza kwenda kufanya kazi yetu. Sasa hilo la kwako, tafuta utaratibu wa Kikanuni, utashauriwa, halafu tutapata namna ya kuliingiza hapa.

Waheshimiwa Wabunge, saa ya kusitisha shughuli za Bunge imefika, wale niliokuwa nawaita walikuwa hawapo, siwezi kuwaita tena, muda wenyewe umeshapita. Kwa hiyo, mchana tukirudi Waziri anayehusika ataanza kujibu hoja za Wabunge.

Nasitisha shughuli za Bunge, mpaka saa 10.:00.

*(Saa 7.10 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**Hoja za Serikali**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeeleza kwamba tutakaporudi kipindi hiki cha jioni tutamruhusu Mheshimiwa Waziri aanze kujibu hoja zetu. Mheshimiwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uzima na baraka nyingi. Mungu roho Mtakatifu kwa maombezi ya Bikira wa Maria Mama wa Huruma, amekuwa akiniongoza mara zote katika kufanya kazi hii ambayo ni ngumu sana. Namuomba azidi kunijalia hekima na busara katika kukabiliana na majukumu yangu mengi na mazito kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru sana viongozi wangu wa kiroho, hasa Askofu wangu Ludovick Joseph Minde na Mashehe, Mapadri, wachungaji na watawa wote wa Kahama ambao siku zote wamekuwa nami katika sala. Nawashukuru sana kwa sala zao na ushauri wao wa mara kwa mara nikutanapo nao. Ninawaomba sana waendelee kuniombea, kwani kama ambavyo wengi wao wanaona na kusikia kwenye vyombo vya habari kazi yangu ni ngumu, ni nzito ni changamoto ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naomba niwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Msalala kwa kuniamini kwa mara nyingine na kunichagua kuwa Mbunge wao. Kama ambavyo nimekuwa nikiwahakikisha mara kwa mara kwamba nitafanya kila niwezalo kuhakikisha kuwa maajabu ya maendeleo tunayotarajia ambayo yameanza kuonekana yanakuwa ni timilifu kweli. Najua kama ambavyo wao wenyewe wanajua kwamba harakati za kuleta mapinduzi ya maendeleo kwenye jimbo letu zimeanza. Kuna miradi kadhaa ambayo hata wao wanaishuhudia sasa hivi, mradi wa kupeleka umeme Mpera unaendelea kutekelezwa, ujenzi wa mabweni pale Isaka unaendelea, matengenezo ya barabara ya Nyambura hadi Ngogwa, Mega, Nyaminji hadi Nyamuguta, Luguya hadi Nyamishega. Pia mkandarasi yupo *site* akichimba visima kwenye vijiji vya Bushinga na Kakola ambavyo vimekuwa na tatizo sugu la maji kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kawaida yetu na kama nilivyokuwa nikiwaambia sitawapotezea muda, muda wao wa kujitafutia maisha kwa kuwaingiza kwenye harakati ambazo hawapaswi kuzifanya. Kwani kuwaingiza kwenye harakati kama maandamano, ni kuonyesha ishara kwamba mimi mwakilishi wao nimeshindwa kuwasemea na hivyo ninawataka wao wajisemee wenyewe kana kwamba hawana mwakilishi. Nitafanya kazi hiyo kwa moyo wangu wote na muda wote nawaomba waendelee kufanya shughuli zao zingine na mimi nitawajibika kuwasemea kama ambavyo nimekuwa nikiwaahidi wakati wa kuomba kura zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua na wananchi wangu wanajua kwamba eneo letu lina matatizo mengi, lakini niwahakikishie kwamba taarifa zote za matatizo ya eneo letu zimekuwa zikifika Serikali na najua wao wanajua kwamba tuna tatizo kubwa sana la uhaba wa chakula sasa hivi. Lakini katika hili kama ambavyo tumekuwa tukikabili matatizo mengine tutashirikiana nao mimi mwenyewe na wao pia pamoja na Serikali yetu kuhakikisha kwamba tunakabiliana nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kipekee niwashukuru sana wana familia wangu, nikianza na mke wangu mpenzi Riberata, watoto wetu pamoja na wazazi wetu wote wa pande mbili ambao wamekuwa wakinishauri, kuniasa na kuniombea. Nawaomba waendelee kuniombea na kunitia moyo katika kufanya kazi ngumu na nzito na muhimu kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo naomba nizungumze hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamechangia. Lakini kabla ya kuzungumzia hoja zao naomba nianze

kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwanza kwa imani kubwa ambayo wanayo kwangu binafsi. Lakini pia kwa kutambua changamoto ambazo Wizara yetu inazo.

Wizara yetu kama mnavyojua inagusa maisha ya watu ya kila siku, Wizara yetu inawagusa watu kiuchumi, inawagusa kimaisha, hasa pale ambapo maisha yao ya kila siku kama kilimo na hata mifugo yanakuwa yanaingiliana na shughuli zetu za uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi ndiyo hizo naziombea fedha leo hii ili tuweze kuzikabili, naamini kwamba pamoja na matatizo mengi yaliyojitokeza kule tulikotoka, tukishirikiana na Watanzania wenzangu na wananchi wenzangu naamini kwamba tutaweza kutatua changamoto hizi. Naomba nitambue michango mbalimbali iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wa kwanza kuzungumza alikuwa ni Mheshimiwa James Lembeli, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wengine waliochangia ni Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Zakia Meghji, Mheshimiwa Joyce Mukya, Mheshimiwa Anne Malecela, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Dkt. Kebwe Kebwe, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mheshimiwa Beatrice Shelukindo, Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Amos Makala, Mheshimiwa John Magalle, babu yangu naona simuoni, lakini namshukuru sana kwa mchango wake, Mheshimiwa Said Arfi na Mheshimiwa Subira Mgalu. *(Makofi*)

Wachangiaji wengine waliochangia kwa maandishi ni hao wafuatao, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa *Engineer* Christopher Chiza, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Rosweeter Kasilika, Mheshimiwa Abass Mtemvu, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Benardetha Mushashu, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Joyce Mukya, Mheshimiwa Augustino Maselle, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangala, Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema, Mheshimiwa Philipa Mturano, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Salome Mwambu, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Regia Mtema, Mheshimiwa Abdulsalaam Seleiman Amer, Mheshimiwa *Engineer* Gerson Lwenge, Mheshimiwa Salvatory Machemli, Mheshimiwa Mohamed Dewji, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Moshi Kasoko, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Moza Saidy, Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Zakaria Shamte, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Abia Nyabakari, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mheshimiwa Omari Nundu, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Godluck Ole-Medeye, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa na Mheshimiwa David Kafulila.

Wengine ni Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa John Chiligati, Mheshimiwa Amina Mwidau, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Donald Max, Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Kheri khatib Ameir, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina, Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuko, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Desderius Mipata na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Dkt. Seif Rashid, Mheshimiwa Amina Makilagi, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Albert Nntabaliba, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Said Bwanamdogo, Mheshimiwa Philipo Mulugo, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi na Mheshimiwa Dkt. David Mallole. *(Makofi)*

Naomba pia Waheshimiwa kama kuna mwingine nitakuwa nimesahau naomba mniletee ki-*note* nitawatambua. Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, na Waheshimiwa wote ambao nitakuwa kidogo nime-*pronounce* vibaya majina yenu, naomba radhi sana hasa wale ambao ni wa Ukanda wa Pwani kwa sababu kwetu kule “r” wa inatupa kazi sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaanza kuhesabu saa moja kuanzia sasa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kama ambavyo nimesema awali michango ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge ni mingi sana. Wamezungumzia maeneo mengi mbalimbali nitajitahidi kupitia hoja zao kwa haraka iwezekanavyo lakini pia kwa kina kadri nitakavyoweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza nizungumzie suala la utoroshaji wa wanyamapori, labda kwanza nieleze kwa kifupi mwanzo wa tatizo au mwanzo wa suala lenyewe. Kwanza biashara hii ya ukamataji wa wanyama, ni halali kwa maana ya kwamba ipo kwenye Sheria ya Wanyamapori, Sheria Na. 5 ya mwaka 2009, Kifungu cha 50. Kifungu kile kinasema kwamba mtu yeyote anaruhusiwa kuomba leseni na kwenye kanuni tumesema biashara hii ni kwa Watanzania. Kwa sababu matarajio ni kwamba biashara hiyo itakuwa ni kwa kiwango kidogo, *small scale business* ambayo ni kwa Watanzania kwa ajili ya kujikimu. Ukihitaji kufanya biashara hiyo unaomba *Trophy Dealers Licenses* kwa hiyo unakuwa *lincesed* kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa kuna kampuni 180 ambazo zina leseni ya kufanya kazi hiyo, leseni inatolewa si mara moja unakuwanayo lakini unakuwa unaomba vibali vya kukamata. Ukishakuwa na leseni kitu cha pili kinachohitajika ni kibali cha kukamata. Lakini kabla ya kupewa kibali unatakiwa uwe umeshajiandaa kibiashara kwa kuwa na eneo la biashara pamoja na eneo la kuwaweka wale wanyama. Utaratibu unadai kwamba wanyama ukishakamata wawekwe kwenye zizi, tunaita *holding ground* ambayo inatambulika na Idara ya Wanyamapori ambapo utawaweka wanyama hao wakati unafanya *logistics* za usafirishaji. Ukishawakamata kwa kutumia *capture permit* ambayo unakuwa umepewa, hatua ya tatu inayofuata ukishakuwa umewaleta mpaka kwenye zizi au kwanza utaratibu wenyewe wa ukamataji. Ukishaomba kukamata ukapewa *capture permit*, unatakiwa kutaja unaenda kukamata kwenye eneo gani na kwenye maelekezo unatakiwa kwenda kuripoti kwa *district game officer* ambaye utaambatana naye pamoja na

wakamataji ambao wanapewa vibali vya kukamata vinaitwa *trepans card*. Ukishakamata unawaleta kwenye zizi, ukiwafikisha pale kwenye zizi unawaombea kibali kingine kinaitwa *ownership certificate*, kwa hiyo, wanakuwa pale kwenye zizi lako, huku ukiwa unawamiliki kihalali na maafisa wetu wa wanyamapori wanakagua mazizi hayo, mara kwa mara. Utawaweka pale kwenye zizi kwa muda fulani kutegemea na *logistics* za usafirishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua ya mwisho inayofuata ni pale ambapo unakuwa ume-*confirm order* na umemaliza mambo ya *logistics* za ndege unaomba kibali cha kusafirisha nje. Wamewekwa kwenye makundi mawili, kuna wanyama ambao wapo kwenye hatari ya kutoweka ambao wapo kwenye mkataba wa *cites* na kuna wanyama ambao hawapo kwenye hatari ya kutoweka wao hawapo kwenye hiyo *list*, kwa hiyo, utakachopewa au kibali utakachoomba ni *cites permit* ambayo ni *document* ya kutumia kusafirisha wanyama na ukishaitoa kule wanakopelekwa wale wanyama na kwenye wanaipokea na wanatunza kumbukumbu. Kama yule hayupo *cites list*, unapewa *export certificate* unasafirisha.

Mheshimiwa Spika, sasa katika mazingira haya ni kwamba biashara hii imekuwa ikifanyika. Kilichotokea ni kwamba tarehe 26 kama tulivyoeleza wanyama walitoroshwa na tunasema walitoroshwa kwa sababu *document* zile tatu za msingi zipo yaani kuna watu ambao wana *trophy dealers license* na katika kukamata walikuwa na *capture permit* na waliweka kwenye mazizi na kuwa na hiyo *ownership certificate*.

Kwa hiyo, watu wa idara ya wanyamapori baada ya kujuliwa kuwa kwamba kuna wanyama walitoka na walitoka katika mazingira yenye utata. Cha kwanza walichokifanya ni kwenda kukagua kwenye mazizi ya watu waliotajwa kwa sababu katika ku-*facilitate* mzigo uondoke walikuwepo watu. Kwa hiyo, walichokifanya ni kwenda kukagua kwenye mazizi ya hao watu wakawakosa wale wanyama. *(Makofi)*

Baada ya kuwakosa, ndiyo wakawaomba kwa kuangalia zile *capture permit*, wakawauliza una *capture permit* za wanyama 120 na una *capture permit* za ndege 16, wako wapi? Baada ya jibu kukosekana na kwa sababu alikuwepo kwenye ile *process* kule ikaonekana kwamba dhahiri ndiyo wale waliotoroshwa. Kwa hiyo, baada ya tukio hili kuwa *reported* polisi, uchunguzi huo ulikuwa ukifanyika pamoja na watu wa polisi, pamoja na watu wetu wa Idara ya Wanyamapori. Baada ya kuwa limejitokeza na wanyama wamekosekana kilichofanyika ni kuwakamata wale watu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wale watu sita walikamatwa wakafunguliwa kesi ya uhujumu uchumi ambao kwa namna moja au nyingine wanahusika na ule mchakato na kuna kesi ya uhujumu uchumi inaendelea Moshi. Ndiyo maana tumekuwa tukilisema suala hili kwa kigugumizi kidogo kwa sababu muda wote watu wanao-*prosecute* wamekuwa wakitutahadharisha sana kwamba kitu chochote ambacho mnakifanya msikiseme *in public* kwa sababu kwa namna moja ama nyingine mnaweza mkaathiri upelelezi. *(Makofi)*

Lakini pia kwa upande wetu tumekuwa tukifanya upelelezi na tulichokubaliana ni kwamba kila *evidence* tunayoipata tuwapatie watu wa *DCI* yaani tumpatie Mwendesha Mashitaka ili aweze kuangalia *evidence* ile kwa kiasi gani inaweza ikatumika kama ushahidi wa kuunganisha kwenye kesi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hili tumekuwa tukilifanya kwa kushirikisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama vya nchi na kabla sijafika mbali nizungumzie suala la ndege. Ile ndege iliyokuja kuchukua wanyama ni ndege iliyokuja kihalali, iliomba kibali kupitia *foreign* kwamba inamleta *Diplomat* kwenye *private visit,* ikapata *clearance* ya watu wa usalama wa anga pamoja na watu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi. Kwa hiyo, kufika kwake siyo kwamba rada zetu hazikuona, ziliona lakini kwa sababu watu wa Ngome na watu wa *TCRA* hawaji kukagua wakati inaondoka kwamba inaondoka na nini, kwa hiyo, wao kusema kweli hatuwezi kusema kwamba kuna matatizo upande huo, matatizo yapo kwenye *ground handling*. Kwa hiyo, ile ndege kwamba haikufika na haikuonekana kwenye vyombo vya ulinzi na usalama wa nchi, hapana, ilionekana! *(Makofi)*

Baada ya kuwa uchunguzi umefanyika na tumefika hapo, Waheshimiwa Wabunge niseme kwa dhati kabisa kwamba mimi binafsi jambo hili pamoja na kwamba limetokea siku chache sana kabla sijaapishwa, Baraza la Mawaziri lilivunjwa tarehe 5 Novemba, 2010 na nikateuliwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii tarehe 24 Novemba na nikaapishwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii tarehe 27 Noemba, saa nne asubuhi na wanyama waliondoka tarehe 26 Novemba usiku. Kwa hiyo, Babu John Shibuda Magalle aliyekuwa akisema kwamba kwa kiasi fulani kwa maana tu ya *timing,* kusema ukweli kikombe kile hakinigusi moja kwa moja. Kwa hiyo, niliona ni vizuri nilifafanue hilo hasa kwa maana ya ku-*clear my personal record*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi kama Waziri mwenye dhamana ninawajibika kufanya kila jitihada kulinda maliasili za nchi yetu na hapa ndiyo kazi yangu kubwa iliopo na ndiyo maana hatua hizi tumezichukua kuhakikisha kwamba wale watu wanachukuliwa hatua. Tumefanya uchunguzi wa ndani, tumesikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge na niseme tu kwamba pamoja na uchunguzi wetu sisi ulikuwa unaendelea, pamoja na tahadhari nyingi ambazo watu wa usalama na wa upelelezi wametueleza kwamba kwa namna moja ama nyingine tuwe na tahadhari tusije tukaharibu upelelezi unaoendelea. Niseme kwamba tumekubaliana kwamba kuna mambo ambayo tunaweza tukayasema kwa sasa, moja ni kwamba kuna mazingira dhahiri ya namna moja ama nyingine watu wetu kutokufanya vizuri na niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwani tunapoongea hapa Bungeni tunaongea kwa kiapo, Mbunge hawezi kusema tu jambo kwa kuonea mtu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana kwamba Mkurugenzi wa Wanyamapori Bwana Obed Mbangwa asimamishwe kazi kwa malipo kuanzia leo tarehe 18 Agosti, 2011 ili kupisha uchunguzi kwenye Ofisi yake. Pili, kuna watumishi wengine wawili ambao wapo chini yake kwa sababu za kiupelelezi naomba nisiwataje kwa sababu na hata humu hawakutajwa. Lakini katika kusimamishwa atasimamishwa na wenzake wawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na Bunge lako tukufu niwahakikishie kwamba tunaomba sana Wabunge wenzangu na Watanzania kwa mujibu wa Ibara ya 27 ya Katiba ya Nchi yetu, maliasili za nchi yetu ni zetu na tunapaswa tuzilinde kwa nguvu zote. Mimi na Ofisi yangu tutafanya kila liwezekanalo kuhakikisha wote waliohusika wanafikishwa kwenye vyombo vya Sheria.

La pili, ni kwamba jitihada za kutafuta wale wanyama zimeshaanza, niishukuru sana Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa kweli wametusaidia sana. Kuna vitu vingi ambavyo mimi binafsi kwa ugeni wa hapa na pale, pamoja na Katibu Mkuu tulikuwa tunapata shida sana. Lakini niseme kwamba Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kusema ukweli ndiyo iliyotugutua kwamba embu angalieni *CITS* wameshajulishwa? Tulikutana na Kamati ya Bunge mwezi Julai mwishoni, baada ya kuwa tumekutana tuka-*find out* tukaona hata *CITS* walikuwa hawajajulishwa, tukawaandikia barua *CITS* tarehe tarehe 2 Agosti, 2011 kuwaomba washiriki na watusaidie kwenye upelelezi na wakatujibu. Lakini hatukuwaandikia *CITS* peke yao tuliwaandikia pia *Lusaka Agreement Task Force* ambayo ni Umoja wa Ushirikiano wa Ulinzi wa Wanyamapori kwenye nchi za *SADC. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vyombo hivi vinatusaidia sana wameshatujibu na tayari wameshafanya mawasiliano na watu waliopo kule kwa sababu *Qatar* ni mwanachama wa *CITS.* Kwa hiyo, upelelezi wa upande huu kujua kwamba wale wanyama wamepelekwa na *final destination* ni wapi na wamefikishwa kule kwa *documents* zipi. Hilo jambo linaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, wapo waliozungumzia kuhusu suala la kuweka *diplomatic protest* au kufanya jitihada zozote zile za kidiplomasia. Washauri wa Kisheria wa suala hili wamesema ni vizuri tukajiridhisha, tusikurupuke. Ukii-*attack* nchi kwamba imeiba halafu ikaja ikaonyesha kwamba wale wanyama walipelekwa kwa *document*, tuchukulie kwamba kuna *document* zilizojitokeza au zilizotolewa na watu wetu *somewhere,* sisi tutalazimika kuomba *apology* kubwa sana. Kwa hiyo, ni lazima tujiridhishe kwa asilimia mia moja kwamba kweli wanyama wale wamekwenda mahali fulani na wamekwenda *illegally* kwa sababu eneo lingine linaloleta shida ni kwamba haiwezekani ndege ya Serikali inakuja kwa *diplomatic permit* ije katika mazingira ya kufanya uhalifu. Kwa hiyo, tulikuwa tumeshauriwa kwamba tukamilishe uchunguzi wa *CITS* pamoja

na *LATF* pamoja na *Interpol*, hivi vyombo vitatu vya ulinzi vitatusaidia kupata habari za uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, habari hizi zitatusaidia ku-*trace* wanyama wako wapi na baada ya hapo sasa yule ambaye atakuwa na *ownership* nao na atakuwa na *possession* ndiyo atawajibika na yeye kuwa *charged* kwenye kesi inayoendelea lakini hatujajua ni nani hasa ambaye anao kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba hilo suala nilimalizie hivyo kwa kuahidi tu kwamba tutafanya kila linalowezekana na Waheshimiwa Wabunge mnapata taarifa nyingi kwani ninyi ni viongozi wa nchi, maliasili hii ni ya kwetu naomba tushirikiane kuilinda. Pale ambapo una taarifa zozote na kama humuamini mtu mwingine yeyote, naamini mimi mnaniamini, basi yeyote kati ya hawa mtupatie taarifa hiyo tutaishighulikia. Pale ambapo utakuwa umetupatia taarifa halafu ukaona kwamba tunai-*handle* vibaya tupo radhi utuletee hapa, uje useme tarehe 20 nilikuletea *document* fulani na hukuchukua hatua. Kwa sasa naomba muamini kwamba tutafanya kila linalowezekana, mimi nimekasirika kuliko muda mwingine wowote wa historia ya utumishi wangu wa umma kwa jambo hili. *(Makofi)*

Naomba nizungumzie jambo lingine ambalo limechangiwa sana na Waheshimiwa Wabunge kuhusu zoezi la ugawaji vitalu. Kwenye eneo hili kuna mambo matatu muhimu yaliyozungumzwa, la kwanza ni kuhusu utaratibu wa utangazaji, la pili ni suala la Kamati na la tatu ni suala la utaratibu wa ufunguaji wa maombi. Katika kulitazama suala hili limekuwa likiangaliwa kwa kufananisha na Sheria ya manunuzi ya umma yaani *tender*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikianza na hili la Kamati, kifungu cha 38 kinachoanzisha Kamati ya ushauri ya Waziri kinasema kwamba watakuwepo Mwenyekiti wa Kamati *Block Allocation Advisory Committee to the Minister* na atakuwepo Mwenyekiti ametajwa na sifa zake, eneo hilo halijazungumzwa kwamba lina matatizo. *(Makofi)*

Pili, kuna wajumbe watano ambao wametajwa kwa nyadhifa zao, ametajwa mtu wa *TANAPA,* Mkurugenzi wa *TAWIRI,* mwakilishi wa *AG,* Mkurugenzi wa Wanyamapori kama Katibu na ametajwa mtu mwingine mmoja sikumbuki ni nani lakini pia kuna watu watano ambao wamejatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu wengine watano ambao wametajwa kwamba Waziri atateua, katika hao watu watano Sheria inasema kwamba katika kuwateua Waziri atazingatia *gender, knowledge and experience in Business Administration, Conservation Matter and Economic Empowerment related matters, u*kisoma kwenye Sheria inataja hayo. Wametajwa Wajumbe wawili ambao wanaonekana kwamba hawatoshi kwa kigezo hicho nilichokisema. Wajumbe hao ni Ndugu Daniel Nsanzugwanko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ndugu Daniel Nsanzugwanko ana *MBA,* ana *Postgraduate Diploma in Business Administration,* amekuwa *Director* wa *Bunge Foundation*, amekuwa Mkurugenzi wa Chuo cha Ushirika akifundisha mambo ya *Business Management,* amekuwa Mbunge, amekuwa Naibu Waziri kwa *Masters in Business Administration*. *Knowledge* inayotakiwa kwa viwango vya kawaida amezidi, kama ni siasa tuseme tunahoji ya milengo ya siasa lakini kama ni kutosha anatosha na kuzidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu mwingine amezungumziwa ni Ndugu Beno Malisa ambaye ni *Graduate* wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 2005 akiwa na Shahada ya Sheria, *Honours*. Huyu sasa hivi anamalizia *Postgraduate Diploma in Economic Diplomacy* kutoka *Centre of Foreign Relations Dar es Salaam*. Lakini amefanya kazi *UNICEF* kwa miaka miwili kama *National Facilitator* wa Mradi wa *Empowerment and Justice.* Kwa kigezo cha *knowledge*, mtu huwezi uka-*graduate* Sheria ukashindwa kwa sababu huyu mjumbe tunataka awe na uwezo wa kuangalia *Business Plan* za waombaji. Akitoka pale wafanye *due diligence,* waende kukagua mahema na magari, sidhani kama mtu mwenye *degree* ya Sheria atashindwa kuona hema na kusema huyu mwombaji ana hema na huyu hana. Kwa hiyo, kwa maana ya *knowledge* basi *basic knowledge* anayo na *basic*

*experience* anayo. Niseme tu kwamba kiukweli kwenye eneo hili zaidi ya kutazama kisiasa angekuwa siyo Mwenyekiti au vyovyote wa UVCCM sidhani kama ingekuwa ni *issue. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba walau kuwa-*clear* kwamba hawa watu na mimi mwenyewe kwamba sijawateua *negligently* na sehemu ya Sheria haijasema kwamba katika kuwateua watu hawa niwatangaze. *The Minister* na *Minister* ni mimi, *will choose five members* wenye sifa za *gender balance, of course* wapo wengine sijawataja kwa sababu hawajazungumziwa, sitawasema sana lakini wenye *knowledge* kama nilivyoeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa upande wa Kamati kwa dhati kabisa sioni kama kuna tatizo, kama ni tatizo la upungufu wa utendaji kazi ni suala la maadili la mtu binafsi lakini siyo kwamba hana *knowledge* wala hana *experience*. Lakini kama kuna *incidences* za namna hiyo ni vizuri tukapeana taarifa, mimi nitachukua hatua lakini si kwa maana ya *knowledge* na *experience*, sijaona kama kuna tatizo kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili lililozungumziwa ni la vitalu vyenyewe kutangazwa. Mimi nilikwenda Idara ya Habari Maelezo tarehe 4 Februari, nikaitisha *press conference, TBC* na televisheni nyingine walitangaza. Nikasema kwamba tarehe 10 Februari tumemaliza mchakato wote uliopaswa kufanyika kwa ajili ya kutangaza vitalu, nimeshateua Kamati, vigezo na Kanuni zimeshakamilika. Tunatangaza tarehe 10 Februari kwa siku 30 kama mpo *interested*, nikawatania hata waandishi wa habari kwamba waandishi wa habari hata kama mnataka kuomba tarehe 10 Februari tunatangaza vitalu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tarehe 10 Februari tukatangaza kwenye magazeti manne mawili ya Kiswahili na mawili ya Kiingereza ambayo kopi zake ninayo hapa. Lakini pia tuka-*post* tangazo hilo kwenye *website* ya Wizara kwa bahati mbaya tu nimesikia Wabunge wengine wanasema kwamba kwenye tangazo lenyewe hatujaandika kwamba *you can refer this advert* kwenye *website* ya Wizara lakini ukiangalia kwenye *www.mnrt.go.tz* utakuta matangazo yaliyotolewa na Wizara na hilo tangazo lipo. Kwa hiyo, kwa maana ya kutangaza matangazo yamekwenda sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua ya tatu inayopaswa kufanyika ni kwamba waombaji wanaleta maombi Wizarani, wanalipa *fees* na wanapewa risiti. Baada ya hapo Kamati inafanya kazi kwa siku 60 za kuwakagua yaani kukagua mambo ya *bond,* kukagua kama hana *bond* labda ana mahema na magari kwa sababu biashara inatakiwa awe na hivyo vitu vingi ambavyo vimetajwa kwenye mwongozo. Kamati inafanya kazi kwa siku 60 ikishamaliza inaleta taarifa yake kwa Waziri, sasa katika kulinganisha suala hili na utaratibu wa *tender* tulisema kwamba suala la vitalu tusiliweke kwenye *tender* kwa sababu kwa kufanya hivyo tutawaweka kwenye nafasi ngumu Watanzania, wapo watu wenye uwezo wanaweza waka-*tender the highest price* kwa vitalu vyote mtamfanyaje?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukasema kwamba tutakuwa tunakaribisha maombi *maximum* ni vitalu vitano vimewekwa kwenye Sheria na katika kufanya hivyo tutahakikisha kwamba 25% ya *shares* za kila kampuni *minimum* ni Watanzania. Lakini pia hata baada ya kuwa tumetangaza na tumetathmini maombi kampuni zote zitakazoomba *maximum* ya kampuni za kigeni zisizidi 15%. Kazi hiyo imefanyika na ikimalizika wakaleta taarifa kwangu iliyoeleza kama nilivyoeleza majuzi na nilieleza pia kwenye vyombo vya habari kwamba hawakukamilisha baadhi ya vitu vikiwemo *bond* pamoja na *Tax Cards* au *Tax Return*, uhalali wa *bond* pamoja na *nationality* ya *shareholders* kwenye zile kampuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hili lina matatizo na maneno mengi, nina wasiwasi sana kwa sababu kwenye ile Kamati tuna mwakilishi wa *AG,* muda wote tumekuwa tukishauriana naye na hata leo nimemuuliza kwamba atuambie katika huu mchakato kwa mujibu wa Sheria kwa sababu Sheria tunayofuata ni Sheria ya Wanyamapori kifungu cha 38 na siyo Sheria ya Manunuzi ya Umma, hatununui au hatu-*dispose,* tunatafuta watu wa kupangisha vitalu, vitalu ni vya Serikali, tunatafuta watu wa kupangisha na utaratibu wa kuwapata umewekwa kwenye Sheria. Kwa hiyo, tumefanya *consultation* na Wanasheria wetu wanasema kwamba *attempt* yoyote kwa *stage* hii inaweza ikaleta matatizo kwa sababu hakuna *ground* yoyote ya kusema kwamba kuna kitu fulani

kimekiukwa kwa Sheria ambayo inaongoza *process* imefuatwa vizuri mpaka hatua hii kama kuna matatizo yanaweza yakatokea basi yatokee kuanzia sasa kwenda huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria inasema kwamba baada ya matokeo kuwa yamekamilika waombaji watajibiwa yaani waliopata watajibiwa kwamba wamepata na waliokosa watajibiwa kuwa wamekosa na wataelezwa kwa nini wamekosa. Sheria inasema kama hajaridhika anafanya *appeal* ya kufanyiwa *Administrative Review*, asiporidhika na hatua hiyo anafungua a*ppeal High Court* kwenye Sheria imeelekeza hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninafikiri kwamba kwa sababu suala hili ni la kisheria na lipo kwenye Sheria ambayo Bunge hili limenitaka niisimamie ninaomba kwamba Bunge liendelee kutuamini tuukamilishe huu mchakato, pale ambapo panaonekana pana matatizo tutachukua hatua zinazostahili kwa mujibu wa Sheria kama ambavyo imeelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu nilizungumzie kwa kifupi sana ni suala la uchimbaji wa Urani kwenye eneo la *Selous.* Kwa kifupi sana tatizo lililotokea ni la *consultation*, inaweza ikawa ni *oversight* kwa upande wetu lakini inategemea jambo hilo tunalitazama vipi. *(Makofi)*

Mimi nilipoteuliwa kuwa Waziri nilipewa Katiba ya nchi, nilipofika Wizarani nikapewa Sheria, Sheria niliyopewa ni ya Wanyamapori inasema kwamba hairuhusiwi kuchimba madini kwenye hifadhi isipokuwa madini ya Urani, gesi na mafuta, hiyo ni ridhaa ya Bunge, hiyo Sheria imepitishwa na Bunge, kwa hiyo, mimi nikaona jambo hili lipo kwenye utekelezaji. Kuliambia Bunge kwamba sasa mlipitisha Sheria niruhusu kuchimba sasa wanataka kuchimba maana yake ni kwamba Sheria inasema kwamba nafasi ya Mkurugenzi ikiwa *vacant* sasa inahitaji kujazwa nije niliambie Bunge kwamba jamani eeh! Sasa nataka kuajiri Mkurugenzi wa Wanyamapori, *is administrative.* Kwa hiyo, kwa sababu lipo kwenye Sheria hivyo ndivyo tulivyolitazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo nikiri kwamba halikufanyika vizuri ni suala la ushirikishaji wa Kamati *for knowledge.* Hili niombe tu kwamba kwa kiasi fulani ni suala la *timing,* kwa sababu tulipopeleka ile taarifa yetu *UNESCO* tulipeleka mwezi Februari, lakini kujibiwa kwamba ajenda yenu itakuwa *discussed* kwa sababu unapeleka ajenda na ule ni Mkutano wa siku kumi kuanzia tarehe 19 mpaka tarehe 29. Mkishapeleka *proposal z*enu au taarifa zenu zinapangwa kwenye ajenda na wanawajibu kwamba *proposal* yenu imeingizwa kwenye ajenda na wakishawajibu ndio mnakwenda.

Kwa hiyo, sisi tulijibiwa tarehe 26 Mei, kwamba ajenda yetu itakuwa *discussed* na tukaambiwa inakuwa *discussed* kati ya tarehe 19 Juni hadi tarehe 29 Juni kipindi ambacho Bunge hili lilikuwa lipo hapa. Ndio tulikuwa tumeomba kwamba walau kwa uwakilishi twende na Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini na Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa niaba ya Wanakamati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye *correspondence* kati ya Wizara na Kamati huwa tunawasiliana kupitia kwa Mwenyekiti. Kwa bahati mbaya Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini alikuwa na udhuru lakini tulikuwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na tulikuwa na Mbunge wa Namtumbo pamoja na timu ya wataalam ambao ni Kamati ilikuwa imeandaliwa kwa ajili ya ku-*facilitate* au kutetea jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wetu Wizara ya Maliasili na Utalii tunachopaswa kufanya sheria yetu haitupi nafasi ya kukataa. Kama angekuja mtu kuomba anataka kuchimba rubi, *Tanzanite* hata kama zingekuwa za thamani gani sheria imetaja madini matatu hapo nitasimama, lakini kwa haya ambayo kwenye sheria nimeambiwa nisikatae kisheria hatuna tatizo, kwa hiyo, eneo pekee lilikuwa ni kwa sababu eneo hili lipo kwenye urithi wa dunia kwa hiyo, ikabidi tuwashirikishe *UNESCO.* Niombe tu kwamba kwa hatua ambazo zinafuata baada ya kuwa tumeshapeleka ombi lile na halijawa *approved* tumepata *provisional approvement* ili tufanye *EIA* kwa mara nyingine pamoja na wao wenyewe *World Heritage Committee* watume wataalam wao kwa ajili ya kuja kushirikiana na watu wa kwetu kufanya mambo ya *environmental impact assessment* na mkutano ujao wa 36 utakaofanyika mwezi Juni, 2012 ndio utakaosema kwamba *UNESCO* imeruhusu au haijaruhusu *the final approval* haijatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe tu tahadhari kwamba jambo hili kwa uchumi na kwa *proposal* tuliyopewa lilionekana ni la muhimu sana. Waheshimiwa Wabunge wenzangu niwaombe sana hasa wa upande wa Chama cha Mapinduzi tunazungumzia kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tumeahidi mambo mengi, tumeahidi barabara za lami ukimuuliza Mheshimiwa Mwakyembe atakwambia *thousands of kilometers*, tumeahidi zahanati kila kijiji, tumeahidi kituo cha afya kila Kata, tumeahidi meli sehemu mbalimbali na kadhalika kama mnavyojua haya yanahitaji fedha. *(Makofi)*

Sasa hivi tuna matatizo makubwa ya umeme lakini tusipokuwa waangalifu tunaweza tukaingia kwenye mtego ambao ni kuifanya Serikali isiwe na *resources* huku kuchangisha au kuwashirikisha wananchi kwenye michango na kwenyewe kunafanyika kampeni wananchi wasichange, huku kutumia maliasili zetu kuchangia kwenye uchumi na kwenyewe inaonekana haiwezakani, tutashinda kutekeleza Ilani yetu. Sheria inasema au cha muhimu cha kuzingatia ni kuzingatia Sheria ya Madini. Sheria ya Madini inasemaje ambayo ni sheria mpya tumeipitisha Bunge lililopita, tumeipitisha mwezi Juni, 2010. Yote zilizokuwa ni *concerns* za kwamba Bulyanhulu kule wana taratibu za ajabu ajabu sijui wapi, sheria hii imefanya maboresho, kwa hiyo ina mazingira tofauti na sheria ya zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba jambo hili kwa utaratibu wa kiuchumi na nchi nyingi za Afrika na nchi zingine ambazo zinaendelea tuna changamoto kubwa sana ku-*balance* kati ya *conservation* na *development.* Tunahitaji barabara, maeneo mengi sasa hivi tunakuja na mijadala ya kuzungumzia kujenga Bwawa la Kidunda kwenye hifadhi. Kesho kutwa tutakuja kuzungumzia kujenga *Stigler's Gorge* kwenye hifadhi, kesho kutwa tunazungumzia kutengeneza reli kutoka Mtwara sijui kwenda kule Liganga inapita *Selous* haya yote ili uyafanye unahitaji kwenda *UNESCO.* *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunahitaji ku-*balance* kwamba *if we real need to use our resources* ili watu wetu waendelee ni lazima tuangalie tunawafanyaje na tuwe na njia nzuri za kutumia rasilimali zetu na sio kuacha kabisa. Uchimbaji wa namna hii wa *uranium* hautafanyika Tanzania peke yake hivi tunavyozungumza Namibia wanachimba, Malawi wameanza kuchimba, Niger, Afrika ya Kusini wanachimba *Uranium.* Wataalam wa *Atomic Agency* kule Arusha wanasema kwamba ile *uranium* ni ya hatari, ikisharutubishwa, ikisafirishwa ilivyo vile madhara yake ni madogo. Sasa hayo yanafanyika na kwingine na hata Malawi hapa wanafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi kwa upande wetu katika Serikali tunaomba kwamba Bunge lako lione kwamba mradi huu ni wa umuhimu na tushirikiane tuzingatie sheria zilizopo, tusome Sheria ya Madini vizuri kabisa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini nasema kwa mfano kwenye sheria ya kifungu cha 10 cha Sheria ya Madini kinasema Migodi yote itakayoanzishwa kuanzia sasa ni lazima Serikali iwe na hisa inaitwa *Government Equity* imetajwa au … *interest* kwenye migodi na mambo mengine mengi ambayo yatakuwepo kwenye migodi inayoanza. Kwa hiyo, niliona hilo jambo nalo nilizungumzie kidogo kwa kirefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya jambo hilo naomba nizungumzie japo kwa haraka kwenye baadhi ya maeneo. Ripoti ya *CAG* ameisema kaka yangu hapa Mchungaji wangu, Kiongozi wangu wa Kiroho, mimi katika watu ninaowaogopa ni Wachungaji. Kiongozi wangu wa Kiroho Baba Mchungaji umesema kwamba tulikosea kushusha gharama za uvunaji, ungekuwepo Bunge lililopita hapa palikuwa hapatoshi. Bei ya mbao watu walikuwa wanaenda kuvuna mbao Malawi, *VAT* ilikuwepo kwenye mti uliosimama Wabunge walichachamaa sana, waulizeni waliokuwepo kwenye Bunge lililopita, kina Dkt. Slaa, walikuwa wamechachamaa kwamba shusheni hizi gharama na kilichoonekana kwamba wananchi hawa tunawaumiza kwa sababu tulikuwa tunawatoza kwenye *standing value* yaani ule mti na matawi yake ambayo ukienda ku-*prone* ule mti wenyewe ambao ni *proccesable* ni *70 percent* ndio tukasema kwamba badala ya kutoza mti pamoja na zile *off cuts* matawi yale tutoze kwenye *70 percent,* kwa hiyo, tukaondoa ile tozo ambayo tulikuwa tunatoza kwenye *100 percent* tukasema tuwe tunatoza kwenye *70 percent.* Kwa kufanya hivyo faida ile sio ufisadi, imekwenda kwa wananchi tungekusanya fedha ile tukaitumia hapo ndio ingesemwa. Tumewapunguzia gharama wananchi, leo tunazungumzia kwamba tupunguze gharama za ujenzi, kuwapunguzia gharama sidhani kama ni ufisadi kwa sababu

wanaonufaika ni Watanzania. Mheshimiwa Baba Mchungaji tumelifanya jambo hili kwa nia njema kabisa na wananchi wa Iringa ndio wamenufaika pia kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililosemwa Mheshimiwa Kabwe Zitto alitushauri ni jambo jema sana tutalifanyia kazi, alisema kwamba tujitahidi tuongeze tozo kwenye mazao ya misitu. Mazao ya misitu tunaweza tukakusanya bilioni 100 na sasa hivi tunakusanya kama bilioni 38 akasema wakati anachangia kwenye Bajeti kuu ya Serikali. Ni jambo jema na ndio maana tunaanzisha *TFC* au Wakala wa Misitu ili iweze kusimamia jambo hili kwa ukamilifu. Niseme wazo la kuongeza tozo hapa na pale na kuimarisha usimamizi hili tutalifanya. Kwa kiwango cha kuongeza bilioni 100 mpya inaweza isiwe rahisi kwa sababu *increase* yake ni zaidi ya *300 percent* na tukifanya hivyo tutakuwa tumeongeza zaidi ya asilimia 270 kutoka zile 30 tulizoshusha hapa hapatatosha Bunge lijalo, kwa hiyo, tutaangalia kuongeza lakini kuongeza *very cautiously*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lililozungumzwa kwa kirefu sana ni suala la *concession fees,* niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, sana tu. Mimi kama ambavyo wote mmenisisitiza nitasimama imara na tumekwishaanza kutafuta mbinu zingine za kukabiliana na tatizo hili.

La kwanza ambalo tumewaambia *TANAPA* wafanye ni kwamba kwenye maeneo yote ambayo watakuwa wameyatangaza kwa ajili ya uwekezaji ikiwezekana na wenyewe wahakikishe wanakuwa na *free carriage interests* kwenye maeneo yale, yaani mtu akija kuwekeza pale *TANAPA* awe na asilimia 30. Wakati wakifanya hivyo maana yake watakuwa na *shares* kwenye hoteli zote zitakazojengwa kwenye hifadhi au *lodges*. Lakini jambo lingine ni kwamba kwa sababu sekta binafsi tumeona wakati mwingine inakuwa haina huruma tumetoka kukabiliana nao juzi kwenye mambo ya mafuta, sasa hivi tena *the same group* tunakabiliana nao kwenye mambo ya hoteli. Katika mazingira haya ni muhimu vyombo vyetu vya Serikali viweze kushiriki. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tumewaambia *TANAPA* maeneo wanapoyatangaza waangalie vyombo vya Serikali vyenye uwezo wa kifedha *National Housing*, *NSSF, TANAPA,* wenyewe Ngorongoro wajenge hoteli, wawakaribishe wenye utaalam wa kuziendesha waziendeshe kama waendeshaji tu. Lakini wakati tunafanya jambo hilo suala la *concession fees* na yote tuliyokubaliana tutayasimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baba Mchungaji amezungumzia suala la barua niliyoandika, ni kweli niliandika barua, baada ya jambo hili kutangazwa wale jamaa walifanya mgomo, walifanya *strike* hawa jamaa na waka-*strike* na hawa *tour operators* kina Mheshimiwa Akunaay wakapeleka magari mengi zaidi ya 200 pale *navigate* yamejaa magari pale Tarangile, watalii wanasumbuliwa na kila siku tunahitaji kuwabembeleza. Nimepigiwa simu na Mabalozi kwamba watu wako getini toka saa 4.00 asubuhi wamezuiwa kuingia hifadhini wanalazimishwa walipe na hawa akina Mzee Akunaay. *(Makofi)*

Mzee Akunaay ni mdau mkubwa sana wa *tour operators* namtaja kwa heshima na sio kwa ubaya. Wakawa wamesema kwamba hawa hawakutaarifiwa kwamba watakuwa Mawakala wetu wa kuwa wanakusanya. Ni kweli waliandikiwa barua, lakini hawakuwa *engaged* kwenye majadiliano. Wageni wapo getini imefika saa 10 hawana pa kulala ndio nikawaambia waruhusuni wageni, msiwaingize kwenye mtego hawa *tour operators* akina Mheshimiwa Akunaay na wageni. Tatizo lenu ni ninyi na hoteli. Waruhusuni wageni waende hotelini wapate mahali pa kulala halafu muwadai wale watu kwa sababu mnajua mhesabu wageni wangapi wamepita hapa getini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, pale getini mfanye kazi ya kuwahesabu wageni halafu kule mkusanye atakayekataa tutashughulika naye ili tuondoe usumbufu kwa wageni. Kilichofanyika pale ilikuwa ni kuokoa sekta. Tulikuwa tunapata *embarassment* kubwa sana ya nchi, wageni wamehangaika pale na wamekwenda na *message* mbaya sana, nimeandika barua ya kuomba radhi kwenye Balozi za nchi za Ulaya na Marekani kwa sababu tumefanya kitu ambacho si kizuri kwa wageni ambao wala hawahusiki na mzozo ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililozungumziwa ni suala la kifuta jasho na kifuta machozi kwamba ni kidogo na kinachelewa. Niseme tu haraka haraka hizi kanuni tumezianza kuzitumia kwa mara ya kwanza tarehe 24 Aprili ndio tumezisaini. Kweli sehemu nyingi tumezungumza na wananchi, juzi tulikuwa kwa rafiki yangu Mheshimiwa Jerome Bwanausi kule Masasi, wananchi wanalalamika kuwa hazitoshi. *(Makofi)*

Niseme Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa sababu ndio tunaanza kuzitumia na tumeona *reaction* ya *public* tutachukua maoni yenu tutaangalia namna ya kuboresha. Suala la kuwaisha kulipa ni suala la utendaji na kwenye suala hili nimemwambia Mkurugenzi na wananchi nimewaomba sana na niwaombe kupitia Bunge lako Tukufu kwamba pale panapotokea matatizo haya taarifa zifikishwe Wizarani, wakatufikishia Wizarani na taarifa zikiwa zimekamilika ndani ya mwezi mmoja yaani siku 30 madai yale yawe yamelipwa. Nimemwomba Naibu Katibu Mkuu alisimamie suala hili kwa ukamilifu na pale ambapo watu watakuwa wanachelewa kulipwa bila sababu za msingi tuweze kuchukua hatua. Kwa hiyo, suala la ucheleweshaji tunalisimamia vizuri na suala la kuboresha *rate* tutaliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine limezungumzwa kwa kirefu sana, suala la Ngorongoro. Suala la Ngorongoro lina mambo mengi, mimi nilikwenda kule baada ya kuwa nimesikia kwenye vyombo vya habari kwamba kuna tatizo kubwa sana la njaa. Nimezungumza na wale wananchi, kikubwa ambacho nakiona pale kwa kweli wale wananchi dhahiri wanaonekana kabisa kwamba hawaridhiki na mchango ambao Ngorongoro inafanya, Ngorongoro imeelekeza kisheria kwamba iwaendeleze wale watu, wala sio iwape kipaumbele iwaendeleze. Kama inavyohangaika kuendeleza utalii, kama inavyohangaika kumlinda faru inahangaika na maendeleo ya hawa watu. Haiwezekani hawa watu ambao umeagiza kisheria uwaendeleze, wanakaa na njaa karibu wiki mbili, mahindi yako kwenye ma-*godown* tumekwenda, tumekuta mahindi yapo kwenye ma-*godown* watu wana njaa karibu ya kufa, nikasema hamuwezi mkafanya hivyo milioni 48 za kusambaza mahindi mmekosa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, vitu vya namna hiyo nimewaambia kwamba ni lazima warudi kwenye sheria, walisimamie jambo hilo, ili waweze kulifanya jambo hilo kwa ukamilifu wawe karibu na wananchi. Nikasema safari za nje zifanyike pale ambapo ni watendaji wanakwenda kufanya kazi husika, haiwezekani kuna wakati nilikwenda kwenye maonyesho Madrid, tumekwenda na watu kule lugha zinazozungumzwa lugha ya Kifaransa na Kiespaniora, tumekwenda na watu wanazungumza Kiswahili na Kiingereza na ni msafara wa watu watano kwa sababu tu amefikiwa zamu ya kwenda kwa sababu safari imekuwa ni ulaji, mimi nikasema hapana, ni lazima tupeleke watu wanaokwenda kufanya kazi. Pale ambapo hakuna sababu za kufanya hivyo tusifanye na ndio nilichokifanya Ngorongoro. Najua wananuna lakini naomba sana tunafanya hayo kwa nia njema sana ili wale watu ambao kweli tunawafanyia kazi waone kwamba tunafanya kazi zinazopaswa kufanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la usimamizi kwa maana ya Bodi, *serious allegations* zimekuwa *raised.* Mimi nimekuwa ninaomba kwanza kwa sababu tuliyemzungumzia ni mtu ambaye kwa kweli hana nafasi ya kufika hapa na kujitetea au kueleza. Sisi ambacho tumekiona kwenye Serikali na tumezungumza na Mkuu wangu Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa kwamba tuunde Tume ya Msingi ya kwenda kuchunguza ni matendo gani ambayo yanafanyika kwenye eneo hilo, baada ya kazi hiyo kukamilika tutachukua hatua. Niwahakikishie tu na waandishi wa habari nilipoteuliwa kuwa Waziri waliniuliza Maige tunakuona mdogo, unachekacheka nikawaambia subirini miaka miwili *unless* pasiwepo sheria, tukigundua kwamba kuna matatizo tutachukua hatua. Kwa hiyo, hilo nawaomba msiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Suala la kujenga hoteli kwenye mapito ya faru tulipata taarifa hizo na niwaambie tu kwa kifupi kwamba jambo hilo tulishalizuia na nilishapata barua ya Mhifadhi *(Conservator)* akiwaandikia wale waliokuwa wamepangiwa kujengewa hoteli kwenye eneo lile au amekuwa *allocated* hilo eneo kwamba wanajengewa watatafutiwa maeneo mengine. Kwa hiyo, kama ambavyo Mheshimiwa Kaika Telele mngekuwa hamuibi ng'ombe Shinyanga ingekuwa vizuri zaidi. Kama ambavyo amesema mtani wangu Telele kwamba hoteli haitajengwa kwenye mapito ya faru na mimi nalihakikishie Bunge hili kwamba hoteli hii haitajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la utangazaji wa utalii yameelezwa mengi, lakini niseme tu kwamba moja ya changamoto kubwa tuliyonayo ni fedha. *TTB* ambacho ni chombo cha kutangaza utalii kinapata fedha kutoka Hazina na kinapata shilingi bilioni nne kwa mwaka tena ndio kiwango cha juu ambacho kinajumlisha mambo ya mishahara na kila kitu. Fedha zinazotumika kwa ajili ya utangazaji wa utalii kuweka matangazo sijui kwenye mpira wa *Premium League* na nini ni chini ya asilimia 35 ya fedha zote ambazo zinakuwa wamepangia, *I mean* chini ya asilimia 35 ya fedha zote walizokuwa wamepangiwa.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi *by far* ndogo huwezi ukalinganisha na wenzetu Kenya, wenzetu Kenya wanazungumzia sisi tuna *about 4 billion shllings* wao wana *about 16 billion dollars.* Afrika ya Kusini wana *about 70 millions dollars* kwa mwaka kwa ajili ya kutangaza utalii ambao kwenye ukanda wetu wao tuna mazingira ya kufafanana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika mazingira hayo nikasema ni vizuri tutafute mbinu za kuhakikisha kwamba tunatangaza *effectively* ndio tukasema kwamba haiwezekani kwamba eti hawa jamaa kwa sababu wana Bajeti kubwa na wana uwezo wa kukusanya sasa wawe wanaenda kwa zamu hata mlinzi aende kutangaza utalii kwa sababu amefikia zamu na kwa sababu safari ndio mtaji wa kupata fedha, tutafute namna ya kutumia fedha hizi vizuri. Ngorongoro waende, lakini waende wataalam na wanaopaswa kufanya kazi hiyo na washiriki kwenye maonesho mengi zaidi iwezekanavyo waende watu wa *TTB,* ndiyo hoja aliyoisema kaka yangu Chifu Lembeli pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hofu tumezungumzia kwamba *TANAPA* watawanyang'anya fedha wasiende kutangaza utalii, hapana. Tumesema kwamba tuwe na *Joint Tourism Promotion Plan* ambayo itawahusisha *TANAPA,* Ngorongoro lakini atakayekuwa anaongoza kufanya kazi hiyo ni mtu wa *TTB.* Kwa hiyo, pamoja na kuomba fedha lakini nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba tutajitahidi kuwa *effective* na kutumia rasilimali tunazozipata vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi sana ni suala la migogoro ya mipaka. Watu wameongezeka, hifadhi zipo, mipaka haiko wazi, tuna migogoro mingi kwenye maeneo mengi. Kwa kifupi sana niseme ifuatavyo; la kwanza niwape pole sana wananchi wa Urambo, nimemsikiliza sana Dada yangu Mheshimiwa Sakaya.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa sana nimesikitika mno. Tumeongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba jambo hili nalo kama lilivyo la Ngorongoro kama ulivyoomba Dada Sakaya chini ya maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tutaunda timu ya watu kwenda kuangalia *independently* na kwa sababu suala hilo linahusu Wilaya nzima maana yake tunahitaji kuchukua watu nje ya Maliasili na nje ya TAMISEMI kwa maana ya uongozi wa Wilaya pale ili tuweze kwenda kuangalia ni kwa kiasi gani jambo hili limefanyika. Kwa sababu kuwatoa watu kwenye hifadhi ni jambo la kawaida kiutaratibu na sehemu zingine operesheni zilifanyika, lakini si kiwango cha Urambo ambacho tumeelezwa leo hii.

Mheshimiwa Spika, niseme tu Tume ile itakapomaliza kazi yake itatusaidia kuweza kufanya maamuzi na moja ya maamuzi ya msingi kuhusu namna ya kutumia ile ardhi kwa pamoja, lakini la pili kuhusu hatua stahiki za kinidhamu ambazo zitaweza kuchukuliwa kwa watu ambao wamefanya mambo hayo ambayo kwenye Sheria yoyote, Sheria ya Maliasili, Sheria yoyote ile inayosema kwamba uchome nyumba na mahindi na mazao mengine ya Mtanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, jambo hilo hatutaliruhusu, tutachukua hatua na tutakufahamisha jinsi hatua zinavyokwenda. Kwa maeneo mengine, niseme tu kwamba tulishaanza kufanya ukaguzi kwa maana tulishaanza kuangalia mazingira ya mipaka nchi nzima. Tabora tulishapata taarifa yake, niombe tu kwamba kwa mwaka huu wa fedha tulioanza na ambao ndiyo naombea fedha leo, suala hili tutalifanya kwa nchi nzima kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Ardhi ili tuangalie na kwenye maeneo yaliyo mengi tumekubaliana kuangalia yale maeneo ambayo *seriously* yanahitajika kiuhifadhi, tutazungumza na wananchi tuwaeleze ni kwa kiasi gani ni ya muhimu. Kwa maeneo mengine ambayo kwa namna moja au nyingine yanayoweza yakaonekana kwamba si ya lazima kiasi hicho kwa uhifadhi, tutazungumza nao, tutafanya utaratibu wa kurekebisha mipaka

ili kuondoa migogoro hii *once and for all.* Kwa hiyo, naomba niliahidi Bunge lako Tukufu kwamba katika kipindi hiki ambacho kinaanza baada ya bajeti hii kupitishwa tutaweza kuyarekebisha hayo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie suala moja ya Mufindi kabla sijaanza yale mengine ambayo ni *specific areas*. Suala la Mufindi na malighafi, ni kweli kwamba kuna matatizo ya namna malighafi hii inavyogawanywa. Ni kweli kwenye mwongozo tumesema kwamba wananchi wanaoishi vijiji jirani na eneo waweze kupata namna fulani ya kunufaika. Hatujawa *very clear* kama tutoe fedha za kuwachangia kwenye miradi yao ya maendeleo au tuwachingie mbao au namna gani lakini kwa kiasi kikubwa tumekuwa tukitoa vibali vya kuvuna. Kosa ambalo tumekuwa tukilifanya ni kwamba tumekuwa tukitoa vibali kwa maombi yanayoandikwa na mtu. Kwa hiyo, mtu yupo Tabora lakini anaandika Francis Mayala, S.L.P. 14 Njombe, S.L.P. 276 Iringa, ili aonekane ni wa eneo jirani kwa sababu jambo hili kwamba wananchi wa jirani wana nafasi zaidi linajulikana. Kwa hiyo, inawezekana wapo watu ambao hawaishi kwenye maeneo yale wanatumia majina na anuani za maeneo yale, tutaimarisha eneo hilo ili kuhakikisha kweli tunaowalenga kuwanufaisha au kuwapa kupaumbele, kipaumbele hicho wanakipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe ushauri wa Bunge lako Tukufu, Waheshimiwa Wabunge wameomba wawe wajumbe wa Kamati hizi za uvunaji, lakini nina tatizo kubwa moja kwamba Wabunge walio wengi na wenyewe wanaomba kuvuna, sasa tukiwaweka kwenye Kamati sijui itakuwaje. Kwa hiyo, nataka hili jambo tuliache kwa ajili ya mjadala lakini sisi tumekuwa tukiona ni haki yake Mbunge kwa niaba ya wananchi wake, anataka labda asaidie madawati, amepewa *CDCF* na kuna Wabunge wenzangu wengi tu hapa wameongea na Magereza kwamba watawasaidia ku-*process* zile mbao na kutengeneza madawati, anaomba kuvuna na anaruhusiwa kama Mtanzania na kama kiongozi tena anapewa heshima zaidi. Ama tusiwape Wabunge wa jirani pale kama anataka kuchangia kwenye madawati ili wawe wajumbe wa Kamati au wasiwe wajumbe wa Kamati ili pale wanapohitaji na wenyewe kuchangia mbao iweze kuwezekana. Ni suala la *conflict of interest*. Kwa hiyo, hili suala sisi hatuna tatizo tutaangalia namna ya kufanya na kweli tumesema kwenye mwaka huu wa fedha tutaliangalia eneo hili. Kwa kifupi hili eneo kwa sababu linahitaji mjadala tutakaa na Waheshimiwa Wabunge na viongozi wengine wa maeneo haya tuweze kushauriana njia nzuri zaidi ya kulifanya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa maslahi ya muda, nizungumzie kwa harakaharaka mambo yafuatayo:-

Moja, kuna suala la mgogoro wa *MPM* kutoza kiasi kidogo. Tatizo lililokuwepo ni kwamba kiwanda hiki kilikuwa ni cha Serikali kikabinafsishwa, wakaingia mkataba kwamba watakuwa wananunua si mbao hasa, sanasana ni yale maotea ambayo watakuwa wana-*prune.* Nimeambiwa kwamba wametoka kwenye kukata maotea sasa wanakata kabisa magogo na ndiyo maana bei yao imekuwa iko chini na jambo hili wala haliko hapa lipo hata sehemu zingine. Kwa hiyo, tumeshakubaliana kwenye mwaka huu wa fedha kwamba malighafi ambayo itakuwa inatolewa kwenye maeneo yote itakuwa na bei moja. Kwa hiyo, suala hili tutalirekebisha lakini dhana iliyokuwepo ilikuwa ni ya kuangalia kwamba wao wanahitaji *material* kwa ajili ya kutengeneza vitu vingine ambavyo vinahitaji vimiti vidogovidogo.

Mheshimiwa Spika, limezungumziwa suala la *TFS* kwamba kuanzisha Wakala wa Misitu unaweza ukaathiri misitu. Jambo hili lilikuwa ni miongoni mwa sababu zilizotuchelewesha kuanzisha *TFS* lakini sababu ya msingi ya kuanzisha Wakala wa Misitu *(TFS)* ni suala la kuhakikisha kwamba kadri itakavyowezakana fedha zinazokusanywa kwenye sekta hii zinatumika kuendeleza sekta hii. Sekta ya misitu inakusanya shilingi bilioni 38, mkipeleka Hazina zinarudishwa shilingi bilioni nane au tisa. Hamwezi kuendeleza yale mashamba ndiyo maana tukaanzisha *LMDA* ambayo ndiyo imesaidia kupanda miti. Ukiangalia mashamba mengi miti iliyopo ni michanga imepandwa katika miaka miwili au mitatu iliyopita kwa sababu vipaumbele vya Serikali ni kwamba fedha zikishakusanywa zinaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, inakuwa si rahisi kurudi kwenye eneo ambalo imetoka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tukaona kwamba ni vizuri tuanzishe wakala ambao utakuwa unakusanya kama wanavyofanya *TANAPA*, kama wanavyofanya Ngorongoro, Ngorongoro

hawajamaliza wanyama, *TANAPA* hawajamaliza wanyama na *TFS* hawatamaliza misitu. Watavuna kwenye mashamba, watakuwa kwenye *harvest plans* na kuangalia miti itakavyokuwa inakuwa na watakuwa wanasimamia hivyo. Kuna uzoefu nchi nyingi zimeanzisha Wakala wa Misitu na zimefanya vizuri sana, baada ya miaka mitatu, minne nakuhakikishia hatutakuwa na uharibifu wa misitu kiasi hiki. Unasikia kabisa kwamba kuna maeneo kama Kilindi watu wanafyeka misitu *left and right,* Askari au Idara ya Misitu hakuna chochote wanachoweza kufanya. Mna-*District Forest* mmoja ambaye kazi yake ni kugawa vibali basi lakini hana uwezo wa kufanya *patrol* kwenye maeneo yote. Kwa hiyo, tumesema kupitia *TFS* tutaajiri *Forest Rangers,* tutawanunulia pikipiki, watakuwa wanafanya doria katika misitu na watakuwa wanapanda miti, sekta itaimarika na changamoto tulizonazo zitaweza kupungua.

Mheshimiwa Spika, haya ambayo sitayatolea ufafanuzi, yasije yakanibana kwenye vifungu, nitawapatia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililozungumzwa ni uboreshaji wa huduma kwenye sekta ya utalii kwamba huduma kwenye sekta ya utalii sio bora lakini pia hata utalii wa Mlima Kilimanjaro kuna matatizo, ameeleza sana Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Tulichokubaliana ni kwamba tuna Sheria mpya ya Utalii ya mwaka 2008. Sheria hii inaelekeza nini kifanyike. Moja, inasema *hotel* ziwekwe kwenye madaraja, wataalam au watumishi wanaofanya kazi kwenye sekta hii wafundishwe na ndiyo maana tuna Chuo cha Utalii na tuna *campus* mpya ya Dar es Salaam ambayo itaongeza udahili wa wakufunzi kwenye eneo hilo ili waweze kutoa elimu zilizo bora. Pia kwa Sheria, *hotel* tutaziweka kwenye *grades* na tutasimamia ubora wake.

Mheshimiwa Spika, kwa *hotel* ama huduma zinazotolewa kwa watalii hasa kwa upande wa mlima, tumezungumza na *KINAPA,* kwa kifupi sana kwa sababu ya muda na wamesema kulikuwa na suala la kuwa wanaruhusu *camping* kule kwenye *crater*. Niliongea na Mheshimiwa Owenya, tumesema jambo hilo tutaliangalia. Kuna sababu za msingi za kusimamisha. Faida ya fedha tunayoipata ni kidogo kuliko hasara ambayo tunaipata. Kwa hiyo, kwa kutumia *KINAPA*, tutaimarisha huduma kwa ujumla kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, nimalizie kwa kifupi sana suala la *WMA* ya Ipole lililotolewa na kaka yangu Mheshimiwa Said Mkumba. Tumekubaliana na nimeshatoa maelekezo kwa wenzangu kwamba utengenezwe Mkataba wa Makubaliano (*MoU*) kati ya *WMA* na watu wa misitu ili *WMA* iwepo, isipokuwa utumiaji wa mazao ya misitu yaliyoko kwenye hiyo *WMA* usimamiwe na Idara ya Misitu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba muda kwa kweli haupo kabisa upande wangu, naomba hoja zote ambazo sijakamilisha kuzijibu, niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba tutazijibu kwa maandishi na wote tutawapatia na kwenye vifungu pale ambapo mnaona kabisa kwamba huyu bwana anaweza akawa hana jibu mkononi basi mlione hilo kwamba ni vizuri mkasubiri lile jibu la maandishi ambalo tutakuwa tumeji-*commit* zaidi pamoja na kwamba kwenye vifungu tutaji-*commit.*

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi na kama nilivyowasilisha hoja jana asubuhi ya kuomba fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mambo ambayo tumeyaombea fedha hapa au tumeyakusudia basi niombe Bunge lako Tukufu liweze kuidhinisha bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hii imeungwa mkono. Kuna *addendum* iligawiwa kipindi kama cha wiki mbili zilizopita kwa sababu mkiangalia *Development Budget* ya Wizara hii, katika Kitabu cha Nne, kuna *zero allocation.* Sasa *addendum* iliyogawiwa, inaonyesha kwamba hawa wamekuwa *allocated* shilingi milioni 107,620,000/-. Sasa kama mngekuwa nayo mngeona maeneo gani yamekuwa *allocated*. Kwa hiyo, kuna hiyo *addendum*. Katibu!

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kif. 1001 *Administration and General* ……….. Tshs 4,030,946,000/=

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge wengi walisimama ili kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri)*

**MWENYEKITI:** Kwanza hela yenyewe mkiangalia ni kidogo, nyie wote mnasimama. Haya, tunaanza na Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ili niweze kupata ufafanuzi kidogo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa kuzungumza, nilizungumzia sana kuhusu hali mbaya ya huduma mbalimbali katika Mlima Kilimanjaro, hususan suala la uchafuzi wa mazingira unaoambatana na kukosekana kwa huduma mbalimbali muhimu kama huduma za vyoo, mabwalo ya kulia, pamoja na mapendekezo kadhaa ambayo nilitoa ya kupunguza tatizo la uzito wa mizigo inayopanda Mlimani. Wakati huohuo nilizungumzia umuhimu wa kushirikisha Wilaya zinazozunguka Mlima Kilimanjaro kwa sababu zinahudumia Mlima huu na ni urithi muhimu kwa Taifa ili nazo ziweze kufaidika kwa njia moja au nyingine kwa kuanzisha *Council Tax* ambazo hazitaiumiza *TANAPA* wala *KINAPA* lakini itaweza kutoa mchango kwa wale wananchi wanaozunguka mlima. Mheshimiwa Waziri ningefurahi sana pamoja na haja ya kupeleka kwa maandishi, ungeweza kutoa kauli tukaweza kuelewa tumesimamia wapi. Ahsante.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwenye maeneo mawili ambayo Mheshimiwa Mbowe ameulizia. La kwanza ni kuhusu huduma za msingi za kibinadamu kwa watalii wanaopanda Mlima Kilimanjaro. Suala hili tumezungumza na *KINAPA*, wamesema kwa mwaka huu wa fedha wamepanga kujenga huduma au kujenga vyoo kwenye maeneo mengi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutumia utaratibu wa ku-*airlift* mizigo ya wageni kwenda Mlimani, wamesema linahitaji utaratibu kwa kuangalia athari zake. Wao wanachohofia ni suala la ajira. Kama nilivyowahi kujibu swali hapa Bungeni kwamba kuna vijana wengi sana wanaofanya kazi ya kubeba mizigo *(Porters)* na wamekuwa wakipewa fedha nyingi, kwa mwaka mzima wanapewa zaidi ya shilingi milioni 700 kwa ajili ya kufanya tu hiyo kazi. Sasa wakasema kwamba hebu jaribu kumshauri Mheshimiwa Mbunge, kwanza tutaangalia, uwezekano wa kufanya hivyo upo, lakini tuangalie athari inayoweza kutokea kwenye ajira. Kwa hiyo, wakawa wamefikiria na mimi ninafikiria kwamba pengine ni jambo jema tuangalie tu uwezekano wa kuboresha huduma kwenye maeneo mengi zaidi kwa maana ya kujenga vyoo vingi zaidi kila baada ya umbali mfupi kabla ya kufikiria kwamba tuwaondoe hawa vijana kwenye ajira, kwa sababu kwa kufanya hivyo kwa kweli tutakuwa tunapata shida kwenye Ilani ya CCM ambayo imesema vijana waweze kupatiwa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Halmashauri, tulishazungumza na Mheshimiwa na tulishaanza kufanya mazungumzo na hata kwenye hotuba yetu tumesema kwamba tutaanza mchakato na Halmashauri za Wilaya zinazozunguka Mlima Kilimanjaro ili zianzishe *Council Tax* kwa ajili ya kuongeza mapato. Jambo hili sisi hatuna tatizo nalo. *Concern* yetu na ushauri wetu ni kuhakikisha kwamba tunashirikishwa vizuri ili tusiwe na tozo nyingi kwa wageni zinazoongeza gharama ya wageni kwenda kule Mlimani. Kwa hiyo, tutazungumza *applicable* au *acceptable rate* na namna nzuri ya kukusanya. Kwa hiyo, jambo hili hatuna matatizo nalo kama Wizara, tutafanya kazi na Waheshimiwa Wabunge na viongozi wengine wa Halmashauri za Mlima huo ili kuweza kuhakikisha kwamba tunakuwa na tozo hiyo.

**MHE. MAGADLENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru Serikali kwa tamko iliyotoa hapa kwamba itaunda Tume kwa ajili ya kushughulikia matatizo sugu ya Wilaya ya Urambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napoongea sasa hivi, wananchi wa Kijiji cha Shela, Kitongoji cha Lugaju Mtoni, hawana mahali pa kukaa, hawana chakula kwa sababu vyakula vyao vyote vimechomwa. Naomba Serikali itoe tamko hapa kwa hatua za haraka ili wananchi hao waweze kuishi, kwa sasa hivi Serikali inawasaidiaje? Nashukuru sana.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo, nirudie tu tena kutoa pole sana kwa Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Urambo. Nilisahau kulieleza hili wakati najibu hoja yake pale, ni kwamba, tumezungumza na Mkuu wa Mkoa, tumezungumza pia na *RPC*, tumewaambia kwamba wahakikishe huduma za msingi za kibinadamu kwa waathirika wote zinatolewa na tukawa tumekubaliana kwamba hatua za haraka zitachukuliwa kuanzia sasa hivi. Naamini kwamba kama siyo yeye, watu wake watakuwa sasa hivi wako kwenye mawasiliano na uongozi wa Wilaya kuhakikisha kwamba huduma za msingi kwa watu hao zinatolewa. *(Makofi)*

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru…

*(Hapa Microphone ilipiga Kelele*)

**MWENYEKITI:** Hama hiyo mashine!

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa maliasili imepanua mipaka yake katika maeneo ya Hifadhi ya *TANAPA* katika Wilaya ya Kondoa katika Kijiji cha Kikeikei, Kisondoko na Chubi na wananchi wale sasa hawana tena maeneo ya kuweza kulima, wamenyang'anywa mazao yao na wamepigwa na kunyanyaswa. Mheshimiwa Waziri, naomba wananchi wale waweze kupatiwa ufumbuzi wa uhakika wa mipaka na migogoro ya eneo lile na *TANAPA* pamoja na wakulima ili waweze kuachiwa eneo lile na kuweza kulima kwani ni eneo lao ambalo wamekuwa wakilima kwa siku zote. Mheshimiwa Waziri, naomba utoe tamko hilo ili wananchi wale wapate unafuu wa maisha na wapate chakula katika eneo hilo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Moza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye majibu wakati najibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwenye hili eneo la migogoro ya mipaka, ni kwamba tumepanga kwenye mwaka huu wa fedha tunaoanza kwamba tutapitia mipaka ya maeneo yote na kukubaliana *in principle* na wananchi kwamba mipaka iwe katika sura ipi. Kwenye maeneo yaliyo mengi, mipaka imewekwa muda mrefu sana wakati wa kuanzisha hizi hifadhi zilizoanzishwa siku nyingi na watu wameingia au kuweka makazi na kwa sababu mipaka haikuwa bayana, kwa hiyo inaleta shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niseme tu kwamba Wilaya ya Kondoa, *TANAPA* hawana hifadhi kwa maana ya *TANAPA*. *TANAPA* wana Hifadhi ya Tarangire ambayo iko Simanjiro pamoja na zingine za Serengeti ambazo ziko mbali. Hifadhi yetu pale ni ya Mkungunero ambayo iko chini ya Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori, kwa hiyo ni hifadhi ya wanyamapori. Kwa hiyo, nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge mwenzangu kwamba katika mkakati wetu wa kutatua matatizo ya mpaka kwenye maeneo mengi ya nchi iwezekanavyo, itakuwa ni pamoja na Kondoa katika kushughulikia tatizo hili.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa nami niulize swali moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunapozungumza, Wilaya ya Kasulu hususan katika mapori ambayo yapo katika Vijiji kama vya Mgombe pamoja na Kagerankanda, wananchi wa kule ikiwa ni pamoja na wakazi wa Kasulu Mjini, tatizo moja la mipaka na maeneo yanayodaiwa kwamba ni hifadhi sasa na eneo hilo limekuwa ni mtambuka hasa kwa shughuli za kilimo na chakula kingi kwa Mkoa wa Kigoma na ambacho ziada huuzwa katika Mikoa Mingine, kinatoka katika eneo hilo na eneo hilo limekuwa likilimwa na wananchi wa Wilaya ya Kasulu kwa zaidi ya miaka 20 iliyopita, leo limetolewa tangazo kwamba watu wale waweze kuondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakumbuka kwamba wakati wa kampeni zipo taarifa na zilikuwepo taarifa, aliyekuwa mgombea wa Ubunge wa Jimbo la Kasulu Vijijini wa Chama cha Mapinduzi ambaye leo hii ni mmoja wa wajumbe ambao uliwateua wanakushauri wewe Mheshimiwa Waziri, Bwana Daniel Nsanzugwanko, aliwahi kusema "mkimchagua Mbunge wa Upinzani, hamtalima katika eneo hilo". Tumeshuhudia siku chache baada tu ya uchaguzi kwisha, wananchi wanafukuzwa kulima katika eneo lile. Hii ni ishara kabisa kwamba kuna siasa ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaona kwamba katika eneo lile, Bwana Daniel Nsanzugwanko hataweza kumshauri vizuri Waziri na wananchi tayari wana *negative attitude* na Bwana Daniel Nsanzugwanko. Sasa kwa maslahi ya wananchi wa Wilaya ya Kasulu, naomba atoe ufafanuzi, ni lini mgogoro uliopo leo hii utashughulikiwa kwa sababu hawaelewi kwamba msimu wa kilimo ukifika kama wataendelea kulima au wataondolewa kama ambavyo tayari Serikali imeshaonyesha dhamira ya kutaka kuwafukuza wakulima wale ambao uchumi wao na maisha yao wanategemea eneo lile. Naomba kauli ya Serikali kama wananchi wale wataendelea kulima au hawataendelea kulima na kama hawataendelea kulima, nini mbadala wao? Ahsante.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufafanua kwenye hili eneo la mpaka kama alivyouliza Mheshimiwa rafiki yangu Machali. Ni kwamba tatizo la mpaka ni kweli lipo na ni tatizo halisi lakini kuna suala lingine la siasa kama alivyolisema. Mimi niseme tu kwamba kinachozingatiwa hapa ni Sheria. Kuna mgongano wa Sheria kwenye maeneo kadhaa, mengi tu. Kuna maeneo ambayo Vijiji vimeanzishwa kwenye hifadhi, kuna maeneo ambayo mashamba yameanzishwa kwenye hifadhi na kadhalika. Ndiyo maana nimesema zoezi la kupitia upya mikapa ni la nchi nzima. Tutakuwa na wenzetu wa Wizira ya Ardhi lakini pia tutafanya kazi na wenzetu wa Wizara ya TAMISEMI kuhakikisha kwamba tunakuwa na mipaka iliyo bayana na inayokubalika kitaalam na pande zote tatu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la kwamba wataondolewa au kutoondolewa baada ya uchaguzi au wakimchagua mtu wa upinzani, mimi niseme tu kwamba, kwenye kampeni unajua Mheshimiwa Machali ambavyo tunachachamaa, tunasema vitu vingi sana. Yawezekana hayo yalisemwa lakini mimi niseme tu kwamba kilichoko kwa sasa na tunachokifanya wakati wote ni kutekeleza Sheria. Hawa watu hawawezi wakawepo au wasiwepo kwa sababu ya Nsanzugwanko au kwa sababu ya mtu yeyote. Ni sheria inayowaruhusu wawepo na ni Sheria inayowataka waondoke kama wanapaswa kuondoka. Kwa hiyo, naomba tu Mheshimiwa Mbunge mwenzangu kwamba haya makombora haya ya kisiasa, mimi nafikiri yalikuwa ya wakati ule na nafikiri hata yeye mwenyewe anajua. Kwa hiyo, hili suala la kwamba *element* ya huyo Mheshimiwa kuwepo pale inaweza kuleta shida, nafikiri lisiwe jambo la kutia hofu sana. Tutazungumza, tutatumia timu hiihii ambayo tutaiunda na naamini kabisa tutapata ufumbuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Buyogera, mradi usirudie hili lililosemwa labda uulize lingine.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mimi langu ni dogo. Kwa kuwa nimeshamwandikia barua Mheshimiwa Waziri, naomba anitamkie, baada ya Bunge yuko tayari kuja Kasulu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya! Waziri majibu! Naona yuko tayari! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana dada yangu Buyogera kwa mwaliko. Ameshaniandikia, tumeshazungumza na sasa amesema. Nimhakikishie tu kwamba nia yangu kwa kweli ni kufanya ziara kwenye maeneo mengi

iwezekanavyo kwa sababu matatizo haya ya mipaka na migogoro yako maeneo mengi kwelikweli. Nitajitahidi kwa kadri itakavyowezekana. Hili nasema siyo kwa sababu ya kwenda Kasulu peke yake, Kasulu nitakwenda lakini naomba nisiji-*commit* kwamba *immediately* baada ya Bunge. Hata maeneo mengine ambayo nitachelewa kwenda, wenzangu katika Wizara nitawaomba na nitawatuma waweze kutangulia kwa yale maeneo ambayo yanahitaji kutembelewa na kuchukuliwa hatua za haraka. Kwa hiyo, kwa mwaliko wake nitampa kipaumbele kuhakikisha kwamba tunakwenda pamoja...

**MWENYEKITI:** Jamani, kubali tu, acha maneno mengi. Si unaenda tu, sasa maneno yote ya kazi gani?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru...

**MWENYEKITI:** Tunasema useme utakwenda tu! Tuokolee muda.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Dkt. Mrema! Waswahili Bwana! *(Kicheko)*

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuuliza swali la msingi kuhusu vijana wa Kilimanjaro wanavyonufaika na biashara ya utalii. Waziri alinijibu kwamba manufaa yapo, kuna *Guide* 400 ambapo mwaka jana walipata shilingi bilioni 1.9, Wapagazi 10,000 wamelipwa shilingi bilioni 4.8 kwa mwaka na Wapishi 500 wamepata shilingi milioni 578 lakini ukiangalia utaratibu wa kuwalipa, *Guide* alipwe Dola 20, mpishi alipwe Dola 15, Mbeba Mizigo alipwe Dola 10, nimejaribu kufanya hesabu na watalaam ikaonekana hao ma-*Guide,* Wapagazi na Wapishi hawalipwi hiki kiwango ambacho kimewekwa. Ni nani anasimamia hawa *Tour Guides* kuhakikisha kwamba hawa ma-*Guide* wanalipwa Dola 20 kama ilivyoandikwa, Wapishi wanalipwa Dola 15, Wabeba Mizigo wanapewa Dola 10? Taarifa tulizonazo ni kwamba wale wananyonywa na kwa sababu ya umaskini wao wanakubali kuajiriwa kwa malipo madogo. Sasa una-*enforce* vipi hii Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi alioomba Mheshimiwa Dkt. Augustino Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri tu kwamba tatizo la malipo ya Wapagazi limekuwa ni kilio cha muda mrefu, limewahi kuulizwa swali hapa mara mbili, mara tatu na hata Mheshimiwa Mbowe amewahi kuuliza. Kwenye majibu yetu tumekuwa tukirejea kwenye Sheria. Tunasema kwamba Sheria za nchi ndizo zinapaswa zifuatwe. Hawa ni wafanyakazi kama walivyo wafanyakazi wengine. Sheria ya Mahusiano Kazini inawalinda. Wana Chama chao cha wafanyakazi kinaitwa CHODAWU (Chama cha Wafanyakazi wa Majumbani, Mahotelini na Sekta isiyo Rasmi). Hawa viongozi wa Chama hiki pamoja na viongozi wa Chama kidogo ambacho watakuwa nacho zaidi ya Chama hiki ambacho ni cha Kisheria, ndiyo wanaopaswa kusimamia kuhakikisha kwamba haya ambayo tumekubaliana yanatekelezwa. Kwetu kama Wizara tunatoa kama bei elekezi kwamba kwa kuangalia mazingira haya pamoja na kwamba *minimum pay* inaweza ikawa iko chini zaidi, lakini walipwe vizuri zaidi ili wawahudumie wageni wetu vizuri zaidi kwa sababu ni sekta ambayo ni *sensitive*. Kwa hiyo, tunashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Kazi na nilishaongea na Mheshimiwa Waziri wa Kazi kuhusu suala hili kwamba wamtume Afisa wa Kazi wa eneo hilo kukaa na hawa *Porters* na hawa *Tour Operators*, kuzungumza nao kuhakikisha kwamba wanawalipa vizuri. Kwa hiyo, tutashirikiana na Wizara ya Kazi kuhakikisha kwamba tunalisimamia jambo hilo.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu na hatua zinazotia matumaini ambazo Waziri amezieleza katika Bunge lako Tukufu ambazo wananchi wa Simanjiro wana matumaini pia ya kutatuliwa tatizo lao la mgogoro na Mkungunero lakini Mheshimiwa Waziri amegusia kwamba zimekuwepo jitihada za pamoja kati ya Wizara na Wizara ya Nishati na Madini katika kushughulikia suala zima la uchimbaji wa Urani katika eneo letu la *Selous*. Sasa kwa kuwa uchimbaji wa *Uranium*, ikichimbwa, kutunzwa, kusafirishwa na kuboreshwa katika mazingira yasiyo salama ni kifo kwa binadamu, viumbe, maji na

mimea yote iliyoko katika eneo hilo. Kwa kuwa Waziri ameeleza kwamba ushirikishwaji wa Kamati ya Nishati na Madini na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira haukuwepo, sasa kwa niaba ya Serikali anaweza kutoa kauli kwamba kabla hawajaendelea na zoezi hilo, Bunge hili lishirikishwe kwa kupitia Kamati hizo mbili ili kuweza kunusuru nchi katika athari zinazoweza kujitokeza kwenye uchimbaji huo wa Urani na hasa ukizingatia kwamba inaweza kuhatarisha usalama wa wanyama katika maeneo hayo na uhifadhi kama mchango wa pamoja hautakuwepo? Nataka *commitment* ya Serikali katika ushirikishwaji. Nakushukuru sana Mwenyekiti! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, tena mjibu kwa kifupi, muda hautoshi, wengine watabakia.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba uchimbaji wa Urani una *International Standards* ambazo lazima ufuate. Sasa kwa hapa Tanzania tuna maeneo hayo mawili, tuna maeneo ya Namtumbo ambapo uchimbaji wake unatarajia kuwa ni *open cast* na uchimbaji wa Manyoni na Bahi ambao ni tofauti na huo bado haujawa *approved*. Uchimbaji ambao unaonekana tunaelekea kuanza ni uchimbaji wa Namtumbo. Uchimbaji huo utafanywa kwa kushirikisha wadau wote na hata leseni hiyo itakapotoka, itabidi washirikishwe watu wa Tanzania *Atomic Energy* ambao wao ndiyo wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchimbaji wenyewe kuna hatua za kwanza za uchimbaji kama alivyosema Waziri wakati akijibu hoja na hatua za pili ambazo ni za kurutubisha, hatua ile ndiyo inakuwa ni hatari, hatua ambayo ina *radiation*. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Sheria na Kanuni zote, siyo za Tanzania tu lakini hata za Kimataifa *in the handling and processing of uranium* zitafuatwa katika kufikia huko tunakokwenda.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, pamoja na pongezi ambazo nilimpa Kamanda wa Kikosi cha Wanyamapori cha Manyoni, Askari Mrina, pia nilimwomba Mheshimiwa Waziri kwamba pale Manyoni wale Askari wamefaulu kukamata baiskeli nyingi na mali nyingi, lakini mali hizo karibu zina zaidi ya miaka sita, mpaka sasa hivi hazina maelekezo zifanyweje, hata uwekaji umekuwa mgumu. Sijui ananipa majibu gani ili waweze kuchukua hatua zinazostahili?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo kuhusu vifaa mbalimbali zikiwemo baiskeli ambazo zimekamatwa na zinatunzwa kwenye Kituo chetu cha Kikosi Dhidi ya Ujangili cha Manyoni. Ni kwamba kuna maeneo mengi ambapo tuna vifaa hivi na moja ya zoezi tutakalolifanya kwenye mwaka huu wa fedha ni kuhakikisha kwamba vifaa vyote ambavyo vimekamatwa na havina *encumbrances* tutavi-*dispose*. Kwa hiyo, tunategemea katika kipindi cha sasa hadi mwezi Disemba baada ya bajeti kuwa imepita, utaratibu wa kuuza na hata namna nyingine yoyote ya *disposition* itakayokubalika itafanyika.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika maelezo yangu ya maandishi, niliomba Waziri aweze kufika Mbarali ili wale wananchi ambao walikuwa wanakosa usingizi na baada ya kuonekana yeye, kilio chao sasa kinaweza kikaisha. Je ni lini atafika na wangependa pengine kusikia kauli yake kwamba sasa atakuja Mbarali kwa ajili ya kumaliza mgogoro ambao ulikuwa unawanyima usingizi, naomba tamko la Waziri.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa utaenda tu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa rafiki yangu Kilufi...

**MWENYEKITI:** Aah! Unaenda au huendi, ufafanuzi gani, amesema uende.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kwa sababu nina muda wa kutosha, nitapata *tension* kidogo, nitashindwa kueleza vizuri, nitumie tu muda wangu vizuri…

**MWENYEKITI:** Tuelewane.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Ndiyo!

**MWENYEKITI:** Huyu anasema mlikubaliana kwamba utakwenda kama utaenda ukajibu kulekule, sasa ukitujibia hapa...

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi nitakwenda lakini nilifikiri ni vizuri nikatoa maelezo zaidi.

**MWENYEKITI:** Basi inatosha Mheshimiwa muda hautoshi, utawanyima nafasi wengi sana hapa watalalamika.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba hapa nchini utalii unachangia kwa asilimia 17 au zaidi katika uchumi wa Tanzania na inawezekana kabisa ukapaa zaidi ya hapa hasa kutokana na ari kubwa tunayomuona nayo Waziri ambaye yupo hivi sasa katika suala zima la kusimamia Wizara yake. Changamoto ambayo tumekuwa tukiitoa hapa kila siku ni kwamba pamoja na kwamba asilimia hii ni kubwa, mchango mkubwa umekuwa ukitoka hasa katika Mbuga za Wanyama pamoja na Mlima Kilimanjaro ambazo zipo katika Ukanda wa Kaskazini. Tulitoa changamoto kwamba sasa Wizara ijielekeze katika Ukanda wa Kusini na Nyanda za Juu Kusini ambako kuna Mbuga nyingi, kuna utalii wa kihistoria, kuna *Eco-Tourism* ya kutosha, lakini miundombinu yake ni mibovu kiasi ambacho utalii huu sasa unalegalega. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuendeleza utalii katika Nyanda za Juu Kusini.

**MWENYEKITI:** Swali ndiyo hilo tu basi, Mheshimiwa Waziri tuna dakika arobaini na tano tu na *guillotine* ndani yake.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Hilda Ngoye kama ifuatavyo kwamba kwenye mpango wetu wa kuendeleza utalii, tumegawanya nchi yetu kwenye Kanda, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, tunaratibu eneo hilo kupitia ofisi yetu tutakayoijenga Iringa na kama nilivyosema kwenye hotuba yetu kwamba tutakuwa na Kituo cha *TTB* Iringa, ambacho kitakuwa kina-*promote* eneo hilo lakini pia wadau wengine kama *TANAPA* na wenyewe tutawashirikisha kuboresha maeneo hayo pamoja na kutangaza.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba maelezo kwa Waziri kwamba kipo Kimondo cha Mbozi ambacho nimewahi kuzungumza katika Bunge la Tisa kwamba hakijapewa *tension* ya kutosha, utalaam lakini kutangazwa na hata nyumba ya mtumishi pale haipo. Nilizungumza na Waziri akasema wametenga pesa lakini nimeangalia vitabu vyote sijaona pesa ambazo zinaweza zikapaendeleza mahali pale ili pawe mahali pazuri zaidi pa kujifunza, naomba kupata maelezo ya Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Zambi kwa kifupi. Kwenye mwaka huu wa fedha, tumepanga kuendeleza maeneo matatu ya utalii ya malikale, kuna eneo la Amboni, Kwihara – Tabora pamoja na Mbozi. Eneo hili tutajenga *Information Centre* na kwa maana hiyo litakuwa tayari kwa kutangazwa. Tumekuwa hatutangazi kwa sababu lilikuwa halijawekwa katika mazingira ya kuweza kutangazwa. Kwa hiyo, kuanzia mwaka huu wa fedha tutaanza kulitangaza.

**MHE. DKT. BILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilielezea matatizo ya mipaka kwenye pori la Mpanga -Kipengere na Hifadhi ya Kitulo, Waziri ameelezea vizuri kwamba watakaa na wananchi na watapitia upya mipaka, kwa hiyo, naamini kwamba limekaa vizuri, nampongeza lakini hajagusia fidia za wale wananchi wa Kata za Mfumbi kwenye Vijiji vya Usalimwani, Ikogho na Kimani ambao walipunjwa malipo yao na hajajibu kwamba ni lini atakwenda kukaa na wananchi wale awaeleze malipo haya yatafanyika lini?

**MWENYEKITI:** Ahsante, hata akilipa ni lazima aje? Waziri naomba ujibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Dokta Mahenge, Mbunge wa Makete kuhusu suala la mapunjo ya fidia pamoja na kuzungumza na wananchi kuhusu mgogoro. Ni bahati mbaya tu muda haukuruhusu lakini moja ya mambo ambayo tunayakusudia katika kutatua migogoro hii ni pamoja na kulipa gharama zozote ambazo zinahusiana na madai yanayoendana na eneo hili. Kwa hiyo, katika mwaka wa fedha ambao tunauombea fedha, jambo hili tutalifanya, nitatuma watalaamu wangu kwenda huko na kama alivyoomba na mimi mwenyewe nitakapopata muda kutegemea na ratiba itakayokuwepo kwa sababu nina maeneo mengi ya kutembelea nitakwenda lakini naomba tu nisiji-*commit* kwamba nitaenda *specifically* lini.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimuulize swali Waziri. Kwa kuwa wanyamapori wamekuwa tishio kwa Jimbo la Nkenge na ukizingatia sasa tunaelekea msimu wa Kilimo na ukiangalia katika ofisi yake kuna Afisa Wanyamapori mmoja tu, hana bunduki wala risasi, Waziri anawaambia nini wananchi wa Nkenge ukizingatia sasa wanakwenda kuanza kulima na hali ya hewa siyo nzuri, mavuno ni machache na robo tatu yote inaondoka na wanyama wanabaki kulia. Naomba awaeleze ni nini kinakwenda kutokea katika msimu huu.

**MWENYEKITI:** Haya upungufu wa Maafisa Wanyamapori na vifaa vyao.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Assumpter Mshama kama ifuatavyo:-

Wizara imekuwa ikisaidia *District Game Officers* kwa kuwapatia *contribution* ya fedha kwa ajili ya kununua risasi kama ambavyo Mheshimiwa ameomba. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba kupitia *TWPF*, tutawapelekea fedha kiasi kwa ajili ya kuwasaidia ili waweze kuwa na risasi za kuweza kufanya kazi hiyo.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza nimshukuru sana Waziri kwa kukubali kuitambua *WMA*. Nina swali dogo tu hapa, kwa kuwa zipo *beacons* ambazo ziligharamiwa na wafadhili wa *WMA* ambao walikuwa ni *USAID* ya Marekani na mtumishi aliyetoka Wizarani aliyepo pale Sikonge amezing'oa zile *beacons* ambazo jana nilisema kwamba ni za gharama ya karibu shilingi milioni 88. Waziri ana maelekezo gani kwamba zile *beacons* zirejeshwe mara moja na vitendo vya namna hiyo visirejewe tena?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Nkumba kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwamba muda haukuruhusu lakini nilidhamiria kumwomba radhi sana kwanza kwa usumbufu ambao umetokea, *is very unfortunately* kwa sababu Afisa Wanyamapori na Afisa Misitu ni watu ambao wote wapo kwenye Wizara moja. Kung'oa *beacons* lilikuwa siyo jambo sahihi na tumeshamwambia atoe maelezo ni kwa nini amefanya hivyo halafu baada ya hapo tutaweza kuona hatua gani za kufanya, lakini niseme tu kwamba, *remedy* ya jambo hili haitagusa wananchi kwa upande wa gharama.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Napenda kupata ufafanuzi kwa maana kwamba imekuwa imezoeleka kwamba katika maeneo mengi ya mbuga za wanyama ambazo mara nyingi zimekuwa ni *National Parks* kama Katavi, kumekuwa na matukio mengi ya ujangili ambayo unakuta kwamba wakati mwingine Askari wa Wanyamapori ni rahisi sana kuwaona wafugaji na ng'ombe zao na siyo majangili. Kwa mfano, katika siku za hivi karibuni majangili wameweza kukamata Tembo kutoka mbuga ya Katavi na kubeba pembe na wakaja kukamatiwa uraiani lakini wafugaji wanapokaribia mipaka wao inakuwa ni rahisi kuonekana, naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Waziri majibu, mimi sijaelewa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Kikwembe kama ifuatavyo:-

Kwanza, majangili ni binadamu na wana akili na wanajua kwamba wanachokifanya ni makosa kwa hiyo kwanza wanachokifanya ni kuhakikisha wamefanya utaratibu au wameweka mazingira ya kutoonekana. Kwa mifugo ni kundi, ng'ombe huwezi ukawaficha, unaweza ukajificha mwenye nao lakini ng'ombe wataonekana tu. Kwa suala la uhalifu unaofanyika ni jambo ambalo tunakabiliana nalo. Kwa hiyo, tutachukua hatua au tutaendelea kuchukua hatua za kudhibiti ujangili lakini wakati huohuo pia tutakuwa tukichukua hatua ambazo zinastahili za kimsingi kwa upande wa kudhibiti mifugo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Waziri anafahamu kwamba mamlaka zetu mbili Ngorongoro na *TANAPA* wanafanyakazi nyingi sana ndani ya hifadhi, kazi ambazo huku nje zinafanywa na Taasisi nyingine kwa mfano, barabara zote za hifadhini wanajenga ama Ngorongoro ama TANAPA. Kwa Ngorongoro kwa mfano, kuna umeme ambao umeingia hifadhini na kwenye nyumba na kwenye maeneo mbalimbali wamejenga mamlaka ya Ngorongoro lakini bado kwa mujibu wa Sheria mbalimbali ambazo Bunge hili lilipitisha hapa au maagizo, Mamlaka hizi zinatakiwa zitoe fedha nyingi sana ama Hazina au hata kwenye kodi. Kwa mfano, gharama ambazo Mamlaka hizi zinaingia kujenga barabara siyo *tax reductable*. Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba tunanyima hifadhi hizi uwezo wa kuweza kutunza hifadhi ambayo ndiyo kazi yao kubwa na ya msingi kuliko kazi nyingine yoyote. Tumesema jambo hili kwa muda mrefu sana, kwa nini Serikali isichukue hatua kuhakikisha kwamba fedha ambazo Mamlaka hizi zina-*incur* kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kimaendeleo kwenye hifadhi zisiwe zinatozwa kodi yaani ziwe *tax reductable* ili waweze kufanya kazi yao ya uhifadhi kama ambavyo Sheria inataka.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa swali la Mheshimiwa Zitto kama ifuatavyo:-

Ni kweli eneo hili limekuwa likileta changamoto au matatizo kwa muda, siku nyingi sana nimeacha kusoma Sheria ya Kodi, sina uhakika kama kuna kipengele chochote mahsusi cha Sheria ya Kodi kinachosema *expenditure* ya namna hiyo siyo *tax reductable*. Tumekuwa tukizungumza na wenzetu wa Hazina kuomba Taasisi hizi zipunguziwe *charges* ambazo haziendani na uhifadhi, hatujafikia makubaliano au hatujapata ruhusa kamili lakini sisi tumekuwa tuki-*pursue* jambo hilo kwa nia njema kabisa ya kuimarisha hifadhi zetu.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, naomba tupewe muda tuendelee kufanya majadiliano na wenzetu wa Hazina ikiwa ni pamoja na wenzetu wa *TRA* kuona umuhimu wa kuacha ku-*charge tax* kwenye maeneo ambayo kwa kweli yanaendana na uhifadhi.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Watanzania wengi wanashindwa kunufaika na ajira itokanayo na utalii kwa sababu ya kukosa elimu ya utalii wa kimataifa na vilevile kwa sababu ya kukosa *International Exposure*. Naomba Waziri atueleze atatatua vipi tatizo hili hatimaye kuwe na ufanisi wa kazi utakaosababisha ongezeko la mapato yatokanayo na utalii nchini?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Leticia Nyerere kama ifuatavyo:-

Ni kweli tatizo lipo, jitihada ambazo Serikali imekuwa ikifanya, moja ni kujaribu kuvihimiza Vyuo vya Elimu ya Juu viwe na mitaala au viwe na kozi zinazohusu utalii, Chuo kama *UDOM* kinatoa kozi hizo. Kwa maana ya *graduate level* tunapata wanafunzi wanaosoma kozi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa upande wa Taasisi au Vyuo vya Wizara, Chuo cha Wanyamapori Mweka wameanza Kozi ya Utalii wa Wanyamapori *(Wildlife Tourism)* ambayo itaanza mwezi Oktoba mwaka huu kufundisha vijana kutoa huduma za kitalii kwa wageni lakini vilevile Chuo chetu cha Utalii cha *National Collage of Tourism* tumesema hapa kwamba tutaanzisha kampasi mpya ya Dar es Salaam ambayo itakuwa inatoa kozi ya huduma kwa watalii.

Kwa ujumla wa yote haya tunategemea kwamba huduma kwa wageni zitaimarika na watoa huduma hizo watapata elimu ambayo tunaitarajia.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sokwe mtu anapatikana katika hifadhi mbili tu, Hifadhi ya Gombe na Mahale lakini hatupati watalii wa kutosha kutokana na matatizo mbalimbali ikiwemo suala la usafiri. Zamani tulikuwa tunapata watalii kwa sababu walikuwa wanatumia Air Tanzania, je, kwa nini *TANAPA* isiwe na ndege zake ili kurahisisha usafiri kwa watalii? Vilevile usafiri wa Ziwa Tanganyika ni maboti ya mbao, kwa nini *TANAPA* wasihakikishe wanapata *speed boats* ili kuhakikisha kwamba mapato ambayo yanatokana na Gombe na Mahale yanaongezeka na pato la Taifa liongezeke?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ipo. *TANAPA* sasa hivi kipaumbele kimekuwa kwenye uhifadhi kwa sababu ni Taasisi ya Uhifadhi. Kuna *query* ambayo imetolewa na Mchungaji hapa kwamba *TANAPA* inatumia fedha karibia zote inazozipata, ni kweli kwa sababu shughuli za kudhibiti ujangili, shughuli za kuendeleza hifadhi na kadhalika zinatumia fedha nyingi zaidi. Kwa hiyo, niombe kwamba kama ambavyo nimesema kwenye suala la huduma za hoteli kwenye *parks*, suala la kuboresha huduma za usafiri ikiwa ni pamoja na wazo kama alilolitoa Mheshimiwa Zitto na kuwa na hisa kwenye mashirika au kampuni ya ndege ya Taifa, waweze kulifikiria, ni jambo jema, tutaliangalia kadri mapato ya *TANAPA* yanavyozidi kuongezeka.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya wananchi wa Kata za Nkimiziwa, Milambo Itobo, Magingati, Mizibaziba na Migua, naomba Waziri atoe kauli hapa ambayo wataisikia kwamba ni lini atawatoa katika mashaka na wasiwasi mkuu ambao wamekuwa nao toka Serikali itoe barua za kuwataka wahame kwenye vijiji ambavyo vilipitishwa kihalali mwaka 1974?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Dkt. Kigwangala, Mbunge wa Nzega kuhusu suala la wananchi kuendelea kuishi kwenye maeneo yao ambayo sasa hivi wanaishi lakini pia yenye *status* ya hifadhi. Kama nilivyosema kwenye majibu ya sehemu nyingi, nilifafanua kwamba kuna maeneo mengi sana yenye sura kama eneo hilo ndiyo maana tumesema kwenye Tume ambayo tutaiunda na itafanya kazi kwenye mwaka huu wa fedha, itakayohusisha Wizara ya Ardhi, Wizara yetu na TAMISEMI, tutaangalia maeneo yote yenye sura za namna hiyo ili maamuzi thabiti yaweze kufanyika. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo wananchi wamekuwa wakiishi miaka thelathini, arobaini, sina uhakika, basi wataendelea kuishi hivyo wakati Tume hii inafanya kazi yake halafu baada ya mapendekezo ya Tume hiyo kuwa yamewasilishwa, Serikali tutaweza kuona sasa hatua gani za msingi tuchukue.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia suala la kupanua ajira kwa vijana katika Jimbo la Ubungo kupitia uwekezaji kwenye msitu wa Hifadhi ya Pande uliopo Mpiji Magoe, Mbezi. Nilizungumzia vilevile suala la kufufuliwa kwa kiwanda pamoja na mafao ya wafanyakazi wa Kiwanda cha Mkumbara wanaotumia msitu wa Shume, naamini hayo nitapata ufafanuzi wa kimaandishi lakini nitaka ufafanuzi wa suala moja la kisera kuhusu Urani, pamoja na majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba utakuwa unarudia suala ambalo limeshatolewa maelezo?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Hapana!

**MWENYEKITI:** Tayari limetolewa maelezo kabisa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lililoulizwa ni kama Kamati za Bunge zitahusishwa, sasa katika majibu ya Waziri ya msingi alisema kwamba hili suala lilikuwa ni *admnistrative* na kwamba Kamati zingehusishwa kwa *knowledge* na kwamba ni *issue* ambayo

ingeleta mapato makubwa. Nitaka kupata ufafanuzi kwa sababu hili jambo pamoja na kuwa Sheria husika inahusisha Mkataba wa *UNESCO* ambao nchi yetu iliridhia na Bunge likauidhinisha. Kuna mjadala mpana sana kuhusu mapato ukizingatia mpaka sasa tumepoteza *almost* bilioni 600 kwa Makampuni haya ya Urani kubadilishana umikiliki kati ya Kampuni ya Australia na Kampuni ya Urusi. Sasa nilitaka kupata jibu ambalo halijajibiwa kutokana na swali la Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka kwa sababu ya kasoro zilizojitokeza, je, Serikali iko tayari sasa kurudi upya kuzihusisha kikamilifu Kamati za Bunge, katika jambo hili kuanzia hatua za awali? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa kifupi sana nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa John Mnyika kwamba tutafanya hivyo kuanzia sasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Lakini Mheshimiwa Waziri utalaam stahili lazima uwepo tusije tukasema sisi ni watalaam wa Urani na kila kitu, naomba sana utalaam makini uwepo maana Bunge wakati mwingine inafikia hadi linachanga watu. *(Makofi)*

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Waziri, napenda kufahamu jambo moja, kwenye Pori la Hifadhi la Swagaswaga lililoko Wilayani Kondoa, sasa hivi kumekuwa na wafugaji wa Kibarabaigi ambao wamevamia eneo lile kiasi kwamba wanyama walioko pale, Tembo, Simba na wengine wameamua kuondoka na kuingia kwenye mashamba ya watu kwenye maeneo ya Gwandi na kwenda kushambulia mazao ya wananchi. Askari Wanyamapori walioko pale Kwamtoro wana usafiri lakini wana bunduki ambazo hazina risasi. Nini kauli ya Serikali kuhusu jambo hili?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Juma Nkamia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yeye mwenyewe alivyokiri kwamba mifugo imeingia hifadhini kwa maana hiyo si jambo ambalo ni sahihi. Kwa maana hiyo, tutakachokifanya kwa upande wetu ni kwamba tutakwenda eneo hilo, tutazungumza na hawa wananchi ambao kimsingi hawapaswi kuwa pale halafu baada ya hapo kwa kutumia mfumo wetu wa kibajeti wa kawaida tutawawezesha Askari wetu walioko pale ili waweze kufanya kazi zao vizuri zaidi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. SEIF S. RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilizungumzia juu ya uhifadhi wa wanyamapori, mpango ambao mwanzoni Mheshimiwa Waziri alijibu kama swali kwamba Serikali itakamilisha mradi huo wa kukamilisha Mpango wa Uhifadhi wa Wanyamapori katika Kata za Muaseni, Ngorongo mpaka Ngarambe mpango ambao unategemea bajeti kutoka kwa wafadhili na siyo bajeti ya Serikali. Nataka nifahamu katika mpango huu na bajeti hii ambayo tunaipitisha sasa Mheshimiwa Waziri ana kauli gani ya kuhakikisha kwamba mpango huu ambao umeanza kwa miaka mitatu sasa unakamilika? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Dkt. Seif kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kwenda Rufiji nikakutana na uongozi na wakanieleza kuhusu suala hili na niliwaambia jambo ambalo nataka kulirudia hapa kwamba moja ya changamoto kubwa ambazo tumekuwa nazo ni pamoja na kutegemea wafadhili watusaidie kwenye jambo hili muhimu kabisa. Kwa hiyo, tumejipanga mwaka huu wa fedha kwamba tutatumia fedha zetu kuzisaidia *WMA* zinazoanza. Sina hakika kama hii ya Mheshimiwa Dkt. Seif ipo lakini najua kwamba kuna *WMA* sita (6) ambazo tutazisaidia kuhakikisha kwamba zinaanza katika mwaka huu wa fedha kwa fedha zetu. Kwa sababu ameliuliza swali hili *specifically* basi hata kama haitakuwemo *WMA* ya eneo lake, tutatafuta namna yoyote kuhakikisha kwamba tunawasaidia kuhakikisha kwamba wanaanzisha. *(Makofi)*

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mbogwe, kuna vijiji vitatu vinavyopakana na Hifadhi ya Pori la Akiba la Kigosi Myowosi. Maliasili wamewazuia watu kunywesha mifugo yao katika Hifadhi ile na wameamua kuchimba Rambo katika Kijiji cha Sango. Sasa nilitaka kujua Mheshimiwa Waziri ana mpango gani kwa wafugaji wa Kijiji cha Nyashimba na Busambilo ambao na wenyewe wana tatizo lilelile?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa swali la Mheshimiwa Augustino Masele, Mbunge wa Mbogwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumekuwa tukiondoa mifugo inapoingia hifadhini lakini hata sisi tunapofanya hivyo hatupendi kwa sababu si jambo jema kwa sababu tunahitaji mifugo ipate malisho. Tumesema katika mwaka huu wa fedha tutaanza kusaidia maeneo ya wafugaji yaliyo pembezoni mwa hifadhi wapate mahitaji yao ya msingi hasa maji kutoka kwenye maeneo ya vijiji vyao. Tokea mwaka jana tulikuwa tumekwishaanza kupeleka fedha, mwaka jana Bukombe na Nsanga tulipeleka shilingi milioni 25 kwa ajili ya kuchimba bwawa. Mwaka huu tutapeleka tena fedha zingine ili kukamilisha bwawa hilo halafu tutaendelea kwenye maeneo mengine.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka hii ya karibuni, Mji wa Mtwara umekuwa na wageni wengi sana wa kitalii na wanaongezeka kila kukicha lakini watalii hawa kutokana na uwezo walionao hulazimika kwenda Dar es Salaam jioni na asubuhi kurudi kule kwa ndege kitu ambacho ni gharama sana. Naomba kupata mawazo ya Mheshimiwa Waziri kwa nini asishirikiane na Bodi yake ya Utalii, kujenga hoteli ya kisasa pale, ambayo itasaidia au hata kutafuta wawekezaji ambao watasaidia kumaliza tatizo na usumbufu unaowapata watalii hawa na hasa sasa hali iliyoko kwamba kuna watu wengi kweli wanaokwenda kufanya utafiti wa gasi na mafuta na hii itakuwa jambo jema sana kwa dhana ileile ya kuongezea Taifa letu pato?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa swali la Mheshimiwa Juma Njwayo kwa kifupi tu kwamba sehemu nyingi za utoaji wa huduma tumekuwa tukipenda kufanya kazi na sekta binafsi, kusafirisha wageni na kuwalaza. Naamini eneo hili yawezekana tu hawa wawekezaji wa sekta binafsi hawajalijua kwamba ni eneo muhimu sana kwa biashara yao. Kwa hiyo, pamoja na nia ambayo tunaweza tukawa nayo sisi ya kutaka kujenga wenyewe kupitia *TTB* au kupitia chombo kingine cha Serikali lakini namwomba Mheshimiwa Mbunge nichukue wazo lake tushirikiane na wadau wetu wa hoteli, kuna *Hotel Associations of Tanzania* pamoja na wengine kuwaambia kuna maeneo muhimu ya Mtwara kwa ajili ya kujenga hoteli. Naamini sekta binafsi wanaweza wakawekeza.

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Wakati tunajadili hapa awali kulitokea tuhuma za karibu Wabunge wawili au watatu kwamba katika Wizara kuna ajira ambazo zinaelekea kwamba ni za kikabila lakini mimi navyofahamu makabila mengi ukienda Wizara nyingi utakuta kuna watu wa makabila yanayofanana na halijatoka lalamiko. Napenda kujua, ikiwa ajira inachukua msingi wa *qualification,* imekuweje katika Wizara kama ni kweli ajira zinazolalamikiwa zifungamane na ukabila? Naomba maelezo Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa swali la Mheshimiwa Dkt. Mgimwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme tu hata mimi niliposikia habari hizi nimestuka na nimesikitika kwa sababu ni jambo ambalo mimi hata nilikuwa sijui nani ni kabila gani. Utaratibu wa ajira Serikalini ni wa kufuata *qualification* na navyoamini ni kwamba hakuna utaratibu wowote katika Serikali wa kusema mtu apewe kazi kwa kufuata kabila au mahali anapotoka au rangi yoyote au namna yoyote ya ubaguzi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, si Sera ya Serikali wala mpango wa Wizara wa kusema watu wa kabila fulani wakae pamoja au wasikae pamoja. Kama wana sifa na wana taaluma inayoendana na kazi wanazozifanya watapata kazi bila matatizo yoyote.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilimueleza Waziri kuhusu tatizo la Kitongoji kimoja kinaitwa Mwambisi pale Kijiji cha Kisarawe. Kitongoji kile karibu nyumba 47 zimevunjwa zote, wananchi karibuni 150 hawana mahali pa kukaa. Nimehangaika sana mpaka Ofisi ya Waziri Mkuu, nadhani Waziri Mkuu analifanyia kazi hilo lakini naona leo ni muda muafaka, wananchi wanapata shida kwelikweli, watoto wanashindwa mpaka kwenda shuleni, wabibi wazee mpaka wamechanganyikiwa hawajui nini cha kufanya. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze, sasa wako katika *television* wanasikiliza nini mustakabali wao, je,

anasemaje kuhusu hilo ambalo limesababisha hata watoto kukosa haki yao ya elimu? Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa Mheshimiwa Jafo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo amesema ni kweli tatizo hili tulishapata taarifa na taarifa pia alishazipeleka hata kwenye ngazi zingine za uongozi wa nchi yetu. Niseme tu kwamba Wizara kama Wizara hatuna nia wala hatutegemei kwa kweli kusababisha usumbufu kwa wananchi bila sababu za msingi. Tumekuwa tukiwashauri wananchi kwamba pale ambapo wameambiwa kwamba eneo hili hawastahili kukaa kwa sababu fulani za kisheria ni vizuri wakafanya hivyo. Eneo kama hili na kuna baadhi ya maeneo ambayo kwa kweli ni *instigation* tu wanashawishiwa kukaa kwenye eneo fulani wakijaribu kujipanga na kuomba kwamba warudi. Tumekuwa tukiwashawishi, tutakuwa tunatoa huduma za msingi za binadamu pale ambapo matatizo yametokea kama ilivyotokea Urambo lakini hoja ya msingi ni kuwashauri kwamba kwa sababu eneo hilo halipaswi kukaa basi watii.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu liko kwenye Uwekezaji kwenye Madini ya Uranium kwenye Pori la Akiba la Selous. Tumekuwa tukishuhudia migogoro mingi sana inatokea kwenye sekta ya madini hasa kwenye maeneo ya uchimbaji kati ya wawekezaji na wananchi. Kwa kuwa mkataba bado hatujaingia, ndio tuko kwenye hatua za awali katika kuchimba *Uranium,* je, Serikali iko tayari sasa kushirikiana na Mashirika ya Umma ili waweze kumiliki hisa asilimia 50 katika mradi huu ili kuepukana na migogoro inayoweza kutokea na vilevile kuwa na *commitment* katika uchimbaji na uuzaji wa madini haya na tukijua kwamba mradi huu ni wa miaka 15 tu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie Wabunge na Watanzania wote kwamba *Mining Development Agreement (MDA)* yote inayoingiwa na wawekezaji kwa sasa hivi inaingiwa kwa Sheria ya Madini ya 2010 ambayo tumeipitisha hapa sisi wenyewe. Katika hilo, Serikali kwanza kabisa tunakwenda mbele na tunaweka msingi wa *free carried interest* ambazo ni hisa ambazo zinaingia kwa manufaa ya sisi Watanzania wenyewe ama itakuwa asilimia 20 au 30 kama itakavyoamuliwa. Naomba niseme tu kwamba hata mwekezaji alishaambiwa hilo na analijua na lipo na litakuwepo katika mkataba huu mpya kwa mujibu wa Sheria.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kupongeza Serikali kwamba imeamua kuwa na Kamati za kwenda kutazama hayo matatizo katika maeneo mbalimbali. Naamini kwamba Kamati hizo zitaheshimu Katiba Ibara ya 63 kwamba Bunge ndio mshauri na msimamizi wa Serikali. Sasa kwa kuwa kiu ya mifugo haisubiri bajeti *allocation*, je, *TANAPA* na maeneo yote ambayo mmepanua hifadhi, hao wanyama ambao wanahitaji maji na maji hayo yaliyokuwepo yakamezwa na upanuzi wa hifadhi, mtakuwa na utaratibu gani wa kuhakikisha mifugo hiyo inapata huduma hiyo na kudhibiti rushwa wanazotozwa wananchi na kubambikizwa kesi? Ahsante.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa suala la Mheshimiwa John Shibuda Magalle, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyomjibu kaka yangu Mheshimiwa Augustino Masele, nia ya Serikali kwa kweli ni kuwasaidia wafugaji kwenye maeneo yao nje ya hifadhi. Katika kulitimiza hilo, tutakuwa tunashirikiana na TAMISEMI na Serikali kwa maana ya Wizara ya Maji kuhakikisha kwamba wanapata huduma hizi za msingi. Kwa hiyo, tumesema tutapitia upya utaratibu wa ujirani mwema wa vyombo vyetu vyote vya ulinzi kwa maana ya *TANAPA* pamoja na Idara ya Wanyamapori, pamoja na *TWPF,* kuona namna ambavyo itafaa kusaidia jamii ambayo kwa kweli wanahamahama kwa sababu ya kutafuta maji.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nipongeze Serikali kwa kazi nzuri ambayo wamefanya hasa kwenye upande wa watalii. Mkoa wa Tanga kuna vivutio vingi mfano Mboni pale Korogwe, kuna sehemu ambayo *Chief* wa Wasambaa Mbega alivuka

maji katika Mto wa Ruvu, ile sehemu mpaka leo hii haipanuki, watalii wengi wanakuja kuangalia lakini haijapata *promotion*. Kule Lushoto kuna sehemu moja inaitwa Gorogoro, kuna mahali ambapo kuna mtu alikanyaga kwenye jiwe unyayo uko mpaka leo. Kwa hiyo, kama tunataka kutangaza utalii, naomba sehemu hizi pia ziangaliwe ili nazo zipate hamasa ili watalii nao wakaangalie hasa pale Mahuruwi ambapo Mto Ruvu umezama kabisa. Alikuja pale akaruka, baada ya kuruka ule Mto ukabaki vilevile mpaka leo hii ni sehemu moja kubwa sana ya utalii. Naomba Mheshimiwa Waziri aangalie na Mkoa wa Tanga, ameangalia tu Mikoa mingine lakini Mkoa wa Tanga amesema tu Amboni na huko vilevile katika Wilaya zake kuna sehemu za utalii twende akaziangalie na alete watu waje waziangalie, ahsante sana.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Ngonyani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ni kutangaza utalii kwa nchi yetu yote kutegemeana na vivutio mbalimbali ambavyo viko kwenye maeneo mbalimbali Mkoa wa Tanga ukiwa mmojawapo. Tatizo kubwa ambalo limekuwa likitusibu ni suala la bajeti, uhaba wa fedha. Ndio maana tumekuwa tukiweka vipaumbele kwamba angalau kwa Mkoa wa Tanga tuwe na vivutio viwili, vitatu ambavyo ni *prompt,* ambavyo ni rahisi kuvitangaza kama tulivyosema suala la Amboni lakini kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya kubaini haya maajabu yaliyoko kwenye maeneo haya, nitatuma watu wangu watakwenda na tutaingiza kwenye mpango wetu wa uendelezaji utalii wa Mkoa wa Tanga.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati nachangia Wizara hii ya Maliasili, nilikuwa nimeomba kupewa ufafanuzi kuhusiana na matatizo kadhaa ambayo yanaikabili Wilaya yangu. La kwanza, nilikuwa nimeomba kupata ufafanuzi kuhusu asilimia 25 ya mapato yanayotokana na uwindaji wa kitalii kwa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale. Mwaka 2006/2007/2008, Wilaya hii haikupelekewa asilimia 25. Naomba kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kwa miaka miwili, mitatu tumekuwa hatupeleki hizi asilimia 25 kwenye maeneo ambayo zimetoka au zinastahili kupelekwa. Tatizo kubwa limekuwa ni fedha. Tumekuwa tukizikusanya tunazipeleka Hazina halafu zinazoletwa, zinaletwa kidogo kwa ajili ya matumizi tu ya Wizara. Hii sisi tumekuwa tukihesabu kwamba ni madeni na tumekuwa tukiendelea kudai kwa wenzetu wa Hazina ili watuletee na tuweze kuzipeleka. Nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu jambo hili ni mipango ya Serikali basi tutakapokuwa tumepata fedha za kutosha tutapeleka kama inavyopaswa kufanyika.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza kabisa, nimshukuru Waziri kwa kueleza Sera ya Serikali kwamba si ya ukabila, ilinisumbua kidogo kwamba inaonekana ndugu zangu Wabena wanasulubiwa kwa sababu ya Ubena wao na siyo Sera ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, usirudie swali ambalo limeshaulizwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya msingi, inaonekana Serikali imechukua hatua baada ya Wabunge kutoa michango yao lakini katika hotuba niliyoitoa nilimtaja aliyekuwa Katibu wa Wizara pamoja na Mkurugenzi wa Wanyamapori wakati ule, hajafafanua ni hatua gani ambazo tulishauri kama Kambi ya Upinzani kwamba na wenyewe wangefanya uchunguzi kama walishiriki katika dira nzima ya kusafirisha wanyama hujafafanua, naomba ufafanuzi katika hilo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Baba Mchungaji Peter Msigwa, Mbunge wa Iringa Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye suala hili kwamba kuna kesi iko Mahakamani na tunafanya uchunguzi, tumetaja wale ambao wanastahili kuchunguzwa, wale

ambao wako ofisini na tukasema kwamba wale kwa maana ya kwamba wametajwa kama ilivyotajwa hapa Bungeni itabidi wasimame kwa malipo ili uchunguzi uweze kufanyika. Kwa wale ambao hawako kwenye utumishi, uchunguzi unaendelea na nisingependa kutaja kwamba akina nani wanachunguzwa lakini kuna uchunguzi mpana sana unaendelea sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Ahsante dakika za kufanya *guillotine* zimefika na nategemea Mheshimiwa Waziri katika lile fungu utatuambia hesabu iliyohusika.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maslahi ya muda, niombe tu kwamba *figure* iliyoko kwenye kitabu ambacho Wabunge wanacho ni sahihi ile niliyosoma kwenye hotuba yangu inatofauti ya shilingi 2000, *figure* ambayo tutatumia ni ile iliyoko kwenye kitabu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif.1002 - *Finance and Accounts* …………… Tshs.1, 832, 048,000/=
Kif.1003 - *Policy and Planning* ……… Tshs. 1,355,139,000/=
Kif.1004 - *Education, Information and Communication*…………..........Tshs.127, 173,000/=
Kif.1005 - *Internal Audit Unit*…………………… Tshs.431, 956,000/=
Kif.1006 - *Procurement Management Unit*..... Tshs. 552,634,000/=
Kif.1007 - *Legal Unit*..................... Tshs. 265,251,000/=
Kif.1008 - *Management Information System*........................................................Tshs.584,258,000/=
Kif.2001 - *Wildlife*......................... Tshs.18,994,851,000/=
Kif.3001 - *Forestry and Beekeeping*…………Tshs.14, 263,434,000/=
Kif.4001 - *Tourism* ………………………………… Tshs.62, 520,000=
Kif.4002 - *Antiquities Unit*................................. Tshs.4,316,542,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Pamoja na mabadiliko yake)*

**KITABU CHA NNE**

**FUNGU 69 - WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

Kif.1001 - *Administration and General*...................................Tshs. 0/=
Kif.1002 - *Finance and Accounts* ................................... Tshs.0/=
Kif.2001 - *Wildlife* …………………………………………… Tshs.0/=
Kif.3001 - *Forestry and Beekeeping*………………………… Tshs.0/=
Kif.4001 - *Tourism*…………………………………………… Tshs.0/=
Kif.4002 - *Antiquities Unit* ……………………… Tshs. 45,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Pamoja na Mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka Fedha 2011/2012, Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu likubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii yamepitishwa na Bunge na tunawatakia utumishi mwema na ile Tume mliyosema mtaunda kuangalia haya manyanyaso wanayopata wananchi, nadhani ni muhimu kufanya hivyo kwa sababu habari tulizozisikia hapa zinatisha na hazieleweki, kwa hiyo, naamini mtaunda Tume itakayofanya kazi kwa makini. Nadhani tutaunganisha na ile nyingine, tutampa Waziri Mkuu, kuhusiana na Mwongozo tuliompa Sakaya, tutakupa majibu lakini kuna eneo fulani tunataka Wizara ya TAMISEMI kuangalia ukweli huo kwamba *DC* alikuwa anaingia kwenye mazizi ananyang'anya mbuzi na hiyo tunapenda pia liweze kuingia katika utaratibu huo.

Baada ya kusema hayo, ninayo matangazo mawili, la kwanza ni kwamba Mheshimiwa John Mnyika, huyu ni Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kwamba kesho tarehe 19 saa saba na robo watakuwa na kikao chao katika ukumbi namba 219.

Tangazo lingine ni kwamba Waheshimiwa Wabunge siku ya Jumamosi tarehe 20 tutakuwa na semina kuhusu madhara ya matumizi na biashara ya madawa ya kulevya itakayoratibiwa na ofisi ya Waziri Mkuu. Najua na wale wengine wadau wa Korosho nao wana kikao, wafahamu taarifa hiyo, bado kikao kile kipo.

Siku ya Jumapili pia tarehe 21 kutakuwa na semina kuhusu masuala ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki itakayotolewa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Vikao vyote kwa siku hizi mbili cha Jumamosi kitaanza saa nne na kikao cha Jumapili kitaanza saa 4.30, naomba mzingatie, tutawakumbusha tena kesho.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sina matangazo mengine. Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.28 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 19 Agosti, 2011 Saa Tatu Asubuhi)*